**4 MEI, 2026**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA TATU**

**Kikao cha Ishirini na Moja - Tarehe 4 Mei, 2026**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mkutano wa Tatu, Kikao cha Ishirini na Moja, leo tarehe 4 Mei, 2026.

Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

**MHE. REGINA H. MIKENZE K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ELIMU, UTAMADUNI NA MICHEZO:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo, kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na maswali Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Mheshimiwa Yahya Ally Mhata, Mbunge wa Nanyumbu, aulize swali lake.

Na. 243

**Ujenzi wa Mabweni Katika Shule za Sekondari – Nayumbu**

**MHE. YAHYA A. MHATA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga Mabweni 10 katika Shule za Sekondari Jimbo la Nanyumbu?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Yahya Ally Mhata, Mbunge wa Nanyumbu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikijenga mabweni katika shule za sekondari za bweni na shule za msingi kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu. Aidha, Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa kushirikiana na wazazi au walezi pamoja na wadau mbalimbali, wamekuwa wakijenga mabweni katika shule za kutwa katika mazingira hatarishi au ambayo wanafunzi wanatembea umbali mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2022/2023 – 2025/2026 Serikali imepeleka shilingi bilioni 4.2 kwa ajili ya ujenzi wa shule ya sekondari ya bweni ya wasichana Mkapa na umaliziaji wa maboma mawili, mabweni mawili katika shule za Sekondari za Lumesule na Mkonona katika Jimbo la Nanyumbu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2026/2027 Serikali imetenga shilingi milioni 320 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa tisa, matundu ya vyoo mawili na nyumba za walimu mbili katika Shule ya Nangaramo na Marata za Jimbo la Nanyumbu. Serikali itaendelea kutenga fedha za ujenzi wa miundombinu ya elimu yakiwemo mabweni katika shule za sekondari kadiri ya upatikanaji wa fedha, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Yahya Ally Mhata.

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza. Kwanza, swali langu lilikuwa linalenga ujenzi wa mabweni katika Jimbo langu la Nanyumbu, majibu yaliyotolewa hapa, yanapotosha ukweli halisi. Unapoitaja Shule ya Sekondari ya Mkapa, ile ni shule maalum kwa wasichana, kila Mkoa imejengwa, moja iko ndani ya Jimbo langu. Kwa hiyo, inawezesha kuonekana fedha nyingi zimeletwa Nanyumbu ambapo kwa hali halisi siyo sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Waziri anaweza akatusaidia hizi shule mbili ambazo zimepelekewa fedha za umaliziaji wa mabweni, anaweza akatuelezea *status* ya mabweni iko vipi na ni shilingi ngapi zimepelewa katika hizi shule mbili? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza, ninampongeza sana Mheshimiwa Yahya Ally Mhata, Mbunge wa Jimbo la Nanyumbu, amekuwa msemaji madhubuti sana wa wananchi wa Jimbo la Nanyumbu, na alishawasilisha hoja ya kuomba ujenzi wa mabweni katika shule zake 10, nami nimhakikishie tu, ninafahamu Mheshimiwa Mbunge, angependa kuona shule zake zote za sekondari zinakuwa na mabweni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo wa Serikali katika eneo la ujenzi wa mabweni ambao tunautumia hivi sasa, kwanza, tunajenga mabweni kwenye shule za sekondari za kidato cha tano na kidato cha sita; pili, tunajenga mabweni kwenye shule za wanafunzi wenye mahitaji maalum; tatu, tunajenga mabweni kwenye zile shule ambazo zina umbali mrefu na changamoto kwa wanafunzi kufika kwenye shule hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo hili, kwenye shule za Kata na Mikoa, Halmashauri zenyewe na wadau wanapewa ruhusa ya kujenga mabweni katika maeneo hayo. Kwa hiyo, nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge katika shule zote za kidato cha tano na sita, hata katika Jimbo la Nanyumbu ujenzi wa mabweni ni kipaumbele na ndiyo maana nimejibu katika jibu langu la msingi kwamba kuna fedha zimepelekwa, lakini kuna fedha zimetengwa kwa ajili ya kwenda kujenga mabweni kwenye shule za kidato cha tano na kidato cha sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuhakikishie kwamba Serikali hii inatambua umuhimu wa kujenga mabweni, kuwezesha wanafunzi kusoma kwa karibu, tutaendelea kwa kadri ya upatikanaji wa fedha kuhakikisha kwamba tunajenga mabweni hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hali ya mabweni haya ambayo fedha zimepelekwa, Mheshimiwa Mbunge baada ya maswali hapa nitafuatilia *status* ya sasa, nitakupa majibu ya

uhakika ili tuweze kuona hatua ambayo inaweza kuendelea. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ester Bulaya.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru nami niulize swali dogo la nyongeza. Shule ya Sekondari ya Bunda, kwa miaka mitatu mfululizo imeongoza Mkoa wa Mara, kwa wanafunzi kufaulu kidato cha tano na kidato cha sita, lakini ina changamoto ya mabweni, pamoja na Shule ya Dkt. Nchimbi. Ni lini sasa zitajengewa mabweni ili watoto wetu waweze kusoma vizuri na kuendelea kufaulu? Ninaomba majibu mazuri ukizingatia wenye Jimbo lao wapo pale juu wananiangalia. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza sana dada yangu, Mheshimiwa Ester Bulaya, mchapakazi, Mbunge jembe sana wa Jimbo la Bunda Mjini, na kwa kweli amefuatilia mara kadhaa kuhusiana na ujenzi wa mabweni katika Shule ya Sekondari ya Bunda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawapongeza sana wananchi wa Bunda Mjini na Walimu wa Shule ya Sekondari ya Bunda kwa kuwa kinara wa matokeo ya kidato cha sita katika Mkoa wa Mara na hiyo ndiyo dhamira ya Serikali kuhakikisha kwamba wanafunzi wetu wanafanya vizuri kwenye mitihani, na leo hii wanafunzi wa kidato cha sita wanaanza mitihani. Kwa hiyo, tunawaombea kila la heri, waweze kufanya mitihani yao vizuri ili waweze kulijenga Taifa letu la Tanzania kwa ufanisi mkubwa zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nimhakikishie Mheshimiwa Bulaya kwamba Serikali inatambua tunao upungufu wa mabweni pamoja kwamba yapo, lakini kuna upungufu kwa sababu kuna ongezeko kubwa la wanafunzi na tayari tumeweka mpango mkakati wa kujenga mabweni katika shule zote za kidato cha

tano na sita na zile nyingine zenye mahitaji maalum kuhakikisha kwamba tunaondoa changamoto ya upungufu wa mabweni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Shule ya Sekondari ya Bunda na shule yenye jina la Mheshimiwa Makamu wa Rais, Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi tutaipa kipaumbele kuhakikisha kwamba tunajenga mabweni na wanafunzi wanasoma katika mazingira bora zaidi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Moses Ludovico Kaegele, Mbunge wa Nkasi Kusini.

Na. 244

**Ujenzi wa Kituo cha Afya Kata ya Ninde – Nkasi Kusini**

**MHE. MOSES L. KAEGELE** aliuliza:-

Je, lini Serikali itatenga fedha kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa Kituo cha Afya Ninde kilichoanza kujengwa tangu mwaka 2013?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Moses Ludovico Kaegele, Mbunge wa Jimbo la Nkasi Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2021/2022 hadi 2025/2026 Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi imepokea jumla ya shilingi bilioni 1.7 kwa ajili ya ujenzi wa hospitali ya Wilaya, shilingi bilioni 3.6 kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya saba na shilingi milioni 840 kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma ya zahanati 16.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo cha Afya Ninde kilianza kujengwa kwa nguvu za wananchi mwaka 2013. Aidha, katika mwaka 2018/2019 Serikali ilitoa jumla ya shilingi 200,000,000 kwa ajili ya ujenzi wa jengo la wagonjwa wa nje *(OPD)* na vyoo vya nje. Jengo limekamilika na huduma za wagonjwa wa nje zimeanza kutolewa mwaka 2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu iliyosalia katika kituo cha afya Ninde ikiwemo jengo la wodi ya wazazi *(maternity),* jengo la upasuaji *(operating theatre),* jengo la maabara, jengo la wagonjwa wa kulazwa *(IPD),* jengo la mionzi, na jengo la kuhifadhia maiti *(mortuary)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Moses Kaegele.

**MHE. MOSES L. KAEGELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimwulize Mheshimiwa Naibu Waziri, maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ni kweli kwamba Serikali ilipeleka shilingi 200,000,000 na ikajenga kweli *OPD* ikakamilika, lakini sasa kituo hiki cha afya kinalisha wakazi zaidi ya 20,000. Ninataka kupata *commitment* ya Serikali, ni lini sasa jengo la maabara, *theatre* pamoja na jengo la kujifungua akina mama litaanza kujengwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Kituo cha Afya cha Ninde kinapatikana umbali wa kilometa 100 kutoka Makao Makuu ya Halmashauri kwa maana ya wilaya, na changamoto imekuwa kubwa sana na kuongeza gharama kutokana na gharama za usafirishaji. Je, ni lini Serikali itapeleka wataalamu kwenda kufanya tathmini ya kujua gharama na hali ya ujenzi wa majengo haya mengine ambayo yamesalia ili sasa kuwezesha Serikali kutenga fedha inayotosha inapokwenda kule, basi ikakamilishe majengo yote haya kwa wakati? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Kaegele, Mjumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kwa kuuliza maswali madogo ya nyongeza kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Nkasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kujibu swali la pili, kwamba tayari timu ya wataalamu wa Halmashauri wakishirikiana na wataalam wa Mkoa, wameshafanya tathmini kuangalia ukubwa wa eneo la kujenga miundombinu hii, majengo matatu muhimu; Jengo la *maternity complex,* maabara na *theatre*. Kwa hiyo, tathmini imeshafanyika na wameshawasilisha andiko Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI. Nimhakikishie Mheshimiwa Kaegele, tumepokea andiko hilo na ndiyo sasa tunakwenda kutekeleza mpango wa pili wa bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba mwaka 2027/2028 tunakwenda kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa kituo hiki cha afya. Mbali na hilo, tayari tumeshapeleka shilingi 250,000,000 kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya Kate. Kwa hiyo, Mheshimiwa Kaegele, ndani ya eneo hilo tayari wananchi wetu wataendelea kupata huduma katika Kituo chetu cha Afya Kate. Ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Anne Kilango Malecela.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa sijaomba kuuliza swali la nyongeza kwenye swali hili, ni swali lililopita. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Sawa, ulikuwa haujabonyeza kuondoka ndiyo maana ninakuona hapa.

Mheshimiwa Dkt. Wilson Charles.

**MHE. DKT. WILSON C. MAHERA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuuliza, ni lini Serikali itajenga kituo cha afya katika

Kata ya Muriaza eneo la Mibango, ambapo wananchi tayari wameshasomba mawe na wametenga eneo?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Mahera, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, Serikali inatambua na kupongeza juhudi za wananchi kuanza kuweka nguvu katika ujenzi wa vituo hivi vya afya, lakini nimhakikishie Mheshimiwa Dkt. Mahera tayari tumefanya ya boma ya vituo vya afya zaidi ya 301 ambavyo tunahitaji zaidi ya shilingi 66,000,000,000 ili kwenda kukamilisha ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Dkt. Mahera, tutakamilisha ujenzi wa kituo hicho cha afya na kuunga juhudi za wananchi katika Jimbo lake.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Waheshimiwa Manaibu Waziri kwa majibu kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI.

Sasa tunaendelea na Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Mheshimiwa Paschal Inyasi Chinyele, Mbunge wa Dodoma Mjini, aulize swali lake.

Na. 245

**Sheria ya Usimamizi wa Uwekezaji wa Umma Nchini**

**MHE. PASCHAL I. CHINYELE** aliuliza:-

Je, lini Serikali itakamilisha mchakato wa kuandaa Sheria ya Usimamizi wa Uwekezaji wa Umma nchini?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Paschal Inyasi Chinyele, Mbunge wa Jimbo la Dodoma Mjini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, itakumbukwa kuwa, Serikali iliwasilisha Bungeni Muswada wa Sheria ya Uwekezaji wa Umma wa Mwaka 2023 na Kusomwa kwa Mara ya Kwanza Tarehe 10 Novemba, 2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu Kusomwa kwa Mara ya Kwanza na kujadiliwa katika Vikao Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma ambayo ilichambua na kupokea maoni ya wadau, kumekuwa na marekebisho mbalimbali yaliyopendekezwa kufanyika katika Muswada huo. Kwa kuzingatia maoni yaliyotolewa, Serikali iliona kuna umuhimu wa kufanya tathmini ya kina ya usimamizi wa uwekezaji wa umma kwa kuwashirikisha wadau wote muhimu ili kubainisha upungufu uliopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa taratibu za ndani ya Serikali zinaendelea katika maboresho ya Muswada wa Sheria ya Uwekezaji wa Umma kulingana na tathmini iliyofanyika ikiwemo kupata idhini ya Mamlaka ya kufanya maboresho yanayopendekezwa ili Muswada urejeshwe tena Bungeni kwa ajili ya taratibu za Kibunge za kupitisha Muswada kuwa Sheria. Ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Paschal Chinyele.

**MHE. PASCHAL I. CHINYELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, ninaomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, Serikali ina mpango gani wa kuendeleza *corridor* ya kuanzia Bihawana –

Nondwa – Chifutuka, kupitia Sanza na Mapori ya Muhesi na Kizigo hadi Rungwa ili kukuza ajira kwa wakazi wa maeneo hayo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Serikali ina mpango gani wa kufungamanisha Reli ya *SGR* katika eneo la Zuzu hadi katika kongani ya viwanda eneo la Nala? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Paschal Inyasi Chinyele, Mbunge wa Jimbo la Dodoma Mjini kwa maswali yake mazuri na amekuwa akiuliza sana maswali hususan kwenye upande wa uwekezaji kwa ajili ya kuwatetea watu wa Jimbo la Dodoma Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo haya, ninaomba nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ninatambua kwamba kuna umuhimu wa kufungua Mkoa wa Dodoma, lakini na Mkoa wa Mbeya hususan kwa *corridor* ambayo ameitaja ambayo inaanzia Bihawana, Kizigo kule kwangu Manyoni, mpaka Rungwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Chinyele amekuwa akiuliza sana kuhusu hii barabara ambayo kimsingi ni ya muhimu kwa ajili ya kuchochea uchumi na uwekezaji. Ninaomba nimhakikishie Mbunge kwamba tayari tulishawasiliana na wenzetu wa ujenzi kuifanyia tathmini hii barabara ambayo ni muhimu sana kwa ajili ya uwekezaji, na baada ya tathmini kufanyika, tutaiingiza kwenye mipango ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, Mheshimiwa Mbunge anaelezea kuhusu Reli ya *SGR*. Hapa Dodoma tuna mpango wa kuanzisha *industrial park* inaitwa *Nala Industrial Park* kwa ajili ya ku-*process critical minerals* ambayo kwenye mpango wa mwaka mmoja huu ipo, na pia kwenye mpango wa miaka mitano, ipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulishawasiliana na wenzetu wa uchukuzi juu ya namna gani tuta-*connect* ile Nala *Industrial Park* na kituo chetu cha Kigwe ili wale watu wanaoleta madini pale kwenye *Nala Industrial Park* wapate urahisi zaidi wa kufikisha madini yao. Ile *Nala Industrial Park* ina malengo mawili. Kwanza, kwa ajili ya ku-*process* yale madini adimu ikiwepo *nickel, silicon, lithium* na kadhalika; pili, tunavutia viwanda kwa ajili ya kutengeneza bidhaa mbalimbali kwa mfano, betri za magari, betri za simu na nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, sisi Serikali tupo *on top on that,* na hili swali lake la pili lipo ndani ya mipango ya Serikali.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shadya Omar.

**MHE. SHADYA HAJI OMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kuipongeza Wizara hii kwa kuendana na kasi ambayo moja kwa moja inamgusa Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Kwa kuwa tumeona kuna vizingiti vingi vya wawekezaji wa ndani ya nchi hii, je, Serikali ina mpango gani wa kuwarahisishia na kuwawezesha wawekezaji wa ndani ya nchi hii katika jitihada ya kuendeleza kipato kwa maslahi ya Taifa?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba bado tuna mwamko mdogo hususan kwa wawekezaji wa ndani ili waweze kushindana na wawekezaji wa nje. Sisi kama Serikali, tumeweka mipango mbalimbali. Mojawapo ya mipango ambayo tunayo na tumeianza mwaka huu, tuna kampeni ya Kitaifa ya kuwahamasisha wawekezaji wazawa ili waweze kuwekeza, hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, mwaka huu tunakuja na *guideline,* mwongozo ambao kimsingi utaenda kutoa mwelekeo, ni jinsi gani tunaweza kuwasaidia wawekezaji wazawa waweze

kupata mikopo na vilevile wawe na fursa sahihi ya kuweza kushindana na wenzetu wageni ambao wanakuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba suala lake ni la muhimu sana, na sisi kama Serikali tutaliwekea mkazo. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Josephine Kapoma.

**MHE. JOSEPHINE J. KAPOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Serikali imeshafanya tathmini ya mashirika ya umma, mengine kuyafuta na mengine kuyaunganisha. Je, ni lini sasa Serikali itatekeleza suala hili?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kwanza kumshukuru Mheshimiwa Josephine, kutoka Mkoa wa Morogoro kwa swali lake zuri. Ni kweli, kwamba Serikali ilifanya tathmini ya zaidi ya mashirika 20 na tayari tulishayatoa kwenye Gazeti la Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mamlaka ilisharidhia kwa ajili ya kuyafuta baadhi ya mashirika, baadhi kuyaunganisha, baadhi ya kuhamisha usimamizi wake, na baadhi ya majukumu yake kuhamishiwa kwenye mashirika mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari kuna baadhi ya Wizara walishaanza hiyo kazi, zikiwepo Wizara ya Kilimo, Wizara ya Mifugo, vilevile *TAMISEMI*. Tunategemea Bunge lijalo kuanzia Septemba, Wizara nyingi zitaleta hapa Bungeni sheria zao kwa ajili ya kufanya marekebisho ya hiyo sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, sisi kama Serikali tunalifuatilia na tutahakikisha azma ya Serikali na azma ya wananchi inatimia. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa majibu hayo kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge kutoka Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji.

Tunaendelea na Wizara ya Uchukuzi, Mheshimiwa Kijakazi Yunus Mohamed, Mbunge wa Viti Maalum aulize swali lake.

Na. 246

**Upanuzi wa Uwanja wa Ndege Kilwa Masoko**

**MHE. KIJAKAZI Y. MOHAMED** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaanza upanuzi wa Uwanja wa Ndege wa Kilwa Masoko sambamba na kuwalipa fidia wananchi?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Kijakazi Yunus Mohamed, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekamilisha zoezi la uthamini wa mali za wananchi wanaopaswa kupisha utekelezaji wa mradi wa ukarabati na upanuzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kilwa Masoko. Kwa sasa Serikali inaendelea na taratibu za upatikanaji wa rasilimali fedha kwa ajili ya kulipa fidia kwa wananchi husika kwa kuzingatia miongozo na taratibu za kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inapenda kusisitiza kuwa ulipaji wa fidia ni hatua ya msingi kabla ya kuanza utekelezaji wa miradi hiyo. Hivyo, baada ya kukamilika kwa zoezi hilo, Serikali itaanza taratibu za maandalizi ya utekelezaji wa mradi, ikiwemo upatikanaji wa fedha za ujenzi kwa lengo la kuhakikisha kuwa upanuzi wa kiwanja unatekelezwa kwa ufanisi na kwa kuzingatia vipaumbele vya maendeleo ya sekta ya usafiri wa anga.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kijakazi Yunus Mohamed.

**MHE. KIJAKAZI Y. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ninayo maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa Bandari ya kimkakati ya Uvuvi ya Kilwa Masoko ipo katika hatua za mwisho kuweza kukamilika, je, Serikali haioni umuhimu wa kutafuta fedha kwa dharura ili kuwalipa fidia wananchi, na vilevile kuweza kujenga uwanja huo ambao utaongeza ufanisi kibiashara katika bandari ya Uvuvi ya Kilwa Masoko?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Wananchi wa Mkoa wa Lindi kwa muda mrefu wamekuwa hawana kiwanja cha ndege, hali ambayo inasababisha kupata huduma hiyo katika mikoa jirani kama vile Mkoa wa Mtwara. Je, ni lini wananchi wa Mkoa wa Lindi watapata uwanja wa ndege, ukizingatia ni sera ya Serikali kila mkoa kuwa na uwanja wa ndege?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi, ninapenda kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Mbunge, Mheshimiwa Kijakazi Yunus Mohamed kwa jinsi ambavyo anapigania maendeleo ya Wanalindi, wakiwemo wanawake, vijana na makundi mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ninakubaliana na Mheshimiwa Mbunge, na Serikali hii ya awamu ya sita chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan inatambua umuhimu wa miradi iliyopo pale Kilwa. Ndiyo maana pamoja na mambo mengi waliyokuwa wameyaomba, imeanza kujenga bandari kubwa ya uvuvi yenye thamani ya zaidi ya shilingi bilioni 280 ambayo utekelezaji wake upo kwa zaidi ya 97%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hatua ya pili, ili kuona umuhimu wa Kiwanja cha Kilwa Masoko, tayari uthamini wa wale wananchi umeshakamilika, ambapo takribani shilingi bilioni sita zinahitajika kwa ajili ya kuwalipa wananchi zaidi ya 400 ambao

wanahitaji kulipwa fidia. Mara baada ya kumaliza hatua hiyo, ninamwomba Mheshimiwa Mbunge atuvumilie. Kama Serikali hii imeweza kutoa shilingi bilioni 280, kwanini awe na mashaka kuhusu kulipwa fedha shilingi bilioni sita zilizobakia? Watakwenda kulipwa, wawe na subira na wakishalipwa Serikali itajenga uwanja huo wa Kilwa Masoko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ni kweli kabisa kuwa uwanja wa Lindi ni muhimu, siyo tu kimkakati, lakini pia tunafahamu tuna miradi mikubwa kama *LNG* katika Mkoa wa Lindi. Serikali kwa kutambua jambo hilo, tayari ilishafanya hatua ya kwanza ya usanifu, ikabaini gharama na imeshampata mkandarasi kwa shilingi bilioni 124. Kwa sasa, Serikali inatafuta fedha ili iweze kujenga uwanja huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Kijakazi Yunus Mohamed atuvumilie, Serikali itajenga Uwanja wa Lindi kama ambavyo viwanja vingine vimejengwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Festo Sanga.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Naibu Waziri atakubaliana na mimi, kwa nyakati tofauti uwanja wa Njombe umeingia kwenye ilani; kwa nyakati tofauti viongozi wamekuwa wakitupatia majibu tofauti wananchi wa Njombe kwamba watajenga uwanja wa ndege?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukifikiria kwamba tuna Liganga na Mchuchuma, na pia kuna mazao ya mbogamboga ambayo yanaenda kuzalishwa Njombe, atupatie lugha ya matumaini wananchi wa MKoa wa Njombe, ni lini Serikali itajenga uwanja kwa Mkoa wa Njombe? Sisi kama Wabunge tumetumia nafasi yetu kwa kuliomba sana hili na bado halijafanyiwa kazi?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakubaliana na ninampongeza Mheshimiwa Sanga kwa jinsi anavyofuatilia Uwanja wa Ndege wa Njombe. Siyo yeye tu,

takribani Wabunge wote wa mkoa wa Njombe, sambamba na mikoa ya Nyanda za Juu Kusini, mara kadhaa wamekuja kwa Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi wakidai na wakihitaji uwanja wa Njombe ujengwe. Siyo tu kama uwanja mojawapo wa kimkoa, ni uwanja muhimu kwa sababu ya kuweza kusafirisha mazao ya mbogamboga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeuingiza kwenye mpango uwanja huu katika viwanja vitatu vya Kitaifa. Uwanja wa Njombe kwa sababu ni muhimu kwa ajili ya mazao ya mbogamboga, Uwanja wa Kiabajwa ambao upo kimakakati mpakani, na Uwanja wa Serengeti kwa ajili ya utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwanja huu wa Njombe siyo tu kwenye kusafirisha mazao ya mbogamboga, lakini pia ndio tunaoutegemea uunganishe na mradi mkubwa sana wa Liganga na Mchuchuma ambao tunategemea kuwa ni mradi ambao unakwenda kubadilisha nchi yetu katika utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwomba Mheshimiwa Sanga atuvumilie, kwa sasa Serikali ipo kwenye hatua za utwaaji ardhi. Mara baada ya kumaliza hatua hiyo tutakwenda kufanya usanifu na kisha tutajenga Uwanja wa Ndege wa Mkoa wa Njombe.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *Engineer* Fadhili.

**MHE. ENG. FADHILI S. CHILOMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona. Uwanja wa Ndege wa Wilaya ya Tunduru, uko *grounded* kwa sababu ya kiusalama, na tayari hivi tunavyozungumza, halmashauri wameshatenga eneo kwa ajili ya kujenga uwanja mwingine mpya. Je, ni lini Serikali itaanza kazi ya kujenga uwanja huo?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa Uwanja wa Ndege wa Tunduru, na changamoto iliyokuwepo pale ilikuwa ni suala la eneo kuwa dogo. Tulikuwa kwenye mazungumzo na halmashauri ili

kubadilishana maeneo. Kwa hiyo, tulikubaliana tutakapokuwa tumekamilisha kupata eneo kubwa na zuri, tutaweza kuendelea na hatua inayofuatia ambayo ni ujenzi wa uwanja huu wa Tunduru.

**MWENYEKITI:** Tunakushukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu hayo ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Sara Msafiri Ally, Mbunge wa Mvomero aulize swali lake.

Na. 247

**Ujenzi wa Chuo cha VETA – Mvomero**

**MHE. SARA M. ALLY** aliuliza: -

Je, lini Serikali itajenga Chuo cha *VETA* Wilaya ya Mvomero?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, ninaomba kujibu swali Na. 247 la Mheshimiwa Sara Msafiri Ally, Mbunge wa Mvomero kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni azma ya Serikali kuhakikisha kuwa kila Wilaya inakua na Chuo cha *VETA* kwa lengo la kuongeza fursa za mafunzo na kusogeza huduma karibu na wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Mvomero ni miongoni mwa wilaya ambazo zipo kwenye mpango wa Serikali wa kujengewa Chuo cha *VETA*. Tayari Wizara imeomba kupatiwa eneo katika Wilaya hiyo, na mara litakapopatikana ujenzi utaanza mara moja. Ninampongeza sana Mheshimiwa Sara Msafiri Ally,

Mbunge wa Jimbo la Mvomero kwa kufuatilia kwa karibu ujenzi wa chuo hiki.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sara Msafiri.

**MHE. SARA M. ALLY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nichukue nafasi hii nimpongeze sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kufanya ziara kwenye Chuo cha *VETA* cha Kihonda, Morogoro na kwa kuzindua mradi wa mafunzo kwa vijana na kugawa zana za kufundishia, ambazo ni zana za kilimo na dhana za teknolojia ya umwagiliaji ambayo ni ahadi ya Mheshimiwa Rais kwa vijana 5,000 kipindi cha uchaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa Serikali ipo tayari kujenga Chuo cha *VETA* ndani ya Jimbo la Mvomero, na tayari eneo lipo, je, Serikali ipo tayari kuanza ujenzi huo haraka kwa kutumia fedha za ndani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali ipo tayari kuanzisha mafunzo ya nje *(outreach training)* kwa vijana wa Jimbo la Mvomero ili waweze kunufaika na fursa hii ya kujiongezea ujuzi, huku tukisubiri ahadi ya ujenzi wa Chuo cha *VETA*?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyojibu kwenye jibu langu la msingi, kwamba Serikali ipo tayari kuanza ujenzi wa chuo hicho mara baada ya kukabidhiwa eneo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa swali lake la pili, ni kwamba *VETA* kwa kushirikiana na Benki ya *NBC* imejipanga kutekeleza mradi wa *NBC* Wajibika *Scholarship,* ambapo vijana 588 wanaenda kunufaika na mradi huu. Nichukue fursa hii kumwomba Mheshimiwa Sara Msafiri Ally kushajihisha ama kuwezesha vijana wake kuomba kufanya programu hii ili waweze kupata elimu ya ujuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, *VETA* kupitia Dakawa na Kihonda itaendelea kutoa huduma za mafunzo ya *outreach progaram*. Hivyo, niombe vijana wa Jimbo la Mvomero waendelee kupata huduma hii kupitia vyuo hivyo ambavyo nimevitaja.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Edifonsi Kanoni.

**MHE. EDIFONSI J. KANONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Kwanza niipongeze Serikali kwa kupokea mradi wa ujenzi wa Chuo cha *VETA* katika Wilaya yetu ya Kalambo ambapo vijana wameendelea kusubiri ili waweze kwenda kupata ujuzi katika chuo hicho Wilaya ya Kalambo. Je, ni lini Serikai itakamilisha ujenzi wa chuo hicho ili vijana wetu waingie pale kwenda kupata ujuzi?

**MWENYEKITI:** Umemwelewa Mheshimiwa, naona kaongea haraka. Majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ninavyojibu kwenye vyuo vingine vya wilaya, ni kwamba vyuo hivi ambavyo vinaendelea na ujenzi vitamalizika mwezi wa Septemba, 2026. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge asiwe na wasiwasi *as long as* chuo chake kimo kwenye orodha ya vyuo vya wilaya, basi chuo hiki kitaenda kukamilika mwezi Septemba, 2026. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Tunaipongeza Serikali kwa ujenzi wa Chuo cha *VETA* Kilolo. Hata hivyo, bado fedha ya umaliziaji tu, kwa sababu wananchi wa Kilolo wamesubiri kwa muda mrefu, je, ni lini sasa tutapatiwa ili tumalizie kile Chuo cha Kilolo?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimwambie tu Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati kwamba tukutane Septemba, 2026.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mecktridis Mdaku.

**MHE. MECKTRIDIS F. MDAKU:** Mheshiimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa Chuo cha *VETA* katika Wilaya ya Malinyi ulianza miaka mitatu iliyopita. Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi huo ili chuo hicho kianze kutoa huduma za mafunzo?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri. Ninaona nchi nzima *VETA* inatakiwa sasa.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema awali na siku zote ninavyosema, ni kwamba ujenzi wa vyuo vya wilaya tunaenda kukamilisha mwaka huu Septemba.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Adonis Bitegeko.

**MHE. ADONIS A. BITEGEKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipa nafasi. Tunaishukuru Serikali kwa ujenzi wa Chuo cha *VETA* katika Wilaya ya Muleba, Jimbo la Muleba Kaskazini katika Kata ya Kamachumu, lakini bado miundombinu ya chuo hiki haijakamilika, kama karakana za umeme, ushonaji na mabweni. Je, ni lini Serikali itatoa fedha za kukamilisha ujenzi wa chuo hiki?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kuwapa imani Waheshimiwa Wabunge kwamba, vyuo hivi vya *VETA* kama tulivyoahidi vinaenda kukamilika mwaka huu Septemba, 2026. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu hayo ya Waheshimiwa Wabunge. Ahsanteni sana, Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, muda wetu wa maswali kwa leo umeishia hapo. Kwa hiyo, sasa nina matangazo hapa ya wageni ambao wapo Bungeni asubuhi hii.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tusikilizane.

Waheshimiwa Wabunge, tuna matangazo ya wageni ambao wapo Bungeni asubuhi hii. Tuna Wageni 18 wa Mheshimiwa Spika ambao ni Madiwani kutoka Bunda, Mkoani Mara. Hawa ni Ndugu Masalo Minza, Mheshimiwa Diwani na Mwenyekiti wa Mji; Ndugu Lucas Daniel, Mheshimiwa Diwani; Ndugu Falvian Chacha, Mheshimiwa Diwani; Ndugu Sea Nyamgaluri, Mheshimiwa Diwani; Ndugu Thomas Tamka, Mheshimiwa Diwani; Ndugu Beatrice Daud, Mheshimiwa Diwani; Ndugu Kigho Nyakimori, Mheshimiwa Diwani; Ndugu Kulwa Ngata, Mheshimiwa Diwani; na Ndugu Daniel Yona, Mheshimiwa Diwani.

Wengine ni Ndugu Magigi Kiboko, Mheshimiwa Diwani; Ndugu Mathayo Juma, Mheshimiwa Diwani; Ndugu Elias Mwita, Mheshimiwa Diwani; Ndugu Michael Kweka, Mheshimiwa Diwani; Ndugu Kalulu Foda, Mheshimiwa Diwani; Ndugu Pasaka Samson, Mheshimiwa Diwani; Ndugu Happiness Nzagi, Mheshimiwa Diwani; Ndugu Theopister Machupa, Mheshimiwa Diwani; na Ndugu Magori Panda, Mheshimiwa Diwani. Waheshimiwa Madiwani wetu kutoka Mkoa wa Mara, karibuni sana katika Bunge letu. *(Makofi)*

Wageni wengine ambao wamekaa kwenye jukwaa la Mheshimiwa Spika ni wageni wa Mheshimiwa Paul Christian Makonda ambaye ni Waziri wetu wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo. Wageni hao ni Ndugu Gerson Msigwa, Katibu Mkuu; Ndugu Methusela Ntonda, Naibu Katibu Mkuu; Mheshimiwa Maximilian Iranghe, Mstahiki Meya, Halmashauri ya Jiji la Arusha;

Dkt. Winfred Ole Soilel, Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi, Wilaya ya Arusha; na Ndugu Jokate Mwegelo, Katibu Mkuu UVCCM Mstaafu. *(Makofi)*

Wapo pia, Dkt. Toba Nguvila, Katibu Tawala wa Mkoa wa Arusha; Ndugu Missaile Musa, Katibu Tawala Mstaafu Mkoa wa Arusha; *IGP* Mstaafu Said Mwema, Mwenyekiti wa Bodi ya Kampuni ya Magazeti ya Serikali; Dkt. Mona Mwakalinga, Mwenyekiti wa Bodi ya Filamu Tanzania; Dkt. Richard Masika, Mwenyekiti wa Bodi ya Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya; na Mhandisi Peter Mwasalyanda, Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania. *(Makofi)*

Yupo pia Ndugu Athumani Nyamlani, Makamu wa Pili wa Rais wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania; Ndugu Miguel Gamondi, Kocha wa Timu ya Taifa; Jackline Mwakyambiki, Katibu wa Umoja wa Wamiliki wa Vyombo vya Habari Tanzania; Ndugu Felix Simbu, Mwanariadha Mshindi wa Medali ya Dhahabu; na Ndugu Ally Kiba, Msanii wa *Bongo Flavor*. Karibuni sana wageni wetu wote mlioko katika jukwaa la Mheshimiwa Spika. *(Makofi)*

Wengine ni wageni wa Waheshimiwa Wabunge. Kuna wageni tisa wa Mheshimiwa Dkt. Florence George Samizi, Naibu Waziri wa Afya. Hawa ni Timu ya Uhamasishaji wa Timu ya Taifa kutoka Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni watatu wa Mheshimiwa Thomas Mgonto Kitima, ambao ni Wajasiriamali kutoka Manyoni Mkoani Singida. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko, ni familia yake kutoka Mkoani Tanga. Karibuni sana. (*Makofi)*

Wapo wageni 39 wa Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, Wainjilisti kutoka Jijini Dodoma. Karibuni sana. *(Makofi)*

Yupo mgeni wa Mheshimiwa Festo Richard Sanga; huyu ni Ndugu Susan Kisinini, mfanyabiashara kutoka Jijini Dar es Salaam. Karibu sana. *(Makofi)*

Wengine ni wageni ambao wametembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo. Tunao Wanafunzi 55 na Walimu wanne wa Shule ya *St. Peter Claver* kutoka Jijini Dodoma. Hawa wameambatana na Walimu wawili na Wanafunzi wanne kutoka Shule ya *Mt. Benno Gymnasium* kutoka Ujerumani. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wengine ni wanafunzi 68 na Mkufunzi mmoja wa Habari na Uhusiano wa Umma kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma *(UDOM)*. Karibuni sana.

Wanafunzi 140 na walimu tisa kutoka Shule ya Sekondari Umonga Jijini Dodoma. Karibuni sana wanafunzi wetu na wageni wote ambao mmekuja leo hapa pamoja na ambao wamekuja kwa ajili ya mafunzo, tunawakaribisha sana katika Bunge letu.

Katibu.

**NDG. JOSHUA CHAMWELA, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

**UCHAGUZI WA WABUNGE WA BUNGE LA AFRIKA MASHARIKI *(EALA)***

*Hapa Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alikalia Kiti*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Maelezo ya Spika kuhusu utaratibu wa kupiga kura katika uchaguzi wa Wajumbe watatu wa Bunge la Afrika Mashariki.

Waheshimiwa Wabunge, tarehe 22 Septemba, 2022 Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lilifanya uchaguzi wa Wajumbe tisa wa Bunge la Afrika Mashariki: Mheshimiwa James Kinyasi Millya; Mheshimiwa Dkt. Ngwaru Jumanne Maghembe; na Mheshimiwa Angela Charles Kizigha ni miongoni mwa Wajumbe waliochaguliwa. Wagombea hao walidhaminiwa na Chama cha Mapinduzi (CCM).

Waheshimiwa Wabunge, tarehe 29 Oktoba, 2025 ulifanyika Uchaguzi Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mheshimiwa James Kinyasi Millya, na Mheshimiwa Dkt. Ngwaru Jumanne Maghembe, waligombea nafasi za Ubunge kupitia

majimbo yao na kuibuka washindi. Vilevile, tarehe 2 Aprili, 2026 Mheshimiwa Angela Charles Kizigha aliteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Mbunge.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya viongozi hawa kuapishwa kuwa Wabunge, ujumbe wao katika Bunge la Afrika Mashariki ulikoma kwa mujibu wa mkataba wa Jumuiya na Sheria ya Uchaguzi ya Bunge la Afrika Mashariki. Kwa hali hiyo, uchaguzi mdogo unapaswa kufanyika ili kujaza nafasi walizoziacha wazi kutokana na nafasi zao kudhaminiwa na CCM, chama hicho ndicho chenye haki ya kuteua wagombea.

Waheshimiwa Wabunge, uchaguzi wa Wajumbe wa Bunge la Afrika Mashariki unasimamiwa na Katibu wa Bunge kwa kuzingatia Mkataba, Sheria za Uchaguzi wa Jumuiya, Katiba ya Tanzania, Sheria za Uchaguzi na Kanuni za Kudumu za Bunge 2025.

Waheshimiwa Wabunge, uchaguzi huu utaanza kwa hatua ya wagombea kujinadi na kuomba kura, Wabunge kupiga kura, kura kuhesabiwa na mwisho msimamizi kutangaza matokeo ya uchaguzi.

Waheshimiwa Wabunge, ninapenda kutoa angalizo kwamba japokuwa haki na utashi wa kumpigia mgombea kura unabaki kwa Mbunge mpiga kura inategemea kwamba Bunge litazingatia yafuatayo: Maslahi ya Taifa katika uwakilishi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Bunge la Afrika Mashariki yatapewa kipaumbele cha kwanza na sifa na uwezo wa mgombea kwa kusimamia na kutetea maslahi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Bunge la Afrika Mashariki. Vilevile, wenye nia ya kuendeleza malengo na madhumuni ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Waheshimiwa Wabunge, katika hatua hii, nimpe nafasi Msimamizi wa Uchaguzi awasilishe maelezo na utaratibu mzima wa Uchaguzi.

Kabla Katibu hajatoa maelezo, ninamkaribisha Mheshimiwa Waziri atoe hoja ya kutengua Kanuni.

## HOJA YA KUTENGUA KANUNI

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, URATIBU NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa hoja ya kutengua Kanuni za Bunge chini ya Kanuni ya 177(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2025.

Kwa kuwa, moja ya shughuli iliyopangwa kufanyika leo tarehe 4 Mei, 2026 ni Uchaguzi wa Wajumbe watatu wa Bunge la Afrika Mashariki.

Na kwa kuwa, kwa mujibu wa Kanuni ya 163(*f*) na Kanuni ya 164(1) wageni hawaruhusiwi kuingia ndani ya ukumbi wa Bunge bali hutengewa sehemu maalumu za kukaa.

Na kwa kuwa, Kanuni ya 11(2) ya Nyongeza ya Tatu za Kanuni za Bunge inaeleza kuwa mgombea ataruhusiwa kuingia ndani ya ukumbi wa Bunge ili kujitambulisha, kujieleza, kuulizwa na kujibu maswali pamoja na kuomba kura.

Kwa hiyo basi, kwa madhumuni ya utekelezaji bora wa shughuli za Bunge na kuwezesha Uchaguzi wa Wajumbe wa Bunge la Afrika Mashariki kufanyika kwa ufanisi, ninaliomba Bunge lako liazimie kwamba, Kanuni ya 163(f) na Kanuni ya 164(1) ambazo kwa ujumla wake zinaelekeza kwamba wageni wanaoruhusiwa kuingia Bungeni wataketi maeneo maalumu yaliyotengwa kwa ajili yao, zitenguliwe na badala yake Wagombea wa Uchaguzi huu waruhusiwe kuingia ndani ya Ukumbi wa Bunge ili waweze kujitambulisha, kujieleza, kuulizwa na kujibu maswali pamoja na kuomba kura.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Hoja imeungwa mkono. Waheshimiwa Wabunge, sasa nitawahoji, Hoja ya kutengua Kanuni.

*(Hoja Ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Kanuni imetenguliwa. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:** Waheshimiwa Wabunge, kama ilivyoelezwa na Mheshimiwa Spika, leo tunafanya Uchaguzi Mdogo wa Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki ambao unafanyika kwa kuzingatia Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wa Mwaka 1999, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, Sheria ya Uchaguzi wa Bunge la Afrika Mashariki ya Mwaka 2011, na Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2025.

Waheshimiwa Wabunge, Uchaguzi huu unalenga kujaza nafasi za Tanzania zilizoachwa wazi na Mheshimiwa Angela Charles Kizigha, Mheshimiwa James Kinyasi Millya, na Mheshimiwa Dkt. Ngwaru Jumanne Maghembe katika Bunge la Afrika Mashariki.

Waheshimiwa tajwa walikoma kuwa Wajumbe wa Bunge hilo baada ya kuchaguliwa kuwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na hii ni kwa mujibu wa Ibara ya 51(3) ya Mkataba wa Kanuni za Jumuiya ya Afrika Mashariki wa Mwaka 1999; na Kifungu cha 7(3) cha Sheria ya Uchaguzi wa Bunge la Afrika Mashariki ya Mwaka 2011.

Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kifungu cha 8(2) cha Sheria ya Uchaguzi wa Bunge la Afrika Mashariki, endapo Kiti cha Ubunge wa Bunge hilo kitakuwa wazi, Bunge la nchi husika linatakiwa kujaza nafasi hiyo ndani ya siku 90 tangu kupokea Taarifa ya Spika wa Bunge la Afrika Mashariki kuhusu Kiti hicho kuwa wazi.

Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni ya 18 ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2025, tumetoa taarifa kwa Spika wa Bunge la Afrika Mashariki kuhusu kuapishwa kwa viongozi hao kuwa Wabunge wa Bunge la Tanzania. Spika huyo alijibu kwa kutoa taarifa iliyoeleza kwamba, kutokana na Wabunge hao kuapishwa katika Bunge la Tanzania, nafasi zao katika Bunge la Afrika Mashariki ziko wazi na kwamba zinatakiwa kujazwa ndani ya siku 90.

Waheshimiwa Wabunge, siku 90 zilizotajwa na Spika wa Bunge la Afrika Mashariki zinahesabiwa kuanzia tarehe tuliyopokea taarifa yake, ambapo taarifa kuhusu Mheshimiwa Kizigha iliandikwa na kupokelewa siku ya tarehe 15 Aprili, 2026. Kadhalika, taarifa kuhusu Mheshimiwa Millya na Mheshimiwa Maghembe iliandikwa na ilipokewa siku ya tarehe 5 Februari, 2026. Hivyo, siku 90 kwa upande wa Mheshimiwa Kizigha zitafika ukomo tarehe 12 Julai, 2026 na kwa upande wa Mheshimiwa Millya na Mheshimiwa Maghembe siku 90 zitafika ukomo wake tarehe 6 Mei, 2026.

Waheshimiwa Wabunge, kwa mantiki hiyo, ninaomba kulithibitishia Bunge hili kuwa Uchaguzi huu Mdogo unafanyika ndani ya muda uliowekwa kwa mujibu wa Sheria ya Uchaguzi wa Bunge la Afrika Mashariki ya Mwaka 2011.

Waheshimiwa Wabunge, Ibara ya 50(1) ya Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki imeweka sharti la Uchaguzi wa Wajumbe wa Bunge la Afrika Mashariki kufanyika kwa kuzingatia na kwa kadiri itakavyowezekana uwakilishi wa makundi yaliyotajwa katika ibara hiyo.

Aidha, Nyongeza ya Tatu ya Kanuni za Kudumu za Bunge katika fasili ya 6(5) na 12(3) imeainisha makundi ya uwakilishi kuendana na Ibara ya 50 ya mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kama ifuatavyo: Kundi *A*, wanawake; Kundi *B*, Zanzibar; Kundi *C*, Walio Wachache Bungeni; na Kundi *D*, Tanzania Bara.

Waheshimiwa Wabunge, Kanuni ya 20 ya Kanuni za Kudumu za Bunge inaeleza kwamba mara baada ya nafasi ya Mjumbe kuwa wazi, Bunge litafanya Uchaguzi kujaza nafasi hiyo.

Waheshimiwa Wabunge, Uchaguzi huu ni wa kujaza nafasi tatu zilizoachwa wazi katika Bunge la Afrika Mashariki. Nafasi moja Kundi *A*, wagombea wanawake iliyoachwa wazi na Mheshimiwa Angela Kizigha; nafasi mbili ni za Kundi *D*, wagombea Tanzania Bara zilizoachwa wazi na Mheshimiwa James Kinyasi Millya na Mheshimiwa Dkt. Ngwaru Jumanne Maghembe. Wajumbe hawa watatu wanadhaminiwa na Chama cha Mapinduzi.

Waheshimiwa Wabunge, Ibara ya 50(2) ya Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki inataja sifa za mtu anayestahili kuchaguliwa kuwa Mbunge katika Bunge la Afrika Mashariki kama ifuatavyo: -

(a) Awe Raia wa nchi husika;

(b) Awe na sifa za kuchaguliwa kuwa Mbunge katika nchi husika;

(c) Asiwe Waziri katika nchi husika;

(d) Asiwe mtumishi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki; na

(e) Awe ni mtu aliyedhihirisha uzoefu wake au kuhusika katika kusimamia na kuendeleza madhumuni na malengo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Waheshimiwa Wabunge, Ibara ya 50(2)(*b*) inaeleza kwamba, mgombea anapaswa kuwa na sifa zilizoainishwa kwenye Ibara ya 67 (1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977. Ibara hiyo inaeleza ifuatavyo: -

Bila kuathiri masharti yaliyopo katika Ibara hii, mtu yeyote atakuwa na sifa za kustahili kuchaguliwa au kuteuliwa kuwa Mbunge, endapo: -

(a) Ni raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyetimiza umri wa miaka 21 na ambaye anajua kusoma na kuandika katika Kiswahili au Kiingereza;

(b) Ni mwanachama na ni mgombea aliyependekezwa na chama cha siasa; na

(c) Katika kipindi cha miaka mitano kabla ya tarehe ya uchaguzi hakuwahi kutiwa hatiani katika Mahakama yoyote kwa kosa lolote la kukwepa au kutolipa kodi yoyote ya Serikali.

Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa fasili ya 5(9) Nyongeza ya Tatu ya Kanuni za Kudumu za Bunge, tarehe 14 Aprili, 2026 ilitoa tangazo katika Gazeti la Serikali. Vilevile, ilitoa taarifa kupitia vyombo vya habari kueleza umma kwamba Wajumbe hawa wamekoma kuwa Wajumbe wa Bunge la Afrika Mashariki baada ya kuwa Wabunge wa Bunge la Tanzania.
Vilevile, ilieleza kwamba nafasi tatu za Tanzania katika Bunge hilo ziko wazi, na zinatakiwa kujazwa. Pia, taarifa hiyo ilieleza zaidi kuwa siku ambayo uteuzi wa wagombea utafanyika pamoja na kutaja siku ya uchaguzi.

Waheshimiwa Wabunge, uteuzi wa wagombea wa nafasi za uwakilishi katika Bunge la Afrika Mashariki ulifanyika tarehe 30 Aprili, 2026. Siku hiyo nilipokea fomu za wagombea zenye picha, taarifa na wasifu wa wagombea pamoja na zinazothibitisha uteuzi uliofanywa na chama chao. Pamoja na fomu hiyo, kila mgombea aliwasilisha uthibitisho wa amana ya shilingi 50,000 itakayogharimia uchaguzi. Uwasilishaji huo ni kwa mujibu wa fasili 6(1), 6(3) na (7) katika Nyongeza ya Tatu ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2025.

Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa fasili ya 6(4) ya Nyongeza ya Tatu ya Kanuni, mwisho wa kurudisha fomu ilikuwa tarehe 30 Aprili, 2026, saa 10.00 jioni. Baada ya muda huo, zoezi la uteuzi wa wagombea lilianza. Fomu zilizopokelewa siku hiyo ni za wagombea wafuatao: -

(i) Ndugu Fatuma Abdallah Kange;

(ii) Ndugu Cosato David Chumi; na

(iii) Ndugu Kambarage Masato Wasira.

Waheshimiwa Wabunge, uchambuzi wa fomu za wagombea ulifanyika kwa kuzingatia sifa, wasifu na vigezo vya wagombea pamoja na vielelezo vilivyowasilishwa sambamba na fomu za uteuzi. Kwa kuzingatia fasili ya Nane ya Nyongeza ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2025, nilijiridhisha kwamba wagombea wote watatu waliowasilisha fomu za uteuzi wana sifa na wamekidhi vigezo vya kugombea nafasi tajwa.

Hivyo, wagombea katika nafasi tatu za Tanzania zilizoachwa wazi katika Bunge la Afrika Mashariki ni kama ifuatavyo: Kundi *A*, wagombea wanawake: mgombea ni Ndugu Fatuma Abdallah Kange; Kundi *D*, wagombea Tanzania Bara, wa kwanza ni Ndugu Cosato David Chumi na wa pili, Ndugu Kambarage Masato Wasira.

Waheshimiwa Wabunge, kabla ya kupiga kura wagombea wataruhusiwa kuingia ndani ya Ukumbi wa Bunge, watapewa fursa ya kujitambulisha na kuomba kura kwa lugha ya Kiingereza. Baada ya hapo, Wabunge wanaweza kuuliza maswali ya papo kwa papo kama yapo kwa idadi itakayoamuliwa na Spika. Utaratibu huu umeainishwa chini ya fasili ya 11 ya Nyongeza ya Tatu ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, ufuatao ni utaratibu utakaotumika wakati wa kupiga kura: -

(i) Kila mpiga kura atapewa karatasi ya kura ambayo itakuwa na majina ya wagombea.

(ii) Mpiga kura atatakiwa kupiga kura ya siri ili kuchagua wagombea kwa kuzingatia utaratibu ufuatao: Kundi *A*, wagombea wanawake mmoja, weka alama ya vema kwenye kisanduku cha ndiyo kumchagua mgombea au weka alama ya

vema kwenye kisanduku cha hapana kumkataa mgombea. Kundi *B*, wagombea wa Tanzania Bara, kuchagua wajumbe wawili katika kundi hili kwa kuweka alama ya vema kwenye kisanduku cha ndiyo ili kumchagua mgombea au kuweka alama ya vema kwenye kisanduku cha hapana ili kumkataa mgombea;

(iii) Mpiga kura atakayeharibu karatasi ya kura kabla ya zoezi la kupiga kura kumalizika, atarejesha karatasi hiyo kwa Msimamizi wa Uchaguzi na anaweza kupewa karatasi nyingine.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya zoezi la kupiga kura kukamilika, litafuata zoezo la kuhesabu kura. Zoezi hili litashuhudiwa na mawakala wawili watakaoteuliwa na Spika; mmoja kutoka upande wa Chama Tawala na mwingine kutoka upande wa Vyama vya Walio Wachache. Utaratibu huu ni kwa mujibu wa fasili ya 13 ya Nyongeza ya Tatu ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kuhesabu kura, Msimamizi wa Uchaguzi atalijulisha Bunge kuhusu kukamilika kwa zoezi hili na atatangaza idadi ya kura zilizopigwa kisha kutangaza washindi kama inayotakiwa fasili hii ya 14 ya Nyongeza ya Tatu za Kanuni za Kudumu za Bunge.

Mheshimiwa Spika, sasa ninaomba uridhie kuanza kwa zoezi la Uchaguzi. Wagombea waitwe mmoja baada ya mwingine ili waweze kujinadi na kuomba kura. Baada ya hapo Wabunge wapewe fursa ya kuuliza maswali kama yapo na kupata majibu kutoka kwa wagombea.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla sijaingia kwenye hatua ya kuita wagombea, kuna wageni wawili. Mgeni wa kwanza ni Kocha wa Timu ya Taifa, ndugu yetu Miguel Gamondi ambaye yupo kwenye Jukwaa la Spika. *Welcome Coach Gamondi, you have been doing a very good job in Tanzania and keep it up*. *(Makofi)*

Mgeni wetu wa pili, huyu ni mchezaji maarufu, na alitaka kusajiliwa na timu ambayo ilikuwa jana inaongoza goli mbili, kwa bahati mbaya mazungumzo hayakuweza kuendelea, au angeleta mabadiliko makubwa nchini Tanzania. Hata hivyo, niwashukuru Waziri wa Michezo, Naibu wake, Serikali kwa kumkaribisha na kumleta leo Didie Drogba. *(Makofi/Kicheko)*

*Mr. Drogba, this is how we honor legends of soccer in Africa.* Drogba amecheza *EPL,* alishakuja Tanzania na timu yake Taifa, mchezaji maarufu sana na tunajivunia Mheshimiwa Waziri, kwa namna unavyoleta *tourists* na *sports* nchini Tanzania. Tumekusikia juzi unasema unataka kuwaalika wale wawili wa masumbwi, sitaki kuwataja, ukifanikiwa italeta heshima kubwa sana Tanzania. *(Makofi/Kicheko)*

Sasa baada ya kuwatambulisha wageni wetu maarufu hawa, na baada ya Katibu kutoa maelezo ya usimamizi na namna ya uchaguzi utakavyokwenda, sasa nawaita wagombea.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, Kuhusu Utaratibu.

**SPIKA:** Kuhusu Utaratibu.

**KUHUSU UTARATIBU**

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, ninasimama kwa kanuni ya 78, kuhusiana na utaratibu. Wakati Katibu wa Bunge akitupatia maelekezo ya mwenendo mzima wa uchaguzi, alieleza moja ya sifa ni kujua kuandika na kusoma Kiswahili na Kiingereza, lakini wakati anaenda mbele kwenye kuhitimisha, aliwataka wagombea waje waongee kwa lugha ya Kiingereza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba tunaamini wagombea wetu wa Chama cha Mapinduzi wanajiweza kabisa kuongea Kiingereza fasaha kabisa, vilevile tunajua kabisa kwamba, Jumuiya ya Afrika Mashariki tuna-*advocate* kuongea Kiswahili zaidi, kwa sababu hata Mataifa mengine ambayo yako

ndani ya Jumuiya Afrika Mashariki wanaongea Kiswahili, sasa, ninaomba tu kupata utaratibu hapo, kwa nini kama ilivyokuwa aidha Kiswahili au Kiingereza, iwe ni *discretion* ya mgombea mwenyewe, akiamua kuongea Kiswahili, aongee Kiswahili; akiamua kuongea Kiingereza, aongee Kiingereza, ili huko nje wajue kabisa kwamba Afrika Mashariki tunataka tuongee lugha ya Kiswahili ili kwa baadaye iende mbele kwa… *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kanuni yetu ya 81, kwenye mwongozo, kwenye taarifa na kwenye utaratibu, maamuzi ya Kiti ni ya mwisho, na Kiti hakihojiwi kwa jambo lolote ndani ya Bunge, na huo ndiyo utaratibu kwa Kibunge, na wote tumepitisha.

Bunge la *EALA* linatumia lugha ya Kiingereza, kwa hiyo, wagombea watajieleza kwa lugha ya Kiingereza. Sasa namwita Ndugu Fatma Abdallah Kange. *(Makofi)*

*(Hapa Ndg. Fatuma Abdallah Kange, Mgombea Ubunge wa Bunge la Afrika Mashariki aliingia ukumbini)*

***SPEAKER:*** *Ndugu, Fatma Abdallah Kange, you have three minutes to solicit for your post for the position of the member of EALA, within the East African Community. You have three minutes, and Members of the House are entitled to ask you three questions if there are any questions.* Karibu.

***MS. FATMA A. KANGE:*** *Honorable Speaker, Honorable Prime Minister, Honorable Attorney General, Honorable Members of Parliament, allow me to greet you with honor, As-salam alaykum, Tumsifu Yesu Kristu, Bwana Yesu asifiwe, Kazi na Utu.*

**WABUNGE FULANI:** Kazi iendelee.

***MS. FATMA A. KANGE:*** *Honourable Speaker, my name is Fatma Abdallah Kange. I stand before you to show you my commitment, my determination to represent the Government of Tanzania in the East African Legislative Assembly. I just want to assure you, my dear leaders, that I hold all the qualifications necessary for this post.*

*Honourable Speaker, I am a holder of a Master's Degree in Marketing and International Business. I am also undergoing my PhD program at The Open University of Tanzania, but I have gone several courses, short courses, that give me a capacity, and I believe I fit well into the position that you are looking for a representative.*

*Honourable Speaker, above all, I have been employed both in Government institution; public and private sector institutions, of which I have gained experience to serve a different capacity, and then I believe the experience from the private sector in the Eastern Community fits very well, and I am ready to represent my country. (Applause)*

*Honourable Speaker, on top of that, the EAC Community has four thematic areas of which you are looking for somebody who understand issue when it comes to common market, legislative issues, political federation, and also marketing in general.*

*Honourable Speaker, may I take this opportunity to congratulate Honourable Madam President, Dr. Samia Suluhu Hassan, for the major project that is going on in our country, from infrastructure development, mining sector; there is a lot that is happening in our country. (Applause)*

*Honourable Speaker, we need a representative whom should be able to understand the policies that will fit well with the economy, especially we have come up with the Vision 2050. I have knowledge in strategic management, leadership skills, monitoring evaluation, budgeting and monitoring. My 15 years working with GS1 Tanzania have given me exposure in this country, at least I know every village… (Applause)*

***SPEAKER:*** Ndugu Fatma, *your three minutes are over, please solicit, request for your votes.*

***Ms. FATMA A. KANGE:*** *With that analysis, I humbly request you to vote for me. Thank you very much. (Applause)*

***SPEAKER:*** *Any questions! Any questions, for the third time! Any questions!*

***HONOURABLE MEMBERS:*** *No, no, no!*

***SPEAKER:*** *Thank you, Madam Fatma. You can go.* Ahsante.

Ndugu Cosato David Chumi. *(Makofi)*

*(Hapa Ndg. Cosato David Chumi, Mgombea wa Bunge la Afrika Mashariki, aliingia ukumbini kuomba kura)*

**SPEAKER:** Ahsanteni. *Ndugu Cosato Chumi you have three minutes to explain yourself and solicit for your votes within the House.*

***MR. COSATO D. CHUMI:*** *Thank you, Honourable Speaker, and Honourable Member of this House. It is my honor and privilege to stand here today as a candidate of the EALA.*

*Honourable Speaker, I will be very brief. My name is Cosato Chumi. I hold a Postgraduate in Management of Foreign Relations from Dr. Salim Ahmed Salim, Center for Foreign Relations and also Masters in Social Science from the University of Amsterdam, and a Bachelor of Arts in Political Science from the University of Dar es Salaam. (Applause)*

*Honourable Speaker and Honorable Members, I have experience of about 24 years in Public Service and in Political Leadership. I have served as a Public Servant in the Ministry of Foreign Affairs and also served in this House as Member of Parliament for the people of Mafinga. (Applause)*

*Honourable Speaker, the experience I have is not only because of the number I have served, but the depth of the experience. I have worked in areas of governance, diplomacy, and regional integration, which favors me to be a good representative for our Nation in the EAC. (Applause)*

*Honourable Speaker and Honourable Members, I can navigate because of that experience on the regional dynamics, contribute well in my country, represent well in different areas so that our country, our voice as a nation remains strong and respected in the EAC. (Applause)*

*Honourable Speaker, I am ready to serve, I have confidence, I am ready to deliver. I thank you for listening, I ask for your votes. Thank you very much. (Applause)*

***SPEAKER:*** *Any questions! Any questions! Any questions!*

***HONOURABLE MEMBERS:*** *No, no, no!*

***SPEAKER:*** *On top of his CV,* Ndugu Chumi *is a* Mnyama*. Thank you very much. Please, exit the House. (Applause/Laughter)*

Ndugu Kambarage Masato Wasira. *(Makofi)*

*(Hapa Ndg. Kambarage Masato Wasira, Mgombea wa Bunge la Afrika Mashariki, aliingia ukumbini kuomba kura)*

***SPEAKER:*** Ndugu Wasira, *you have three minutes to solicit for your votes and if there are any three questions within the House, you have to answer.* Karibu.

**MR. KAMBARAGE M. WASIRA:** *Honourable Speaker, thank you very much. Honourable Members of Parliament of the National Assembly, good morning. If you allow me to introduce myself, my name is Kambarage Masato Wasira, I am a business leader and I am an engineer by training. I hold a Bachelor of Science in Electrical Engineering and a Master's in Business Administration from Morgan State University in Baltimore, Maryland, United States. I first and foremost would like to thank God Almighty for giving us this blessing to be here this morning and the opportunity to address this August House. (Applause)*

*Honourable Speaker, secondly, I would like to thank my party, CCM, Chama Cha Mapinduzi, under the stewardship of Dr.*

*Samia Suluhu Hassan, who has given us the opportunity to serve this country. Myself, since a young age, I have always been patriotic and I had a love for country. Growing up in northern Tanzania of Manyamanyama, Mara, Bunda, a son of two public servants, a young regional commissioner and a registered nurse at Manyamanyama, patriotism has been embedded in my DNA.*

*Honourable Speaker, it is the greatest honor to stand in this August House to present myself as a candidate for the East African Legislative Assembly. This East African Legislative Assembly is just not a regional block, this is actually a vision for hope and prosperity crafted in 1967 by the founder of the Nation, Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, and the leaders of Kenya and Uganda, later on re-established in the year 2000 by the signing of the East African Community Treaty, which started at the beginning of the millennium. (Applause)*

*Honourable Speaker, today, the block has eight member states, a combined GDP of 751, billion dollars and 350,000,000 people. We have to foster this integration and we have to make it work.*

*Honourable Speaker, I stand in front of this body today, I am ready to carry this vision forward, and I have certain priorities that I would like to promote to assist the private sector, the common market, and we also have to be vigilant with security of the region. (Applause)*

*Honourable Speaker and Honourable Members of Parliament, I would love to have an opportunity to work with you. We will have another time to discuss how best we can do it. Today, I do ask for your votes. I do ask this opportunity to be a Member of the East African Legislative Assembly. Thank you very much for giving me this opportunity. God bless you very much. (Applause)*

***SPEAKER:*** *Any questions! Any questions! Any questions! Honourable Matiko.*

***HONOURABLE MEMBERS:*** *No, no, no!*

***SPEAKER:*** *Thank you very much. (Applause)*

Niombe sasa *Sergeant At Arms,* upige kengele kila Mbunge arudi ndani, tupate idadi ya Wabunge na kura zipigwe.

*(Hapa Sergeant At Arms, alipiga kengele ili Waheshimiwa Wabunge warudi ndani)*

**SPIKA:** Katibu tupate idadi.

Katibu ananiambia hii mitambo ni *dicentis,* imeshamhesabu kila Mheshimiwa Mbunge humu ndani na sasa hivi tupo 293.

Katibu tuendelee na upigaji kura. Kura zigaiwe.

*(Hapa Zoezi la Upigaji Kura kwa Wagombea Ubunge wa Bunge la Afrika Mashariki (EALA) lilifanyika)*

**SPIKA:** Kura zipigwe na zikusanywe. Kura zote zimepigwa? Kule juu, Chima! Waheshimiwa, wote tumepiga kura?

Mheshimiwa Prof. Shemdoe umeshapiga kura? Kuna mgeni mlangoni pale. Nimeambiwa una mgeni mlangoni, na ameshika karatasi ya kliniki. *(Kicheko)*

Haya funga maboksi, pelekeni ndani. Mawakala, Mheshimiwa Festo, simama hapo na Mheshimiwa Bulaya.

Waheshimiwa Wabunge, kanuni zetu zinataka mmoja awe *opposition na* mmoja CCM. Kwa hiyo, kati ya ninyi wawili mmoja ajiondoe. Mawakala ni wawili, mmoja Chama cha Mapinduzi na mmoja kutoka Chama cha Walio Wachache Bungeni. Kati ya Mheshimiwa Festo na Mheshimiwa Bulaya, mmoja wenu arudi kukaa.

Upande wa huku Mheshimiwa Agnesta. Jamani, mmeona mawakala wetu? Katibu, kura zihesabiwe. *(Makofi)*

**4 MEI, 2026**

Katibu.

**NDG. JOSHUA CHAMWELA, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027**

**SPIKA:** Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo na Mwenyekiti wa Kamati ya kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni, Michezo iliyochambua Bajeti ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo katika Bunge lako Tukufu, ninaomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupokea, kujadili, na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo Fungu 96 kwa Mwaka 2026/2027. Ninaomba Hotuba yangu yote iingie katika Kumbukumbu Rasmi za Bunge kama ilivyowasilishwa.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kuendelea kutupatia uhai, afya njema na kutuwezesha kukutana tena siku ya leo kujadili ustawi wa sekta ya habari, utamaduni, sanaa na michezo. Tuendelee kumwomba Mwenyezi Mungu atuongoze katika kujadili hotuba hii ya bajeti kwa dhamira ya kuhakikisha sekta ya habari, utamaduni, sanaa na michezo inakuwa na mchango mkubwa katika maendeleo ya ustawi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, kwa unyenyekevu mkubwa, nitumie fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniamini na kuniteua kwanza kuwa Naibu Waziri wa Habari, na pia kuwa Waziri kamili wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo. Hii ni heshima kubwa sana kwangu na kwa familia yangu, na ninachuka kama chachu ya kuendelea kulitumikia Taifa hili kwa bidii, weledi na uadilifu mkubwa. Nimhakikishie Mheshimiwa Rais

ya kwamba utumishi alionipatia nitahakikisha ninamlipa kwa uadilifu mkubwa.

Mheshimiwa Spika, niruhusu nitumie fursa hii kumpongeza tena Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake mahiri na maono mapana yanayolenga kuleta maendeleo kwa mwananchi mmoja mmoja na uchumi wa Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, pia, ninampongeza kwa kuendelea kuliongoza Taifa vyema katika kipindi hiki ambacho dunia inakumbana na changamoto mbalimbali hususani migogoro ya kivita Mashariki ya Kati na vita ya Urusi na Ukraine ambayo imeathiri kwa kiasi kikubwa uchumi wa dunia ikiwemo kupanda kwa bei za mafuta, na bidhaa mbalimbali. Pamoja na changamoto hizo, Mheshimiwa Dkt. Samia ameendelea kuonesha uongozi imara na mahiri, kuhakikisha kwamba Taifa linabaki moja na tunaendelea kusonga mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niruhusu tena nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa Hotuba yake ya bajeti aliyotoa mwelekeo wa utekelezaji wa malengo ya Serikali katika mwaka 2025/2026 na mwelekeo wa shughuli za Serikali katika mwaka 2026/2027.

Mheshimiwa Spika, pamoja na masuala mengine, hotuba hiyo imetoa maelezo kuhusu sekta zilizo chini ya Wizara. Wizara yangu imezingatia na itatekeleza maelekezo yote yaliyotolewa na Waziri Mkuu Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba.

Mheshimiwa Spika, kipekee, ninaomba nikupongeze wewe Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuliongoza kwa busara na weledi mkubwa Bunge la Kumi na Tatu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Maelekezo na miongozo yako yamekuwa na msingi wa ufanisi mkubwa wa Bunge katika kusimamia Serikali kutekeleza vyema majukumu yetu.

Mheshimiwa Spika, vilevile, ninampongeza Mheshimiwa Daniel Sillo, Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kukusaidia na kushauriana vyema katika utekelezaji wa majukumu yake. Pia, ninawapongeza sana Waheshimiwa Wenyeviti: Mheshimiwa Deodatus Mwanyika, Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso pamoja na Mheshimiwa Najma kwa kusimamia vyema, na kwa ustadi mkubwa mijadala katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kuishukuru kwa dhati Kamati ya Kudumu ya Bunge, Elimu, Utamaduni, Michezo chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko na Mheshimiwa Cornel Lucas Magembe, Makamu Mwenyekiti wa Kamati pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wote wa Kamati kwa maelekezo, ushauri, na maoni yao kwa Wizara yangu ambayo yametusaidia sana katika kuboresha utendaji kazi. Maelekezo yao yamesaidia kwa kiwango kikubwa katika uwasilishaji wa hotuba hii mbele yako.

Mheshimiwa Spika, Kamati hii imekuwa nguzo muhimu katika usimamizi madhubuti wa utekelezaji wa bajeti na ukaguzi wa miradi ambapo imefanikiwa kuhakikisha rasilimali za umma zinatumiwa kwa ufanisi na kwa manufaa ya umma kama misingi ya nyumba imara, ndivyo uongozi wa Kamati hii ulivyojenga misingi madhubuti kwa maendeleo unaoleta mafanikio endelevu na mabadiliko chanya katika jamii yetu.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2025/2026 Bunge lako Tukufu lilipatwa na misiba mbalimbali ya Waheshimiwa Wabunge. Misiba hiyo ni pamoja na Mheshimiwa William Lukuvi aliyekuwa Mbunge wa Ismani na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu; Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Peramiho; na Mheshimiwa Halima Iddi Nassor aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum akiwakilisha wafanyakazi.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wizara na wadau wetu tunatoa pole kwako, Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge, familia za Marehemu, ndugu, jamaa na marafiki na

Watanzania wote kwa ujumla. Mwenyezi Mungu azilaze roho za Marehemu mahali pema Peponi. Amina.

Mheshimiwa Spika, mafanikio yaliyopatikana katika kipindi chote hiki ni kutokana na ushirikiano mzuri miongoni mwa wadau wa Wizara wakiwemo viongozi, watumishi na wadau, washirika wa maendeleo ya Wizara. Natambua mchango mkubwa wanaoutoa kwa Wizara, ambao umeleta matunda ninayoweza kujivunia mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, pia, kwa dhati ya moyo wangu, ninamshukuru Mheshimiwa Hamis Mwinjuma, Mbunge, Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa ushirikiano anaonipa katika kutekeleza majukumu yangu ya Wizara. Ninamshukuru Ndg. Gerson Msigwa, Katibu Mkuu; Ndg. Methusela Ntonda, Naibu Katibu Mkuu; Wakuu wa Idara na Vitengo; Wakuu wa Taasisi zilizoko chini ya Wizara; na watumishi wote wanaofanya kazi kwa bidii na wanaohakikisha mipango ya Wizara inatekelezwa kama ilivyopangwa.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ni mhimili wa maendeleo ya jamii na Taifa kwa ujumla, ambapo kwa maneno mengine, ninaweza kusema ni Wizara yenye ushawishi *(soft power)* ya nchi hii na kulitambulisha Taifa letu kwa Mataifa. Sekta ya habari imekuwa na mchango mkubwa katika kuhabarisha, kuelimisha, kuburudisha na kuhakikisha kuwa wananchi wanapata taarifa mahsusi zinazowawezesha kushiriki kikamilifu katika maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, aidha, utamaduni wetu ni uti wa mgongo wa Taifa letu. Hivyo, kupitia sekta ya utamaduni, Serikali imeendelea kujenga uzalendo, kuhifadhi mila na desturi, pamoja na maadili ya Mtanzania.

Mheshimiwa Spika, Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuona umuhimu wa sekta hii, hususan michezo, imefanya uwekezaji mkubwa unaolenga kuinua Taifa katika ramani ya michezo. Mheshimiwa Rais amewekeza zaidi ya shilingi

trilioni 1.2 katika michezo ikiwa ni sehemu ya kuifanya Tanzania kuwa mwenyeji wa *AFCON* 2027. Uwekezaji huu upo katika Timu ya Taifa, uendeshaji wa michezo, pamoja na miundombinu mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, mapitio ya utekelezaji wa majukumu kwa kipindi cha mwaka 2025/2026; mapato na matumizi ya Wizara; katika mwaka wa fedha 2025/2026, Wizara ilikadiriwa kukusanya shilingi 1,036,000,000 ambapo hadi kufika mwezi Aprili, 2026 shilingi 699,706,093 sawa na 67.5% ya lengo la mwaka lililokusudiwa zimekusanywa.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Taasisi zilizo chini ya Wizara. Kiasi kilichokadiriwa kukusanywa kilikuwa ni shilingi 40,295,192,000 ambapo hadi mwezi Aprili, 2026, shilingi 17,020,636,000 sawa na 42% ya lengo zilikuwa zimekusanywa.

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya Wizara na Mtiririko wa Fedha. Katika mwaka wa fedha 2025/2026, Wizara iliidhinishiwa bajeti yenye jumla ya shilingi 519,660,073,000. Kati ya fedha hizo, mishahara ilikuwa shilingi 33,408,000,000, matumizi mengineyo ni shilingi 28,065,000,000 na miradi ya maendeleo ilikuwa ni shilingi 458,190,788,000.

Mheshimiwa Spika, hadi mwezi Aprili, 2026, Wizara ilikuwa imepokea jumla ya shilingi 352,942,454,472.97 sawa na 67.9% ya bajeti yote. Kati ya fedha zilizopokelewa, mishahara ilikuwa shilingi 27,684,544,158.90 sawa na 82.9%. Bajeti ya mishahara na matumizi mengineyo ni shilingi 20,925,566,233.81 sawa na 74.6%. Bajeti ya matumizi mengineyo na miradi ya maendeleo ni shilingi 304,332,344,080.26 sawa na 66.4% ya bajeti ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Utekelezaji Wa Majukumu ya Wizara kwa Mwaka 2025/2026 Wizara, kupitia Idara ya Habari na Msemaji Mkuu wa Serikali, imeendelea kuisemea Serikali kwa kutoa taarifa mbalimbali kuhusu utekelezaji wa miradi ya maendeleo nchini. Katika kipindi cha kuanzia Julai, 2025 hadi Aprili, 2026 Wizara

imefanikiwa kuandaa mikutano 22 ya Msemaji Mkuu wa Serikali na vyombo vya habari.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha wananchi wanaendelea kupata taarifa sahihi kuhusu mambo mbalimbali yanayofanywa na Serikali, Wizara imeratibu na kufanikisha mikutano 30 ya Taasisi za Serikali, kuzungumza na Waandishi wa Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari.

Mheshimiwa Spika, aidha, Wizara iliratibu mikutano 15 ya Waheshimiwa Mawaziri kuelezea utekelezaji wa majukumu na utekelezaji wa ahadi za Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, katika kipindi cha siku 100 za muhula wake wa pili wa Serikali ya Awamu ya Sita. Vilevile Wizara imechapisha nakala 20,000 za Jarida la Nchi Yetu linalohusu mafanikio ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Serikali.

Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia *TBC* imeendelea na utekelezaji wa Mradi wa Upanuzi wa Usikivu kwa kujenga vituo vya kurusha matangazo ya redio, masafa ya *FM,* katika wilaya 18 nchini. Ujenzi unaendelea katika Wilaya za Kalambo (Rukwa), Liwale (Lindi), Rufiji (Pwani), Biharamulo (Kagera), Urambo na Igunga (Tabora). Karatu (Manyara), Kilolo (Iringa), Ulanga (Morogoro), Iramba (Singida) na Ngara (Kagera).

Mheshimiwa Spika, wakati huo huo *TBC* imepokea mitambo ya masafa ya *FM,* kwa ajili ya Wilaya za Tanganyika (Katavi), Gairo (Morogoro), Hanang (Manyara), Siha (Kilimanjaro) na Mpwapwa (Dodoma). Aidha, *TBC* inashirikiana na wadau wengine wa maendeleo ya mawasiliano na teknolojia ya habari ikiwemo Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote, ambapo mradi wa upanuzi wa usikivu unatekelezwa katika Wilaya 10 za Kyerwa (Kagera), Chunya (Mbeya), Kiteto (Manyara), Chemba (Dodoma) na Mkinga (Tanga).

Mheshimiwa Spika, maeneo mengine ambayo mradi unatekelezwa ni Bukombe (Geita), Usangi (Kilimanjaro), Rombo (Kilimanjaro), Buhigwe (Kigoma) na Tunduru (Ruvuma).

Mheshimiwa Spika, *TBC* kwa kushirikiana na Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari imetekeleza Mradi wa Upanuzi wa Usikivu Katika Wilaya 15. Kazi ya ufungaji wa mitambo ya kurusha matangazo, imekamilika kwa vituo vya Arumeru (Arusha), Meatu (Simiyu), Sengerema (Mwanza), Kilosa (Morogoro), Mpwapwa (Dodoma) na Momba (Songwe). Aidha, ujenzi wa majengo ya kuhifadhi mitambo unaendelea kwenye Halmashauri za Iringa Vijijini (Iringa), Lushoto (Tanga), Simanjiro (Manyara), Mpimbwe (Rukwa), Nyang'hwale (Geita), Kilombero (Morogoro), Nkasi Kusini (Rukwa), Itigi (Singida) na Mkalama (Singida).

Mheshimiwa Spika, kukamilika kwa ujenzi wa vituo hivi kutaongeza usikivu wa 98%. Hadi kufikia Aprili, 2026 usikivu wa Redio za *TBC* umefika Wilaya zote 139.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kuwa *TBC* inawafikia vijana kwenye majukwaa ya mtandaoni, maboresho makubwa ya kimaudhui na mifumo, yamefanyika kupitia *Bongo FM, TBC*2 na *TBC* Mtandao. Chaneli hizi za kimkakati zimekuwa chachu kwa kuongeza watazamaji, wafuatiliaji na wasikilizaji.

Mheshimiwa Spika, vilevile *TBC,* kupitia chaneli yake ya Tanzania Safari, ambayo ni mahsusi kwa ajili ya kutangaza fursa za utalii na utajiri wa maliasili za nchi yetu, imewezesha kuandaa maudhui na kutafsiri na kurusha jumla ya vipindi 10,125 katika lugha tano za Kimataifa ambazo ni Kireno, Kiarabu, Kiingereza, Kifaransa na Kichina.

Mheshimiwa Spika, tarehe 2 Septemba, 2022 Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alipokuwa Bagamoyo kwa ajili ya maandalizi ya filamu ya *the Royal Tour* aliiagiza *TANAPA* kuitangaza njia ya utumwa kuwa kivutio cha utalii. Kufuatia agizo hilo, Wataalamu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa kushirikiana na *TANAPA* wamefanya utafiti na kuwasilisha ripoti iliyobainisha vivutio na mikakati ya utangazaji. Wizara, kupitia *TBC,* imetekeleza agizo hilo kwa kutambua njia ya misafara ya utumwa na wapagazi na

kuitangaza kupitia kampeni ya The *Slave Caravan* inayorushwa na Chaneli ya Utalii ya Tanzania Safari.

Mheshimiwa Spika, kampeni hii inalenga kutangaza njia ya utumwa na vivutio vyake ambavyo havijulikani sana kwa Watanzania na wageni. Kupitia kampeni hii, vituo 14 vimebainishwa kutoka Zanzibar, Bagamoyo hadi Ujiji Kigoma vitakavyotumika kuhifadhi historia ya watumwa, utumwa, masuria na maisha baada ya kukomeshwa kwa utumwa kupitia kampeni hii ya *The Slave Caravan*. Serikali inatarajia kuigeuza historia chungu ya utumwa kuwa fursa ya elimu, hifadhi na maendeleo ya utalii nchini Tanzania.

Mheshimiwa Spika, channeli ya *TBC1*, *TBC*2 na Tanzania Safari kwa kupitia mtandao wa Televisheni ya *Canal International* zimeweza kufikia nchi 46 zinazoongea Kiingereza, Kifaransa na Kireno. Nchi hizo ni pamoja na Angola, Benin, Bukinafaso, Botswana, Burundi, Kameruni, Jamhuri ya Afrika ya Kati, Chadi, Congo, Jamhuri ya Kidemokrasia ya *Congo*, *Djibouti*, *Equatorial Guinea*, Ethiopia, Eritrea, Gabon, Gambia, Ghana, Guinea Bissau, *Ivory Coast*, Kenya, Liberia, Lesotho, Mali, Malawi, Mauritania, *Mozambique*, Namibia, Nigeria, Niger, Rwanda, *Senegal*, Sierra Leone, Somalia, Sudani, Afrika Kusini, Sudani ya Kusini, Uganda, Tanzania, Togo, Zambia na Zimbabwe. Aidha, kupitia Azam nchi saba zimefikiwa ambazo ni Tanzania, Kenya, Burundi, Uganda, Rwanda, Malawi na Zimbabwe.

Mheshimiwa Spika, Wizara, kupitia *TSN,* imeendelea kutekeleza mradi wa ufungaji wa mitambo mipya ya kisasa ya uchapaji kwa kujenga jengo la kiwanda cha uchapaji na kununua mitambo mipya ya kisasa ya uchapaji. Hatua ya ujenzi wa jengo la kiwanda cha uchapaji imefikia 83.1%. Ununuzi wa mitambo mipya ya kisasa ya uchapaji umefikia 85%.

Mheshimiwa Spika, Wizara, kupitia *TSN,* imeendelea kuboresha uandaaji wa uchapaji wa maudhui kupitia magazeti, chaneli za mitandao na majukwaa ya mitandao ya kijamii. Maudhui haya yamejulikana katika kuhabarisha mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt.

Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hadi kufikia Aprili, 2026 *TSN* imeandaa na kuchapisha jumla ya makala 2,973 za kimkakati.

Mheshimiwa Spika, *TSN* imeanzisha mkataba maalum wa historia kwa kuweka matoleo ya zamani ya magazeti na picha kwenye mfumo wa kidijitali. Jumla ya matoleo 12,600 ya *Daily News* na Habari Leo, picha zaidi ya 2,499 na makala maalum zaidi ya 2,100 yamepatiwa alama za utambuzi. Mfumo huu umehifadhi nyaraka zote muhimu zinazohusu historia ya nchi, historia kuhusu viongozi wakiwemo waasisi wa Taifa, historia ya harakati ya ukombozi wa uhuru kwa nchi za kusini mwa Afrika na historia, kuhusu masuala ya kidiplomasia kutokana maktaba hii ya *TSN* kuhifadhi nyaraka na kumbukumbu za kihistoria.

Mheshimiwa Spika, kampuni imefanikiwa kuwa chanzo kikuu cha taarifa kwa ajili ya Kitabu cha Rais wa Awamu ya Tatu, Hayati Benjamin William Mkapa; Rais wa Awamu ya Pili, Hayati Ali Hassan Mwinyi, Kitabu cha Muungano na Picha zote zinazopamba Ukumbi wa Kimataifa wa Mikutano wa Julius Nyerere.

Mheshimiwa Spika, katika hatua ya uimarishaji wa mfumo wa kidigitali, kampuni imeunda mfumo wa *TSN integrated management information system* unaounganisha *digital archive* na tovuti ya kampuni ili kuwezesha kutoa huduma na kupata taarifa zote popote duniani.

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Ithibati ya Waandishi wa Habari katika kipindi cha Julai, 2025 hadi 2026 imepokea maombi na kusajili waandishi wa habari 4,139 kupitia mfumo wa *TAI-Habari,* ambapo waandishi wa habari 3,357 wenye vigezo vinavyoainishwa kwa mujibu wa sheria wamepatiwa ithibati. Malalamiko 14 ya uvunjifu wa maadili ya taaluma ya habari yameshughulikiwa.

Mheshimiwa Spika, Wizara, kupitia Bodi ya Ithibati ya Waandishi wa Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, imeandaa mwongozo maalum. Ninaomba nisome vizuri, taratibu; "Wizara, Kupitia Bodi ya Ithibati ya Waandishi wa Wizara

ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, imeandaa Mwongozo Maalumu wa Kisheria utakaowezesha wanahabari wakongwe walioathiriwa na mfumo wa ithibati kurejea katika mfumo rasmi kwa kuzingatia Masharti ya Sheria Huduma za Habari Sura Na. 229, ambayo ilitungwa kwa ajili ya kukuza Taaluma ya Uandishi wa Habari kwa kuweka mfumo wa kitaasisi utakaosimamia Sekta ya Habari. Mwongozo huu unaweka utaratibu wa kisheria wa kutambua na kudhibitisha umahiri wao kupitia tathmini maalum ya uzoefu, uweledi na maadili ya taaluma na kuwawezesha kupata ithibati kwa mujibu wa Sheria."

Mheshimiwa Spika, kupitia ushirikiano kati ya Bodi ya Ithibati ya Waandishi wa Habari na Mfumo wa Utamaduni, Mfuko wa Utamaduni wa Sanaa wa Tanzania, Serikali imeendelea kuwezesha mitaji ya kukuza, kuendeleza na kuzalisha kazi zao za kuboresha unaokidhi mahitaji ya soko kupitia mikopo yenye masharti nafuu.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza hayo, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ametoa shilingi 20,000,000,000 kwa ajili ya Mfuko wa Utamaduni. Tayari shilingi 200,000,000,000 kwa ajili ya mikopo ya watengeneza maudhui mtandaoni, yaani *content creator,* zimetoka kwa lengo la kuwasaidia kupata vitendea kazi na kuongeza uzalishaji wa kazi zao.

Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Mfuko wa Utamaduni na Sanaa, imetoa mafunzo kwa watengeneza maudhui mtandaoni wenye lengo la kuwawezesha kutengeneza kazi zenye ubora kwa soko shindani la ndani na nje ya nchi. Mafunzo kwa Awamu ya Kwanza yametolewa kwa watengeneza maudhui mtandaoni 931, ambapo kati yao wanawake ni 574 sawa na 62% na wanaume ni 357 sawa na 38% kutoka mikoa mitatu ya Dar es Salaam, Mwanza na Arusha.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Maudhui imepewa jukumu la kusimamia maudhui yanayotolewa katika vyombo vya habari na kuchukua hatua pale inapotokea ukiukwaji wa Sheria, Kanuni na Maadili. Kabla ya kuchukua hatua za kisheria, Serikali hutanguliza

mazungumzo, ushauri na utoaji wa maelekezo kwa vyombo husika ikilenga kutoa fursa ya kujirekebisha. Hatua hizi huchukuliwa pale ambapo ukiukaji unaendelea, unajirudia au unasababisha madhara makubwa kwa umma.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Aprili, 2026 Wizara kupitia Kamati ya Maudhui ya Mamlaka ya Mawasiliano, imetekeleza majukumu yafuatayo: kufanya vikao tisa vya Kamati ya kushughulikia masharti dhidi ya watoa huduma 14 ambao walikiuka Sheria, Kanuni na Masharti ya leseni zao. Kufanya mapitio ya taarifa ya ukiukaji wa kanuni za utangazaji dhidi ya watoa huduma 11, maudhui ya utangazaji yaliyobainika kuwa na ukiukaji wa mara kwa mara wa Sheria, Kanuni, Masharti ya leseni na kushiriki kwenye vikao vitatu vya mashauriano na watoa huduma wa utangazaji na maudhui kuhusu uzingatiaji wa Sheria, Kanuni, Masharti ya leseni na Maadili ya Uandishi na Utangazaji wa Habari.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Maendeleo ya Utamaduni. Tanzania imejaliwa kuwa na utajiri mkubwa wa uanuai wa urithi wa utamaduni. Katika kuhakikisha kuwa, urithi huu unalindwa, unahifadhiwa na kuendelezwa, Serikali imefanya utafiti wa kutambua, kuorodhesha na kulinda urithi wa utamaduni usioshikika kwa manufaa ya kizazi cha sasa na kijacho. Utafiti huo uliofanyika kwa kushirikiana na wadau wa utamaduni ulijikita katika kutambua na kuorodhesha vazi la kanga, kama moja ya alama muhimu ya utambulisho wa Utanzania na urithi wa utamaduni.

Mheshimiwa Spika, kufuatia utafiti huo, andiko la vazi la kanga liliwasilishwa Shirika la Umoja wa Mataifa, Elimu, Sayansi na Utamaduni *(UNESCO)* kwa lengo la kuingizwa kwenye orodha ya urithi wa dunia wa utamaduni usioshikika inayosimamiwa na shirika hilo. Manufaa ya kutambuliwa kwa Urithi wa Utamaduni wa Tanzania katika orodha ya urithi wa dunia ni pamoja na kuongeza hadhi ya Utamaduni wa Kimataifa, kupata fursa ya ufadhili wa uendelezaji wa uhifadhi wa urithi kutoka kwenye Mifuko ya Kimataifa inayoratibiwa na *UNESCO*, kutangaza Urithi wa

Utamaduni wa Tanzania, pamoja na utalii wa kiutamaduni duniani.

Mheshimiwa Spika, jitihada nyingine zilizofanywa na Serikali, kupitia Wizara, ni kukamilisha uandaaji wa Mwongozo wa Kitaifa wa kulinda urithi wa utamaduni usioshikika, yaani *National Framework Safeguarding Intangible Cultural Heritage*. Katika kukubaliana na suala la mmomonyoko wa maadili nchini, umeandaliwa Mkakati wa Taifa wa kukabiliana na mmomonyoko wa maadili nchini. Mbali na mkakati huo, kupitia Televisheni ya Taifa *TBC,* kumeanzishwa kipindi maalumu cha maadili, uzalendo na Utaifa kinachojulikana kwa jina la Sisi ni Tanzania. Kipindi hiki ni mahususi kwa ajili ya kuukumbusha umma wa Watanzania kuhusu umuhimu wa kurejea kwenye misingi ya maadili, mila, desturi, miiko, uzalendo na uadilifu wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha Kiswahili kinaendana na mabadiliko ya teknolojia Wizara, kupitia BAKITA, imeandaa Kongoo ya Kiswahili ya Taifa, yaani KOKITA kwa kipindi cha Julai, 25 hadi Aprili, 26. BAKITA imekusanya, imehariri na kuingiza maneno milioni 22 katika Kongoo ya Kiswahili ya Taifa, ambapo hadi Aprili, 2026 Kongoo hiyo ina jumla ya maneno milioni 61 na lengo ni kufikisha maneno milioni 100. Kongoo hii itakuwa daraja la kuongeza ufanisi wa Kiswahili katika teknolojia ya kompyuta, hususan katika matumizi ya akili unde, yaani *AI*. Pia Baraza linaendelea kukuza ushirikiano na wadau mbalimbali wakiwemo Taasisi ya Mozilla, ili kuwezesha kuimarisha Kiswahili katika teknolojia.

Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia BAKITA umeongoza umma wa wazungumzaji, wadau na wapenzi wa Kiswahili, Afrika na duniani kote, kushuhudia hatua kubwa ya Kiswahili kukubalika kuwa lugha rasmi ya Mkutano Mkuu wa Shirika la Umoja wa Mataifa, Elimu, Sayansi na Utamaduni *UNESCO*. Kiswahili ni lugha ya kwanza ya Afrika kupata hadhi hiyo na hivyo yalijiri katika Mkutano Mkuu wa 43 wa shirika hilo Oktoba hadi Novemba 13, 2025.

Mheshimiwa Spika, kwa muktadha huo, Kiswahili sasa ni lugha rasmi ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, Jumuiya ya Maendeleo kwa Nchi ya Kusini mwa Afrika, Umoja wa Afrika, Umoja wa wazalishaji, Almasi Afrika na *UNESCO*. Vilevile Kiswahili ni lugha ya pekee ya Afrika iliyotengewa siku ya kuadhimishwa ambapo ni tarehe 7 Julai kila mwaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hatua nyingine, Wizara kupitia BAKITA imefanya kikao na *UNESCO* pamoja na wadau wa maudhui ya mitandaoni kuhusu nafasi ya Kiswahili katika mitandao mikubwa ya kijamii *Meta, TikTok* na *Google* ili wapanue nafasi ya Kiswahili katika mitandao hiyo na hivyo kuongeza ajira na kipato kwa waandaji wa maudhui kupitia mitandao ya kijamii.

Mheshimiwa Spika, katika kuelekea mashindano ya Kombe la Mataifa ya Afrika *(AFCON)*, Serikali kupitia BAKITA inaendelea na shughuli ya usanifishaji wa istilahi za michezo ambapo hadi sasa jumla ya istilahi 420 za michezo zimesanifishwa.

Mheshimiwa Spika, wahenga wanasema, "Asiyefahamu lugha, hafahamu mila." Wizara kupitia BAKITA imeendelea kuelimisha umma kuhusu kuzingatia matumizi ya Kiswahili fasaha na sanifu pamoja na utamaduni wake. Shughuli hii imehuishwa kuandaa na kurushwa hewani jumla ya vipindi 1,057 kupitia vituo vya redio na televisheni. Mafunzo ya msasa ya matumizi ya Kiswahili fasaha na sanifu pamoja na utamaduni wake yametolewa kwa Waandishi Wawezeshi Ofisi 844, Makatibu na Makatibu wa Halmashauri 12 pamoja na wa hudumu wa mapokezi ya huduma kwa wateja 52.

Mheshimiwa Spika, Baraza limeandaa na kufanya kongamano la tano la Idhaa zinazotangaza kwa Kiswahili duniani ikiwa na kaulimbiu "Tasnia ya habari msingi wa maendeleo ya Kiswahili duniani". Lengo kuu la kongamano la Idhaa ni kuimarisha uhusiano wa taasisi za Kiswahili na vyombo vya habari ambavyo vinatekeleza jukumu kubwa la kukikuza na kukieneza Kiswahili ndani na nje ya nchi. Kongamano hilo lilifanyika katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Arusha *AICC* Jijini Arusha, Tarehe 24 - 27 Machi, 2026.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ina jumla ya vituo 55 vya kufundisha Kiswahili kwa wageni, ambapo vituo 20 vipo nje ya nchi na vituo 35 vipo nchini. Ufunguaji wa vituo hivi umeongeza chachu ya kujifunza Kiswahili kwa wageni.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Kituo cha Urithi wa Ukombozi wa Bara Afrika inaendelea kudumisha hadhi ya Tanzania kama Mama wa Ukombozi Afrika, kwa kuhakikisha kuwa mchango wetu wa kihistoria unatambulika, unahifadhiwa na kuendeleza kwa manufaa ya vizazi vya sasa na vizazi vijavyo.

Mheshimiwa Spika, katika kuonyesha dhamira hiyo, tunamshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uamuzi wake wa kimkakati wa kutekeleza mradi wa ujenzi wa Makao Makuu ya Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika kama ilivyoazimiwa na Umoja wa Afrika. Hatua hii inaakisi uongozi thabiti na dira ya kulinda historia ya Taifa letu huku tukiweka katika nafasi ya Kimataifa kama kitovu cha kumbukumbu za ukombozi wa Bara la Afrika.

Mheshimiwa Spika, katika hatua ya utekelezaji, Wizara kupitia Kituo, imetenga eneo lenye ukubwa wa hekari 426.6 katika Wilaya ya Kongwa Mkoani Dodoma kwa ajili ya ujenzi wa kituo kikuu cha uhifadhi wa urithi wa ukombozi wa Bara la Afrika kitakachokuwa ni sehemu ya taasisi ya Umoja wa Afrika. Eneo hilo liko tayari na limeshakamalishwa kupatiwa hati hatua inayoweka msingi imara wa utekelezaji wa mradi huu wa kimkakati wa Kimataifa na kibara.

Mheshimiwa Spika, katika sekta ya sanaa, ninatoa shukrani za dhati kwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake madhubuti na juhudi zake zinazopelekea kufanikisha Tanzania kupata heshima kubwa kuwa mwenyeji wa mashindano makubwa zaidi ya ulimbwende duniani *(Miss World)*. Kama unavyoona pale jukwaani kwenye *gallery* yako upande wako wa kulia, utakapopata nafasi ya kutambulisha, tunao tayari warembo wameingia ndani ya Bunge lako Tukufu ili kushuhudia jitihada na kazi kubwa inayofanywa na Mheshimiwa Dkt. Samia.

Mheshimiwa Spika, mashindano hayo yanatarajiwa kuleta manufaa makubwa kiuchumi na kijamii kupitia mapato ya viingilio, huduma za utalii, udhamini, biashara za wageni pamoja na kutoa fursa kwa wabunifu wa ndani kujifunza na kujitangaza Kimataifa. Aidha, tukio hili litasaidia kuitangaza Tanzania duniani kama kitovu cha utalii wa asili na utamaduni, kuimarisha diplomasia ya Kimataifa, kuthibitisha usalama wa nchi kwa wageni.

Mheshimiwa Spika, mashindano ya *Miss World* Tanzania 2026 yaliofanyika tarehe 19 Aprili, ambapo mlimbwende Latricia Ian Sawe aliibuka mshindi na ataiwakilisha Tanzania katika mashindano yatakayofanyika *Vietnam* Septemba, 2026 ambapo Tanzania inatarajia kukabidhiwa rasmi bendera ya uenyeji kwa mwaka 2027.

Mheshimiwa Spika, mashindano ya *Miss World* 2027 yatatumika kama kichocheo cha hamasa kuelekea *AFCON* 2027 na kuongeza mwamko wa Kitaifa pamoja na ushiriki wa wananchi katika maandalizi ya tukio hilo kubwa la kihistoria kwa Bara Afrika.

Mheshimiwa Spika, mashindano haya ya *Miss World* ambayo Mheshimiwa Rais amefanikisha kuyaleta Tanzania, katika nchi 54 za Bara Afrika, Tanzania ni nchi ya pili kuwa mwenyeji wa mashindano haya ukitoa nchi ya kwanza ambayo ilikuwa ni *South Africa*. Kutokana na mazungumzo mazuri yaliyofanywa na Mheshimiwa Dkt. Samia, nasi tukiwa wawakilishi wake, mwandaaji wa mashindano haya ameridhia Tanzania kuwa mwenyeji wa waandaaji wa mashindano ya *Miss World,* itafanyika miaka mitatu mfululizo na kuleta nchi zaidi ya 180 katika Taifa la Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Wizara iliratibu Tamasha la *CHAN* Singeli lililofanyika tarehe 2 Agosti, 2025 katika eneo la nje la Uwanja wa Benjamin Mkapa, ikiwa ni sehemu ya sherehe za uzinduzi wa mashindano ya Kombe la Mataifa ya Afrika kwa wachezaji wa ligi ya ndani. Tamasha hili lilikuwa na mafanikio makubwa ambapo zaidi ya wasanii 30 wa muziki wa singeli walipata fursa ya kutumbuiza.

Mheshimiwa Spika, kupitia jukwaa hili, muziki wa Singeli uliweza kutangazwa Kimataifa kama sehemu ya utambulisho wa utamaduni wa Tanzania. Sambamba na hilo, Serikali imeendelea kuratibu Tamasha la Singeli *Music Festival*. Tamasha hili linalotarajiwa kufanyika tarehe 30 Mei, 2026, linalenga kutumika kama jukwaa la kuhamasisha ushiriki wa wananchi katika mashindano ya *AFCON* 2027.

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Filamu Tanzania imeratibu tamasha na tuzo za filamu. Tamasha hilo lenye dhima ya filamu ni biashara, lililohusisha matukio kama midahalo, warsha na mafunzo kwa wadau ya filamu na michezo ya kuigiza, lilifanyika Jijini Dar es Salaam kuanzia tarehe 3 Julai hadi 16 Agosti, 2025, ambapo jumla ya wadau 1,600 walishiriki zikiwemo nchi za Zambia, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Kenya, Somalia, Uganda, Rwanda na nchi kutoka nje ya Afrika, ambazo ni Uswizi na Marekani.

Mheshimiwa Spika, tamasha hilo lilihitimishwa kupitia kilele cha usiku wa tuzo za filamu lililofanyika tarehe 14 Februari, 2026 Jijini Dar es Salaam, ambapo jumla ya wadau 1226 walishiriki, na jumla ya tuzo 28 zilitolewa katika tamasha hilo.

Mheshimiwa Spika, *COSOTA* inaendelea kufuatilia ukusanyaji wa tozo ya haki miliki yaani *copyright levy*. *COSOTA* inaratibu mgao wa fedha zinazotokana na tozo ya haki miliki, ambapo jumla ya shilingi 988,656,103.92 sawa na 60% ya makusanyo yote ya shilingi 1,647,660,173.20 yaliyofanyika kuanzia Septemba, 2023 hadi Juni, 2025 zitagawiwa kwa wabunifu wa kazi za sanaa na uandishi. Mchanganuo wa mgao ni daraja la muziki 20%, filamu 15%, sanaa ya uandishi asili 10%, sanaa ya ufundi asili asilimia saba nukta tano, na sanaa ya maonesho asilimia saba nukta tano.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Utamaduni wa Sanaa Tanzania umewezesha upatikanaji wa mikopo kwa wasanii kwa kushirikiana na taasisi za Kifedha. Serikali kupitia mfuko imetoa mikopo yenye thamani ya shilingi 3,535,000,000 kwa miradi 229 ya utamaduni na sanaa. Aidha, sekta zilizonufaika na mikopo hiyo ni

filamu, ufundi, muziki, lugha na *fashion*. Imewezesha pia katika Mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Morogoro, Manyara, Arusha, Mwanza, Kagera na Shinyanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, makofi yanavyozidi, ndivyo ambapo fedha hizi zitapelekwa kwa ajili ya hawa wasanii. Ninaomba kurudia tena. Katika mikoa hiyo 15 ni Mkoa wa Dar es Salaam, Pwani, Morogoro, Manyara, Arusha, Mwanza, Kagera, Shinyanga, Mara, Geita, Mbeya, Kilimanjaro, Ruvuma, Tabora. Hali kadhalika, kupitia miradi hii iliyotekelezwa, jumla ya ajira 75,537 zimezalishwa na kuwanufaisha wananchi zaidi ya 971,285.

Mheshimiwa Spika, maendeleo ya michezo. Wizara imeratibu kwa ufanisi michuano ya mpira wa miguu ya Afrika kwa wachezaji wa ndani, *CHAN*, 2024. Mashindano ya *CHAN* ni kigezo ambacho Shirikisho la Soka Afrika, *CAF*, hutumia kama kipimo cha nchi kuwa mwenyeji wa mashindano ya *AFCON*.

Mheshimiwa Spika, Mashindano hayo yalifanyika nchini kuanzia tarehe 2 hadi tarehe 30 Agosti, 2025, ambapo nchi ya Tanzania, Kenya na Uganda zilikuwa mwenyeji. Timu ya Taifa, Taifa *Stars,* ilishiriki na kuonyesha kiwango cha juu cha ushindani kwa kufanikiwa kufika hatua ya robo fainali, hatua inayodhihirisha kuimarika kwa soka letu la ndani.

Mheshimiwa Spika, aidha, kutokana na ubora wa maandalizi ya usimamizi wa mashindano hayo, *CAF* ilimtunuku tuzo ya heshima Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kazi nzuri, njema na ufanisi mkubwa ulionekana katika maandalizi ya *CHAN*.

Mheshimiwa Spika, sambamba na mashindano hayo, Serikali kupitia Wizara, imeendelea na maandalizi ya mashindano ya Kombe la Mataifa ya Afrika, 2027 kwa kutekeleza kwa ufanisi majukumu mbalimbali, hususan ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya michezo katika Miji wenyeji wa Dar es Salaam, Arusha, ambapo ni ukarabati wa uwanja wa Benjamin Mkapa umefikia 95%, ukarabati wa viwanja vitatu vya mazoezi, yaani Gymkhana pamoja na *Major General* Isamuyo na Shule ya Sheria

imekamilika. Ujenzi wa viwanja vitatu vingine vya mazoezi farasi, *Leaders Club* na *Gymkhana Two* vipo katika hatua za awali.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa Uwanja wa Arusha wenye uwezo wa kuchukua Watanzania zaidi ya 32,000 umefikia 77.5% na ujenzi wa uwanja, kimoja cha mazoezi kinachojengwa katika eneo la Uwanja wa Arusha umefikia 60%. Ni matarajio yetu kuwa ifikapo Agosti, 2026 Serikali itakamilisha miundombinu yote kwa ajili ya *AFCON* ikiwa ni pamoja na ujenzi wa viwanja vidogo vidogo vya mazoezi vitatu ambavyo viko katika eneo la Magereza, viko eneo la Engutoto pamoja na kiwanja cha Mgambo Jijini Arusha.

Mheshimiwa Spika, katika kudhihirisha dhamira ya dhati ya Serikali kuhakikisha tunafanikisha mashindano ya *AFCON* 2027, tayari Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ameridhia kutoa kiasi cha Dola za Kimarekani milioni 30 sawa na shilingi 76,157,100,000 kama ada ya uandaaji wa mashindano husika. Hii ndiyo tafsiri halisi ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kama mwanamichezo namba moja nchini Tanzania.

Mheshimiwa Spika, sambamba na maandalizi ya miundombinu ya *AFCON* 2027, Serikali imeendelea kuwekeza katika maendeleo ya miundombinu mingine ya michezo nchini kwa kutekeleza miradi mikubwa ya kimkakati yenye lengo la kukuza vipaji na kuboresha huduma za michezo kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, miradi mingine inayotekelezwa ni ujenzi wa *academy* za michezo katika Kituo cha Maendeleo ya Michezo, Malya ambapo utekelezaji wake umefikia 49%. Ujenzi wa Uwanja wa Mpira wa Miguu Jijini Dodoma wenye uwezo wa kuchukua watu 32,500 umefikia asilimia tano. Ujenzi wa kituo cha mazoezi na kupumzikia wananchi Jijini Dodoma ambao umefikia 73.5%. Ujenzi wa kituo cha mazoezi ya kupumzikia wananchi Jijini Dar es Salaam kilichofikia 49% na ukarabati wa Uwanja wa Uhuru ambapo umefikia 70%.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Baraza la Michezo la Taifa limeendelea kuwezesha ushiriki wa wanamichezo na Timu za Taifa

katika mashindano ya Kimataifa. Serikali inampongeza mwanariadha Alphonce Felix Simbu (nina imani yupo ndani ya jengo lako Tukufu), aliyefanikiwa kushinda medali ya dhahabu katika Mashindano ya Riadha ya Dunia yaliyofanyika Septemba, 2025 Jijini Tokyo, Japan, ikiwa ni medali ya kwanza ya dhahabu ya kwanza Tanzania katika mashindano hayo tangu kupata Uhuru. Pia kuibuka mshindi wa pili wa kushinda medali ya fedha katika mashindano ya *Marathon* ya Kimataifa yaliyofanyika Tarehe 20 Aprili, 2026 Jijini Boston, Marekani.

Mheshimiwa Spika, pia tunampongeza Mwanariadha Johny Were aliyetwaa medali ya dhahabu katika mashindano ya Nusu *Marathon* yaliyofanyika tarehe 19 Aprili, 2026 nchini Poland. Hao washindi wetu wote tumewaleta pia kwenye bajeti yetu ikiwa sehemu ya kupata heshima ya Bunge lako Tukufu kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuiwakilisha Tanzania.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, Serikali inaipongeza Timu ya Taifa ya Mpira wa Miguu, *Taifa Stars*, kwa kufika hatua 16 bora katika mashindano ya *AFCON* 2025 yaliyofanyika nchini Morocco na kufika hatua ya robo fainali ya mashindano ya *CHAN* yaliyofanyika 2024.

Mheshimiwa Spika, pia Serikali inaipongeza Timu ya Wanawake pia kwa kushiriki Kombe la Dunia 2025 nchini Ufilipino na kufikia hatua ya makundi. *Twiga Stars* iliotwaa ubingwa wa *CECAFA Senior Women Championship* 2025 na kufuzu *WAFCON* ya 2026. Pamoja na timu ya mpira wa miguu kwa wenye ulemavu kwa kushiriki mashindano ya Afrika Mashariki na Kati nchini Burundi.

Mheshimiwa Spika, aidha, Wizara inatoa pongezi kwa timu ya Taifa ya ngumi kwa kushinda jumla ya medali 18. Zoezi la ngumi au mashindano ya ngumi haya siyo ya mchezo, kwa sababu unaweza ukashangaa taya linatoka, lakini tumepata medali 18; dhahabu ni moja, fedha ni nne na za shaba ziko 13 katika mashindano ya kanda ya tatu ya Afrika yaliyofanyika Kenya mwaka 2025.

Mheshimiwa Spika, pia timu ya mpira wa kikapu ya Dar *City* iliyoshiriki mashindano ya kikapu Afrika yaliyofanyika nchini Afrika Kusini, ilifanikiwa kufuzu kucheza fainali ya mashindano hayo yatakayofanyika nchini Rwanda Mei, 2026. Hii timu ya *Dar City* pia ni katika historia ya Taifa letu hatujawahi kuwa na timu iliyoshiriki katika mashindano ya *basketball,* ambapo sasa *Dar City* imechukua nafasi hiyo ya kuiwakilisha Tanzania na kupeperusha bendera vyema huko duniani na kuingia katika mashindano yanayokwenda kufanyika nchini Rwanda.

Mheshimiwa Spika, ninaomba pia kumleta kwako na kwa Bunge lako Tukufu Bondia Ibrahim Class, aliyepigana na kupata mikanda miwili ya *WBC* na *WBO*. Huyu kapata ushindi mkubwa na mikanda hiyo ina thamani kubwa. Hivi tunavyoongea, tuko naye ndani ya Bunge lako Tukufu ikiwa ni sehemu ya kupata heshima ya Waheshimiwa Wabunge chini ya Bunge lako katika kazi kubwa nzuri unayofanya.

Mheshimiwa Spika, pia, tunaye Bondia Lupakisyo Mohamedi Shoti ambaye alishinda mikanda wa *IBO Africa*, tunaye pia Amani Bariki aliyeshinda mkanda wa *WBC Intercontinental*, Frank Changembe aliyeshinda mkanda wa *WBO* Afrika uzito wa kilo 90. Yusufu Changalawe ameshinda mkanda wa *WBC* Afrika, Halima Vunjabei aliyeshinda mkanda wa *PST*. Mafanikio hayo yanaonesha maendeleo chanya ya michezo nchini.

Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia *BMT* kwa kushirikiana na Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania, liliratibu Mkutano wa Kamati ya Utendaji wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika, *CAF* ambapo ulifanyika tarehe 13 Februari, 2026 Jijini Dar es Salaam. Mkutano huo uliwaleta pamoja vigogo wa soka Barani Afrika ukiwa na lengo la kujadili na kuweka mikakati ya kukuza vipaji, kuimarisha ushindani wa vilabu na timu za Taifa pamoja na kuongeza uwekezaji katika miundombinu ya mpira wa miguu.

Mheshimiwa Spika, Tanzania kwa kuwa mwenyeji wa mkutano huo ni kielelezo cha uwezo wa nchi yetu kuandaa mikutano mikubwa na umeongeza hadhi ya Tanzania katika ramani ya soka Afrika, hususan wakati wa Mataifa kujadili fainali

za *AFCON* 2027. Ujio wa viongozi hao unaweka wazi kuwa nchi yetu inazidi kuaminiwa kama kitovu cha maamuzi makubwa ya michezo Barani Afrika.

Mheshimiwa Spika, maelezo ya kina kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa mwaka 2025/2026 yanapatikana katika ukurasa wa 13 hadi ukurasa wa 148 wa kitabu cha hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, katika Mpango wa Bajeti wa Mwaka wa Fedha 2026/2027, Wizara na taasisi zake kwa kushirikiana na wadau, utekelezaji wa jukumu mbalimbali kwa kuzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2050, Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa Miaka Mitano, Ilani ya uchaguzi wa Chama cha Mapinduzi, maelezo ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alipolihutubia Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Tarehe 14 Novemba, 2025, maelekezo ya hotuba ya Waziri Mkuu, Dkt. Lameck Mwigulu Nchemba kuhusu mwelekeo wa kazi za Serikali 2026/2027, Mpango Mkakati wa Wizara, Malengo ya Umoja wa Mataifa kuhusu maendeleo Endelevu ya Mwaka 2030, na sera, sheria, miongozo mbalimbali ya sekta ya habari, utamaduni, sanaa na michezo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na muda, ninaomba uniruhusu niende kwenye ukurasa wa 15.

Mheshimiwa Spika, kuelekea mashindano ya *AFCON* 2027 yatakayofanyika kuanzia tarehe 19 Juni hadi 17 Julai, 2027, Wizara imejipanga kikamilifu kwa kushirikiana na wadau wote kuhakikisha kwamba mashindano hayo siyo tu yanafanyika, bali yanaweka historia na alama isiyofutika kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, tayari tunazo Kamati mbalimbali za uratibu Kitaifa na Kimataifa. Katika hili, nimshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye ndiye Mwenyekiti wa Kamati Kuu ya Kitaifa ya Waheshimiwa Mawaziri wote kwa kushirikiana na wadau mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, pamoja na miundombinu iliyoelezwa hapo awali, tayari Serikali imewaunganisha pamoja wadau katika sekta ya utalii na ukarimu, hususan migahawa, hoteli na huduma za malazi, huduma za usafiri na usafirishaji; magari, treni, ndege, na meli. Utaendelea kuona namna ambavyo picha tulizoziandaa ndivyo ambavyo mwonekano wa maandalizi yetu na magari yetu ikiwa pamoja na ndege na treni zitakavyoweza kuonekana.

Mheshimiwa Spika, maeneo ya starehe na burudani kwa mashabiki *(fan zone)*, maboresho ya mwonekano wa miji yetu, vivutio vya utalii, mbuga, fukwe na malikale, matibabu ya kibingwa, ulinzi na usalama, uhamiaji na mikakati mahususi ya hamasa kuelekea *AFCON* 2027 imeandaliwa, ambapo itazinduliwa hivi karibuni.

Mheshimiwa Spika, ninakuhakikishia kuwa kila Mtanzania anakuwa sehemu ya mashindano haya kwa lengo la kunufaika na fursa za *AFCON* na kuitangaza Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hayo yote, tumeendelea kushirikiana na wadau na wanamichezo maarufu walioonekana kusaidia au kutoa mchango mkubwa kwa nchi zao na dunia katika soka. Hapa niruhusu nimtambulishe tena kwako na kwa Bunge lako Tukufu mwanamichezo maarufu Didier Drogba ambaye ni mchezaji bora wa wakati wote na nahodha wa zamani wa Timu ya Taifa ya *Ivory Coast*. Pia amewahi kuvitumikia vilabu vikubwa vya mpira wa miguu duniani ikiwemo Chelsea; na ni mmiliki wa klabu ya *Phoenix Rising* ya Marekani. Uwepo wake leo ni uthibitisho tosha kwa namna gani Serikali imeamua kuitumia *AFCON* 2027 kuitangaza taswira ya Tanzania Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, maelezo ya kina kuhusu mpango wa bajeti wa Wizara kwa mwaka 2026/2027 yanapatikana katika ukurasa wa 151 hadi 173 wa kitabu cha hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuhitimisha hotuba yangu, nitumie nafasi hii kuwashukuru wadau mbalimbali ambao kwa namna moja au nyingine wamechangia kufanikisha utekelezaji

wa majukumu ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo.

Mheshimiwa Spika, ushirikiano na misaada yao ya kifedha, kiufundi na kitaaluma imekuwa nguzo ya mafanikio yaliyopatikana katika mwaka 2025/2026. Wadau hao ni pamoja na nchi wahisani, mashirika mbalimbali ya Kimataifa, taasisi za fedha, vyombo vya habari, na taasisi za hiari zisizokuwa za kiserikali.

Mheshimiwa Spika, siyo rahisi kuwataja wote, lakini kwa upekee nitambue mchango wa kampuni ya Azam *Media* na leo tuko naye ndugu yetu, Bwana Yahya akiwa anawakilisha, na *MultiChoice Tanzania* katika kupeleka Kiswahili kwenye nchi zenye wazungumzaji wengi wa Kifaransa.

Mheshimiwa Spika, kwenye upande wa michezo, ni ukweli usiopingika ya kwamba Azam imetoa mchango mkubwa sana wa kukuza sekta ya michezo; na kwa kazi kubwa tunayoendelea kuifanya, tunao mpango wa kuwatambua kama wachangiaji wakubwa na wawezeshaji wa kuifanya Tanzania iendelee kuonekana.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hivyo, nimesema hapa Azam na nimesema *MultiChoice Tanzania*, hawa wametusaidia sana kufanya uwezekano wa Kiswahili chetu kuwa sehemu ya habari kwenye nchi zinazozungumza Kifaransa.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania *(TCRA),* Benki ya *NMB, CRDB, NBC,* Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote, Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania *(TFF),* 361 *Degrees Africa Limited,* Serikali ya Mji wa Busan nchini Korea Kusini, Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni *(UNESCO)* na Kituo cha Sanaa na Utamaduni cha *Alliance Française.*

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine tena nimshukuru sana kwa dhati ya moyo wangu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa maono yake,

maelekezo na miongozo yake katika utekelezaji wa majukumu ya sekta ya habari, utamaduni, sanaa na michezo.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii tunakiri kuwa tunadaiwa matokeo, na Mheshimiwa Rais amemaliza kazi yake. Nimhakikishie kuwa katika kipindi alichoniamini kusimamia majukumu haya, sitamwangusha. Watanzania tuendelee kumwombea kwa Mwenyezi Mungu Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, Mungu amjalie afya njema ili aendelee kutuongoza vyema.

Mheshimiwa Spika, niwashukuru viongozi wa dini wa madhehebu yote wanaoendelea kuliombea Taifa letu, na wengine leo wapo wakiongozwa na viongozi wa dini wa Mkoa wa Arusha. Tuko naye pia Kadhi wa Mkoa, tuko na Maaskofu ambao wamekuja kwa pamoja kuendelea kutuombea ikiwa ni sehemu ya kulinda amani na umoja wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, ninakishukuru tena Chama changu cha Mapinduzi chini ya Mwenyekiti Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kunipendekeza kuwa mgombea na hatimaye kuchaguliwa kwa kura nyingi na wananchi kuwa Mbunge wa Jimbo la Arusha Mjini. Ninaahidi kulipa imani hii kubwa kwa utumishi wenye matokeo chanya kwa chama changu cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine tena niwashukuru wananchi wa Jimbo la Arusha Mjini kwa ushirikiano wanaonipa katika utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya jimbo letu. Arusha tulichelewa sana, na sasa kutekeleza shughuli za msingi za maendeleo ni sasa. Wananchi wameamua kubadili sura ya Arusha kwa kufanya kazi. Ninawashukuru sana Waheshimiwa Madiwani wakiongozwa na Mheshimiwa Mstahiki Meya wa Jiji la Arusha na Madiwani wote wa Jiji la Arusha, wako humu ndani kwenye Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, kufika kwangu hapa leo wapo watu ambao Mwenyezi Mungu kwa kusudi lake aliwatumia katika namna moja au nyingine. Nilitamani wangekuwepo wakaona kazi waliyoifanya, lakini niruhusu tu kwa upendo mkubwa na kwa

kuwaheshimu nitambue sana mchango wa Hayati Samuel John Sitta, aliyekuwa Mbunge wa Urambo, na Spika wa Bunge la Tisa la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, aliyefanya kazi kubwa ya kunilea, na kunifundisha kazi kubwa ya uongozi.

Mheshimiwa Spika, niruhusu pia nitambue mchango wa Hayati Reginald Mengi, baba wa wengi aliyetoa mchango mkubwa katika maisha yangu, ikiwa ni pamoja na kulipa ada wakati ninasoma Chuo Kikuu. Ninaomba nitambue pia mchango wa Marehemu Bernard Membe, aliyekuwa Mbunge wa Mtama, na Waziri wa Mambo ya Nje, ambaye yeye naye pia ni miongoni mwa watu waliofanya kazi kubwa ya kunilea na kunifundisha kazi ya uongozi.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, leo tunaye kaka yangu Mheshimiwa Mwambalaswa akishirikiana na Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe ambao walifanya kazi kubwa ya kuwa makaka wa kunilea na kunifikisha hapa leo nilipofika. Matokeo haya tunayoyaona ya kazi nilizozifanya katika nafasi mbalimbali nilizopewa ni michango yao isiyosahaulika ndani ya moyo wangu na maisha yangu.

Mheshimiwa Spika, hotuba yangu leo itakuwa ni rahisi sana kutokana na matokeo ya jana. Wakati ninajiandaa kuja hapa Mheshimiwa Waziri Mkuu alinipigia simu akaniomba nisionyeshe furaha yangu kutokana na matokeo ya jana. Nami nikamwambia Mheshimiwa Waziri Mkuu kuwa, kwa matokeo ya jana sitaonyesha furaha yangu, lakini niruhusu nionyeshe furaha yangu ya matokeo ya Kombe la Muungano."

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa matokeo ya Kombe la Muungano yalimpa wakati mgumu Mheshimiwa Waziri Mkuu kulazimika kueleza uvumilivu ambao Simba wameendelea kuuonyesha, basi nimhakikishie Mheshimiwa Waziri Mkuu, nitasimamia vilabu vyote na kuhakikisha kwamba vinaleta ushindani sahihi na kuleta matokeo chanya ya kukuza mpira wetu wa miguu.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiopingika kwamba, utambuzi wa Wizara yetu katika mchango chanya uliotolewa na vilabu hivi viwili hauwezi kuepukika. Simba na Yanga wamekuwa nguzo ya mchezo wa mpira wa Tanzania na tunawaombea kila la heri katika uimarishaji wa uongozi wao ili waendelee kuwa mwalimu na kuleta fursa nyingi zaidi kwa timu zetu za ndani.

Mheshimiwa Spika, niishukuru familia yangu hususan mke wangu kipenzi Maria Felix Masenge na watoto wangu wote akiwepo Keagan Paul Makonda, Kenzel Paul Makonda na Kenzlin Paul Makonda ambao leo mke wangu ameniambia hatakuja kwenye Bunge, atabaki kuliinua Jina la Bwana ili kazi hii ifanywe kwa utukufu mkubwa.

Mheshimiwa Spika, pia ninao watoto ambao ninawalea akiwepo Tina na wengine ambao wapo pale nyumbani wanaoendelea kuomba kuhakikisha kwamba baba yao anaifanya kazi iliyokamilika. Ninafahamu ya kwamba mchango wa wadada hawa, tena wadada wa kazi ambao wananipa chakula, lakini wako kwenye mfungo kumwombea baba yao wakiongozwa na dada yao Ella ili nifanye kazi ya utukufu wa Mungu katika mimbari hii.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kutoa shukrani zangu za dhati kwako binafsi, Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wenyeviti wa Bunge na Waheshimiwa Wabunge na wananchi wote kwa kunisikiliza.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sasa niruhusu nihitimishe.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2026/2027 Wizara inatarajia kukusanya jumla ya shilingi 1,058,000,000. Aidha, kwa upande wa taasisi 12 zilizopo chini ya Wizara, kiasi kinachotarajiwa kukusanywa ni shilingi 40,898,692,000.

Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza majukumu ya Wizara katika Mwaka wa Fedha 2026/2027, ninaomba Bunge lako Tukufu liridhie na kuidhinisha Bajeti ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na

Michezo kwa Mwaka 2026/2027 yenye jumla ya shilingi 525,327,457,000. Kati ya bajeti hiyo shilingi 39,071,597,000 ni kwa ajili ya mishahara, shilingi 28,065,472,000 ni matumizi mengineyo, na miradi ya maendeleo shilingi 458,190,778,000.

Mheshimiwa Spika, kwa unyenyekevu mkubwa ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**HOTUBA YA MHESHIMIWA PAUL CHRISTIAN MAKONDA (MB.), WAZIRI WA ABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO, AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2026/27 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

## 1.0 UTANGULIZI

**1.** ***Mheshimiwa Spika,*** kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo iliyochambua Bajeti ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo katika Bunge lako Tukufu, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupokea, kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo (Fungu 96) kwa mwaka wa Fedha 2026/27.

**2.** ***Mheshimiwa Spika,*** awali ya yote, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kuendelea kutupatia uhai, afya njema na kutuwezesha kukutana tena siku ya leo kujadili ustawi wa sekta za habari, utamaduni, sanaa na michezo. Tuendelee kumwomba Mwenyezi Mungu atuongoze katika kujadili hotuba hii ya bajeti kwa dhamira ya kuhakikisha Sekta za Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo zinakuwa na mchango mkubwa katika maendeleo na ustawi wa Taifa letu.

**3.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa unyenyekevu mkubwa nitumie fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniamini na kuniteua kwanza, kuwa Naibu Waziri na baadaye Waziri kamili wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo. Hii ni heshima kubwa sana

kwangu na kwa familia yangu na naichukulia kama chachu ya kuendelea kulitumikia Taifa hili kwa bidii, weledi na uadilifu mkubwa. Ninamwahidi utumishi uliotukuka katika kuzisimamia sekta za habari, utamaduni, sanaa na michezo. Sekta hizi ni za kimageuzi, zikisimamiwa vizuri zitazalisha ajira kwa vijana. Hili litakuwa lengo langu katika kipindi chote nikiwa katika nafasi hii. Kama alivyosema Mheshimiwa Rais wakati ananiapisha, VIJANA TUNAELEWANA NA TUTAKWENDA PAMOJA.

**4.*Mheshimiwa Spika,*** niruhusu nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muuungano wa Tanzania, kwa uongozi wake mahiri na maono mapana yanayolenga kuleta maendeleo kwa mwananchi mmoja mmoja na uchumi wa Taifa kwa ujumla. Pia, nimpongeze kwa kuendelea kuliongoza Taifa vyema katika kipindi hiki ambacho dunia inakabiliwa na changamoto mbalimbali, hususan migogoro ya vita ya Mashariki ya Kati na vita ya Urusi na Ukraine ambayo imeathiri kwa kiasi kikubwa uchumi wa dunia, ikiwemo kupanda kwa bei za mafuta na bidhaa mbalimbali. Pamoja na changamoto hizo, Mheshimiwa Rais ameendelea kutuongoza kama Taifa kubaki katika umoja, mshikamano na amani.

**5.*Mheshimiwa Spika,*** naomba nichukue fursa hii ya kuwapongeza Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuchaguliwa kwake kwa awamu nyingine ya pili, na Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuteuliwa kwake kushika nafasi hiyo. Aidha, nawapongeza viongozi hawa wote kwa kutekeleza majukumu yao kwa weledi na ufanisi mkubwa katika kumsaidia Mheshimiwa Rais. Viongozi hawa wamekuwa chachu na msaada kwa Mheshimiwa Rais kwa kutupatia maelekezo pamoja na ushauri unaosaidia kuboresha sekta za habari, utamaduni, sanaa na michezo. Ninawashukuru na kuwapongeza sana.

**6.*Mheshimiwa Spika,*** nizidi kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa Hotuba yake ya Bajeti iliyotoa utekelezaji wa malengo ya Serikali katika mwaka 2025/26 na mwelekeo wa shughuli za Serikali kwa mwaka 2026/27. Pamoja na masuala mengine hotuba hiyo imetoa maelezo kuhusu Sekta zilizo chini ya Wizara. Wizara yangu imezingatia na itatekeleza maelekezo yote yaliyotolewa.

**7.*Mheshimiwa Spika,*** kipekee naomba nikupongeze wewe Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu (Mb.), Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuliongoza kwa busara na weledi mkubwa Bunge la 13 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Maelekezo na miongozo yako imekuwa msingi wa ufanisi mkubwa wa Bunge katika kuisimamia Serikali kutekeleza vema majukumu yake. Vilevile, ninampongeza Mheshimiwa Daniel Baran Sillo (Mb.), Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kukusaidia na kukushauri vema katika majukumu yako ya kuliongoza Bunge. Nawapongeza sana Wenyeviti wa Bunge, Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika (Mb.), Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso (Mb.) na Mheshimiwa Najima Murtaza Giga (Mb.) kwa kusimamia vema na kwa ustadi mkubwa mijadala katika Bunge lako Tukufu.

**8.*Mheshimiwa Spika,*** nichukue fursa hii kuishukuru kwa dhati Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko (Mb.), na Mheshimiwa Cornel Lucas Magembe (Mb.), Makamu Mwenyekiti wa Kamati pamoja na wajumbe wote wa Kamati kwa maelekezo, ushauri na maoni yao kwa Wizara yangu ambayo yametusaidia sana katika kuboresha utendaji kazi. Maelekezo yao yamesaidia kwa kiwango kikubwa katika uwasilishaji wa hotuba hii mbele ya Bunge lako Tukufu. Kamati hii imekuwa nguzo muhimu katika usimamizi madhubuti wa utekelezaji wa bajeti na ukaguzi wa miradi, ambapo imefanikisha kuhakikisha rasilimali za umma zinatumiwa kwa ufanisi na kwa manufaa ya umma. Kama misingi ya nyumba imara, ndivyo uongozi wa Kamati hii ulivyojenga msingi madhubuti wa maendeleo, unaoleta mafanikio endelevu na mabadiliko chanya katika jamii yetu.

**9.** ***Mheshimiwa Spika***, pia, nitumie fursa hii kuwashukuru waheshimiwa wabunge wote kwa maoni, ushauri na maelekezo ambayo yamekuwa yakiisaidia Wizara kuboresha vipaumbele, mikakati na pia kuweka msingi imara wa utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa ufanisi zaidi.

**10.** ***Mheshimiwa Spika,*** ni masikitiko yangu kwamba katika kipindi cha mwaka 2025/26 Bunge lako Tukufu lilipatwa na misiba mbalimbali ya Waheshimiwa Wabunge. Misiba hiyo ni pamoja na msiba wa Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi, aliyekuwa Mbunge wa Isimani na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu, Mheshimiwa Jenista Joachim Mhagama aliyekuwa Mbunge wa jimbo la Peramiho, na Mheshimiwa Halima Idd Nassor aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalumu akiwawakilisha Wafanyakazi. Kwa niaba ya Wizara na wadau wetu, tunatoa pole kwako Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge, familia za marehemu, ndugu, jamaa na marafiki na watanzania wote kwa ujumla. Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi. Amina.

**11.** ***Mheshimiwa Spika,*** mafanikio yaliyopatikana katika kipindi chote hiki ni kutokana na ushirikiano mzuri miongoni mwa wadau wa Wizara wakiwamo viongozi, watumishi na washirika wa maendeleo. Natambua mchango wao mkubwa wanaoutoa kwa Wizara ambao umeleta matunda ninayojivunia mbele ya Bunge lako Tukufu leo hii.

**12.** ***Mheshimiwa Spika,*** niruhusu kwa dhati ya moyo wangu nimshukuru Mheshimiwa Hamis M. Mwinjuma (Mb.), Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa ushirikiano na msaada mkubwa anaonipa katika kutekeleza majukumu ya Wizara. Aidha, nimshukuru Bw. Gerson P. Msigwa, Katibu Mkuu; Bw. Methusela S. Ntonda, Naibu Katibu Mkuu; Wakuu wa Idara na Vitengo; Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara; na watumishi wote wanaofanya kazi kwa bidii na wanaohakikisha mipango ya Wizara inatekelezwa kama ilivyopangwa. Rai yangu ni kuwa tuendeleze ushirikiano huu.

**13.** ***Mheshimiwa Spika,*** pia, niwashukuru Washirika wa Maendeleo na wadau wengine ikiwa ni pamoja na mashirika ya kimataifa, mashirikisho, vyama, vilabu na kila mdau kwa nafasi yake katika Sekta za Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa kuhakikisha Sekta hizi zinakua na kufanikisha malengo yaliyokusudiwa kwa mujibu wa sera.

**14.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninawashukuru wapiga kura wangu wananchi wa Jimbo la Arusha Mjini kwa kuniamini na kunipigia kura nyingi. Pia, kwa kunipatia ushirikiano mkubwa wakati wa utekelezaji wa majukumu yangu; na wakati wa kukabiliana na changamoto mbalimbali zinazokabili jimbo letu la Arusha. Ushirikiano wenu kwangu, moyo wa uzalendo, na utayari wenu ni nguzo kuu katika kulipatia maendeleo jimbo letu la Arusha Mjini. Naomba wananchi wa Arusha waendelee kuniamini kwani nitaendelea kuwa mtumishi wao ambaye nitawatumikia kwa uadilifu mkubwa.

**15.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara hii ni mhimili kwa maendeleo ya jamii na Taifa kwa ujumla, ambayo kwa maneno mengine naweza kusema ni Wizara yenye nguvu shawishi (***soft power***) ya nchi inayobeba Taifa letu na kulitambulisha kwa Mataifa. Sekta ya habari imekuwa na mchango mkubwa katika kuhabarisha, kuelimisha, kuburudisha na kuhakikisha kuwa wananchi wanapata taarifa muhimu zinazowawezesha kushiriki kikamilifu katika maendeleo ya nchi yetu. Aidha, utamaduni wetu ni uti wa mgongo wa Taifa letu. Hivyo, kupitia sekta ya utamaduni Serikali imeendelea kujenga uzalendo, kuhifadhi mila na desturi pamoja na maadili ya Mtanzania.

**16.** ***Mheshimiwa Spika***, sekta za habari, utamaduni, sanaa na michezo zimeendelea kutoa mchango mkubwa katika uchumi wa nchi hususan kwenye ukuaji na mchango wa shughuli za kiuchumi katika pato la Taifa. Mathalani kwa mwaka 2024 sekta za sanaa na burudani ziliongoza kwa kukua kwa asilimia 17.1. Kwa upande wa mchango wa shughuli za kiuchumi katika pato la Taifa, sekta hizi, zilichangia kwa wastani wa asilimia 0.4. Hii inadhihirisha wazi kuwa sekta hizi ni vichocheo vya uchumi hususan kwenye sekta nyingine za kiuchumi kama vile utalii,

huduma za malazi na fedha.

**17.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mujibu wa taarifa ya Hali ya Uchumi kwa mwaka 2024, shughuli za habari na mawasiliano zilikua kwa asilimia 14.3 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 7.6 mwaka 2023. Aidha, mchango wa shughuli za Habari na mawasiliano katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 1.6 mwaka 2024 ikilinganishwa na asilimia 1.5 mwaka 2023.

**18.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa sekta ya sanaa, imekuwa na nafasi kubwa katika uzalishaji wa ajira hususan kwa vijana. Aidha, wasanii wetu wameendelea kuwa mabalozi wa nchi yetu ndani na nje ya mipaka yetu. Michezo nayo ni kiungo muhimu katika kujenga fahari ya maendeleo ya Taifa letu. Michezo siyo burudani tu, bali pia ni nyenzo ya kuimarisha afya, umoja na mshikamano wa taifa na ni chanzo cha ajira kwa vijana wetu.

**19.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa muktadha huo Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuona umuhimu wa sekta hizi hususan ni michezo inafanya uwekezaji mkubwa unaolenga kuibadili kabisa Tanzania katika ramani ya michezo. Mheshimiwa Rais amewekeza zaidi ya shlingi trilioni 1.2 katika michezo ikiwa ni sehemu ya kuifanya Tanzania kuwa mwenyeji wa AFCON 2027. Uwekezaji huo upo katika timu za Taifa, uendeshaji wa michezo pamoja na miundombinu ya michezo ikiwemo ujenzi wa viwanja vya mpira wa miguu katika Jiji la Arusha na Dodoma, ujenzi wa Akademia ya Michezo katika Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya, ujenzi wa vituo vya michezo na kupumzikia wananchi jijini Dar es Salaam na Dodoma, na ujenzi wa viwanja vidogo (vya mazoezi) kumi na moja (11) ikiwa vitano (5) Arusha na sita (6) Dar es Salaam.

**20.** ***Mheshimiwa Spika,*** hotuba hii imezingatia maelekezo ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alipohutubia Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 14 Novemba, 2025; Hotuba ya Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb.), Waziri Mkuu

wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu Mapitio ya Utekelezaji wa Kazi za Serikali kwa Mwaka 2025/26 na Mwelekeo wa Kazi za Serikali kwa Mwaka 2026/27 aliyoiwasilisha hapa Bungeni tarehe 01 Aprili, 2026; Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050; Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2026/27 - 2030/31); Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (2025 - 2030); Mpango Mkakati wa Wizara (2026/27 - 2030/31); na sera, sheria na miongozo mbalimbali ya Sekta za Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo; na maelekezo mbalimbali ya viongozi wakuu wa Serikali.

**21.** ***Mheshimiwa Spika,*** hotuba yangu imegawanyika katika sehemu saba (7): Sehemu ya Kwanza ni Utangulizi; Sehemu ya Pili ni Dira, Dhima, Majukumu, Misingi ya Mwelekeo, na Vipaumbele vya Wizara na taasisi zinazosimamiwa na Wizara; Sehemu ya Tatu inaelezea Mapitio ya Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara kwa Kipindi cha Mwaka 2025/26 na Sehemu ya Nne inabainisha changamoto zilizojitokeza na hatua zilizochukuliwa ili kuzipatia ufumbuzi. Aidha, Sehemu ya Tano ni Mpango na Bajeti ya Wizara kwa Mwaka 2026/27; Sehemu ya Sita Shukrani; na Sehemu ya Saba ni Hitimisho.

## 2.0 DIRA, DHIMA, MAJUKUMU, MISINGI YA MWELEKEO NA VIPAUMBELE VYA WIZARA NA TAASISI ZILIZO CHINI YA WIZARA

**22.** ***Mheshimiwa Spika,*** Dira ya Wizara ni "*Kuwa na Taifa linalohabarishwa kikamilifu, linaloshamirika kiutamaduni, lenye kazi bora za sanaa na lenye umahiri katika michezo*" na dhima ni ***"****Kuendeleza utambulisho wa Taifa kwa kuwezesha upatikanaji stahiki wa habari, kukuza utamaduni, sanaa na michezo kwa lengo la kuleta maendeleo ya jamii kiuchumi.****"***

**23.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kufikia Dira ya Wizara, majukumu ya msingi ya Wizara ni pamoja na: kuandaa na kusimamia utekelezaji wa Sera, Sheria, Mipango, Miradi na Programu mbalimbali katika Sekta za Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo; kuendeleza shughuli za Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo; na kusimamia shughuli za filamu na michezo ya kuigiza. Majukumu mengine ni kuimarisha utendaji na Rasilimaliwatu wizarani na kusimamia

utendaji wa Taasisi zilizo chini ya Wizara ambazo ni Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC), Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN), Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA), Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA), Bodi ya Filamu Tanzania (TFB), Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSUBa), Ofisi ya Hakimiliki Tanzania (COSOTA), na Baraza la Michezo la Taifa (BMT). Vilevile, Wizara inaratibu na kusimamia Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya, Kituo cha Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika, Bodi ya Ithibati Tanzania na Mfuko wa Utamaduni na Sanaa Tanzania. Aidha, Wizara inaratibu Kamati ya Maudhui ambayo Kimuundo ipo chini ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) katika Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari.

**24. *Mheshimiwa Spika*,** katika kutekeleza na kuimarisha utendaji kazi, Wizara inaongozwa na misingi mitano (5) ya kimkakati na kimageuzi ambayo ni Kuwafikia Wadau *(Outreach Programmes)*; Mageuzi ya Taasisi *(Institutional Reforms)*; Utawala Bora *(Good Governance)*; Ujenzi wa Miundombinu *(Infrastructure Development)*; na Utafutaji wa Rasilimali *(Resources Mobilization)*.

**25. *Mheshimiwa Spika*,** chini ya misingi hiyo, katika mwaka 2026/27, Wizara imejipanga kutekeleza maeneo mbalimbali ya kipaumbele. Maeneo hayo ni pamoja na:-

(i) Kukamilisha kukarabati, kuboresha, kujenga na kuendelea kutunza miundombinu katika sekta za habari, utamaduni, sanaa na michezo;

(ii) Kukamilisha maandalizi ya Tanzania kuwa mwenyeji wa mashindano ya AFCON 2027 yatakayofanyika Juni hadi Julai 2027;

(iii) Tanzania kuwa mwenyeji wa Mashindano ya 74 ya Urembo ya Dunia (Miss World);

(iv) Kukamilisha kutunga na kuhuisha Sera, Sheria, mikakati, miongozo na kanuni mbalimbali katika kuimarisha usimamizi na utekelezaji katika sekta za Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo;

(v) Kuimarisha na kustawisha kiswahili kikanda na kimataifa;

(vi) Kuimarisha, kuziwezesha na kufanikisha ushiriki wa timu za Taifa katika mashindano mbalimbali ya Kimataifa;

(vii) Kuboresha elimu na mafunzo katika tasnia za utamaduni, sanaa na michezo;

(viii) Kuweka na kuboresha mazingira wezeshi na kuimarisha ushiriki wa sekta binafsi katika kukuza na kuendeleza sekta za Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo; na

(ix) Kuratibu, kuendesha na kusimamia matamasha, shughuli na matukio makubwa ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo.

**26.** ***Mheshimiwa Spika***, maeneo mengine ni kuziimarisha na kuziongezea uwezo taasisi zilizo chini ya Wizara ili ziweze kusimamia na kutekeleza majukumu ya Sekta za Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo; kuimarisha ushirikiano na Wizara nyingine katika utendaji kazi hususan zile zinazohusika na masuala ya Kazi na Ajira, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Elimu, Afya, Maliasili na Utalii, Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki; na kuimarisha ushirikiano na wadau mbalimbali wa maendeleo ikiwamo Sekta Binafsi katika maendeleo kwa kufadhili na kusukuma mbele gurudumu la Sekta za Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo.

## 3.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU KWA KIPINDI CHA MWAKA 2025/26

### 3.1 MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA

#### 3.1.1 Ukusanyaji wa Maduhuli

**27.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2025/26, Wizara ilikadiria kukusanya shilingi Bilioni Moja na Milioni Thelathini na Sita Elfu (shilingi 1,036,000,000) kutoka kwenye vyanzo sita (6) ambavyo ni mapato yatokanayo na viwanja vya Benjamin

Mkapa na Uhuru; ada za mafunzo na mitihani kutoka Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya; vitambulisho vya waandishi wa habari; machapisho ya picha, mabango na majarida; usajili wa magazeti; na ada ya mwaka ya magazeti.

**28.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufika mwezi Aprili 2026 shilingi Milioni mia sita tisini na tisa, laki saba na sita elfu, tisini na tatu (shilingi 699,706,093), sawa na asilimia 67.5 ya lengo la mwaka zilikuwa zimekusanywa. Miongoni mwa sababu za kutofikia kwa lengo ni pamoja na kupungua kwa matukio katika viwanja vya Benjamin Mkapa na Uhuru kutokana na kufungwa kulikotokana na ukarabati unaoendelea katika viwanja hivyo.

**29.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Wizara inaendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ya kuongeza makusanyo ya maduhuli ikiwamo kufanya ukarabati mkubwa wa miundombinu ya viwanja, ili kuwezesha kuvutia mashabiki wengi zaidi; kuongeza hamasa katika michezo ikiwemo zawadi mbalimbali kwa washindi ili kuhamasisha matokeo mazuri yatakayochochea ushabiki na hatimaye mapato.

**30.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa Taasisi zilizo chini ya Wizara, kiasi kilichokadiriwa kukusanywa ni shilingi Bilioni Arobaini, Milioni Mia Mbili Tisini na Tano, Mia Moja Tisini na Mbili Elfu (shilingi 40,295,192,000), ambapo hadi mwezi Aprili 2026, shilingi Bilioni Kumi na Saba, Milioni Ishirini, Sitini na Tatu Elfu na Mia Sita Themanini na Nne (shilingi 17,020,063,684), sawa na asilimia 42 ya lengo zilikuwa zimekusanywa. Miongoni mwa sababu zilizochangia kutofikiwa kwa malengo ni pamoja na baadhi ya taasisi kushindwa kulipa kwa wakati huduma za matangazo zilizotolewa na taasisi zilizo chini ya Wizara ikiwemo TSN na TBC. Kwa upande wa vyuo, moja ya sababu ni wanavyuo kutokulipa ada kwa wakati kutokana na changamoto mbalimbali.

**31.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Taasisi inaendelea kutoa elimu kwa wadau na kufanya kampeni mbalimbali ili kuweza kukabiliana na changamoto hizo. Kampeni hizo ni pamoja na kuhamasisha usajili na kufuata taratibu za uzalishaji na usambazaji wa kazi za sanaa; kuongeza kasi ya kuibua vyanzo vipya vya

mapato kwa taasisi; utekelezaji wa mabadiliko ya Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki Sura ya 218 na kuhamasisha wanavyuo kulipa ada kwa wakati.

### 3.1.2 Bajeti ya Matumizi ya Wizara na Mtiririko wa Fedha

**32.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2025/26, Wizara iliidhinishiwa bajeti yenye jumla ya shilingi Bilioni Mia Tano Kumi na Tisa, Milioni Mia Sita Sitini, na Sabini na Tatu Elfu (shilingi 519,660,073,000). Kati ya fedha hizo, Mishahara ni shilingi Bilioni Thelathini na Tatu, Milioni Mia Nne na Tatu, Mia Nane Kumi na Tatu Elfu (shilingi 33,403,813,000), Matumizi Mengineyo ni shilingi Bilioni Ishirini na Nane, na Milioni Sitini na Tano, Mia Nne Sabini na Mbili Elfu (shilingi 28,065,472,000) na Miradi ya Maendeleo ni shilingi Bilioni Mia Nne Hamsini na Nane, Milioni Mia Moja Tisini, Mia Saba Themanini na Nane Elfu (Shilingi 458,190,788,000).

**33.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi mwezi Aprili 2026, Wizara ilikuwa imepokea jumla ya shilingi Bilioni Mia Tatu Hamsini na Mbili, Milioni Mia Tisa Arobaini na Mbili, Mia Nne Hamsini na Nne Elfu, Mia Nne Sabini na Mbili na Senti Tisini na Saba (shilingi 352,942,454,472.97) sawa na asilimia 67.9 ya bajeti yote. Kati ya fedha zilizopokelewa, Mishahara ilikuwa shilingi Bilioni Ishirini na Saba, Milioni Mia Sita Themanini na Nne, Mia Tano Arobaini na Nne Elfu, Mia Moja Hamsini na Nane na Senti Tisini (shilingi 27,684,544,158.90) sawa na asilimia 82.9 ya bajeti ya Mishahara; Matumizi Mengineyo ni shilingi Bilioni Ishirini, Milioni Mia Tisa Ishirini na Tano, Mia Tano Sitini na Sita Elfu, Mia Mbili Thelathini na Tatu na Senti Themanini na Moja (shilingi 20,925,566,233.81) sawa na asilimia 74.6 ya bajeti ya Matumizi Mengineyo; na Miradi ya Maendeleo ni shilingi Bilioni Mia Tatu na Nne, Milioni Mia Tatu Thelathini na Mbili, Mia Tatu Arobaini na Nne Elfu, Themanini na Senti Ishirini na Sita (shilingi 304,332,344,080.26) sawa na asilimia 66.4 ya bajeti ya Miradi ya Maendeleo.

## 3.2 UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA KWA MWAKA 2025/26

### 3.2.1 SEKTA YA HABARI

**34.** ***Mheshimiwa Spika***, majukumu ya Sekta ya Habari ni pamoja na kuratibu, kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa Sera ya Habari na Utangazaji ya Mwaka 2003; Sheria ya Huduma za Habari Sura ya 229 na kuisemea Serikali kuhusu utekelezaji wa sera, mikakati, programu na miradi mbalimbali inayotekelezwa na Serikali ya kuwaletea wananchi maendeleo. Wizara kupitia sekta hii imetekeleza majukumu yafuatayo:

#### 3.2.1.1 IDARA YA HABARI

**35.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kuratibu, kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa Sera ya Habari na Utangazaji ya mwaka 2003; Sheria ya Huduma za Habari Sura ya 229 na kuisemea Serikali kuhusu utekelezaji wa sera, mikakati, programu na miradi mbalimbali inayotekelezwa na Serikali ya kuwaletea wananchi maendeleo. Wizara kupitia sekta hii imetekeleza majukumu yafuatayo:

**36.** ***Mheshimiwa Spika,*** sekta ya habari imeendelea kuwa kichocheo muhimu cha ukuaji wa uchumi nchini kwa kuibua, kukuza vipaji, ajira na kuhakikisha upatikanaji wa taarifa sahihi na kwa wakati. Kwa kutambua umuhimu huo, Wizara kupitia Idara ya Habari na Msemaji Mkuu wa Serikali imeendelea kuisemea Serikali kwa kutoa taarifa mbalimbali kuhusu utekelezaji wa miradi ya maendeleo nchini. Hatua hii imelenga kuwapatia wananchi taarifa sahihi na za uhakika kuhusu mafanikio yanayopatikana, pamoja na hatua zinazochukuliwa na Serikali katika kuboresha huduma za kijamii na kukuza uchumi wa Taifa.

**37.** ***Mheshimiwa Spika,*** kupitia jitihada hizi, wananchi wameendelea kufahamishwa kuhusu juhudi za Serikali katika kukuza uchumi na kuimarisha uwekezaji, hususan katika miundombinu ya usafiri ikiwemo reli, barabara, maji na anga. Maboresho haya yameiweka Tanzania katika nafasi nzuri ya ushindani, kikanda na kimataifa. Baadhi ya miradi ambayo imekuwa ikitolewa taarifa kwa umma ni pamoja na maendeleo

ya ujenzi na uendeshaji wa huduma za treni ya kisasa ya SGR; ukarabati mkubwa wa reli ya TAZARA; pamoja na miradi ya kuboresha na kuongeza uwezo wa viwanja vya ndege ili kuhudumia abiria na mizigo kwa ufanisi zaidi. Aidha, Serikali imeendelea kuwekeza katika upanuzi na uboreshaji wa bandari za Dar es Salaam, Mwanza, Tanga, Mtwara, Bukoba na Kigoma, hatua inayochochea biashara na kukuza uchumi wa Taifa.

**38.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Wizara imeisemea Serikali kuhusu kukamilika kwa mradi wa ujenzi wa daraja la JP Magufuli (Kigongo – Busisi) mkoani Mwanza ambalo limekua mkombozi kwa wananchi na wafanyabiashara wa mikoa ya kanda ya ziwa na nchi jirani. Aidha, imeisemea Serikali kuhusu kukamilika kwa mradi wa ujenzi wa meli ya MV Mwanza; miradi ya ukarabati wa vivuko na uimarishaji wa huduma za usafirishaji wa abiria na mizigo katika Ziwa Viktoria, Tanganyika, Nyasa na Bahari ya Hindi; mradi wa ujenzi wa maghala ya kuhifadhia dawa ya Bohari ya Dawa (MSD) Kanda ya Kati Dodoma; juhudi za Serikali kukuza sekta ya utalii; na taarifa kuhusu kuimarika kwa uzalishaji wa umeme kulikochangiwa na ufanisi wa Bwawa la kuzalisha umeme la Julius Nyerere (JNHPP).

**39.** ***Mheshimiwa Spika,*** mbali na Msemaji Mkuu wa Serikali kuwaeleza wananchi mafanikio ya utekelezaji wa miradi hiyo, ameendelea kutoa ufafanuzi kuhusu masuala mbalimbali yanayoendelea nchini. Miongoni mwa masuala hayo yanahusu maandalizi ya Tanzania kwa kushirikiana na Kenya na Uganda kuwa mwenyeji wa Mashindano ya AFCON 2027 ambapo Serikali chini ya uongozi imara wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaendelea kutekeleza miradi mikubwa ya ujenzi na ukarabati wa viwanja vya michezo katika jiji la Dar es salaam na Arusha. Aidha, Wizara kupitia Msemaji Mkuu wa Serikali kwa nyakati tofauti imekuwa ikiwaeleza wananchi kuhusu mpango wa Serikali wa kuendelea kuimarisha sekta ya anga kwa kununua ndege mpya kupitia Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL); na manufaa ya mradi wa bomba la mafuta ghafi kutoka Uganda kwenda Tanga.

**40.** ***Mheshimiwa Spika,*** miradi mengine ni ujenzi wa soko kuu

Mwanza ambalo sasa linatumiwa na wafanyabiashara; Wizara kuhamia na kuanza kutumia majengo mapya katika Mji wa Serikali Mtumba; kuanza kwa mradi wa ujenzi wa matanki matano yatakayosambaza maji kwenye maeneo mbalimbali ya Jiji la Mwanza; kukamilika kwa Mradi wa Shule ya Wasichana Shelukindo mkoani Tanga na mradi wa ujenzi wa daraja jipya la Pangani mkoani Tanga. Vilevile taarifa zimetolewa kuhusu uboreshaji wa Huduma za Matibabu ya Kibingwa na Ubingwa Bobezi nchini katika ngazi ya Hospitali za Rufaa na Kanda zikiwemo Hospitali ya Taifa Muhimbili, Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), Hospitali ya Benjamin Mkapa, na Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI).

**41.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile Wizara imehabarisha umma kuhusu uwekezaji maalumu wenye kulenga kukuza na kutoa ajira kwa vijana kupitia mfumo wa vijana na kukuza viwanda kupitia kongani maalumu za uwekezaji (TISEZA) ambao umerahisisha taratibu, kupunguza urasimu, na kuvutia miradi itakayoongeza ajira na ujuzi kwa vijana. Mwelekeo huu unaenda sambamba na hatua za Serikali za kuendeleza programu za uwekezaji zinazoweka vijana katikati, ikiwemo uanzishaji wa mikakati ya vijana kumiliki na kuendesha miradi ya uzalishaji.

**42.** ***Mheshimiwa Spika***, hatua hizi zimeendelea kusaidia kuongeza uelewa wa wananchi kuhusu utekelezaji wa miradi ya kimkakati, sambamba na kuimarisha uwazi na mawasiliano kati ya Serikali na umma. Wizara imeendelea kuratibu ziara za waandishi wa habari kwenda kutembelea na kujionea miradi mbalimbali ya maendeleo inayotekelezwa na Serikali ya Awamu ya Sita. Kupitia ziara hizo, waandishi wa habari wamepata fursa ya kuona kwa karibu utekelezaji wa miradi hiyo, hivyo kupata uelewa wa kutosha unaowawezesha kutoa taarifa sahihi na uhakika kwa ajili ya kujenga uelewa kwa umma, kuimarisha uwazi na uwajibikaji wa Serikali kwa wananchi.

**43.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuendelea kujenga uaminifu kwa umma na kuzuia kusambaa kwa taarifa zisizo sahihi ambazo zimekua na athari hasi kwenye jamii yetu, Wizara kupitia Idara ya Habari-MAELEZO imeendelea kuratibu na kuandaa mikutano ya

Msemaji Mkuu wa Serikali na vyombo vya habari kwa lengo la kuhabarisha umma kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Serikali ya Awamu ya Sita. Katika kipindi cha kuanzia Julai 2025 hadi Aprili 2026, Wizara imefanikiwa kuandaa mikutano 22. Kupitia mikutano hii, wizara kupitia Idara ya Habari na Msemaji Mkuu imetoa ufafanuzi kuhusu masuala mbalimbali yenye maslahi kwa umma, sambamba na kuwakumbusha waandishi wa habari wa ndani na nje ya nchi kuzingatia maadili ya taaluma ya uandishi wa habari na utangazaji kwa kuhakikisha wanathibitisha taarifa kabla ya kuzichapisha au kuzitangaza kupitia vyombo vyao vya habari na mitandao ya kijamii ili kuepuka kutoa taarifa zisizo rasmi zinazoweza kuchochea taharuki na kuvuruga amani katika jamii.

**44.** ***Mheshimiwa Spika***, habari za uzushi zisipodhibitiwa zinaweza kuleta madhara makubwa kwenye jamii ikiwemo kuharibu heshima ya watu kwenye jamii, kupotosha ufanyaji maamuzi, kuharibu uchumi na biashara na kuchochea unyanyasaji mtandaoni. Wizara kupitia Idara ya Habari-MAELEZO na Bodi ya Ithibati ya Waandishi wa Habari kwa nyakati tofauti imekua ikihimiza wananchi na wadau wa sekta ya habari kuepuka kusambaza habari ambazo hazijathibitishwa. Pia, imekua ikishirikiana na taasisi nyingine za Serikali likiwemo Jeshi la Polisi na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) kutoa elimu kwa wadau wa tasnia ya habari na wananchi kwa ujumla namna ya kujilinda dhidi ya taarifa potofu, uzushi, uhalifu na ulaghai mitandaoni na kuwahimiza wananchi kuongeza umakini katika matumizi ya mitandao, kuepuka kusambaza taarifa hizo, na kuzifuta pindi wanapozipokea kupitia mitandao ya kijamii.

**45.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuendelea kukabiliana na wimbi la taarifa za upotoshaji na ongezeko la mitandao isiyo rasmi na matumizi mabaya ya akili unde, Wizara kupitia Idara ya Habari-MAELEZO na Msemaji Mkuu wa Serikali imeratibu na kuendesha zoezi la urasimishaji na uthibitisho wa akaunti za mitandao ya kijamii za Wizara, mikoa, taasisi, wakala, Halmashauri na mashirika ya Serikali. Lengo la zoezi hili ni kulinda usalama wa taarifa na kuimarisha utambulisho rasmi wa taasisi za Serikali ambapo kupitia zoezi hilo, jumla ya akaunti 412 za mtandao wa Instagram; 200 za mtandao wa Facebook; na zaidi ya 300 za mtandao wa X

zamani Twitter zimethibitishwa. Hatua hii imesaidia kulinda taswira na kuongeza uaminifu wa taarifa zinazotolewa na Serikali kupitia majukwaa hayo. Kwa ujumla, juhudi hizi zinaonesha dhamira thabiti ya Serikali ya kuhakikisha wananchi wanapata taarifa kutoka vyanzo sahihi na kwa wakati, huku ikiendelea kulinda maslahi ya Taifa.

**46.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuhakikisha wananchi wanaendelea kupata taarifa sahihi kuhusu mambo mbalimbali yanayofanywa na Serikali, Wizara kupitia Idara ya Habari-MAELEZO, imeratibu mikutano ya taasisi za Serikali kuzungumza na waandishi wa habari ambapo katika kipindi cha Julai hadi Aprili, 2026, Wizara imeratibu na kufanikisha mikutano 30. Aidha, Wizara iliratibu mikutano 15 ya Waheshimiwa Mawaziri kuelezea utekelezaji wa majukumu na utekelezaji wa ahadi za Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha siku 100 za muhula wa pili wa Serikali ya Awamu ya Sita. Wizara zilizoshiriki katika mikutano hiyo ni pamoja na Wizara ya Viwanda na Biashara; Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Makundi Maalumu; Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia; Ofisi ya Rais – Maendeleo ya Vijana; Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; pamoja na Ofisi ya Rais – Mipango na Uwekezaji. Wizara nyingine ni Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari; Wizara ya Maji; Wizara ya Madini; Wizara ya Uchukuzi; na Wizara ya Afya. Hatua hizi zimeendelea kuimarisha mawasiliano kati ya Serikali na wananchi, pamoja na kuhakikisha umma unapata taarifa sahihi kuhusu utekelezaji wa sera, programu na miradi ya maendeleo ya Taifa.

**47.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imeendelea kuratibu na kufanya tathmini ya utoaji wa taarifa za Serikali kwa umma ili kuhakikisha wananchi wanapata taarifa sahihi na kwa wakati kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Serikali. Kutokana na tathmini hiyo, Wizara iliitisha Kikao Kazi cha Wakuu wa Idara na Vitengo vya Mawasiliano Serikalini wa Wizara kilichofanyika tarehe 11 Desemba, 2025. Katika kikao kazi hicho, jumla ya Wakuu wa Idara na Vitengo vya Mawasiliano Serikalini 520 walipatiwa mafunzo kuhusu mikakati mbalimbali ya kuimarisha utoaji wa taarifa za

utekelezaji wa majukumu ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2025/26.

**48.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuratibu vyombo na waandishi wa habari wa ndani na nje ya nchi katika matukio mbalimbali ya kitaifa na ziara za viongozi, kwa lengo la kuhakikisha wananchi wanapata taarifa sahihi na kwa wakati kuhusu shughuli muhimu za Serikali na Taifa. Katika kipindi cha kuanzia Julai 2025 hadi Aprili 2026, waandishi wa habari waliratibiwa kushiriki katika matukio mbalimbali ikiwemo Maonesho ya Kimataifa ya Biashara ya Sabasaba 2025; uzinduzi wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050; Maadhimisho ya Siku ya Mashujaa; pamoja na uzinduzi wa Kituo cha Biashara na Usafirishaji Ubungo. Aidha, waandishi hao waliratibiwa katika ziara za Mheshimiwa Rais katika mikoa ya Simiyu, Mara na Mwanza, ambapo alizungumza na wananchi na kuzindua miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwemo Daraja la JP Magufuli (Kigongo – Busisi). Vilevile, Wizara iliratibu vyombo vya habari katika matukio mengine muhimu ya kitaifa, yakiwemo Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani wa mwaka 2025, mikutano na shughuli mbalimbali za Serikali.

**49.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imeendelea kuratibu waandishi wa habari wa ndani na nje ya nchi katika matukio mbalimbali ya kitaifa na kimataifa, ili kuhakikisha wananchi wanapata taarifa sahihi na za uhakika na kwa wakati kuhusu shughuli za maendeleo ya Taifa. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Aprili 2026, waandishi wa habari waliratibiwa kushiriki katika matukio makubwa mbalimbali ikiwemo; Mkutano Mkuu wa Mahakimu na Majaji; vikao vya Bunge la 13 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mkutano wa 16 wa Wataalamu wa Bodi ya Ununuzi na Ugavi (PSTPB); Kongamano la Anwani za Makazi na Maonesho ya Kiteknolojia ya Huduma za Posta; Maadhimisho ya Siku ya Sheria Nchini; Hafla ya kufungua Soko la Kimataifa la Kariakoo; na Mashindano ya CHAN 2024. Matukio haya yameongeza uwazi na uwajibikaji wa Serikali kwa wananchi.

**50.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuhakikisha kuwa wananchi wanapata taarifa kikamilifu kuhusu Serikali yao, Wizara

imechapisha nakala 20,000 za Jarida la NCHI YETU linalohusu mafanikio ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Serikali ya Awamu ya Sita. Jarida hili linataarifa mbalimbali za miradi iliyotekelezwa na inayoendelea kutekelezwa na Serikali. Aidha, Wizara kupitia Idara ya Habari-MAELEZO inaendelea kutoa kila siku jarida hili mtandaoni.

### 3.2.1.2 Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC)

**51.** ***Mheshimiwa Spika***, Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) linasimamiwa kupitia Sheria ya Shirika la Utangazaji Tanzania, Sura 239. Majukumu ya TBC ni kutoa huduma ya utangazaji kwa kuhabarisha, kuelimisha, kuburudisha na kutafakarisha. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2025/26, Shirika limetekeleza majukumu mbalimbali ambayo yanafafanuliwa ifuatavyo:

**52.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia TBC imeendelea na utekelezaji wa mradi wa Upanuzi wa Usikivu kwa kujenga vituo vya kurusha matangazo ya redio, masafa ya FM katika Wilaya 18 nchini. Mradi huu uko katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Ujenzi unaendelea katika Wilaya za Kalambo (Rukwa), Liwale (Lindi), Rufiji (Pwani), Biharamulo (Kagera), Urambo na Igunga (Tabora), Karatu (Manyara), Kilolo (Iringa), Ulanga (Morogoro), Iramba (Singida) na Ngara (Kagera). Kazi zilizokamilika ni: ujenzi wa minara, ununuzi na ufungaji wa mitambo ya umeme, ujenzi wa vyumba vya kuhifadhi mitambo na ununuzi wa mitambo ya kurusha matangazo ya redio (transmitter). Wakati huo huo, TBC imepokea mitambo ya masafa ya FM kwa ajili ya Wilaya za Tanganyika (Katavi), Gairo (Morogoro), Hanang (Manyara), Siha (Kilimanjaro) na Mpwapwa (Dodoma) ambapo tayari hatua za awali za maandalizi ya ufungaji wa mitambo zinaendelea.

**53.** ***Mheshimiwa Spika***, TBC inashirikiana na wadua wengine wa maendeleo ya mawasiliano na teknolojia ya habari ikiwemo Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) ambapo mradi wa upanuzi wa usikivu unatekelezwa katika Wilaya kumi (10) za Kyerwa (Kagera), Chunya (Mbeya), Kiteto (Manyara), Chemba (Dodoma) na Mkinga (Tanga). Kazi ya ujenzi wa majengo ya kuhifadhi mitambo inaendelea na imefikia hatua mbalimbali za

utekelezaji. Maeneo mengine ambayo mradi unatekelezwa ni katika maeneo ya: Bukombe (Geita), Usangi (Kilimanjaro), Rombo (Kilimanjaro), Buhigwe (Kigoma) na Tunduru (Ruvuma) ambapo kazi ya ununuzi wa mitambo ya kurusha matangazo inaendelea.

**54.** ***Mheshimiwa Spika,*** TBC kwa kushirikiana na Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari inatekeleza mradi wa upanuzi wa usikivu katika Wilaya 15 na kazi ya ufungaji wa mitambo ya kurushia matangazo imekamilika kwenye vituo vya Arumeru (Arusha), Meatu (Simiyu), Sengerema (Mwanza), Kilosa (Morogoro), Mpwapwa (Dodoma) na Momba (Songwe). Aidha, ujenzi wa majengo ya kuhifadhi mitambo inaendelea kwenye halmashauri za Iringa Vijijini (Iringa), Lushoto (Tanga), Simanjiro (Manyara), Mpimbwe (Rukwa), Nyang'hwale (Geita), Kilombero (Morogoro), Nkasi Kusini (Rukwa), Itigi (Singida) na Mkalama (Singida).

**55.** ***Mheshimiwa Spika***, miradi hii ni hatua muhimu ya kupeleka mawasiliano ya redio kwa wananchi wote hususan waishio maeneo ya mipakani na yale yenye usikivu hafifu. Hadi Aprili 2026, usikivu wa redio za TBC umefikia Wilaya zote 139 na kukamilika kwa ujenzi wa vituo hivi kutaongeza usikivu hadi asilimia 98 na hivyo kuondoa changamoto ya usikivu kwenye maeneo yenye usikivu hafifu na yasiyokuwa na usikivu kabisa. Mkakati wa Serikali ni kufikisha Usikivu wa redio za TBC kwenye Halmashauri zote 184 nchi nzima baada ya lengo la usikivu katika Wilaya zote nchini kufikiwa.

**56.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kupitia TBC imeendelea na utekelezaji wa majukumu yake ya kuhabarisha, kuelimisha na kuburudisha umma wa Watanzania kwa weledi. Serikali imewezesha upatikanaji wa huduma ya utangazaji muda wote kwa kulipia masafa ya Satelaiti, simu na intaneti kwa ajili ya kurusha matangazo mbashara ya redio na televisheni. Aidha, Serikali imewezesha upatikanaji wa huduma ya utangazaji kwa kuboresha masafa ya satelaiti kutoka uwezo wa 3MHZ hadi 7MHZ ili kukidhi mahitaji yanayotokana na ongezeko la chaneli za televisheni (TBC1, TBC2 na Tanzania Safari Chaneli), idhaa za redio (TBC taifa, BONGO FM, TBC International na redio za Kanda, redio

jamii Arusha na Dodoma) na TBC Mtandaoni. Uwezeshaji huu umekuwa na tija kubwa kwa kuongeza uwezo wa TBC kurusha matangazo mbashara yenye manufaa kwa umma ambapo Katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026 TBC ilirusha jumla ya matangazo mbashara 403 yenye thamani ya Shilingi 5,565,590,825 yaliyohusu ziara na matukio yanayohusu viongozi wa kitaifa.

**57.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kupitia TBC imeboresha na kuimarisha chaneli zake za kimkakati ili kukidhi mahitaji ya wakati na kuendana na mabadiliko ya teknolojia ya habari na Utangazaji. Serikali imewekeza jumla ya shilingi 1,317,523,580 kwa ajili ya studio za TBC kwa kufunga mifumo mipya ya kisasa ya kidijiti, kununua mitambo na vifaa vipya vya utangazaji na hivyo kuongeza ubora wa picha na sauti. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2025/26, TBC ilinunua kamera za kisasa 15, *wireless microphone* 38, vifaa kwa ajili ya urushaji wa matangazo mbashara ya televisheni (LiveU-6), vifaa vya kurushia matangazo ya mbashara ya redio (Quantum- 1), vifaa vya kuchanganya sauti na picha za video (video mixer – 3) na gari moja (1) aina ya Coaster na gari moja la kurusha matangazo mbashara ya Televisheni (OB-Van) lenye kamera sita lililogharimu Shilingi 3,800,000,000 kwa ajili ya shughuli za utangazaji. Aidha, TBC imefanya maboresho katika studio za BONGOFM kwa kuzihamishia TBC1 - Mikocheni kutoka barabara ya Nyerere. Maboresho mengine yaliyofanyika ni katika studio za TBC Zanzibar, Dodoma na TBC Mtandao. Fauka ya hayo, TBC imefunga mfumo wa kuchambua na kuchakata takwimu za uchumi na biashara - TBC Arc na kufunga mfumo maalumu wa AR/VR kwa ajili ya kuboresha muonekano wa graphics maalum katika muundo wa 3D.

**58.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha kuwa TBC inawafikiwa vijana kwenye majukwaa ya mtandaoni hasa wanafuatilia kwenye majukwaa ya mtandaoni maboresho makubwa ya kimaudhui na mifumo yamefanyika kupitia BongoFM, TBC2 na TBC Mtandao. Chaneli hizi za kimkakati zimekuwa chachu kwa kuongeza watazamaji, wafuatiliaji na wasikilizaji hivyo kukidhi malengo ya kuanzishwa kwake. Hadi

mwezi Aprili 2026 BongoFM ina wafuatiliaji *475,000* kwenye mtandao wa *Instagram*, watazamaji wa machapisho kwenye kurasa ya *YouTube* wamefika *19,239,386*. Kwa upande wa TBCDigita inawafuatiliaji *2,200,000* katika ukurasa wa *Instagram na* watazamaji wa machapisho *61,055,545* kwenye ukurasa wa *YouTube*. Serikali kupitia TBC itaendelea kuwekeza katika uandaaji wa maudhui hasa ya mtandaoni kwenye chaneli zake za vijana.

**59.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali kupitia TBC imeendelea kuboresha uandaaji wa vipindi vya redio, televisheni na TBC Mtandaoni vinavyoelimisha na kuhabarisha umma kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Serikali pamoja na utekelezaji wa shughuli za viongozi wakuu wa Serikali. Katika kipindi cha 2025/26, TBC imeandaa vipindi vya redio na televisheni vyenye maudhui mbalimbali yenye lengo la kuelimisha umma wa watanzania: Uzalendo vipindi 1,920 (baadhi ya vipindi vyenye maudhui haya ni pamoja na *Mada Kuu*, *Mizani*, *Focus on this Week na Tanzania Today)*, Afya 415, uchumi na Biashara 601, Elimu 132, utunzaji wa mazingira 112, malezi ya watoto 130, mchango wa vijana katika kukuza uchumi 982 na sheria 34. Vipindi vingine vinahusu haki na umuhimu wa amani vipindi 617 (kipindi cha *Sisi ni Tanzania*) pamoja na masuala yahusuyo upatikanaji wa fursa mbalimbali za kiuchumi na kijamii kwa makundi ya watu wenye ulemavu na wanawake vipindi 77 (Kipindi cha *Wape nafasi*). Aidha, kupitia idhaa ya Bongo FM vipindi vikivyoandaliwa ni pamoja na: *Flyover, Bao la Asubuhi, Kijora na Power Bank.* Kwa upande wa TBC2 vipindi vilivyoandaliwa ni *2DJ Night, Kibajaji on Point, JABA na Binti bora*. Fauka ya hayo, TBC imeendelea kutekeleza mikakati ya kukuza lugha adhimu ya Kiswahili kwa kuwa Balozi mzuri Duniani kote kupitia kipindi cha *Lulu za Kiswahili*. Mkakati wa TBC ni kuhakikisha inaandaa vipindi vya redio, televisheni na mitandao ya kijamii vitakavyowawezesha Watanzania kuifahamu vizuri Dira ya Maendeleo ya Taifa 2050.

**60.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kutekeleza maelekezo ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kutangaza Utalii wa nchi yetu na kuhakikisha Sekta ya Utalii inakua kwa kasi kuelekea Utekelezaji wa Dira 2050, TBC kupitia chaneli yake ya Tanzania Safari

ambayo ni mahsusi kwa ajili ya kutangaza fursa za utalii na utajiri wa maliasili za nchi yetu imewezesha kuandaa maudhui na kutafsiri na kurusha jumla ya vipindi 1,125 katika lugha tano (5) za kimataifa ambazo ni Kireno, Kiarabu, Kiingereza, Kifaransa na Kichina. Matumizi ya lugha za Kimataifa yamewezesha kuongezeka kwa mawanda ya watazamaji na wafuatiliaji duniani kote na hivyo kufikia malengo ya kitaifa katika kuongeza idadi ya watalii nchini. Aidha, maudhui ya chaneli hii yanapatikana mtandaoni kupitia tovuti ya *www.safarichannel.go.tz* na katika mtandao wa *Youtube* ambapo machapisho yametazamwa na watu 729,471 na wafuatiliaji 85,100 kwenye ukurasa wa mtandao wa Instagram.

**61.** ***Mheshimiwa Spika***, tarehe 2 Septemba 2022, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, akiwa mjini Bagamoyo wakati wa maandalizi ya filamu ya Tanzania '*The Royal Tour*", alielekeza Tanzania National Parks Authority (TANAPA) kuitangaza njia ya utumwa kama kivutio cha utalii. Kufuatia agizo hilo, wataalamu kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa kushirikiana na TANAPA walifanya utafiti na kuwasilisha ripoti iliyobainisha vivutio mbalimbali pamoja na kupendekeza mikakati ya kuitangaza njia hiyo kupitia vyombo vya habari. Katika kutekeleza maelekezo ya Mheshimiwa Rais, Wizara kupitia TBC inashiriki zoezi la utambuzi wa njia ya misafara ya utumwa na wapagazi na kutangaza vivutio vya utalii vilivyoko katika njia hii kupitia Kampeni ya *Slave Caravan*.

**62.** ***Mheshimiwa Spika***, kampeni ya *Slave Caravan* inahusisha utangazaji wa njia hii na vivutio ambavyo, isivyo bahati, havijulikani kwa Watanzania na wageni wanaotembelea Tanzania licha ya kuwa na utajiri mkubwa wa historia. Aidha, utangazaji wa njia hii unakwenda sambamba na kuhifadhi kumbukumbu za wazee na kuandaa makala mbalimbali za kumbukumbu hizo katika jamii ambazo njia hii imepita kutoka Zanzibar hadi Bara (Ujiji – Kigoma) ambapo tayari kampeni imebaini vituo 14 vitakavyotumika kama sehemu ya kuhifadhi kumbukumbu. Kuhifadhi kumbukumbu za wazee wanaofahamu maeneo mbalimbali ya njia hii kutasaidia kuhifadhi urithi huu muhimu katika historia ya Tanzania kwa kuhifadhi maelezo kuhusu

watumwa, utumwa, masulia na maisha baada ya kukomeshwa kwa utumwa. Hatua hii inalenga kukuza utalii wa kiutamaduni na kihistoria, kuongeza idadi ya watalii wa ndani na nje ya nchi, na kuchochea ukuaji wa uchumi. Njia hii, inayotarajiwa kuvutia wageni kuanzia Zanzibar, Bagamoyo hadi Ujiji, pia itasaidia kuhifadhi na kutangaza urithi wa taifa kwa vizazi vijavyo.

**63.** ***Mheshimiwa Spika,*** TBC imeanzisha kampeni maalumu zenye lengo la kuhakikisha kunakuwepo na uhamasishaji wa matumizi ya nishati safi ya kupikia ili kupunguza madhara yanayotokana na uvunaji wa miti kwa ajili ya kutumika kama nishati ya kupikia pamoja na athari za afya zinazotokana na moshi. Jukumu hili linatekelezwa kupitia kampeni ya "Pika Kijanja". TBC kupitia idhaa yake ya redio ya BongoFM imeendesha matamasha manne (4) na makongamano (2) kwa lengo la kuelimisha na kuhamasisha matumizi ya nishati safi katika maeneo mbalimbali nchini. Baadhi ya maeneo yaliyofikiwa na kampeni hii kwa kupitia matamasha na makongamano ni mikoa ya Dar es Salaam, Lindi (Ruangwa) na Zanzibar (Kizimkazi). Katika nyakati zote makundi ya watu mbalimbali wakiwemo *mamalishe* na *babalishe* wameshiriki na kugawiwa mitungi ya gesi kwa ajili ya kutumika kama nishati mbadala. Hadi Aprili 2026, zaidi ya mamalishe na babalishe 9,000 walishiriki makongamano na matamasha na zaidi ya mitungi ya gesi 5,000 ilitolewa bure.

**64.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika jitihada za uhifadhi wa mazingira na ustahimilivu wa mabadiliko ya tabianchi, Wizara kupitia TBC kwenye kipindi cha JAMBO TANZANIA imeendelea kuendesha na kusimamia kampeni ya upandaji miti nchi nzima inayofahamika kwa jina la **"27 ya Kijani"** inayofanyika kila **tarehe 27** ya kila mwezi. Kampeni hii ilizinduliwa mwezi Januari mwaka 2023. Tarehe 27 Januari, 2026 Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliiongoza timu ya TBC na wana mazingira wengine nchini kote kwa kupanda miti katika kumbukizi ya siku yake ya kuzaliwa hafla iliyofanyika Kizimkazi, Wilaya ya Kusini Unguja ambapo jumla ya miti 169,310 ilipandwa siku hiyo katika mikoa yote nchini. Hadi Aprili, 2026, zaidi ya miti 10,000,000 imepandwa maeneo mbalimbali nchini tangu kuasisiwa kwa kampeni hiyo.

**65.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia TBC inaendesha kampeni mahususi kwa ajili ya kutoa elimu kuhusu utunzaji wa mazingira inayojulikana kwa **Jicho la Mpita Njia.** Kampeni hii inarushwa kupitia kipindi cha ARIDHIO, ambapo wanahabari wa TBC hupita katika maeneo yaliyokithiri kwa uchafu na hatimaye kutafuta suluhisho la kutatua changamoto hiyo. Kipindi hiki kimekuwa na matokeo chanya kwa maeneo yote ambayo waandishi wa TBC wamefanikiwa kufika. Hadi Aprili, 2026 TBC imefanikiwa kufika Zanzibar na maeneo 18 ya mikoa ya Arusha, Dodoma, Dar es Salaam, Mwanza, Mbeya, Kilimanjaro, Kagera, Kigoma, Tanga, Njombe, Simiyu, Songwe, Manyara, Mtwara, Mara, Singida, Geita na Morogoro na kufanikiwa kuandaa makala zaidi ya 200 zinazochochea usafi na utunzaji wa mazingira.

**66.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza azma ya Serikali kuhamia Makao Makuu ya nchi jijini Dodoma, Wizara kupitia TBC imeendelea kutekeleza mradi wa ujenzi wa Makao Makuu ya TBC jijini Dodoma eneo la Vikonje. Awamu ya Kwanza ya Ujenzi inatarajiwa kugharimu jumla ya shilingi 54,204,499,116.46 ambapo hadi mwezi Aprili 2026, kiasi cha shilingi 19,592,179,456.58 kimepokelewa kwa ajili ya malipo ya Mkandarasi na Mshauri elekezi wa ujenzi wa jengo la utawala, studio za redio, televisheni na mitandao ya kijamii. Ujenzi umefikia asilimia 52 ambapo kazi zilizotekelezwa ni kuanza ufungaji wa mifumo ya muhimu ya utangazaji kwenye studio za redio, televisheni na mitandao ya kijamii. Kukamilika kwa mradi huu mkubwa ni hatua ya wazi katika kuipa heshima tasnia ya habari nchini na historia ya Tanzania katika kuhabarisha umma toka enzi za Redio Tanzania Dar es Salaam - RTD kwa uwepo wa majengo, studio na vifaa vya kisasa vya utangazaji. Mradi huu awamu ya kwanza unatarajiwa kukamilika Juni, 2026 kulingana na mkataba.

**67.** ***Mheshimiwa Spika,*** TBC kikiwa ni chombo cha utangazaji cha umma kimeendelea kuwa na jukumu la kuimarisha mahusiano na vyombo vingine vya kimataifa kwa kuingia makubaliano (MoU) ya kubadilishana maudhui na vipindi, mafunzo kwa watumishi na kuitangaza lugha adhimu ya Kiswahili kupitia vyombo vya habari vya mataifa hayo. Vyombo vya habari ambavyo ni washirika na TBC ni pamoja na Voice of Nigeria

(VoN), RT ya Russia, Southern Africa Broadcasting Association (SABA), NHK ya Japan na African Union of Broadcasting (AUB). Washirika hawa wamekuwa ni chachu katika kuitangaza Tanzania kimataifa ikiwa ni pamoja na kuongeza ushawishi wa Tanzania kupitia maudhui mbalimbali yaliyotafsiriwa kwa Lugha adhimu ya Kiswahili. Kwa upande mwingine TBC imekuwa ni mlezi wa vyombo vya habari ambavyo vinamilikiwa na Halmashauri mbalimbali nchini kwa kutoa mafunzo kwa watendaji katika kuwajengea uwezo kutokana na ukuaji wa haraka wa tasnia ya habari na utangazaji. TBC imeimarisha chaneli ya matangazo yake ya taarifa ya habari kwa lugha ya kiingereza (English News) ili kuitangaza nchi kimataifa.

**68.** ***Mheshimiwa Spika***, TBC inajivunia mafanikio katika nyanja zote za kihabari, mifumo, miundombinu ya utangazaji na maslahi ya watumishi yaliyoboreshwa. Matokeo ya maboresho haya ni kuongezeka kwa ubunifu kihabari hivyo kuwezesha TBC kupata tuzo mbalimbali za kihabari kitaifa na Kimataifa. Katika kipindi cha mwaka 2025/26 TBC kama taasisi, wanahabari, watozi na watumishi wake wameweza kupata tuzo mbalimbali wakiwemo Bw. D'jaro Deus Arungu kupitia kipindi chake cha Papaso (*ZIKOMO AFRICA AND CARIBBEAN AWARDS 2025*) kipengele cha *Media Legend of the Year*, 2025 Bw. Sam Clinton na Bi.Caroline Malewo walipata Tuzo ya *AFRICA MEDIA AWARD*, 2025 kwenye Kipengele cha *Best Outstanding Interview of the Year* kupitia kipindi cha *Focus on this week* kinachotangazwa na chaneli ya TBC1. Fauka ya hayo, TBC ilipata tuzo za CHOMBO BORA CHA MAWASILIANO KWA UMMA NA USHIRIKISHWAJI WA WANANCHI, 2025. Tuzo hiyo ilitolewa na Taasisi ya Tuzo za Ubunifu wa Sekta ya Umma; KIPINDI BORA CHA ELIMU KWA WAJASILIAMALI WADOGO kupitia kipindi cha *Ngazi* kinachorushwa na Chaneli ya TBC1, tuzo iliyotolewa na Umoja wa Wanawake Wajasiliamali Tanzania. Kupatikana kwa tuzo hizi kunadhihirisha wazi kuwa TBC imekuwa na mchango mkubwa katika kutekeleza dhima yake ya kuelimisha, kuhabarisha, kuburudisha na kutafakarisha kwa kuzingatia ubunifu na misingi ya weledi kwenye taaluma ya uandishi wa habari.

**69.** ***Mheshimiwa Spika,*** Chaneli za TBC1, TBC2 na Tanzania

Safari Chaneli kwa kupitia mtandao wa televisheni wa *Canal+International* zimeweza kufikia nchi 46 zinazoongea *Kingereza, Kifaransa na Kireno*. Nchi hizo ni pamoja na Angola, Benin, Burkina Faso, Botswana, Burundi, Kameruni, Jamhuri ya Afrika ya Kati, Chad, Kongo, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Djibouti, Equatorial Guinea, Ethiopia, Eritrea, Eswatini, Gabon, Gambia, Ghana, Green Cape, Guinea Conakry, Guinea Bissau, Ivory Coast, Kenya, Liberia, Lesotho, Mali, Malawi, Mauritania, Mozambique, Namibia, Niger, Nigeria, Rwanda, Sao Tome, Senegal, Sierra Leone, Somalia, Sudani, Afrika Kusini, Sudani Kusini, Uganda, Tanzania, Togo, Zambia, Zimbabwe. Aidha, kupitia AZAM nchi saba (7) zimefikiwa ambazo ni Tanzania, Kenya, Uganda, Burundi, Rwanda, Malawi na Zimbambwe.

### 3.2.1.3 Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN)

**70.** ***Mheshimiwa Spika,*** Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN) ilianzishwa kwa tamko la Rais la mwaka 1970. Aidha, TSN inatekeleza majukumu chini ya sheria ya Makampuni Sura ya 212 ikiwa na jukumu la kuhabarisha na kuelimisha umma kwa kuchapa na kusambaza magazeti ya Serikali ambayo ni *Daily News, Sunday News*, HabariLEO na SpotiLEO. Vilevile, TSN huchapisha habari kupitia nyanja za kidigiti; tovuti na mitandao ya kijamii kwa lugha za Kiswahili na Kiingereza ikiwamo *Facebook, Instagram na Youtube*. Katika kipindi cha mwaka 2025/26, Wizara kupitia TSN imetekeleza majukumu yafuatayo:

**71.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia TSN imeendelea kutekeleza mradi wa ufungaji mitambo mipya ya kisasa ya uchapaji kwa kujenga jengo la kiwanda cha uchapaji na kununua mitambo mipya ya kisasa ya uchapaji. Hatua ya ujenzi wa jengo la kiwanda cha uchapaji imefikia asilimia 83.1 ambapo kazi zilizofanyika ni pamoja na uwekaji wa vigae, uwekaji wa milango na madirisha, ufungaji wa mifumo ya maji, umeme, TEHAMA, utambuzi na udhibiti wa moto na kupaka rangi jengo. Ununuzi wa mitambo mipya ya kisasa ya uchapaji umefikia asilimia 85. Mitambo iliyonunuliwa ni pamoja na *Hybrid Web Offset Press, Computer to Plate (CTP) Machine, Compressor (Large Size) 38kw, Guillotine/Cutting Machine, Six Color Fed Machine,*

*Gatherer, Stitcher na Knife Trimmer* yenye thamani ya Shilingi 17,821,368,600.

**72. *Mheshimiwa Spika***, Wizara kupitia TSN imeendelea kuboresha uandaaji na uchapaji wa maudhui kupitia Magazeti, Chaneli ya mtandaoni na majukwaa ya mitandao ya kijamii. TSN imeimarisha uandaaji wa maudhui ya kimkakati yaliyolenga kujenga na kuendeleza taswira chanya ya nchi na Serikali, ndani na nje ya mipaka ya Taifa. Maudhui hayo yalijikita katika kuhabarisha mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan. Hadi Aprili 2026, TSN imeandaa na kuchapisha jumla ya makala 2,973 za kimkakati, ambapo makala 178 za Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, makala 140 za Bunge la Wawakilishi Zanzibar, makala 144 za utekelezaji wa miradi ya kimkakati ya maendeleo, makala 656 za elimu ya mpiga kura na uraia, makala 180 za maboresho ya huduma za kijamii, makala 288 za ukuaji wa uchumi, na makala 1,387 za elimu juu ya sera, mikakati na miongozo na nafasi ya Tanzania katika diplomasia ya kikanda na kimataifa. Aidha, TSN imeendelea kusambaza jumla ya nakala za magazeti 1,909,752, wasomaji wa gazeti tepe wameongezeka kwa asilimia 24 na ufuatiliaji wa majukwaa ya kidigitali umeongezeka kwa asimilia 19.

**73. *Mheshimiwa Spika,*** TSN imeanzisha maktaba maalum ya historia kwa kuweka matoleo ya zamani ya magazeti na picha kwenye mfumo wa kidijiti. Jumla ya matoleo 12,600 ya *Daily News* na *HabariLeo*, picha 2,499 na makala maalumu 2,100 zimepatiwa alama ya utambuzi *(indexing)*. Mfumu huu umehifadhi nyaraka zote muhimu zinazohusu historia ya nchi, historia kuhusu viongozi wakiwemo waasisi wa Taifa, historia ya harakati za ukombozi wa Uhuru kwa nchi za Kusini mwa Afrika na historia kuhusu masuala ya kidiplomasia. Kutokana na maktaba ya TSN kuhifadhi nyaraka na kumbukumbu za kihistoria Kampuni imefanikiwa kuwa chanzo kikuu cha taarifa kwa ajili ya Kitabu cha Rais wa Awamu ya Tatu Hayati Benjamin William Mkapa; Rais wa Awamu ya Pili, Hayati Ally Hassan Mwinyi; Kitabu cha Muungano; na picha zote zilizopamba Ukumbi wa Kimataifa wa Mikutano wa Julius Nyerere. Katika hatua ya uimarishaji wa mfumo wa kidigiti, kampuni imeunda

mfumo wa *TSN Intergreted Management Information System (TIMIS)* unaounganisha *Digital Archive* na tovuti ya Kampuni ili kuwezesha kutoa huduma na kupata taarifa zote popote duniani.

**74.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kutekeleza maono ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kutangaza utalii, kipekee TSN imeendelea kuandaa na kuchapa makala maalumu zenye maudhui kuhusu sekta ya utalii. Jumla ya makala 172 ziliandaliwa ikiwa yanalenga kuibua na kuonesha vivutio vya utalii, mafanikio ya sekta ya utalii, fursa za ajira na uwekezaji, pamoja na mchango wa sekta ya utalii katika kukuza pato la Taifa na ustawi wa wananchi. Makala maalumu zilikuwa na lengo kimkakati la kuitangaza Tanzania kimataifa kama kivutio bora cha utalii na uwekezaji.

**75.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kupitia TSN imeimarisha maktaba maalumu ya kidigiti kwa ajili ya kuboresha utunzaji wa kumbukumbu za magazeti na picha zilizotumika katika habari zilizochapishwa. Hadi Aprili 2026, magazeti ya Daily News yenye zaidi ya miaka 90 na HabariLEO yenye miaka 20 yaliyobeba taarifa muhimu kuhusu historia ya Tanzania, historia ya viongozi mashuhuri nchini na nje ya nchi, habari za uhusiano wa kidiplomasia, habari za harakati za ukombozi wa nchi za Kusini mwa Afrika na historia ya masuala ya kijamii, kisiasa, kiuchumi, kiutamaduni na kimichezo yameihifadhiwa kwenye maktaba, ambapo huduma ya upatikanaji wa taarifa za Maktaba ya kidigiti zinapatikana kupitia anuani ya ePaper.tsn.go.tz.

**76.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kupitia TSN imefanya utafiti wa masoko ili kuboresha ubora wa bidhaa na huduma zinazotolewa na TSN. Februari 2026, TSN ilikamilisha na kuwasilisha taarifa ya utafiti wa masoko katika Bodi ya Wakurugenzi ambapo utafiti ulijikita katika maeneo ya mahitaji ya soko, aina ya wateja, biashara pamoja na ubora wa bidhaa. Matokeo ya utafiti yamewezesha kuboresha usambazaji wa magazeti kwa njia ya nakala ngumu, matumizi ya teknolojia katika usambazaji wa magazeti kwa njia ya mfumo. Sambamba na hayo, maboresho ya *ePaper App* yamelenga kuendana na mabadiliko ya

teknolojia kwa kuongeza jitihada katika uuzaji wa gazeti tepe ili kuongeza mapato.

**77.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhimiza jitihada za matumizi bora ya mifumo kwa ajili ya kurahisisha utoaji huduma, Wizara kupitia TSN imeendelea na maboresho ya mifumo ya utoaji wa huduma ikiwa na lengo la kuongeza ufanisi wa uendeshaji wa shughuli za Kampuni, ambapo hadi Aprili 2026, TSN imeboresha mifumo miwili (2) ambayo ni mfumo wa ankara *(TSN billing system)* kwa ajili ya kumrahisishia mteja kufikia huduma kwa urahisi na kukamilisha malipo ya huduma husika na kuboresha upatikanaji wa gazeti mtandao *(TSN ePaper)* kwa ajili ya kuwezesha upatikanaji wa gazeti tepe kwa njia ya mtandao kwa ubora na wakati sahihi.

### 3.2.1.4 Bodi ya Ithibati ya Waandishi wa Habari

**78.** ***Mheshimiwa Spika,*** Bodi ya Ithibati ya Waandishi wa Habari ilianzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Huduma za Habari, Sura ya 229, kwa lengo la kusimamia, kuimarisha na kuhakikisha taaluma ya uandishi wa habari nchini inazingatia misingi ya weledi, maadili na uwajibikaji, pamoja na kuratibu utoaji wa mafunzo kwa Waandishi wa Habari. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Aprili 2026, Bodi ya Ithibati imetekeleza majukumu yafuatayo:

**79.** ***Mheshimiwa Spika***, Bodi ya Ithibati imepokea maombi na kusajili waandishi wa habari 4,139 kupitia mfumo wa Tai Habari ambapo Waandishi wa Habari 3,357 wenye vigezo vilivyoainishwa kwa mujibu wa sheria wamepatiwa ithibati.

**80.** ***Mheshimiwa Spika***, ili kuhakikisha kuwa Maadili ya Taaluma ya Waandishi wa Habari yanazingatiwa, Wizara kupitia Bodi ya Ithibati imeshughulikia malalamiko 14 ya uvunjifu wa maadili ya taaluma ya habari katika kipindi cha Julai 2025 hadi Aprili 2026. Malalamiko hayo yameshughulikiwa kwa njia mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuwaita wahusika kuzungumza nao na kuwaonya na wale ambao hawakuwa na vigezo kuwashauri kuacha kufanya kazi za kihabari na kutafuta sifa za taaluma kwa mujibu wa Sheria.

**81.** ***Mheshimiwa Spika,*** Bodi ya Ithibati imeandaa mwongozo maalumu wa kisheria utakaowezesha wanahabari wakongwe walioathiriwa na mfumo wa ithibati kurejea katika mfumo rasmi, kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Huduma za Habari, Sura ya 229 ambayo ilitungwa kwa ajili ya kukuza taaluma ya uandishi wa habari kwa kuweka mfumo wa kitaasisi utakaosimamia sekta ya habari. Mwongozo huu umeandaliwa kwa kutambua kwamba kumekuwepo na kundi la waandishi wa habari waliopata ujuzi na uzoefu wa muda mrefu kazini bila kuwa na sifa rasmi za kitaaluma kama zinavyotambuliwa kisheria na wamechangia kwa kiwango kikubwa katika maendeleo ya taaluma ya habari. Mwongozo huu unaweka utaratibu wa kisheria wa kutambua na kuthibitisha umahiri wao kupitia tathmini maalumu ya uzoefu, weledi na maadili ya taaluma, na kuwawezesha kupata ithibati kwa mujibu wa sheria. Utekelezaji wa mwongozo huo unatarajiwa kuanza mwaka wa fedha 2026/27.

**82.** ***Mheshimiwa Spika***, kwa lengo la kuhakikisha kuwa Waandishi wa Habari wanakuwa na weledi katika taaluma yao Bodi iliratibu mafunzo ya muda mfupi ya Waandishi wa Habari. Bodi ya Ithibati kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (Shule Kuu ya Uandishi wa Habari) ilifanikiwa kutoa mafunzo katika Kanda tano (5) ambazo ni Kanda ya Mashariki tarehe 11 Agosti, 2025; Kaskazini tarehe16 Agosti, 2025; Kanda ya Kati, tarehe 14 Agosti, 2025, Nyanda za Juu Kusini tarehe19 Agosti, 2025 na Kanda ya Ziwa, tarehe 07 Agosti, 2025 ambapo Waandishi wa Habari 1,071 walipewa mafunzo kuhusu uzingatiaji wa maadili ya uandishi wa Habari katika utekelezaji wa majukumu yao.

**83.** ***Mheshimiwa Spika***, ili kuwa na kumbukumbu sahihi za Waandishi wa Habari, Serikali imeendelea kuimarisha utunzaji wa kanzidata ya Ithibati ya Waandishi wa Habari. Wizara kupitia Bodi ya Ithibati ya Waandishi wa Habari kwa kushirikiana na Mamlaka ya Serikali Mtandao na Idara ya Habari-MAELEZO ilifanikiwa kutengeneza Mfumo wa Ithibati wa kidijiti kwa ajili ya usajili na kutunza Kanzidata ya Waandishi wa Habari unaojulikana kwa jina la **TAI – HABARI**. Mfumo huu umeleta mageuzi makubwa katika

Sekta ya Habari ambapo Waandishi wa Habari wanajisajili mahali walipo na kupata vitambulisho vya kidijiti (Digital Press Card). Aidha, Mfumo umerahisisha upatikanajii wa taarifa na takwimu sahihi za Waandishi wa Habari wanaofanya kazi za kihabari nchini ambapo hadi Aprili 2026, jumla ya Waandishi wa Habari 4,139 wamejisajili.

**84.** ***Mheshimiwa Spika,*** kupitia ushirikiano kati ya Bodi ya Ithibati ya Waandishi wa Habari na Mfuko wa Utamaduni na Sanaa Tanzania, Serikali inaendelea kuchukua hatua za kuwawezesha vijana wanaojiajiri katika sekta ya habari kwa kuwawezesha mitaji ya kukuza, kuendeleza na kuzalisha kazi zao katika ubora unaokidhi mahitaji ya soko kupitia mikopo yenye masharti nafuu. Katika kutekeleza hayo, **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** anatoa shilingi 20,000,000,000 kwa ajili ya Mfuko wa Utamaduni na tayari 2,000,000,000 kwa ajili ya mikopo kwa Watengeneza Maudhui Mtandaoni *(content creators)* zimetoka kwa lengo la kuwasaidia kupata vitendea kazi na kuongeza uzalishaji wa kazi zao.

**85.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mfuko wa Utamaduni na Sanaa umetoa mafunzo kwa watengeneza Maudhui Mtandaoni yenye lengo la kuwawezesha kutengeneza kazi zenye ubora kwa soko shindani la ndani na nje ya nchi. Mafunzo kwa awamu ya kwanza yametolewa kwa watengeneza Maudhui Mtandaoni 931 ambao kati yao wanawake ni 574 sawa na asilimia 62 na wanaume ni 357 sawa na asilimia 38 kutoka mikoa mitatu (3) ya Dar es Salaam (347), Mwanza (250) na Arusha (334). Aidha, mada zilizofundishwa ni pamoja na umuhimu na aina za urasimishaji, kubiasharisha maudhui, maadili na miongozo ya utoaji huduma mtandaoni, elimu ya fedha, masoko, uwekezaji pamoja na usimamizi na uandishi wa miradi.

### 3.2.1.5 Kamati ya Maudhui (TCRA)

**86.** ***Mheshimiwa Spika***, Kamati ya Maudhui ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania huundwa na Waziri mwenye dhamana na sekta ya Habari na Utangazaji kwa mujibu wa Kifungu cha 27 cha Sheria ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania, Sura ya 172,

Marejeo ya Mwaka 2023. Kwa mujibu wa Kifungu hicho, Mjumbe mmojawapo wa Bodi ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania ndiye huwa Mwenyekiti wa Kamati ya Maudhui ambayo ina wajumbe wasiozidi watano (5). Muda wa wajumbe hao utakuwa miaka mitatu (3) kuanzia tarehe ya kuteuliwa. Wajumbe hao wanaweza kuteuliwa tena kwa muhula mwingine mmoja.

**87.** ***Mheshimiwa Spika***, Kamati ya Maudhui ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania hutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Kifungu cha 28 cha Sheria hiyo na kuyatolea taarifa kwa Waziri mwenye dhamana ya Habari na Utangazaji. Majukumu ya Kamati hii ni kusimamia maudhui yanayotolewa katika vyombo vya habari na kuchukua hatua pale kunapotokea ukiukwaji wa Sheria, Kanuni na maadili. Kabla ya kuchukua hatua za kisheria, Serikali hutanguliza mazungumzo, ushauri na utoaji wa maelekezo kwa vyombo husika ikilenga kutoa fursa ya kujirekebisha. Hatua hizi huchukuliwa pale tu ambapo ukiukaji unaendelea, unajirudia au unasababisha madhara makubwa kwa umma. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Aprili 2026, Wizara kupitia Kamati ya Maudhui ya Mamlaka ya Mawasiliano imetekeleza majukumu yafuatayo:-

(i) Kufanya vikao tisa (9) vya Kamati vya kushughulikia mashauri dhidi ya watoa huduma 14 ambao walikiuka Sheria, Kanuni na Masharti ya Leseni zao;

(ii) Kufanya mapitio ya taarifa ya ukiukaji wa kanuni za utangazaji dhidi ya watoa huduma11 wa maudhui ya utangazaji waliobainika kuwa na ukiukaji wa mara kwa mara wa Sheria, Kanuni na Masharti ya Leseni; na

(iii) Kushiriki kwenye vikao vitatu (3) vya mashauriano na watoa huduma wa utangazaji wa maudhui kuhusu uzingatiaji wa Sheria, Kanuni, Masharti ya Leseni na Maadili ya Uandishi na Utangazaji wa Habari.

### 3.2.2 SEKTA YA MAENDELEO YA UTAMADUNI

**88.** ***Mheshimiwa Spika***, utamaduni ndio mtima wa Taifa, hakuna Taifa linaloweza kujitambulisha kwa utamaduni wa nchi

nyingine. Aidha, Tanzania ni taifa pekee katika Afrika Mashariki na Kati lililofanikiwa kwa kiasi kikubwa kuhimili misukosuko inayotokana na tamaduni za kigeni kwa kudumisha utamaduni wake. Tanzania imefanikiwa kudumisha misingi ya umoja, mshikamano, upendo, amani na utangamano wa kitaifa bila kujali wingi wa jamii tulizonazo.

### 3.2.2.1 Idara ya Maendeleo ya Utamaduni

**89.** ***Mheshimiwa Spika,*** sekta ya utamaduni imekasimiwa majukumu ya kulinda, kuhifadhi na kuendeleza urithi wa utamaduni wa Taifa ikijumuisha lugha, mila, desturi, historia na maadili ya Taifa. Aidha, sekta hii ina jukumu la kudumisha na kuendeleza utambulisho wa Taifa letu; kuhamasisha na kukuza thamani ya utamaduni wa Taifa kwa wananchi hususan watoto na vijana ambao ndio hazina ya Taifa la sasa na baadaye; kuratibu na kusimamia maendeleo ya lugha adhimu na aushi ya Kiswahili ndani na nje ya nchi pamoja na kuratibu na kufanya tafiti za urithi wa utamaduni usioshikika hususani lugha za kijamii ambazo ni kibebeo kikuu cha urithi wa utamaduni wa Taifa letu. Vilevile, sekta hii ina jukumu la kuratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli za Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) na Kituo cha Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Aprili, 2026, sekta ya utamaduni imetekeleza majukumu mbalimbali yafuatayo:

**90.** ***Mheshimiwa Spika,*** Tanzania imejaliwa kuwa na utajiri mkubwa wa uanuai wa urithi wa utamaduni. Katika kuhakikisha kuwa urithi huu unalindwa, unahifadhiwa na kuendelezwa, Serikali imefanya utafiti wa kutambua, kuorodhesha na kulinda urithi wa utamaduni usioshikika kwa manufaa ya kizazi cha sasa na kijacho. Utafiti huo uliofanyika kwa kushirikisha wadau wa utamaduni ulijikita katika kutambua na kuorodhesha Vazi la Kanga kama moja ya alama muhimu ya utambulisho wa Mtanzania na urithi wa Utamaduni. Kufuatia utafiti huo, andiko la Vazi la Kanga liliwasilishwa Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO) tarehe 31 Machi, 2026 kwa lengo la kuingizwa kwenye orodha ya Urithi wa Dunia wa Utamaduni Usioshikika inayosimamiwa na Shirika hilo. Manufaa ya

kutambuliwa kwa urithi wa utamaduni wa Tanzania katika Orodha ya Urithi wa Dunia ni pamoja na kuongeza hadhi ya utambuzi wa kimataifa; kupata fursa za ufadhili wa uendelezaji na uhifadhi wa urithi huo kutoka kwenye mifuko ya kimataifa inayoratibiwa na UNESCO; kutangaza urithi wa utamaduni wa Tanzania pamoja na utalii wa kiutamaduni duniani.

**91.** ***Mheshimiwa Spika***, jitihada nyingine zilizofanywa na Serikali ni kukamilisha uandaaji wa Mwongozo wa Kitaifa wa miaka mitano (5) 2026/27 - 2030/31 wa Kulinda Urithi wa Utamaduni Usioshikika *(National Framework for Safeguarding Intangible Cultural Heritage)* ili kuhakikisha urithi wetu wa utamaduni unaendelea kulindwa na kudumishwa. Vilevile, katika kupanua wigo wa uelewa kwa wadau wa masuala ya urithi wa utamaduni, Serikali kupitia Wizara iliratibu warsha ya wadau wa utamaduni iliyofanyika tarehe 11 Novemba, 2025 jijini Dar es Salaam ambapo takribani washiriki 150 kutoka Tanzania Bara na Zanzibar walihudhuria.

**92.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kukabiliana na suala la mmomonyoko wa maadili nchini, Serikali kupitia Wizara imeandaa Mkakati wa Taifa wa miaka 10 yaani 2026/27 hadi 2036/37 wa kukabiliana na Mmomonyoko wa Maadili nchini. Maandalizi ya mkakati huo yameshirikisha wadau mbalimbali wakiwamo; Wizara, taasisi za umma, asasi za kiraia, sekta binafsi, viongozi wa dini na vyombo vya ulinzi na usalama.

**93.** ***Mheshimiwa Spika***, mbali na mkakati huo, Serikali kupitia televisheni ya Taifa TBC imeanzisha kipindi maalumu cha Maadili, Uzalendo na Utaifa kinachojulikana kwa jina la ***"Sisi ni Tanzania"***. Kipindi hiki ni mahususi kwa ajili ya kuukumbusha umma wa Watanzania kuhusu umuhimu wa kurejea kwenye misingi ya maadili, mila, desturi, miiko, uzalendo na uadilifu.

**94.** ***Mheshimiwa Spika***, pamoja na jitihada zinazochukuliwa na Serikali katika kukabiliana na mmomonyoko wa maadili nchini, ulinzi wa maadili na utamaduni wetu ni jukumu mtambuka na linamgusa kila mtu katika jamii kwani Serikali pekee haiwezi. Familia, Taasisi za dini, mashirika na watu binafsi wanapaswa

kushiriki kikamilifu katika kulinda na kurithisha maadili kwa jamii hususan watoto na vijana. Wazazi na Walezi wanahimizwa kusimamia malezi bora, ikiwamo kudhibiti maudhui wanayoyapata watoto kupitia vyombo vya habari. Ushirikiano wa wadau wote ni msingi wa kulinda utamaduni na maadili ya Taifa. Hivyo, nitoe wito kwa jamii nzima, kila mtu katika nafasi yake kulinda maadili ya Taifa na Utamaduni wetu kwa wivu mkubwa kwani hatuwezi kuwa Taifa lenye maendeleo kama tusipotengeneza kizazi chenye maadili.

**95.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuhakikisha kuwa watanzania wanaendelea kujivunia, kusherehekea, kuenzi, kuthamini na kunufaika na urithi wa utamaduni wao, Serikali iliratibu matamasha manne (4) ya utamaduni yaliyoandaliwa na wadau. Matamasha hayo ni Tamasha la 16 la Muziki wa Cigogo lililofanyika katika viwanja vya Mshikamano vilivyopo Wilaya ya Chamwino, Dodoma tarehe 25 - 27 Julai, 2025; Tamasha la Utalii na Utamaduni la Serengeti (Serengeti Cultural Festival) lililofanyika tarehe 22 - 25 Julai, 2025 Mgumu wilayani Serengeti, mkoani Mara; Tamasha la Utamaduni wa Wamaasai (Orkwaak le Maa Festival Week) lililofanyika tarehe 23 - 24 Agosti, 2025 Siha mkoani Kilimanjaro na Tamasha la Utamaduni la Jamii ya Wahaya (Ijuuka Omuka) lilifanyika tarehe 18 - 22 Desemba, 2025 mkoani Kagera.

Aidha, Wizara ilishiriki katika matukio mawili (2) ya kimila na kihistoria ambayo ni uzinduzi wa sherehe ya Kimila ya ubadilishanaji rika wa jamii ya Kimaasai ya Enkipaata iliyofanyika tarehe 18 - 21 Oktoba, 2025 mkoani Arusha; pamoja na Kumbukizi ya Mashujaa wa Vita vya Majimaji na Tamasha la Utalii wa Utamaduni lililofanyika tarehe 19 - 27 Februari, 2026 Songea mkoani Ruvuma. Kufanyika kwa matamasha ya utamaduni na matukio ya kimila na kihistoria ni muhimu sana kwani kunaimarisha mshikamano wa kitaifa, kurithisha tamaduni na kukuza utalii wa kiutamaduni.

**96.** ***Mheshimiwa Spika***, Utamaduni ni msingi wa utambulisho wa Taifa. Katika Taifa letu utamaduni umejengwa kwenye misingi ya utu, upendo, mshikamano, udugu na utaifa. Moja ya nyenzo muhimu ya kufanya utamaduni uwe hai ni kufanya matamasha

ya utamaduni. Hivyo, ni wajibu wetu kuuenzi, kuuhifadhi na kuuendeleza kwa manufaa ya kizazi cha sasa na kijacho. Kwa msingi huo, Serikali inasisitiza kuendelea kufanyika kwa matamasha ya utamaduni na matukio ya kihistoria katika jamii mbalimbali nchini kwa sababu yanaufanya utamaduni wetu kuendelea kuishi. Tukishindwa kuuenzi utamaduni wetu tutapoteza sifa ya kuwa taifa. Hivyo, tujivunie, tuuenzi na kuuendeleza urithi wa utamaduni wetu.

**97.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imefanya tathmini ya utekelezaji wa Sera ya Utamaduni ya mwaka 1997 kwa lengo la kubainisha mafanikio, changamoto na mapungufu ya utekelezaji wa Sera hiyo. Hatua inayofuata ni kukamilisha uhuishaji wa sera hiyo.

**98.** ***Mhesimiwa Spika,*** katika kuhakikisha kuwa tunaimarisha utendaji kazi wa wataalamu na kuongeza tija na ufanisi kwenye utoaji wa huduma kwa wananchi, Serikali kupitia Wizara iliratibu Kikao Kazi cha kumi na sita (16) cha Maafisa Utamaduni nchini kilichofanyika tarehe 28 - 31 Machi, 2026 katika ukumbi wa AICC jijini Arusha. Kikao kazi hicho kiliwakutanisha Maafisa Utamaduni zaidi ya 250 kutoka Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini kwa ajili ya kujadili hali ya utekelezaji wa majukumu; kubainisha changamoto zinazokabili utendajikazi; na kupendekeza namna bora ya kuzitatua ili kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma kwa wananchi. Kufanyika kwa vikao vya kisekta ni jukwaa muhimu la kuwakutanisha watunga sera (Wizara) na watekelezaji wa Sera (Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa) kubadilishana uzoefu na kunoa ujuzi. Miongoni mwa matokeo ya vikao hivi ni kuongezeka kwa ufanisi na utendajikazi wa Maofisa Utamaduni katika maeneo yao; kupanuka kwa wigo wa ushirikiano miongoni mwao; na kuimarishwa kwa ari ya utoaji wa huduma kwa wananchi.

### 3.2.2.2 BARAZA LA KISWAHILI LA TAIFA (BAKITA)

**99.** ***Mheshimiwa Spika,*** Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) liliundwa kwa Sheria ya Baraza la Kiswahili la Taifa Sura ya 52. Kwa mujibu wa Sheria hiyo, Baraza ni chombo cha Serikali chenye dhamana ya kusimamia matumizi na maendeleo ya lugha ya

Kiswahili na kufuatilia maendeleo yake ndani na nje ya nchi. Katika kutekeleza jukumu hilo la msingi, BAKITA inatekeleza Mkakati wa Taifa wa Kupeleka Kiswahili kimataifa, inasimamia matumizi sahihi ya lugha ya Kiswahili na kuzuia upotoshaji wake. Pia, inatoa ithibati ya matumizi ya lugha ya Kiswahili sanifu na fasaha katika vitabu vinavyoandikwa kwa Kiswahili pamoja na kutoa tafsiri rasmi ya lugha ya Kiswahili. Majukumu mengine ni pamoja na kuratibu vyama, asasi na wadau wote wanaojishughulisha na ukuzaji na uendelezaji wa lugha ya Kiswahili na kuhimiza matumizi ya lugha ya Kiswahili katika shughuli za Serikali na umma na kushirikiana na mamlaka nyingine zinazohusika katika kuanzisha tafsiri sanifu ya istilahi za Kiswahili katika nyanja mbalimbali. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Aprili 2026, BAKITA imetekeleza majukumu mbalimbali yafuatayo:

**100.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuhakikisha Kiswahili kinaendana na mabadiliko ya teknolojia, BAKITA imeandaa Kongoo ya Kiswahili ya Taifa (KOKITA), shughuli hii ya pekee kwa lugha ya Kiswahili inayolenga kusheheneza Kiswahili katika teknolojia ya kikopyuta na kuhifadhi pamoja na kuonyesha muktadha wa matumizi ya maneno ya Kiswahili katika Nyanja mbalimbali na kuwa na nyenzo za kuwasaidia wanafunzi wa Kiswahili kama lugha ya kigeni, wanaleksikografia, waandishi wa vitabu na watafiti wa lugha mbalimbali. Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Aprili 2026, BAKITA imekusanya, imehariri na kuingiza maneno milioni 22 katika Kongoo ya Kiswahili ya Taifa (KOKITA), ambapo hadi Aprili 2026, kongoo hiyo ina jumla ya maneno milioni 61 na lengo ni kufikisha maneno milioni 100. Kongoo hii itakuwa daraja la kuongeza nafasi ya Kiswahili katika teknolojia ya kikompyuta hususani katika matumizi ya Akili Unde (AI). Pia, Baraza linaendelea kukuza ushirikiano na wadau mbalimbali wakiwamo Taasisi ya Mozilla ili kuwezesha kuimarisha Kiswahili katika Teknolojia.

**101.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kupitia BAKITA imeongoza umma wa wazungumzaji wa Kiswahili, wadau na wapenzi wa Kiswahili Afrika na Duniani kote kushughudia hatua kubwa ya Kiswahili kukubalika kuwa lugha rasmi ya Mkutano Mkuu wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO). Kiswahili ni lugha ya kwanza ya Afrika kupata hadhi hiyo na hayo

yalijiri katika Mkutano Mkuu wa 43 wa Shirika hilo uliofanyika Samarkand - Uzbekstani tarehe 30 Oktoba hadi 13 Novemba, 2025. Kwa muktadha huo, Kiswahili sasa ni lugha rasmi ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, Jumuiya ya Maendekleo kwa Nchi za Kusini mwa Afrika, Umoja wa Afrika, Umoja wa Wazalishaji Almasi Afrika na UNESCO. Vilevile, Kiswahili ni lugha pekee ya Afrika iliyotengewa siku ya kuadhimishwa ambayo ni tarehe 7 Julai kila mwaka. Katika hatua nyingine, Wizara kupitia BAKITA imefanya kikao na UNESCO pamoja na wadau wa maudhui ya mtandaoni kuhusu nafasi ya Kiswahili katika mitandao mikubwa ya kijamii ya META, TikTok na Google ili wapanue nafasi ya Kiswahili katika mitandao hiyo na hivyo kuongeza ajira na kipato kwa waandaaji wa maudhui kupitia mitandao ya kijamii.

**102.** ***Mheshimiwa Spika***, nyota ya Kiswahili imeendelea kuangaza Kimataifa baada ya Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO) kuridhia Lugha hiyo kuwa mojawapo ya Lugha rasmi zitakazotumika katika Mikutano Mikuu ya Shirika hilo. Hatua hii inaifanya lugha ya Kiswahili kuwa lugha ya kwanza yenye asili ya Afrika kupewa hadhi hiyo. Jitihada hizi ni hatua za makusudi za Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kuhakikisha Kiswahili kinapata hadhi katika majukwaa ya kimataifa, ambapo kwa sasa Kiswahili ni Lugha rasmi ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), Jumuiya ya Maendeleo ya nchi za Kusini mwa Afrika (SADC), Jumuiya ya Wazalishaji Almasi Afrika (ADPA) na Umoja wa Afrika (AU).

**103.** ***Mheshimiwa Spika***, pia, Lugha ya Kiswahili imetengewa Siku Maalumu ya Kuadhimishwa Duniani na Shirika la UNESCO ambapo hufanyika kila ifikapo tarehe 7 Julai kila mwaka. Kwa kuenzi siku hiyo, Serikali kupitia BAKITA kwa kushirikiana na BAKIZA iliungana na balozi mbalimbali ndani na nje ya Tanzania pamoja na mashirika mbalimbali ya kimataifa ikiwamo UNESCO kufanya maadhimisho ya Nne ya siku ya Kiswahili Duniani ambayo kitaifa yalifanyika Zanzibar kuanzia tarehe 05 - 07 Julai, 2025. Maadhimisho hayo yalitanguliwa na Mbio za Masafa za Kimataifa za Kiswahili zilizofanyika tarehe 28 Juni 2025 jijini Arusha chini ya Kaulimbiu “Kiswahili Fahari ya Afrika, tukienzi na kukiendeleza”.

Aidha, maadhimisho yaliendelea tarehe 5 Julai, 2025 kwa tukio la Usiku wa Mwanamke Hazina lililokuwa na mada ya "Nafasi ya mwanamke katika Utawala na Uongozi" kwa mtazamo wa Fasihi ya Afrika. Tukio hilo lilikwenda sambamba na usiku wa Mswahili uliofanyika katika Ukumbi wa New Amani Hotel, Zanzibar.

**104.** ***Mheshimiwa Spika***, matembezi ya wanafunzi na wadau wa Kiswahili yaliendelea tarehe 6 Julai, 2025 ambayo yalianzia Skuli ya Sekondari ya Tumekuja na kuishia katika Viwanja vya Polisi Ziwani Zanzibar. Matembezi hayo yalilenga kuhimiza matumizi ya Lugha ya Kiswahili miongoni mwa Wanafunzi na wadau wa Kiswahili. Kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Kiswahili Duniani (MASIKIDU) kilifanyika katika Ukumbi wa Polisi Ziwani Zanzibar mnamo tarehe 7 Julai 2025, ambapo Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla, Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar aliyemwakilisha Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika kufunga maadhimisho hayo. Maadhimisho hayo yalikuwa na kaulimbiu: "Kiswahili kwa Amani na Mshikamano."

**105.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, BAKITA iliratibu ushiriki wa Tanzania katika maadhimisho ya Nne ya kikanda ya siku ya Kiswahili Duniani kwa nchi za jumuiya ya Afrika Mashariki, yaliyoratibiwa na Kamisheni ya Kiswahili ya Afrika Mashariki (KAKAMA) yaliyofanyika Kikanda Kigali, Rwanda. Pia maadhimisho hayo yalifanyika kwenye Maonyesho ya Dunia ya Biashara, Osaka Expo 2025 nchini Japani. Halikadhalika, balozi mbalimbali za Tanzania ziliadhimisha siku hiyo ya Kiswahili na kuonyesha masuala mbalimbali ya utamaduni wa Mswahili ikiwa ni pamoja na vyakula na mavazi.

**106.** ***Mheshimiwa Spika***, BAKITA ilipata nafasi ya kushiriki katika Kongamano la Kiswahili na Tuzo za Wasta lililofanyika tarehe 10 - 11 Oktoba, 2025 jijini Nairobi, Kenya na kongamano la Kiswahili lililoandaliwa Uganda tarehe 13 - 17 Aprili, 2025. Aidha, BAKITA ilishiriki Kongamano la Chama cha Kiswahili Duniani (CHAUKIDU) liliofanyika tarehe 14 - 16, Desemba, 2025 nchini Kenya. Makongamano haya yote yalikuwa na lengo la kuwaleta pamoja walumbi, wataalamu na wadau wa Kiswahili kujadili mambo

mbalimbali ya kukienzi na kukiendeleza Kiswahili.

**107.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha Kiswahili kinasheheni msamiati mpya na unaokidhi mahitaji katika nyanja mbalimbali, BAKITA kwa kushirikiana na wadau mbalimbali vikiwamo vyuo vikuu, Wizara, pamoja na wataalamu wa lugha katika uga wa istilahi, isimu na lahaja waliunda jopo la pamoja na kuandaa Mwongozo wa Usanifishaji Mkubwa wa Pili (II). Usanifishaji huu unafanyika baada ya ule wa mwaka 1,930, ambao unalenga kuboresha na kukusanya maneno mengi zaidi kutoka katika lugha za Afrika ili kujenga umiliki wa pamoja wa lugha ya Kiswahili barani Afrika. Halikadhalika, BAKITA inaendelea kufanya utafiti wa maneno, ambapo maneno 1,371 yamekusanywa kutoka lugha mbalimbali za Kibantu kama Luganda, Kinyarwanda, Kilingala, Kioshiwambo, na Kizulu, ikiwa ni sehemu ya maandalizi ya mradi wa usanifishaji mkubwa. Kazi hii ni hatua muhimu baada ya Kiswahili kupata hadhi maalumu katika jumuiya za kikanda na kimataifa.

**108.** ***Mheshimiwa Spika,*** sambamba na hilo katika kuelekea mashindano ya Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON) 2027, Serikali kupitia BAKITA inaendelea na shughuli ya usanifishaji wa Istilahi za michezo, ambapo hadi sasa jumla ya istilahi 420 za michezo zimesanifishwa.

**109.** ***Mheshimiwa Spika***, Wahenga wanasema, "Asiyefahamu lugha, hafahamu mila". BAKITA imeendelea kuuelimisha umma kuhusu kuzingatia matumizi ya Kiswahili fasaha na sanifu pamoja na utamaduni wake. Shughuli hii imehusisha kuandaa na kurusha hewani jumla ya vipindi 1,057 kupitia vituo vya TBC Taifa, Radio One, UFM, Times FM, Clouds FM, Kiss FM, Wapo Redio, Channel Ten TV, Shine FM, Redio Maria, Idea FM na Radio Umoja wa Mataifa. Aidha, Baraza liliandaa maudhui 758 ya mtandaoni na kutoa elimu ya matumizi ya lugha ya Kiswahili kupitia mitandao ya kijamii ambayo ni *facebook*, *youtube*, na *instagram*, pamoja na kuandaa Makala 42 zilizochapishwa katika gazeti la HabariLEO toleo la kila siku ya Ijumaa. Jitihada hizi ni hatua muhimu za kuhakikisha wananchi wote wanatumia Kiswahili fasaha na sanifu katika shughuli za kila siku.

**110. *Mheshimiwa Spika,*** katika kutimiza azma ya Serikali ya kuwezesha Watanzania kunufaika na fursa za Kiswahili duniani, BAKITA imeendelea kuwanoa walimu wenye stadi za kufundisha Kiswahili kama lugha ya kigeni kwa kutoa mafunzo ya kuimarisha stadi za kufundisha Kiswahili kwa wageni. Baraza liliendesha kozi hiyo ya muda mfupi kwa walimu 83 jijini Dar es Salaam. Aidha, lilitoa Mafunzo hayo kwa walimu saba (7) katika Chuo Kikuu cha St. Johns jijini Dodoma, ambapo yalikuwa ni mafunzo ya kimkakati kwani walimu watano (5) walipata nafasi ya kufundisha Kiswahili kwa wenyeji nchini Afrika Kusini. Pia, Baraza lilitoa mafunzo ya aina hiyo kwa waongoza watalii 17. Mafunzo hayo yalifanyika jijini Arusha katika Shule ya Msingi Meru, ikiwa ni sehemu ya kukuza lugha ya Kiswahili kupitia utalii. Mafunzo haya yameongeza chachu kwani Watanzania wameendelea kunufaika na fursa za kujiajiri kupitia taaluma za Kiswahili na stadi nyingine husianifu, mathalani hadi Aprili 2026 jumla ya watanzania 507 wanafanya kazi ya ufundishaji wa Kiswahili nje ya nchi.

**111. *Mheshimiwa Spika,*** kuhusu Kiswahili kutumika kikamilifu katika utoaji wa huduma za umma, BAKITA imeendelea kutoa mafunzo ya msasa ya matumizi ya Kiswahili fasaha na sanifu pamoja na utamaduni wake kwa makundi maalumu. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Aprili 2026, Baraza kwa kushirikiana na Chama cha Waandishi Waendesha Ofisi Tanzania (TAPSEA), lilitoa mafunzo ya matumizi ya Kiswahili fasaha na sanifu na utamaduni wake kwa Waandishi Waendesha Ofisi (WWO) 844. Halikadhalika, mafunzo hayo yameendelea kwa Makatibu wa kamati za Halmashauri 12 pamoja na Wahudumu wa Mapokezi na Huduma kwa Wateja 52. Kwa ujumla washiriki 2,094 waliopatiwa mafunzo hayo. Natoa rai kwa kada zote kushiriki mafunzo haya, ili kujengewa uwezo wa kuwasiliana na kuandika nyaraka kwa Kiswahili fasaha na sanifu katika mazingira rasmi.

**112. *Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha vyombo vya habari vinaongeza wigo wa matumizi fasaha na sanifu ya lugha ya Kiswahili. Serikali imeendelea kutoa elimu na semina kwa wanahabari kwa nia ya kutilia mkazo matumizi ya Kiswahili fasaha na sanifu. Katika kutekeleza jukumu hilo, Baraza limeandaa na kufanya Kongamano la tano (5) la Idhaa zinazotangaza kwa

Kiswahili Duniani likiwa na kaulimbiu "Tasnia ya Habari, Msingi wa Maendeleo ya Kiswahili Duniani". Lengo kuu la Kongamano la Idhaa ni kuimarisha uhusiano wa taasisi za Kiswahili na vyombo vya habari ambavyo vinatekeleza jukumu kubwa la kukikuza na kukieneza Kiswahili ndani na nje ya nchi. Kongamano hili lilihusisha wamiliki wa vyombo vya habari, wahariri, watangazaji na waandishi katika redio, televisheni, magazeti na blogu za Kiswahili duniani. Aidha, washiriki wengine ni pamoja na maafisa habari wa Wizara, Idara, Taasisi, Kampuni na Mashirika yaliyomo nchini na watozi wa studio za muziki, filamu na matangazo. Pia, makundi mengine yaliyoshiriki ni pamoja na wawakilishi wa mashirika ya kimataifa, wataalamu wa lugha ya Kiswahili walio katika taasisi za Kiswahili, wawakilishi wa vyama vya Kiswahili, wachapishaji, wahadhiri na wanafunzi wa vyuo vikuu na walimu wa Kiswahili wa shule za sekondari za jijini Arusha. Kongamano lilifanyika katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Arusha (AICC) jijini Arusha tarehe 24 hadi 27 Machi, 2026.

**113.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuhakikikisha umahiri wa lugha ya Kiswahili kwa wageni wanaojifunza Kiswahili, BAKITA imeendesha mtihani wa kupima umahiri wa lugha ya Kiswahili kwa wageni. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Aprili 2026, Wizara kupitia Baraza iliandaa na kusimamia mtihani wa kupima umahiri wa lugha ya Kiswahili kwa wanafunzi wageni 29 kutoka nchi za Kenya (7), Ghana (5), Zimbabwe (3), Malawi (2), Somalia (1), Uingereza (1), Sudani (2), India (1), Nigeria (4), Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (3) na Jamhuri ya Cheki (1). Aidha, miongoni mwao ni madaktari 21 waliokuja nchini kufanya mafunzo ya vitendo chini ya Baraza la Madaktari Tanganyika (MCT). Aidha, upimaji wa Umahiri wa lugha ulifanyika kwa wanafunzi 25 wa shule ya kimataifa ya Breaburn ya jijini Arusha. Hatua hii ya msingi inaunga mkono jitihada za Serikali katika utoaji wa huduma bora kwa wananchi hasa zile zinazotolewa na wageni.

**114.** ***Mheshimiwa Spika,*** pia Serikali inaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kukuza na kueneza matumizi ya Kiswahili katika majukwaa ya kimataifa. Hatua hizo ni pamoja na kushirikiana na mashirika ya kimataifa na nchi rafiki katika kufundisha Kiswahili pamoja na kuandaa programu za mafunzo ya lugha hiyo kwa

wageni. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Aprili 2026, Wizara kupitia BAKITA ilitoa mafunzo ya lugha ya Kiswahili kwa wageni 57 kwa njia ya mkondoni, wakiwemo Wanafunzi 53 wa Chuo cha Triumphant na Wanadiplomasia wanne (4) kutoka nchini Namibia. Aidha, wageni 20 walipata mafunzo hayo kwa njia ya ana kwa ana yaliyotolewa katika ofisi za BAKITA jijini Dar es Salaam. Wageni hao walitoka nchi za Uingereza (2), Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (3), Jamhuri ya Cheki (Czech) (1), Uturuki (1), Zimbabwe (4), Uganda (3), Sudani Kusini (1), Ghana (2), Botswana (2) na China (1). Vilevile, zaidi ya wageni 607 wamepatiwa mafunzo hayo kupitia vituo vinavyofundisha Kiswahili kwa wageni, vinavyosimamiwa na BAKITA ndani na nje ya nchi.

**115.** ***Mheshimiwa Spika,*** BAKITA imefanya Tafiti kwa lengo la kuongeza maneno kwenye Kongoo ya Kiswahili ya Taifa (KOKITA). Tafiti tisa (9) zimefanywa katika nyuga za siasa, mazingira, elimu, sayansi na teknolojia, afya, uchumi, sanaa, michezo na kilimo. Utafiti huu umefanywa kwa kushirikiana na vyuo vikuu, wataalamu wa istilahi, wataalamu katika sekta husika pamoja na wadau mbalimbali wa lugha ya Kiswahili ambapo umewezesha kuongeza takribani maneno milioni 22 katika kongoo ya Taifa (KOKITA).

**116.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha huduma ya ukalimani inaimarika pamoja na kuchangamkia fursa zinazotokana na mikutano ya kitaifa na kimataifa inayofanyika ndani na nje ya nchi, BAKITA ilitoa mafunzo ya msasa ya kuwajengea uwezo wakalimani 18. Mafunzo hayo yalifanyika kwa wiki mbili kuanzia tarehe 17 hadi 28 Novemba, 2025 katika darasa maalumu la Ukalimani lililopo ofisi za BAKITA jijini Dar es Salaam. Idadi hii inafanya nchi kuwa na jumla ya wakalimani 183 waliotambuliwa na BAKITA. Aidha, Baraza liliratibu na kutoa huduma za ukalimani katika mikutano 19 ya kitaifa na kimataifa. Miongoni mwa mikutano hiyo ni: Pan Africa ILGA Conference in Johannesburg, South Afrika – Mistry Hills Hotel; The forth International Conference on Business Management and Economic Develpment (ICBMED): *Creativity, Innovation and Business for Economic Development* – Gold Crest Hotel Mwanza; *Regional Training and Certification Program for Biosafety and*

*Biosecurity Professionals* – NPHL Dar es Salaam; Haki za Wanawake katika Majiji – Zanzibar; Kusikiliza shauri la kesi ya madai – Mahakama Kuu pamoja na Shauri la kukutwa na nyara za Serikali (Kasa na Kobe wa majini) – Kituo cha Polisi Sitakishari, Ukonga - Dar es Salaam.

**117.** ***Mheshimiwa Spika,*** ufunguaji wa vituo vya kufundishia Kiswahli kwa wageni ni sehemu ya utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa kufanya Kiswahili kuwa bidhaa ya miaka kumi (10) kutoka 2022 – 2032. Katika kuhakikisha dhamira ya Serikari ya awamu ya sita katika kukuza na kuendeleza Kiswahili duniani, BAKITA imetambua na kusajili jumla ya vituo vitano (5). Vituo hivyo ni pamoja na *Kiswahili Centre of Excellence in South Afrika* (KCESA), *Tanzania Kiswahili Cultural Centre* vyote vya nchini Afrika ya Kusini na vinamilikiwa na Watanzania waishio Afrika Kusini. Aidha, kituo kimoja (1) cha Imani Languages Academy kinachomilikiwa na Mtanzania kimesajiliwa nchini Japani. Vituo viwili (2) vimefunguliwa ndani ya nchi, ambapo ni pamoja na St. Constantine's International school jijini Arusha na Laoshi Institute of Languages cha jijini Dar es Salam. Hatua hii inafanya kuwe na jumla ya vituo 55 vya kufundisha Kiswahili kwa wageni, ambapo vituo 20 vipo nje ya nchi na 35 vipo nchini. Ufunguaji wa vituo hivi umeongeza chachu ya ujifunzaji wa Kiswahili kwa wageni.

**118.** ***Mheshimiwa Spika***, Fauka ya hayo, nafasi ya Kiswahili Kimataifa inategemewa kuimarisha ajira na fursa kwa wataalamu wa Kiswahili katika Ufundishaji, Tafsiri, Ukalimani, Uandishi wa Vitabu na Utangazaji. Ni azma ya Nchi yetu kukuza diplomasia, shughuli za kiuchumi, uwekezaji, kilimo, utalii, madini, viwanda na biashara kupitia lugha ya Kiswahili. Pamoja na kazi kubwa iliyofanywa katika eneo hili la lugha adhimu na aushi ya Kiswahili, naomba kulitaarifu Bunge lako tukufu kuwa hadi sasa Kiswahili ni miongoni mwa lugha kubwa saba (7) duniani zilizotambuliwa na kupangiwa siku yake ya kuadhimishwa. Kiswahili ni lugha pekee ya Afrika katika lugha hizo. Kwa msingi huo tuna kila sababu ya kujivunia mafanikio makubwa tuliyoyapata ya lugha ya Kiswahili, moja ya Tunu muhimu na urithi wa Taifa letu.

### 3.2.2.3 KITUO CHA URITHI WA UKOMBOZI WA BARA LA AFRIKA

**119.** ***Mheshimiwa Spika***, Kituo cha Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika (ALHC) kinaratibiwa na Wizara kwa mujibu wa Azimio la Umoja wa Afrika la mwaka 2011 (Assembly/AU/Dec.357 (XIV)), lililoridhia Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa kitovu cha uhifadhi wa kumbukumbu za harakati za ukombozi wa Afrika kwa manufaa ya kizazi cha sasa na kijacho. Uamuzi huu haukuwa wa bahati mbaya, bali ni matokeo ya mchango mkubwa na wa kihistoria wa Tanzania katika mapambano ya ukombozi wa nchi nyingi za Afrika.

**120.** ***Mheshimiwa Spika***, kituo hiki kina jukumu pana na la kimkakati la kutambua, kukusanya, kuhifadhi na kuendeleza urithi wa ukombozi unaojumuisha nyaraka, picha, filamu, hotuba za viongozi, ramani, nyimbo, sare, pamoja na maeneo muhimu ya kihistoria kama vile makaburi ya mashujaa, kambi za wapigania uhuru na miundombinu ya ukombozi. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Aprili 2026, Wizara kupitia Kituo hiki imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa kama ifuatavyo:

**121.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali inaendelea kudumisha hadhi ya Tanzania kama "Mama wa Ukombozi wa Afrika" kwa vitendo, kwa kuhakikisha kuwa mchango wetu wa kihistoria unatambulika, unahifadhiwa na kuendelezwa kwa manufaa ya vizazi vya sasa na vijavyo. Katika kuonesha dhamira hiyo, tunamshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa uamuzi wake wa kimkakati wa kuutekeleza mradi wa ujenzi wa Makao Makuu ya Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika kama ilivyoazimiwa na Umoja wa Afrika. Hatua hii inaakisi uongozi thabiti na dira ya kulinda historia ya Taifa letu huku tukiiweka katika nafasi ya kimataifa kama kitovu cha kumbukumbu za ukombozi wa Bara la Afrika.

**122.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika hatua ya utekelezaji, Wizara kupitia Kituo imetenga eneo lenye ukubwa wa ekari 424.6 katika Wilaya ya Kongwa, Mkoa wa Dodoma kwa ajili ya ujenzi wa Kituo Kikuu cha Uhifadhi wa Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika kitakachokuwa Taasisi ya Umoja wa Afrika. Eneo hilo tayari limeshamilikishwa rasmi kwa Wizara, hatua inayoweka msingi

imara wa utekelezaji wa mradi huu wa kimkakati wa kitaifa na kibara. Aidha, maandalizi yanaendelea ikiwa ni pamoja na taratibu za kumpata Mshauri Elekezi na Mkandarasi wa ujenzi. Hakika, Kituo hiki hakitakuwa tu alama ya kihistoria ya urithi wa ukombozi, bali pia kitakuwa kichocheo cha maendeleo ya kiuchumi kupitia utalii wa kihistoria, kitaongeza ajira kwa vijana, na kuleta manufaa kwa Wilaya ya Kongwa na Taifa kwa ujumla, sambamba na kuimarisha mshikamano wa kitaifa na nafasi ya Tanzania kama kielelezo cha uongozi na mshikamano wa Bara la Afrika katika kuendeleza urithi na uchumi wa utamaduni.

**123.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imeendelea kuonesha dhamira ya dhati na isiyotetereka katika kulinda na kuhifadhi urithi wa ukombozi ambao ni msingi wa historia, heshima na utambulisho wa Taifa letu. Ni dhahiri kuwa bila historia imara Taifa hupoteza dira, na bila kuilinda tunahatarisha mustakabali wa vizazi vijavyo. Katika kutekeleza azma hiyo, Wizara kupitia Kituo ilipanda miche 700 ya mianzi kandokando ya Mto Ngerengere katika eneo la Mazimbu, Mkoa wa Morogoro kwa lengo la kudhibiti mmomonyoko wa udongo uliokuwa unatishia makaburi ya mashujaa wa ukombozi. Hatua hii imeimarisha ulinzi wa mazingira ya maeneo ya kumbukumbu za kihistoria na kuhakikisha makaburi hayo yanaendelea kuhifadhiwa kwa usalama, hivyo kuthibitisha kuwa Serikali ni sikivu, inachukua hatua na inaweka msingi imara wa kizazi kijacho kujivunia chimbuko lake.

**124.** ***Mheshimiwa Spika***, sambamba na hilo, Serikali imechukua hatua madhubuti za kuimarisha utambuzi na heshima kwa mashujaa wa harakati za ukombozi. Wizara kupitia Kituo imeweka vibao 35 vya utambulisho katika makaburi ya wapigania uhuru wa Afrika Kusini yaliyopo Mazimbu na Dakawa, hatua iliyoongeza upatikanaji wa taarifa sahihi kwa wageni, wanafunzi na watafiti, pamoja na kuinua hadhi ya maeneo hayo kuwa vituo hai vya elimu ya historia ya ukombozi. Aidha, mabango nane ya utambulisho wa kihistoria yamesimikwa katika maeneo ya Kaole (Pwani), Mazimbu na Dakawa (Morogoro), pamoja na Kongwa (Dodoma) ili kuboresha utoaji wa taarifa kwa umma. Vilevile, maboresho ya mfumo wa maji katika eneo la makaburi ya Dakawa yamefanyika ili kuwezesha umwagiliaji wa maua na

kuboresha mandhari ya eneo hilo, hatua inayochangia kuhifadhi heshima na hadhi ya maeneo ya kumbukumbu za mashujaa wetu.

**125.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali inaendelea kubaki mstari wa mbele katika kuimarisha uhifadhi wa rasilimali za kumbukumbu ambazo ni mhimili muhimu wa historia ya Taifa na Bara kwa ujumla. Katika kutekeleza jukumu hilo, Wizara kupitia Kituo ilifanya kazi ya kitaalamu ya kuchambua, kupanga na kuhifadhi nyaraka za kihistoria zilizopo katika Ofisi za Kituo cha Maendeleo Dakawa. Nyaraka hizo zinajumuisha vitabu na machapisho yaliyotumiwa na wanafunzi wa chama cha African National Congress (ANC) waliokuwa wakisoma nchini Tanzania wakati wa harakati za ukombozi. Zoezi hili lilifanyika kwa kuzingatia viwango vya kitaalamu vya uhifadhi wa kumbukumbu, ikiwemo matumizi ya maboksi maalumu yanayolinda nyaraka dhidi ya uharibifu wa kimazingira, na hivyo kuongeza usalama na uendelevu wa nyenzo hizi muhimu kwa matumizi ya tafiti, elimu na rejea za kihistoria.

**126.** ***Mheshimiwa Spika,*** sambamba na juhudi hizo, Kituo kilifanya mahojiano na mashuhuda 40 wa harakati za ukombozi wa Afrika kwa lengo la kuhifadhi simulizi na ushuhuda binafsi wa matukio ya kihistoria. Hatua hii imewezesha kuhifadhi historia hai ya ukombozi ambayo ni rasilimali adimu na yenye thamani kubwa kwa tafiti za kitaaluma, elimu ya kizazi kipya na uendelezaji wa utambulisho wa Bara la Afrika. Miongoni mwa mashuhuda hao ni Bi. Sophia Halfani Namananda, aliyewahi kufundisha watoto wa wapigania uhuru wa FRELIMO katika Shule ya Msingi Lusewa, Songea mkoani Ruvuma, ushuhuda wake ukiwa kielelezo hai cha mchango wa Tanzania katika kuandaa na kulea kizazi cha wapigania uhuru barani Afrika.

**127.** ***Mheshimiwa Spika***, kwa lengo la kuandaa na kusambaza maarifa ya kihistoria kwa vizazi vya sasa na vijavyo, Serikali imejipambanua kwa vitendo zaidi. Kituo imekamilisha uandaaji wa rasimu tatu (3) za vitabu ambavyo ni *Maeneo ya Urithi wa Ukombozi*; *Mchango wa Wanawake katika Harakati za Ukombozi wa Afrika*; pamoja na *Hotuba za Viongozi wa Afrika*. Machapisho

hayo yataongeza upatikanaji wa taarifa sahihi kuhusu historia ya ukombozi wa Afrika na mchango wa Tanzania katika harakati hizo. Aidha, vitabu hivi vitatumika kama nyenzo muhimu katika taasisi za elimu, tafiti za kihistoria na katika kuhamasisha vijana kuelewa na kuthamini historia ya Bara la Afrika. Katika kipindi cha hadi mwezi Aprili 2026, Kituo kinaendelea na hatua za kitaalamu za uhakiki wa maudhui, uhariri pamoja na maandalizi ya uchapishaji ili kuhakikisha ubora na usahihi wa machapisho hayo kabla ya kusambazwa kwa umma.

**128.** ***Mheshimiwa Spika***, kwa msukumo wa dhati, Serikali imejipanga kuimarisha utalii wa kihistoria na kuongeza uelewa kuhusu mchango wa Tanzania katika ukombozi wa Afrika kupitia uratibu wa ziara 16 zilizofanyika katika maeneo muhimu ya kihistoria yaliyopo katika mikoa ya Morogoro, Pwani, Ruvuma, Dar es Salaam, Dodoma na Iringa. Ziara hizi zilihusisha wadau mbalimbali wakiwemo maafisa wa Serikali, wanafunzi, watafiti, pamoja na wageni kutoka nje ya nchi. Ziara hizi zimechangia kwa kiasi kikubwa kuongeza uelewa wa historia ya ukombozi, kukuza utalii wa urithi na kuimarisha ushirikiano wa kikanda na kidiplomasia. Vilevile, ziara za viongozi wa ngazi za juu, akiwemo Makamu wa Rais wa Zimbabwe Mheshimiwa Kembo Campbell Mohadi aliyetembelea Kaole, Bagamoyo tarehe 31 Agosti, 2025, zimeendelea kuimarisha uhusiano wa kihistoria na kuthibitisha nafasi ya Tanzania kama kitovu cha urithi na historia ya ukombozi wa Bara la Afrika.

**129.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imeendelea kuimarisha uelewa wa historia ya ukombozi wa Afrika kwa kizazi cha sasa na kijacho kupitia kampeni za elimu, uhamasishaji na ushirikiano wa kimkakati, zikiwemo ziara 10 za elimu katika shule za Dar es Salaam, matumizi ya vyombo vya habari na mitandao ya kijamii, pamoja na ushiriki katika majukwaa ya maonesho ya kitaifa ikiwemo Sabasaba, kumbukizi ya Vita vya Maji Maji na mikutano ya kitaifa ya Sekta mbalimbali hatua zilizowezesha kuwafikia maelfu ya wananchi na vijana. Kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali ikiwemo Shirika la Utangazaji Tanzania na Taasisi ya Elimu Tanzania, Kituo kimeendesha vipindi maalum vya elimu na kutoa mafunzo kwa wadau wa sekta ya elimu, hatua

zinazodhihirisha dhamira thabiti ya Serikali ya kuendeleza urithi wa ukombozi kama chachu ya uzalendo, utambulisho wa Taifa na mshikamano wa kijamii.

**130.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha uelewa wa vijana na umma kuhusu harakati za ukombozi wa Afrika, Kituo iliratibu Maadhimisho ya Siku ya Ukombozi wa Nchi za Kusini mwa Afrika tarehe 23 Machi 2026 jijini Dar es Salaam, yaliyobebwa na kaulimbiu inayohamasisha ukuaji wa viwanda, mabadiliko ya kilimo na mpito wa nishati kwa SADC imara. Maadhimisho hayo yamekumbusha na kuimarisha mshikamano wa kihistoria wa ukombozi, huku yakisisitiza kuwa urithi huo ni chachu ya ushirikiano wa kikanda na maendeleo ya pamoja, na hivyo kuendeleza dhamira ya nchi wanachama kushirikiana kwa karibu zaidi kwa ustawi wa wananchi wa ukanda wa Kusini mwa Afrika.

**131.** ***Mheshimiwa Spika***, chini ya maelekezo na msukumo wa Serikali ya Awamu ya Sita, Serikali imeendelea kuchukua hatua za kimkakati kuhakikisha urithi wa kihistoria wa Taifa unalindwa na kudumu kwa manufaa ya vizazi vya sasa na vijavyo. Kituo imeendelea kufanya ufuatiliaji na tathmini ya uhifadhi wa maeneo muhimu ya kihistoria ikiwamo Kongwa - Dodoma, Kaole – Pwani, na Kinondoni – Dar es Salaam, kwani maeneo ya urithi wa ukombozi yamekuwa yakikumbwa na changamoto ya kuharibika kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo mabadiliko ya tabianchi na mazingira, shinikizo la kibiashara, maendeleo ya miji, pamoja na ukosefu wa uelewa wa jamii kuhusu umuhimu wa maeneo hayo.

**132.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imechukua hatua kadhaa za kuzuia hali hiyo isiendelee kwa kuongeza juhudi za ukarabati na matengenezo katika baadhi ya maeneo hayo. Pamoja na changamoto hizo, Serikali imeongeza kasi ya ukarabati na matengenezo ya maeneo hayo, huku ikiimarisha ushirikiano na taasisi za kikanda na kimataifa kama Umoja wa Afrika kwa lengo la kubadilishana uzoefu na kujenga mikakati madhubuti ya pamoja ya kuhifadhi urithi wa ukombozi, hatua ambazo zinaendelea kudhihirisha nia ya dhati ya Serikali ya kuhakikisha maeneo haya yanabaki salama na kuendelea kuwa sehemu ya

fahari ya Taifa.

**133.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali ya Awamu ya Sita inaendelea kuimarisha utambulisho wa Taifa kupitia uhifadhi na utangazaji wa urithi wa kihistoria kama kichocheo cha maendeleo na utalii. Kituo kimefanikisha kutangaza maeneo saba (7) ya historia ya ukombozi wa Bara la Afrika na Hifadhi ya Malikale kuwa urithi wa Taifa ili yatambuliwe, yahifadhiwe na kulindwa kisheria kupitia Tangazo la Serikali na 582 la tarehe 26 Septemba, 2025 ambapo maeneo yaliyotangazwa ni Kambi ya Wapigania uhuru wa Chama cha ANC iliyopo Mazimbu - Morogoro, Kambi ya Wapigania Uhuru wa chama cha FRELIMO iliyopo katika Shule ya Sekondari Samora Machel - Ruvuma, Kambi ya Wapigania Uhuru ya Kihesa Mgagao - Iringa, Makazi ya Mtemi Fundikira - Tabora na Mtemi Isike - Singida na maeneo mengine ya kihistoria hivyo kufikisha idadi 15 ya maeneo ya historia yaliyotangazwa. Hatua ya kutangazwa kwa maeneo hayo inalenga kuyatambua, kuyahifadhi na kuyalinda kupitia sheria ya Malikale na kutangazwa kuwa maeneo ya kichocheo cha vivutio vya utalii wa kihistoria nchini.

**134.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuratibu kwa mafanikio mchakato wa kukifanya Kituo cha Urithi wa Ukombozi wa Afrika kuwa miongoni mwa taasisi rasmi zilizo chini ya Umoja wa Afrika; ambapo katika kikao cha Baraza la Mawaziri la Umoja wa Afrika kilichofanyika mwezi Februari, 2026, azimio la kukitambua na kukiridhia Kituo hicho lilipitishwa rasmi, sambamba na kutoa wito kwa nchi zote wanachama wa Bara la Afrika, Jumuiya za Kikanda pamoja na Mashirika ya Kimataifa kushirikiana na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika utekelezaji wake. Uamuzi huu una manufaa makubwa kwa nchi yetu, ikiwa ni pamoja na kuimarisha hadhi ya Tanzania kimataifa kama kitovu cha historia ya ukombozi wa Afrika, kuvutia rasilimali na uwekezaji katika uhifadhi na utalii wa urithi, kukuza ajira na utafiti wa kitaaluma, pamoja na kuimarisha elimu ya uzalendo na mshikamano wa Kiafrika kupitia ujumuishaji wa urithi wa ukombozi katika mitaala ya elimu kwa vizazi vya sasa na vijavyo.

### 3.2.3 SEKTA YA MAENDELEO YA SANAA

**135.** ***Mheshimiwa Spika****,* Sekta ya Maendeleo ya Sanaa nchini ina jukumu la kuratibu na kusimamia maendeleo ya Sanaa. Sekta hii ni moja ya maeneo muhimu sana katika maendeleo ya nchi yetu kutokana na mchango wake katika kutoa ajira hususan kwa vijana, kukuza utalii na kuitangaza nchi kimataifa. Sekta ya Sanaa inahusisha Idara ya Maendeleo ya Sanaa, Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA), Bodi ya Filamu Tanzania, Ofisi ya Hakimiliki Tanzania (COSOTA), Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSUBa) na Mfuko wa Utamaduni na Sanaa Tanzania.

#### 3.2.3.1 Idara ya Maendeleo ya Sanaa

**136.** ***Mheshimiwa Spika***, majukumu makuu ni kuandaa, kushauri na kusimamia sera, sheria, mipango na mikakati mbalimbali inayolenga kuleta mageuzi katika ukuaji wa Sekta ya Sanaa hapa nchini. Vipaumbele vya sasa ni kuimarisha miundombinu ya Sanaa, kuimarisha zaidi ulinzi wa hakimiliki, kupambana na uharamia, kulinda maadili katika kazi za Sanaa na kuhakikisha sekta inachangia kikamilifu uchumi wa mhusika mmoja mmoja na katika pato la Taifa. Katika kipindi cha Julai, 2025 na Aprili, 2026 Serikali imeandaa Katiba ya Mfano itakayotumiwa na Mashirikisho na Vyama vya Sanaa nchini kikiwa ni chombo cha kimkakati kinachounganisha mageuzi ya sanaa na maono mapana ya Taifa. Katiba hii itakapoanza kutumika mwaka 2026/2027 inatarajiwa kuwa mwarobaini wa migogoro isiyoisha na kuvifanya vyama na mashirikisho kuwa taasisi imara zinazojitegemea, zinazojisimamia, zenye hadhi sawa na zinazozalisha ajira na mapato. Katiba hizi zilizoandaliwa kwa ushirikiano mkubwa na wadau wenyewe zinatoa usawa katika maeneo muhimu ya uzingatiwaji wa sheria za kitaifa na kimataifa, maadili ya Taifa, elimu, mafunzo na uzoefu kwa viongozi, vipindi vya uongozi, hatma ya mali za Chama na Shirikisho pale uhai wake utakapokoma, uwazi kwenye mapato na matumizi, mifumo ya mawasiliano pamoja na uzingativu wa hirakia na taasisi nyingine. Taasisi hizi sasa zinakwenda kuwa kiungo muhimu kati ya Serikali na wadau wa kisekta na hivyo kurahisisha mawasiliano na mipango ya maendeleo.

**137.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Aprili 2026, Serikali ilifanya tathmini ya utekelezaji wa majukumu ya taasisi za BASATA, Bodi ya Filamu na Michezo ya Kuigiza, TaSUBa, COSOTA, pamoja na Mfuko wa Utamaduni na Sanaa Tanzania kwa lengo la kuhakikisha mipango ya muda mfupi na muda mrefu inazingatia malengo ya Dira ya Maendeleo ya Taifa 2050 inayoitambua sekta ya Sanaa na Burudani kama moja ya maeneo ya mageuzi ya kimkakati ya kulifikisha Taifa katika Uchumi wa Dola Trilioni Moja ifikapo mwaka 2050. Miongoni mwa matokeo ya tathmini hii ni kuongezeka kwa ushiriki wa vijana na watoto katika fani mbalimbali za Sanaa; kuimarika kwa mifumo ya kidijiti, kuongezeka kwa ulinzi wa hakimiliki na mapato ya wasanii, pamoja na maboresho ya miundombinu na upatikanaji wa mikopo na ruzuku kwa wadau. Aidha, maadili ya kazi za Sanaa yameendelea kuimarika, huku ukusanyaji wa takwimu ukisaidia kupanga maendeleo ya sekta kwa ufanisi zaidi. Mikakati iliyoafikiwa kujumuishwa katika mipango ya Taasisi ni uimarishaji wa miundombinu ya Sanaa, usimamizi wa hakimiliki, uimarishaji wa mifumo ya utoaji wa huduma kidijiti na uboreshaji wa huduma za kifedha miongoni mwa wadau wetu.

**138.** ***Mheshimiwa Spika,*** kufuatia utajiri wa asili wa nchi yetu, utamaduni, ukarimu amani, mshikamano na uzoefu uliopatikana kupitia mashindano ya *Miss and Mister Deaf International* yaliyosimamiwa na Serikali hapa nchini mwaka 202I, 2022 na 2023; waandaaji wa mashindano makongwe na makubwa zaidi ya ulimbwende duniani ya Miss World wameshawishika na kukubali Tanzania iwe mwenyeji mwaka 2027. Kati ya Julai 2025 hadi Aprili 2026 waandaaji hao wamefika hapa nchini mara tatu kwa lengo la kuiona nchi, kutembelea vivutio vyake na kujiridhisha na miundombinu yake. Katika ziara hizo, Tanzania imekuwa mwenyeji wa Miss World, Opal Suchata kutoka Thailand, Miss World Africa, Hasset Dereje kutoka Ethiopia na Bi. Julia Evelyn Morley, Mwenyekiti na Mkurugenzi Mkuu wa Miss World Limited. Kutokana na mashindano haya, Tanzania itanufaika kiuchumi kupitia viingilio, huduma kwa wageni, udhamini na mauzoo ya bidhaa kwa wageni; wabunifu wetu kupata kazi na uzoefu; nchi kutangazwa kupitia televisheni na mitandao duniani kote katika nyanja za utalii wa asili na utamaduni; kuimarisha diplomasia na

zaidi ya yote kuifanya dunia iamini tena kuwa Tanzania ni mahala salama kwa watu wote. Aidha, kufuatia kuhitimishwa kwa mashindano ya Miss World Tanzania tarehe 19 Aprili, 2026 mlimbwende Bi. Latricia Ian Sawe ameshinda na ataiwakilisha Tanzania katika mashindano ya Miss World nchini Vietnam mwezi Septemba 2026.

**139.** ***Mheshimiwa Spika***, Mashindano ya Miss World 2027 yatatumika kama kichocheo cha hamasa kuelekea AFCON 2027 na kuongeza mwamko wa kitaifa pamoja na ushiriki wa wananchi katika maandalizi ya tukio hilo kubwa la kihistoria barani Afrika.

**140. *Mheshimiwa Spika***, sambamba na hilo, Serikali imeendelea kuratibu Tamasha la Serengeti Music Festival ambalo limekuwa likifanyika kila mwaka tangu 2020 kama jukwaa muhimu la kukuza na kuendeleza vipaji vya wasanii wa Kitanzania kupitia Sanaa ya Muziki kwa ujumla, pamoja na kuwaunganisha Wasanii na masoko ya kitaifa na kimataifa. Kila mwaka, pamoja na malengo yake ya jumla, tamasha hili huwa na malengo mahsusi ambapo kwa mwaka huu, tamasha hili linalotarajiwa kufanyika tarehe 30 Mei, 2026 linalenga kutumika kama jukwaa la kuhamasisha ushiriki wa wananchi katika mashindano ya AFCON 2027. Tangu kuanzishwa kwake, tamasha hili lilifikia kilele cha mafanikio mwaka 2025 ambapo Mgeni Rasmi alikuwa Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa wakati huo. Kutokana na mchanganyiko mzuri wa waandaaji unaojumuisha Serikali na sekta binafsi hasa kutoka Vyombo vya Habari na Shirikisho la Muziki Tanzania, tamasha hili limekuwa jukwaa la wasanii wote wa Tanzania bara na Zanzibar bila kujali ushindani wao wa kimuziki.

**141.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2025 hadi Aprili 2026, Serikali imeendelea kuratibu kwa ufanisi shughuli za uhamasishaji kupitia Sanaa sambamba na michuano ya Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa ligi za Ndani (African Nations Championship 2024) na maandalizi ya Africa Cup of Nations (AFCON 2027) kwa lengo la kuhamasisha ushiriki wa

wananchi, kukuza uzalendo, na kuitangaza Tanzania kimataifa kupitia Sanaa na burudani. Katika utekelezaji huo, Wizara kwa kushirikiana na Baraza la Sanaa la Taifa na Baraza la Michezo la Taifa iliratibu Tamasha la CHAN-SINGELI lililofanyika tarehe 2 Agosti 2025 katika eneo la nje la Uwanja wa Benjamin Mkapa, ikiwa ni sehemu ya sherehe za uzinduzi wa mashindano hayo. Tamasha hili lilikuwa na mafanikio makubwa ambapo zaidi ya wasanii 30 wa muziki wa singeli walipata fursa ya kutumbuiza, wakihamasisha maelfu ya mashabiki wa soka kutoka ndani na nje ya nchi kushiriki sherehe hizo. Kupitia jukwaa hilo, Muziki wa singeli uliweza kutangazwa kimataifa kama sehemu ya utambulisho wa utamaduni wa Tanzania.

**142.** ***Mheshimiwa Spika***, katika muktadha huo huo, Serikali iliratibu Tamasha la Muziki Mchanganyiko lililofanyika tarehe 22 Agosti, 2025 katika eneo la nje ya Uwanja wa Benjamin Mkapa, jijini Dar es Salaam. Tamasha hili lilikuwa na lengo mahsusi la kuhamasisha wananchi kushiriki kikamilifu katika mashindano hayo, sambamba na kuishangilia Timu ya Taifa wakati wa mchezo wa Robo Fainali dhidi ya Timu ya Taifa ya Morocco.

#### 3.2.3.2 BARAZA LA SANAA LA TAIFA (BASATA)

**143.** ***Mheshimiwa Spika***, Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA) limeanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Baraza la Sanaa la Taifa Sura 204. Majukumu ya BASATA ni pamoja na kufufua na kukuza maendeleo ya sanaa nchini; kufanya tafiti za masuala mbalimbali kuhusu sanaa; kutoa ushauri na misaada ya kitaalamu kwa wasanii na wadau wa sanaa; kusajili wasanii na miundombinu ya sanaa nchini; na kutengeneza kanuni na miongozo ya kusimamia ubora wa kazi za sanaa.

**144.** ***Mheshimiwa Spika***, majukumu mengine, ni kuishauri Serikali kuhusu maendeleo ya sanaa nchini; kutunza kanzidata za wasanii na wadau wanaojishughulisha na kazi za sanaa; kuhimiza uzingatiaji wa maadili na tamaduni za Kitanzania katika kazi za sanaa miongoni mwa wasanii na wadau wa sanaa; kuhamamsisha maendeleo ya sanaa kwa njia ya maonesho, mashindano, matamasha, warsha na semina; kutoa na

kuimarisha mipango ya mafunzo kwa wadau wa sanaa; kuhimiza uanzishwaji wa vyama au mashirikisho ya sanaa kwa lengo la kuongeza idadi ya vikundi vinavyojishughulisha na kazi za sanaa; na kuchukua hatua za kinidhamu dhidi ya watu, vikundi, taasisi, vyama, au wamiliki wa miundombinu wanaojishughulisha na kazi za sanaa kwa kukiuka Sheria ya Baraza la Sanaa la Taifa.

**145.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali ya Awamu ya Sita imeendelea kuonesha dhamira thabiti ya kuendelea kutumia mifumo ya TEHAMA katika utoaji wa huduma kwa njia ya kidigiti. BASATA imeendelea kutekeleza jukumu la kuboresha mfumo wa AMIS (Artist Management Information System) na kuunganisha na mifumo mingine ya Serikali kama vile TRA Portal, NIDA, BRELA, GePG, TAUSI, NaPA, Mfumo wa Hakimiliki (CRIMIS) pamoja na NeST ili kurahisisha upatikanaji na ubadilishanaji wa taarifa mbalimbali. Aidha, ili kufanikisha azma hiyo, BASATA imeingia mkataba na Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA) kwa ajili ya kuboresha mfumo wa AMIS pamoja na kutengeneza programu tumizi ya simu (BASATA Mobile App) ambayo itarahisisha zaidi upatikanaji wa huduma za BASATA kwa njia ya kidigiti. Pia, Baraza limefanya mapitio ya kina ya mfumo wa biashara wa BASATA (Business Process System Review) yaliyolenga kuboresha taratibu za utoaji huduma, kuongeza uwazi, kupunguza urasimu na kuhakikisha huduma zinatolewa kwa haraka na kwa ufanisi zaidi kwa wasanii na wadau wa sanaa.

**146.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali katika kuhakikisha inawafikia wasanii wote nchini, BASATA imeendelea kukusanya na kuhifadhi takwimu za usajili wa wasanii, vikundi na taasisi za sanaa nchini ambapo hadi Aprili 2026 jumla ya wasanii 21,875 wamesajiliwa ikilinganishwa na wasanii 1,935 waliosajiliwa mwaka wa fedha 2024/25 sawa na ongezeko la asilimia 91. Takwimu hizi hutumika kama msingi muhimu katika kufanya tafiti, kuandaa mipango na kusaidia Serikali katika kufanya maamuzi ya kisera yanayolenga kuendeleza sekta ya sanaa na ubunifu nchini.

**147.** ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie nafasi hii kupongeza Serikali kwa kuweka mazingira wezeshi ya kufanya shughuli za sanaa. Aidha, BASATA imeendelea kuratibu na kusimamia matamasha pamoja

na utoaji wa Tuzo za Muziki kwa lengo la kutambua na kuthamini mafanikio ya wasanii nchini. Hatua hii inalenga kuhamasisha ubunifu, kuongeza ushindani chanya miongoni mwa wasanii na kukuza maendeleo ya sekta ya sanaa nchini. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Aprili 2026 Wizara kupitia BASATA imefanikiwa kuratibu na kusimamia jumla ya matukio 25 kati ya matukio 27 yaliyokuwa yamepangwa kufanyika, ambayo ni sawa na asilimia 93 ya utekelezaji. Baadhi ya matukio hayo ni Bongo Flava Honors lililofanyika tarehe 02 Agosti, 2025 jijini Dar es salaam), Matukio ya Ubunifu na Mitindo (Swahili Fashion Week and awards lililofanyika tarehe 5 hadi 7, Desemba 2025 jijini Dar es Salaam; Shindano la Miss Grand International lililofanyika tarehe 18 Octoba, 2025 jijini Dar es Salaam; Shindano la Miss Universe lililofanyika tarehe 23 Agosti, 2025 jijini Dar es Salaam; na AFA Fashion Night lililofanyika tarehe 5 Disemba 2025 jijini Dar es Salaam), CIGOGO Music Festival lililofanyika tarehe 27 Julai, 2025 Chamwino, Dodoma. Aidha, BASATA imeendelea kuwawezesha wasanii chipukizi hasa vijana kwa kuanzisha programu mbalimbali za sanaa ikiwemo *BASATA Rising Star Award* iliyozinduliwa tarehe 27 Februari 2026. Lengo la Programu hii ni kuibua, kukuza na kuendeleza vipaji vya wasanii chipukizi ambapo kila mwezi tuzo ya nyimbo bora ya mwezi ya msanii chipukizi hutolewa.

**148.** ***Mheshimiwa Spika***, Sekta ya sanaa ni mhimili muhimu katika kukuza uchumi wa ubunifu na ajira kwa vijana wetu. BASATA imeandaa miongozo 7 kwa ajili ya usimamizi wa Shughuli za Sanaa ambayo ni Mwongozo wa Usuluhishi wa Migogoro ya Wasanii na Wadau wa Sanaa; Mwongozo wa Ulinzi wa Mtoto Msanii katika Sanaa; Mwongozo wa Uendeshaji wa Matukio ya Sanaa; Mwongozo wa Uendeshaji wa Mashindano ya Uchoraji; Mwongozo wa Uendeshaji wa Mashauri ya Kimaadili; Mwongozo wa Kamati za Sanaa za Mikoa na Kamati za Sanaa za Wilaya; na Mwongozo wa Uendeshaji wa Mashindano wa Ngoma za Asili. Miongozo hii imesaidia kurahisisha usimamizi wa shughuli za sanaa, kupunguza migogoro katika sekta ya sanaa, kuimarisha ubora wa kazi za sanaa, kuimarisha hadhi ya sanaa ya Tanzania kimataifa, kuongeza tija na kulinda maslai ya wasanii na kufungua fursa mpya za kiuchumi.

**149.** ***Mheshimiwa Spika***, BASATA imekuwa ikipokea migogoro ya wasanii kupitia dawati la usuluishi linalosimamiwa na Kitengo cha Huduma za Sheria katika kushauri na kutoa msaada wa kisheria kulingana na changamoto mbalimbali zinazowakumba wasanii. Hadi Aprili 2026 jumla ya migogoro 20 imepokelewa, migogoro 10 imetatuliwa na migogoro 10 inaendelea na taratibu za utatuzi.

**150.** ***Mheshimiwa Spika***, napenda kulikumbusha Bunge lako tukufu kuwa sanaa ni kioo cha maadili ya jamii yetu. Pale ambapo sanaa inapoteza mwelekeo Taifa nalo hupoteza dira**.** Hivyo kamwe hatutokubali sanaa iwe chanzo cha kuporomoka kwa maadili ya Taifa letu. Kutokana na hali hiyo, BASATA imefanya maboresho ya Kanuni za BASATA za mwaka 2018 ili ziendane na mabadiliko ya sheria ya BASATA ya mwaka 2019 na taratibu za mwisho za kukamilisha Kanuni hizo zinaendelea na zinatarajiwa kukamilika na kuanza kutumika rasmi tarehe 1 Julai, 2026. Kanuni hizi zimeboreshwa ili kuweka misingi imara ya maadili, kupunguza au kufuta kabisa tozo na ada, kuimarisha uwajibikaji wa wasanii na kuhakikisha kazi za sanaa zinachangia kujenga jamii yenye maadili mema. Aidha, maboresho hayo ya Kanuni yanaimarisha zaidi dhana ya sasa ya Serikali ya uwezeshaji sekta badala ya udhibiti.

**151.** ***Mheshimiwa Spika***, pamoja na uwezeshaji huo, BASATA limekuwa likichukua hatua mbalimbali kwa wasanii wanaokiuka maadili. Aidha, wakatimwingine BASATA imekuwa ikijielekeza zaidi kwenye kutoa elimu kama mbadala wa hatua za kinidhamu kwa wasanii wasiozingatia maadili na katika kipindi hicho, BASATA imewafikia zaidi ya wasanii 1,437 kwa lengo la kuwapa elimu ya uzingatiaji wa maadili katika kazi za Sanaa na kutoa adhabu kwa wasanii 10 kutokana na kutozingatia maadili katika kazi zao kama ilivyoainishwa kwenye Kanuni ya 25 ya Kanuni za Baraza la Sanaa la Taifa.

### 3.2.3.3 BODI YA FILAMU TANZANIA (TFB)

**152.** ***Mheshimiwa Spika,*** Bodi ya Filamu na Michezo ya Kuigiza Tanzania ni Taasisi ya Serikali iliyoanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Filamu na Michezo ya Kuigiza, Sura 230, ikiwa na jukumu la

kusimamia, kuendeleza na kukuza tasnia ya filamu na michezo ya kuigiza nchini. Kupitia Taasisi hii, Serikali imeendelea kuweka mazingira bora ya ukuaji wa tasnia ya filamu na michezo ya kuigiza ambayo imeendelea kuwa moja ya sekta muhimu katika kukuza uchumi na ubunifu, kuongeza ajira kwa vijana na kuitangaza Tanzania kimataifa.

**153.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imeendelea kuipa kipaumbele tasnia ya sanaa na ubunifu kwa kutambua mchango wake katika maendeleo ya uchumi wa Taifa. Katika muktadha huo, Bodi ya Filamu na Michezo ya Kuigiza imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa weledi na kwa kuzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 ya kukuza sekta za ubunifu ili ziwe chanzo kikubwa cha ajira na kipato kwa Watanzania.

**154.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuendelea kuweka majukwaa muhimu ya kutambua, kukuza na kuendeleza wasanii hususan wa filamu na michezo ya kuigiza nchini, Wizara kupitia Bodi ya Filamu imeratibu Tamasha na Tuzo za Filamu (TAFFA) linalofanyika kila mwaka ambalo hadi sasa ni msimu wa nne tangu kuanzishwa kwake. Malengo makuu ya tamasha hili ni kuanzisha na kuratibu program za kuibua, kukuza na kuendeleza vipaji vya utamaduni na sanaa ikiwemo filamu na michezo ya kuigiza ili kuongeza hamasa kwa wanatasnia kuzalisha kazi zenye ubora na kusisimua masoko na fursa ya uwekezaji katika tasnia ya filamu na michezo ya kuigiza.

**155.** ***Mheshimiwa Spika***, tamasha hili la kipekee nchini lenye dhima ya 'Filamu ni Biashara' lililohusisha matukio kama midahalo, warsha na mafunzo kwa wadau wa filamu na michezo ya kuigiza lilifanyika Jijini Dar es Salaam kuanzia tarehe 03 Julai, hadi 16 Agosti, 2025 ambapo jumla ya wadau 1,600 walishiriki zikiwemo nchi za Zambia, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Kenya, Somalia, Uganda, Rwanda na Nchi kutoka nje ya Afrika ambazo ni Uswizi na Marekani. Ushiriki huu umeendelea kufungua milango ya ushirikiano wa kimataifa na kuimarisha nafasi ya Tanzania katika tasnia ya filamu na michezo ya kuigiza duniani.

**156.** ***Mheshimiwa Spika***, tamasha hilo lilihitimishwa kupitia kilele

cha usiku wa Tuzo za Filamu kilichofanyika tarehe 14 Februari, 2026 Jijini Dar es Salaam ambapo jumla ya wadau 1,226 walishiriki. Jumla ya tuzo 28 zilitolewa katika tamasha hilo. Kati ya tuzo hizo, 26 zilikuwa za ushindani (Categorical Awards) zenye kuleta chachu ya ubunifu katika vipengele tofauti na mbili (2) zilikuwa za heshima (Lifetime Achievement Awards) zilizotolewa kwa wadau walioweka alama na kuwa na mchango mkubwa katika maendeleo ya tasnia ya filamu na michezo ya kuigiza nchini kwa kipindi cha muda mrefu.

**157.** ***Mheshimiwa Spika***, sambamba na hilo, Bodi ya Filamu imeendelea kuratibu na kushiriki katika matamasha na maonesho mbalimbali kwa lengo la kuitangaza tasnia ya filamu na michezo ya kuigiza kitaifa na kimataifa. Matamasha hayo ni pamoja na *Kigamboni Festival* lililofanyika tarehe 06 Julai, 2025 katika Wilaya ya Kigamboni jijini Dar es Salaam na kuhudhuriwa na wadau 600. Katika tamasha hilo, jumla ya Tuzo 25 zilitowela ambapo Tuzo 12 zilikuwa za ushindani na Tuzo 13 zilikuwa za heshima *(Lifetime Achievement Awards)*.

**158.** ***Mheshimiwa Spika***, tamasha la *Sauti Zetu Film Festival* ambalo lilikuwa na kauli mbiu ya "kupeleka sinema kwa watu" lilifanyika tarehe 05 hadi 13 Septemba, 2025 katika mikoa ya Dar es Salaam, Arusha, Morogoro na Pwani. Tamasha hili lilikuwa na lengo la kutoa mafunzo ambapo jumla ya wadau 20 walishiriki kuhusu namna ya kuomba fedha za miradi katika utayarishaji wa filamu pamoja na kuonesha filamu zenye jumbe za kuelimisha jamii kwa kutumia nguvu ya sinema katika kuhamasisha mabadiliko chanya na kutetea haki za binadamu. Kilele cha tamasha hilo kilifanyika tarehe 15 Oktoba, 2025 jijini Arusha. Vilevile, tamasha *la Iringa Film Festival* lililofanyika tarehe 13 Disemba, 2025 katika Mkoa wa Iringa ambapo mgeni rasmi alikua Mhe. Benjamin Sita, Mkuu wa Wilaya ya Iringa na kuhudhuriwa na wadau 850 na kauli mbiu ya "Uwekezaji katika Sanaa ni kukuza Utalii". Katika tamasha hilo, jumla ya tuzo 20 zilitolewa ambapo tuzo 16 zilikuwa za ushindani (Categorical Awards) na nne (4) zilikuwa za heshima *(Lifetime Achievement Awards)*.

**159.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imeendelea kuwajengea uwezo

wasanii wa filamu na michezo ya kuigiza kupitia programu mbalimbali za mafunzo. Programu hizo ni pamoja na *Mtaa kwa Mtaa*, *Tailor Made Training* pamoja na *Film Screening Sessions* ambazo zimeendelea kuwajengea uwezo wasanii katika maeneo mbalimbali ya kitaalamu. Fauka ya hayo, kupitia programu hizo, jumla ya wasanii 906 walipata mafunzo katika fani mbalimbali ikiwemo uongozaji wa filamu, uigizaji, uandishi wa miswada, uhariri wa picha pamoja na upigaji picha. Mafunzo haya yameendelea kuchangia kuimarika kwa ubora wa kazi za filamu zinazozalishwa nchini.

**160.** ***Mheshimiwa Spika***, Bodi ya Filamu na Michezo ya Kuigiza iliratibu na ilishiriki katika mafunzo ya kuwajengewa uwezo watumishi na wadau wa filamu ambayo yalifanyika kuanzia tarehe 07 hadi 20 Septemba, 2025 nchini Korea Kusini. Mafunzo hayo yalifadhiliwa na Shirika la Maendeleo la Korea (KOICA) ikiwa na jumla ya washiriki 15 ikijumuisha wadau wa filamu wanne (4), Watumishi 10 kutoka Bodi ya Filamu na mtumishi mmoja (1) kutoka Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo.

**161.** ***Mheshimiwa Spika***, Bodi imeendelea kushirikiana na Wadau mbalimbali ikiwemo Kituo cha Sayansi na Utamaduni cha Urusi nchini; Ubalozi wa China pamoja na Kituo cha Utamaduni wa China; Tanga Yetu kupitia mradi wake wa Global Opportunity Youth Network (GOYN) kwa kushirikiana na Jiji la Tanga. Kupitia ushirikiano huo, Bodi imewajengea uwezo wanatasnia wa Mkoa wa Tanga na mikoa ya jirani ili kuwawezesha vijana kupata fursa za ajira, kujiongezea kipato, kupata mikopo, kuanzisha biashara endelevu na kuchangia ukuaji wa uchumi wa jamii zao na nchini kwa ujumla ambapo hadi Aprili 2026 Bodi imefanikiwa kusaidia kuandaa Mpango Mkakati wa filamu (Tanga Film Strategic Plan) wa miaka mitano kuanzia mwaka wa fedha 2026/27 hadi 2030/31 ya kuifanya Tanga iwe kitovu cha utengenezaji wa filamu nchini.

**162.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha tasnia ya filamu inaendelea kukua kwa kuzingatia maadili, sheria na utamaduni wa Taifa letu, Bodi ya Filamu imeendelea kusimamia maudhui ya filamu na michezo ya kuigiza ili kukidhi viwango vya ubora vya kitaifa na kimataifa kwa kuhakiki na kupanga madaraja kabla ya

kurushwa kwa hadhara. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Aprili 2026 Bodi imehakiki na kupanga madaraja kwa filamu na tamthilia 206 sawa na asilimia 103 ya lengo la filamu na tamthilia 200 pamoja na jumla ya sehemu (Episodes) 1,126 kati 1,500 sawa na asilimia 75 ya lengo ambapo kazi 124 zilikua filamu na tamthilia za ndani ya nchi na 82 zilikua filamu na tamthilia kutoka nje ya nchi.

**163.** ***Mheshimiwa Spika***, vilevile, hakukua na filamu wala tamthilia iliyowasilishwa Bodi ambayo ilikiuka maadili, sheria na utamaduni wa Taifa. Wizara kwa kushirikiana na Bodi imeendelea kuonya, kukemea na kudhibiti maudhui potofu kwa wanatasnia wa filamu na michezo ya kuigiza hasa yanayorushwa mitandaoni bila kuwasilishwa kwa ajili ya uhakiki na kupangiwa madaraja. Vikao mbalimbali vya kinidhamu vimekuwa vikifanyika kwa kushirikisha Jeshi la Polisi na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) ili kulinda maadili, amani, umoja na mshikamo wa Taifa letu. Sambamba na hayo, Bodi imeendela kufanya maboresho ya Sheria ya Filamu na Michezo ya Kuigiza, Sura 230 kwa kushirikiana na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ili Sheria ziendane na mabadiliko ya teknolojia yanayokua kwa kasi katika mnyororo wa tasnia ya filamu na michezo ya kuigiza nchini.

**164.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha mazingira ya uwekezaji katika tasnia ya filamu na michezo ya kuigiza, Serikali imeendelea kutoa elimu kwa wanatasnia juu ya urasimishaji kwa kutumia vyombo mbalimbali kama televisheni, redio na mitandao ya kijamii ili kufuata taratibu za kutambulika rasmi katika tasnia ya filamu na michezo ya kuigiza kwa kujirasimisha kidijiti katika Mfumo wa *Artist Management Information System* (AMIS) ambapo wanatasnia wanaweza kujirasimisha kokote waliko nchi bila kufika katika ofisi za Bodi. Jumla ya vitambulisho 148 vimetolewa sawa na asilimia 49 ya lengo la vitambulisho 300. Pia, vibali 103 vimetolewa sawa na asilimia 34 ya lengo la vibali 300. Kati ya vibali vilivyotolewa, vibali 56 vilitolewa kwa wazalishaji wa ndani na 47 vilitolewa kwa wazalishaji kutoka nje ya nchi.

**165.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa ujumla, utekelezaji wa majukumu haya unaonesha dhamira thabiti ya Serikali ya kuendelea kukuza

tasnia ya filamu na michezo ya kuigiza nchini ili iweze kuchangia kikamilifu katika maendeleo ya uchumi wa taifa, kuongeza ajira kwa vijana pamoja na kuitangaza Tanzania kimataifa kupitia sanaa na utamaduni.

### 3.2.3.4 TAASISI YAHAKIMILIKITANZANIA (COSOTA)

**166.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Hakimiliki Tanzania (COSOTA) ilianzishwa kwa Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki Sura ya 218 (Rekebu ya mwaka 2023). Majukumu ya Ofisi ya Hakimiliki Tanzania ni pamoja na kukuza na kulinda maslahi ya Watunzi, Waandishi, Wasanii, Wafasiri, Watayarishaji wa kurekodi sauti, Watangazaji, Waongozaji na Wachapishaji kwa kulinda haki zao; kusaidia uanzishwaji na kusimamia Kampuni za Kukusanya na Kugawa Mirabaha (Collective Management Organizations - CMOs); na kupambana na uharamia wa kazi za wabunifu. Aidha, Ofisi hii ina jukumu la kutunza rejista ya kazi za wasanii na vyama vya watunzi, wasanii, wafasiri, watayarishaji wa sauti zilizorekodiwa, watangazaji na wachapishaji.

**167.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha kwamba Kampuni za Kukusanya na Kugawa Mirabaha zinasimamiwa ipasavyo, COSOTA imetekeleza mojawapo ya jukumu lililopangwa kwa mwaka 2025/26 ambalo ni kusimamia Kampuni za kukusanya na kugawa mirabaha katika madaraja ya kazi za muziki na kazi za maandishi. COSOTA imeainisha madaraja manne (4) ya wadau wa sanaa na ubunifu ambayo yanastahili kuwa na kampuni za kukusanya na kugawa mirabaha. Madaraja hayo ni ya muziki, filamu, kazi za maandishi, sanaa za maonesho na ufundi. Katika kutelekeza jukumu hili COSOTA imetoa leseni kwa Kampuni za kukusanya na kugawa mirabaha (Collective Management Organizations - CMOs) katika madaraja mawili (2) ya muziki na kazi za maandishi. Leseni hizi zimetolewa kwa kampuni ya Society of Music Advocacy (SOMA) kwa kazi za muziki na Tanzania Reproduction Rights Society (TANRRS) kwa kazi za maandishi. Aidha, COSOTA imeratibu uanzishwaji wa CMOs katika daraja la filamu na taratibu za utoaji wa leseni ya uendeshaji zipo katika hatua ya tathmini ya maombi. Ofisi inaendelea kuhamasisha wadau kuanzisha na kusajili CMO katika madaraja ya sanaa za

maonesho na sanaa za ufundi ili kuhakikisha kuwa ukusanyaji wa mirabaha unafanyika kikamilifu.

**168.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha kuwa kampuni za kukusanya na kugawa mirahaba (CMOs) zinatekeleza majukumu yake kwa ufasaha, katika kipindi cha Julai 2025 hadi Aprili 2026, COSOTA imewajengea uwezo wa kutekeleza majukumu yao na kuzingatia Sheria na Kanuni; kufanya uchambuzi wa taarifa za kibenki za mirabaha iliyokusanywa na Kampuni ya daraja la Muziki ya SOMA; na kufanya mapitio ya Viwango vya tozo (tariff rates) vya Kampuni ya TANRRS kwa ajili ya utoaji leseni kwa watumiaji wa kazi za maandishi.

**169.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha kuwa Serikali inakusanya Mirabaha kikamilifu na wasanii wananufaika na kazi zao, Wizara kupitia COSOTA iliendelea kufuatilia ukusanyaji wa tozo ya hakimiliki (Copyright Levy) kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ambapo jumla ya kiasi cha shilingi 522,596,890.57 kimekusanywa kwa kipindi cha mwezi Julai 2025 hadi Aprili 2026. COSOTA inaratibu mgao wa fedha zitokanazo na Tozo ya Hakimiliki ambapo jumla ya shilingi 988,656,103.92, sawa na asilimia 60 ya makusanyo yote ya shilingi 1,647,760,173.20 yaliyofanyika kuanzia Septemba 2023 hadi Juni 2025 ambazo zitagawiwa kwa wabunifu wa kazi za sanaa na uandishi. Mchanganuo wa mgao ni daraja la muziki asilimia 20, filamu asilimia 15, sanaa ya uandishi asilimia 10, sanaa za ufundi asilimia 7.5 na sanaa za maonesho asilimia 7.5.

**170.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali inathamini sana mchango wa tasnia ya sanaa na Ubunifu katika kukuza pato la Taifa, pia inawathamini wabunifu wote pamoja na mchango wao katika maendeleo ya sanaa nchini. Hivyo, COSOTA imeendelea kutekeleza mkakati wa kupambana na uharamia wa kazi za ubunifu kwa kufanya operesheni maalumu, kutoa elimu na kushughulikia malalamiko/ migogoro. Jumla ya programu za elimu kwa umma nane (8) na operesheni mbili (2) zimefanyika. Tarehe 30 Januari hadi 9 Februari, 2026 COSOTA ilifanya oparesheni ya uharamia katika mkoa wa Mwanza ambapo mtuhumiwa mmoja (1) alikamatwa na jalada la uchunguzi

lilifunguliwa. Aidha, kwa kushirikiana na Kampuni ya MultiChoice Tanzania pamoja na Jeshi la Polisi Tanzania, COSOTA imefanya doria mtandaoni na kukamata maharamia wawili (2) ambao walikiri makosa na kulipa faini ya shilingi 2,000,000 kwa mujibu wa Kanuni ya Hakimiliki na Hakishiriki ya Ufifilishaji wa Makosa *(Copyrights and Neighbouring Rights (Compounding of Offenses)* za mwaka 2020. Pia, ili kuhakikisha wabunifu na watu wote wanaohusika na tasnia hii wanasikilizwa na kutatuliwa kero zao ipasavyo kupitia dawati la malalamiko, COSOTA imepokea na kusikiliza jumla ya migogoro 28 ambapo 21 imesuluhishwa na saba (7) inaendelea na usuluhishi.

**171.** ***Mheshimiwa Spika,*** jukumu jingine la COSOTA ni kukusanya na kugawa mirabaha kwenye maeneo ambayo hayana Kampuni za kukusanya na kugawa mirabaha. Ili kufanikisha jukumu hili kwa ufanisi mkubwa, COSOTA ilianza mchakato wa kuandaa Kanuni za kutekeleza jukumu hili kwa madaraja ya filamu, sanaa za maonesho na sanaa za ufundi. Hadi Aprili 2026, Wizara kwa kushirikiana na COSOTA imeandaa rasimu ya Kanuni ya vielelezo vya kusikia na kuona (*Audiovisual Regulations*) ili kuwezesha kukusanya na kugawa mirabaha kwa upande wa kazi za filamu. Aidha, Wizara kupitia COSOTA, ilifanikiwa kuandaa Kanuni ya haki ya kunufaika na mauzo endelevu (Resale rights) kwa ajili ya kusimamia kazi za sanaa za ufundi na maonesho zinapouzwa kwa mara ya pili na kuendelea.

**172.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuhakikisha usimamizi wa Hakimiliki nchini unawanufaisha wabunifu nchini, COSOTA imewasilisha mapendekezo ya mabadiliko ya Sheria ya Hakimiliki na Hashiriki Na 7 ya mwaka 1999 kupitia Sheria ya Fedha ili kuhakikisha inakidhi mabadiliko ya teknolojia pamoja na kufuata miongozo ya kimataifa ambayo Tanzania tumeridhia. Mabadiliko hayo yatahusisha kuongeza kiwango cha asilimia inayotozwa pamoja na idadi ya vifaa vinavyotumika kuzalisha, kuhifadhi, kunakili na kusambaza kazi za wabunifu. Hali hii itawezesha kuongezeka kwa makusanyo ya mirabaha yatokanayo na Tozo ya Hakimiliki na hatimaye kuwezesha ugawaji wa mirabaha kwa kiwango kikubwa na hivyo wabunifu kunufaika na kazi zao.

**173.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali ya Awamu ya Sita ina nia thabiti ya kuhakikisha kuwa wasanii na wabunifu katika madaraja mbalimbali kote nchini wanakuwa na uelewa kuhusu masuala ya Hakimiliki. COSOTA ilitoa elimu kwa umma kuhusu masuala ya hakimiliki kwa mwaka 2025/26 kwa kuzingatia mpango wa utoaji elimu ya hakimiliki na hakishiriki kwa umma wa mwaka husika. COSOTA ilitoa elimu iliyowezesha kuanzishwa kwa kampuni za kukusanya na kugawa mirabaha, elimu kwa viongozi wa Shirikisho la Filamu ili waweze kuanzisha CMOs katika daraja la kazi zao. Aidha, elimu ilitolewa kupitia vyombo vya habari ambapo hadi Aprili 2026 jumla ya vipindi 15 vilitayarishwa na kurushwa kwa hadhara kupitia stesheni za EFM Redio, TBC Taifa, Redio One, Rick Media Online Tv, Wasafi Online Tv, Crown FM, Uhai Fm Redio, Azam TV, Furaha FM na ITV jijini Dar es Salaam. Vilevile vipindi 8 vilitayarishwa na kurushwa kupitia redio za AFM, CFM, Dodoma FM, Point FM, TBC redio jamii , Ngassa Online TV, Millard Ayo Tv na Jambo online TV jijini Dodoma.

**174.** ***Mheshimiwa Spika,*** fauka na hayo, COSOTA ilitoa elimu ya hakimiliki Jijini Dar es Salaam na Dodoma katika matukio mbalimbali kama vile Tamasha la Samia Master Class, maadhimisho ya Maonesho ya Kimataifa ya Vitabu ambapo wageni 120 waliofika kwenye banda walipatiwa elimu. Maeneo mengine ni Mkutano Mkuu wa wadau wa sanaa za Maonesho Tanzania ambao ulifanyika TaSUBa na wadau 100 walipatiwa elimu. Aidha, wadau wa sanaa waliopatiwa elimu ya hakimiliki ni pamoja na Shirikisho la Kazi za Maandishi Dar es Salaam, Wanafunzi 200 wa Chuo cha Sanaa na Utamaduni Bagamoyo TaSUBa tarehe 5 Desemba, 2025, Kampuni ya kukusanya na kugawa mirabaha kwa kazi za Muziki ya Society of Music Advocacy (SOMA), wanafunzi 150 kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) pamoja na vijana 450 wa kikundi cha "Vijana Innovation" mwezi Februari, 2026. Aidha, tarehe 2 hadi 3 Februari 2026 COSOTA ilitoa elimu kwa Wanafunzi 50 wa DIT, na Januari 2026 wanafunzi 100 kutoka Chuo cha Kilimo na Uvuvi (LITA), Wasanii 113 wa sanaa za Ufundi wa chama cha wasanii wachongaji (CHAWASAWATA) walipatiwa elimu ya hakimiliki tarehe 24 Januari, 2026 Dar es Salaam. Watayarishaji wa kazi za sanaa (Producers) 130 walipatiwa elimu Machi 18, 2026 katika

kituo cha Urithi wa Ukombozi na Benjamini Mkapa walipatiwa elimu ya hakimiliki. Tarehe 11 Machi, 2026 elimu kuhusu Hakimiliki na namna ya kupambana na uharamia wa kazi za wabunifu ilitolewa kwa Maafisa 721 wa Chuo cha Dar es Salaam Police Academy Kurasini. Pia, COSOTA imetoa elimu kwa umma kwa njia ya mitandao ya kijamii ambapo jumla ya vibango 23, na makala jongefu mbili (2) za elimu ya hakimiliki vimetolewa na kusambazwa katika mitandao ya kijamii ya Instagram, Whatsapp na Facebook. Aidha, elimu ilitolewa jijini Dodoma kwa Wahadhiri 17 na wanafunzi 18 wa Chuo cha mipango Dodoma (IRDP) walipatiwa elimu ya Hakimiliki, Maafisa Utamaduni wa jiji na mkoa wa Dodoma, Jeshi la Polisi kitengo cha Makosa ya jinai (DCI), Wamiliki wa baa na Hoteli pamoja na viongozi wa Chemba ya Taifa ya Biashara (TNCC).

**175.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kukuza ushirikiano wa kitaifa na kimataifa kwenye usimamizi na ulinzi wa hakimiliki na hakishiriki, COSOTA ilishirikiana na Taasisi za ndani nne (4) ambazo ni Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) katika kukusanya Tozo ya Hakimiliki, Chuo cha Sanaa Bagamoyo (TaSUBa) kutoa elimu ya hakimiliki pamoja na kufanya usajili wa kazi za Sanaa, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) katika kuweka mpango mkakati wa kupambana na uharamia wa kazi za wabunifu kidijitali, pamoja na Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) kutekeleza mradi wa *"IP School Club"* na kutoa elimu ya Hakimiliki kwa Walimu 20 waliosajiliwa pamoja na Wanafunzi 100 katika shule tano (5) za Sekondari ambazo ni Makongo, na St. Joseph zilizopo Dar es Salaam, Tanga Technical iliyopo Tanga, Sikirali iliyopo Kilimanjaro pamoja na Kiembesamaki Zanzibar.

**176.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika ngazi ya kimataifa, COSOTA ilishirikiana na mashirika ya kimataifa matano (5) kwa lengo la kukuza ushirikiano wa kimataifa kwenye usimamizi na ulinzi wa hakimiliki na hakishiriki. Mashirika hayo ni; Shirika la Kikanda la Miliki Bumifu Afrika (African Regional Intellectual Property Organization - ARIPO); Shirikisho la Kimataifa la Vyama vya Waandishi na Watunzi (International Confederation of Societies of Authors and Composers - CISAC) ambapo tarehe 12 Desemba, 2025 Ofisi ilishiriki katika kikao kazi cha *Working Licensing Africa* kwa lengo

la kujengewa uwezo juu ya kusimamia masuala ya utoaji leseni kwa vyombo mbalimbali vinavyorusha na kupokea matangazo. Pia, COSOTA ilishiriki kikao cha 7 na 8 cha Kamati ya Haki za Miliki Bunifu (Committee on Intellectual Property Rights) kujadili itifaki za Miliki Bunifu (IPR Protocols) ikiwemo itifaki ya hakimiliki kwenye Eneo Huru la Biashara Afrika (African Continental Free Trade Area - AfCFTA) uliofanyika tarehe 20 Julai hadi tarehe 02 Agosti, 2025 nchini Djibouti kuhakikisha masuala ya Hakimiliki na Hakishiriki yanasimamiwa na kuzingatiwa vyema.

Aidha, COSOTA ilishiriki kongamano lililofanyika Harare Zimbabwe 21 Oktoba, 2025 lilioandaliwa na Shirika la Kikanda la Miliki Bunifu Afrika (ARIPO) kuhusu namna bora ya kushirikiana kwa kuzingatia mifumo ya Sheria na Sera za kusimamia masuala ya Hakimiliki. Pia COSOTA ilishiriki Mkutano wa Kimataifa wa Hakimiliki wa mwaka 2025 (2025 International expo and China Copyright forum) ulioandaliwa kwa pamoja na “National Copyright Administration of China” (NCAC), CISAC, na Shirika na Miliki Bunifu Duniani (World Intellectual Property Organization - WIPO) tarehe 13 - 17 Oktoba, 2025 katika mji wa Qingdao - China, kwa lengo la kujadili mchango wa sekta ya ubunifu na mifumo ya Hakimiliki katika kuchochea maendeleo na mabadiliko ya kidigiti.

**177.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ili kuhakikisha kuwa Serikali ina kanzi data ya wabunifu wote nchini pamoja na kazi zao, COSOTA imeendelea kutekeleza jukumu lake la kusajili kazi za kibunifu na wabunifu ambapo jumla ya kazi 959 zilisajiliwa na pia wabunifu 316 walisajiliwa kuanzia Julai 2025 mpaka Aprili 2026. Vilevile, katika kuhakikisha kuwa kanzidata hiyo ni salama na wabunifu wanaweza kujisajili popote watakapokuwa, COSOTA imekamilisha ujenzi wa mfumo wa usajili wa kazi za ubunifu yaani Copyright Registration Management Information System (CRMIS) ambao uliwezesha kuunganishwa na mfumo wa usajili wa AMIS wa BASATA, NIDA na NaPA.

### 3.2.3.5 MFUKO WA UTAMADUNI NA SANAA TANZANIA

**178.** ***Mheshimiwa Spika***, Mfuko wa Utamaduni na Sanaa Tanzania umeanzishwa kwa Sheria ya Ujumuisho wa Wadhamini

(Trustees' Incorporation Act 2002) iliyorejelewa mwaka 2023 kupitia Sura 318 (CAP. 318 R.E. 2023) na kupewa hati ya usajili yenye namba 1776 tarehe 30 Septemba, 2020. Lengo la uanzishwaji wake ni kuinua ubora wa kazi za Utamaduni na Sanaa ili zijiendeshe kibiashara, kuzalisha ajira na kuchangia pato la Taifa. Mfuko unatoa huduma za mitaji kwa wadau wa Utamaduni na Sanaa kupitia mikopo yenye masharti nafuu, huwajengea uwezo kwa kutoa mafunzo mbalimbali hususan yanayohusika na urasimishaji wa kazi zao, elimu ya fedha, masoko, uwekezaji pamoja na hifadhi ya jamii.

**179.** ***Mheshimiwa Spika***, Mfuko wa Utamaduni na Sanaa unawezesha upatikanaji wa mikopo kwa wasanii kwa kushirikiana na Taasisi za Fedha ambazo ni Benki ya CRDB na NBC. Mfuko uliamua kushirikiana na Taasisi hizo katika utoaji wa huduma hii ili kutumia miundombinu ya Ofisi za matawi ya Benki yaliyoenea nchi nzima. Lengo likiwa ni kupunguza gharama za uendeshaji ambapo ili kuwafikia wasanii wengi Mfuko ungelazimika kuwa na Ofisi hadi katika ngazi ya Wilaya, kuwa na watumishi wengi na vitendea kazi vya kutosha kama vile magari, kompyuta, viti, meza, n.k. Kutumia wataalamu wa Benki walio na uzoefu katika ukaguzi wa miradi, utoaji wa mikopo, ufuatiliaji wa marejesho na usimamizi wa mikopo, kwa ujumla pamoja na kuulinda mtaji ili ukue, uwe endelevu na hatimaye uweze kuwafikia wasanii wengi zaidi ilikuwa ni lazima Mfuko uingie makubaliano na Benki.

**180.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali kupitia Mfuko imetoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 3.535 kwa miradi 229 ya Utamaduni na Sanaa. Aidha, Sekta zilizonufaika na mikopo hiyo ni Filamu (miradi 61) imewezeshwa shilingi 1,008,133,655.91, Ufundi (miradi 68) imewezeshwa shilingi 1,268,433,172.05; Maonesho (miradi 45) imewezeshwa shilingi 525,372,235.95, Muziki (miradi 44) imewezeshwa shilingi 433,060,936.09 na Lugha na Fasihi (miradi 11) imewezeshwa shilingi 300,000,000.

**181.** ***Mheshimiwa Spika***, kupitia miradi 229 iliyowezeshwa, miradi 55 inayomilikiwa na Makampuni iliwezeshwa shilingi 1,088,662,802.42, miradi 48 inayomilikiwa na vikundi iliwezeshwa shilingi 613,745,732.53, miradi 59 inayomilikiwa na Wanawake

iliwezeshwa shilingi 595,322,866.26 na miradi 67 inayomilikiwa na Wanaume iliwezeshwa shilingi 1,237,268,598.79. Aidha, Miradi iliyowezeshwa imefikia Mikoa 15 ambayo ni Dar es Salaam, Pwani, Morogoro, Manyara, Arusha, Mwanza, Kagera, Shinyanga, Mara, Geita, Mbeya, Njombe, Kilimanjaro, Ruvuma, na Tabora. Halikadhalika, kupitia miradi iliyowezeshwa jumla ya ajira 75,537 zimezalishwa na kuwanufaisha wananchi 971,285.

**182.** ***Mheshimiwa Spika***, matokeo ya uwezeshaji wa mitaji kwa wasanii yamesaidia ununuzi wa vifaa kwa studio 72 za Muziki na Filamu, ununuzi wa vifaa kwa vyuo kumi na moja (11) vya kati vilivyosajiliwa na Serikali katika ngazi ya Cheti, Diploma na kozi fupi kwa ajili ya kutoa elimu ya ujuzi kwa fani mbalimbali kama vile ushonaji, mapambo, ususi, upishi nk. Vyuo hivi vimezalisha wasanii 3,579, ununuzi wa majukwaa ya kisasa kumi (10) yanayotumika katika hafla mbalimbali hususani mikutano mikubwa. Aidha, uwezeshaji huo umechagiza uzalishaji wa Filamu 287 ambapo filamu 253 zimekubalika katika vituo vya Televisheni vya DSTV, Azam TV, Star Times na ZUKU na uzalishaji wa sehemu (episodes) kwa tamthilia tisa (9) zinazoendelea kurushwa katika vituo vya Televisheni vya DSTV na Azam TV. Halikadhalika, utengenezwaji wa nyimbo za audio 107 na video 85 za Muziki pamoja na kukua kwa utalii wa kiutamaduni katika Mkoa wa Arusha kupitia uwezeshaji wa mitaji kwa wasanii wa Sanaa za Ufundi katika Soko la Maasai ambalo limekuwa kichocheo na kivutio cha utalii katika Mkoa wa Arusha.

**183.** ***Mheshimiwa Spika***, Mfuko umewezesha upatikanaji wa mafunzo ya urasimishaji, uendelezaji wa biashara na ushauri wa kibiashara kwa wasanii kwa lengo la kuwaimarisha katika usimamizi wa shughuli zao za sanaa, kuwakutanisha wasanii ili kubadilishana mawazo na uzoefu pamoja na kuwasaidia kukabiliana na changamoto zinazojitokeza katika utekelezaji wa kazi zao. Mfuko kwa kushirikiana na wadau umewajengea uwezo wasanii 11,556 ambao kati yao wanawake ni 6,125 sawa na asilimia 53 na wanaume ni 5,431 sawa na asilimia 47 kutoka mikoa 11 ambayo ni Wasanii 1,140 - Dodoma, Wasanii 2,235 Dar es Salaam, Wasanii 338 - Geita, Wasanii 724 - Kagera, Wasanii 531- Mara, Wasanii 1,224 - Mwanza, Wasanii 1,178 - Mtwara, Wasanii

1,277 - Shinyanga, Wasanii 627 – Tabora, Wasanii 753 - Arusha na Wasanii 1,529 - Tanga. Aidha, mada zilizofundishwa ni umuhimu na aina za urasimishaji, elimu ya fedha, masoko, uwekezaji, usimamizi na uandishi wa miradi pamoja na hifadhi ya jamii.

**184.** ***Mheshimiwa Spika***, urasimishaji wa wasanii na kazi zao una umuhimu mkubwa katika kuimarisha utambuzi, ulinzi na usalama wa kazi za wabunifu, kujenga uaminifu kwa wadau na wawekezaji katika sekta ya sanaa, sambamba na kutambua mchango wao katika kukuza uchumi wa Taifa na kuendeleza utambulisho wa jamii. Katika kutekeleza azma hiyo, Wizara kupitia Mfuko imechochea urasimishaji wa kazi za sanaa kwa jumla ya wasanii 5,627 katika Mamlaka mbalimbali. Hatua hizo zilijumuisha ufunguaji wa akaunti 3,275 za benki, usajili wa wasanii 749 kupitia Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA), usajili wa wasanii 573 kupitia Bodi ya Filamu, usajili wa majina 103 ya biashara, usajili wa makampuni 27, upatikanaji wa namba za utambulisho wa mlipakodi (TIN) kwa wasanii 217, utoaji wa leseni mpya za biashara 89, uhuishaji wa vibali vya sanaa 481 pamoja na uhuishaji wa leseni za biashara 113.

**185.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imeendelea kuelimisha wasanii kuhusu umuhimu wa kuzalisha na kutoa huduma kutokana na mahitaji ya soko la ndani na nje ya nchi. Katika kufikia jitihada hizo, Mfuko umewezesha wasanii 257 katika eneo la muziki, ufundi na maonesho kushiriki katika masoko ya kimataifa katika nchi 19. Hatua hii imeleta manufaa kwa wasanii kupanua wigo wa soko la bidhaa zao, kubadilishana maarifa ya biashara kwa kuboresha bidhaa na mbinu mpya za teknolojia. Vilevile, kuongeza utambulisho wa wasanii wa Tanzania katika soko la kimataifa. Aidha, nchi zilizofikiwa ni Ufaransa, Italia, Ujerumani, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Burundi, Kenya, Uganda, Rwanda, Madagascar, Zimbabwe, Nigeria, Komoro, Uingereza, Marekani, Zambia, Kuwait, Dubai, China na Afrika Kusini.

**186.** ***Mheshimiwa Spika***, ili kufuatilia thamani ya fedha za miradi ya wanufaika binafsi kubaini matokeo ya uwezeshaji kiuchumi kwa mnufaika binafsi, jamii na nchi kwa ujumla wake, Mfuko umefanya ufuatiliaji na tathmini ya miradi 135 iliyowezeshwa

ambapo matokeo ya shughuli hiyo yalibainisha kuwa, kukamilika kwa malengo ya wanufaika kwa asilimia 89 ambao wameweza kuongeza vifaa vyenye ubora na kuzalisha kazi zenye ubora zaidi, kukamilisha programu zilizokuwa zinaendelea kama vile utengenezaji wa Filamu, Tamthilia, Muziki, Matamasha na utengenezaji wa kazi za mikono kama vile batiki, vikapu, mikoba, kununua vitambaa vya Mapambo, maua, maturubai, majukwaa n.k. Wategemezi 10,175 wamenufaika kutokana na ajira zilizozalishwa. Aidha, wategemezi wa wamiliki wa miradi hiyo na waajiriwa wao wanahusisha watoto, wenza, wakwe pamoja na ndugu na jamaa; asilimia 40 ya wanufaika wameweza kujiunga na programu za bima za afya na familia zao na hatimaye kupunguza gharama walizokua wakitumia katika matibabu; na asilimia 61 ya waombaji wa mikopo wamepata kiwango walichoomba kutokana na kuongezeka kwa uelewa kwenye masuala ya uwekezaji katika masoko ya mitaji na hatifungani, elimu ya biashara pamoja na utunzaji wa akiba.

### 3.2.3.6 TAASISI YA SANAA NA UTAMADUNI BAGAMOYO (TaSUBa)

**187.** ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSUBa) ilianzishwa mnamo tarehe 2 Novemba, 2007 kwa tangazo Namba 220 lililochapishwa kwenye Gazeti la Serikali kwa mujibu wa sheria ya Wakala wa Serikali namba 30 ya mwaka 1997. Mwaka 2012, TaSUBa iliteuliwa kuwa Kituo cha Jumuiya ya Afrika Mashariki chenye Ubora Uliotukuka *(Centre of Excellency)* katika ufundishaji wa fani za utamaduni na sanaa. Hivyo, ni kituo cha ufundishaji wa fani za utamaduni na sanaa chenye hadhi ya kimataifa.

**188.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza adhma ya Serikali katika kuibua, kukuza, kulinda na kuendeleza vipaji vya vijana katika sekta ya sanaa kwa lengo la kuzalisha fursa za ajira na ukuaji wa uchumi wa Taifa, Serikali kupitia TaSUBa imeendela kutekeleza majukumu yake ya utoaji wa mafunzo, ushauri na utafiti katika masuala ya sanaa na utamaduni.

**189.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika utekelezaji wa afua za Serikali ya Awamu ya Sita za kuendeleza vipaji vya vijana katika kuzalisha

fursa za ajira na kuongeza mchango wa ukuaji wa uchumi wa Taifa kupitia sekta ya Sanaa na Utamaduni, Wizara kupitia TaSUBa imefanikiwa kudahili jumla ya wanafunzi 947 sawa na asilimia 118.3 ya lengo la kuwapatia mafunzo ya sanaa na utamaduni kwa ngazi ya Astashahada na Stashahada. Mafanikio haya ya kuongezeka kwa udahili ya wanafunzi ni moja ya matokeo ya juhudi za makusudi zinazoendelea kufanywa na Serikali inaendelea kuboresha na kuimarisha miundombinu mbalimbali ya chuo kwa kuendelea kujenga madarasa na maktaba za kisasa; kujenga uzio kuzunguka majengo ya chuo; na ununuzi wa vifaa vya kujifunzia na kufundishia. Sambamba na hayo, imeendele na mikakati ya kuanzisha na kufungua vituo vya mafunzo ya muda mrefu na mfupi ya masuala ya Sanaa na Utamaduni katika mikoa mbalimbali kama Dar es Salaam, Songea na Dodoma ili kuwafikia vijana wengi wenye vipaji vya Sanaa na Utamaduni.

**190.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuendelea kutekeleza azma ya Serikali ya kutangaza na kuuza kazi za Sanaa na Utamadani ndani na nje ya nchi, TaSUBa ilikuwa na jukumu la kutangaza shughuli na mazao ya kazi za Sanaa na Utamaduni zinazozalishwa na chuo. Wizara kupitia TaSUBa imeendelea kukamilisha uanzishwaji wa redio na televisheni mtandao (Online Tv) kupitia fedha za maendeleo ambapo mpaka kufikia Aprili 2026 ukamilishaji wa uanzishaji upo kwenye hatua ya mwisho. TaSUBa imeendelea kushirikiana na wasanii maarufu wa ndani hasa wa Filamu kuwa mabalozi bora katika kukitangaza chuo na shughuli zake ambapo Taasisi iliingia makubaliano na msanii wa filamu Bw. Salim Ahmed Issa (Gabo Zigamba) kuwa Balozi wa chuo kitaifa na kimataifa. Pia, Taasisi imeendelea kutumia vyombo vya habari vya Televisheni (*TBC, ITV, Channel Ten* na *Azam Tv*), Radio, Magazeti (*HabariLEO, Mwananchi, Uhuru na Daily News*) na akaunti za mitandao ya kijamii (Facebook, Instagram na Tiktok) kutangaza shughuli zinazofanywa na chuo na mazao yake.

**191.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kutekeleza malengo ya Serikali, sambamba na Dira ya Maendeleo ya Taifa 2050 kwa kujenga na kuboresha miundombinu ya sekta ya Sanaa na Michezo ili

kuzalisha fursa nyingi za ajira kwa vijana na mchango kwa pato la Taifa. Wizara kupitia TaSUBa imeendelea kusimamia na kuratibu mradi wa ukarabati wa chuo cha Sanaa Bagamoyo kwa kupitia fedha za maendeleo ambapo, kiasi cha shilingi 750,000,000 zilizotolewa na Serikali kwa ajili ya kufanyika kwa shughuli mbalimbali za uboreshaji wa miundombinu ya chuo ikiwemo kukamilisha ujenzi wa uzio kwa asilimia 100; ujenzi wa darasa na maktaba ya kisasa ambao umefikia asilimi 70 na ununuzi wa vifaa vya kisasa vya kujifunzia na kufundishia.

**192.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kukuza na kuongeza ubora na thamani ya kazi za Sanaa na Utamaduni zinazozalishwa na wasanii wetu, TaSUBa imeendelea na taratibu za kutoa huduma ya ushauri (Consultancy) kwa vyuo, mashirikisho ya sanaa na utamaduni, vikundi vya sanaa, na taasisi mbalimbali binafsi na umma, ambapo Chuo cha Taaluma ya Urekebishaji Tanzania (Tanzania Correction Training Academic - TCTA) kilichopo Ukonga jijini Dar es salaam kilipata ushauri wa uendeshaji wa mafunzo ya sanaa na utamaduni kwa vijana 27. Aidha, Ubalozi wa India ulipata ushauri juu ya uendeshaji wa mashindano ya uchoraji wa picha za rangi ambapo yalifanyika chuoni TaSUBa na vijana 20 walinufaika; na Taasisi ya *Ongala Music Open Forum* ilipewa ushauri juu ya uendeshaji mafunzo ya muziki wa dansi ambapo vijana 20 walinufaika. Katika kuwawezesha na kuwafikia wadau mbalimbali wa sanaa na utamaduni kupata huduma ya ushauri ili kukuza na kuongeza thamani ya kazi zao, Wizara kupitia TaSUBa kwa mwaka wa fedha 2025/26 imeshiriki katika maonesho ya kimataifa ya biashara Sabasaba tarehe 01 – 13 Julai, 2025 ambapo wadau, wasanii na vikundi mbalimbali walihudhuria kwenye banda la TaSUBa na kupata ushauri kutoka kwa wataalamu wa TaSUBa.

**193.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika hatua za makusudi za Serikali ya awamu ya sita zinazoendelea kuchukuliwa katika kuongeza nafasi za ajira na ushindani katika soko la ajira hasa kwa vijana, TaSUBa imeendelea kujipambanua zaidi kwa kuwajengea uwezo vijana katika sekta ya sanaa na utamaduni kwa kuendelea kuandaa na kuhuisha mitaala mipya ya masomo. Vilevile, kwa kushirikiana na NACTVET imeendelea kukamilisha uandishi wa

mitaala mitatu ya masomo ambayo ni Urithi wa Kitamaduni na Utalii (*Cultural Heritage and Tourism*), Usimamizi wa Sanaa na Masoko (*Arts Management and Marketing*) na Utendaji wa Muziki (*MusicPerformance)* ambapo masomo haya yameonekana kuwa na umuhimu katika uongeza nafasi za ajira kutokana na mahitaji ya soko la ajira.

**194.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuwawezesha wasanii na vikundi vya sanaa na utamaduni kwa kuwapa jukwaa la kutangaza na kujitangaza kitaifa na kimataifa kupitia kazi zao za sanaa na utamaduni. TaSUBa ilifanya shughuli mbalimbali za maandalizi ya Tamasha la 44 la Kimataifa la Sanaa na Utamaduni Bagamoyo la tarehe 26 mpaka 29 Novemba, 2025. Maandalizi yaliyofanyika ni pamoja na kuanda Mpango Kazi wa uendeshaji wa Tamasha (Festival Action plan); kuandaa na kutuma mialiko kwa wasanii na vikundi vya sanaa ndani na nje ya nchi; kutafuta wafadhili mbalimbali wa Tamasha; kuandaa na kutengeneza matangazo mbalimbali kuhusu Tamasha; na kuunda kamati mbalimbali za kusimamia shughuli za Tamasha.

**195.** ***Mheshimiwa Spika***, TaSUBa ilifanikiwa kuingia makubaliano ya mwaka mmoja na kampuni ya Vision Investiment katika kushirikiana kutafuta wafadhili ambao watasaidia kufadhili uendeshaji wa shughuli za Tamasha. Hata hivyo, Tamasha halikuweza kufanyika kutokana na kutokea kwa mabadiliko ya ratiba ya kufunguliwa kwa muhula wa masomo iliyotolewa na NACTVET ambapo tarehe ya kufunguliwa ilibadilika na kuwa tarehe 17 na 24 Novemba, 2025 hivyo kusababisha kutopata muda wa kutosha kufanya maandalizi ya shughuli mbalimbali za Tamasha ambapo pia ni sehemu ya masomo ya wanafunzi.

### 3.2.4 SEKTA YA MAENDELEO YA MICHEZO

**196.** ***Mheshimiwa Spika,*** Sekta ya Maendeleo ya Michezo ni nyenzo muhimu ya kuzalisha ajira, kuimarisha afya za wananchi pamoja na kuwaletea furaha Watanzania. Pia, kupitia sekta ya michezo nchi yetu inaendeleza ushirikiano na mataifa mbalimbali kupitia diplomasia ya michezo. Kwa kutambua umuhimu huo Serikali inao wajibu wa kujenga mazingira rafiki kwa ukuaji wa

sekta ya michezo. Sekta hii kwa sasa inatekeleza majukumu yake kwa kufuata Sera ya Maendeleo ya Michezo ya Mwaka 1995 pamoja na Mkakati wa Maendeleo ya Michezo wa mwaka 2022. Sekta hii ni miongoni mwa mihimili inayotoa ajira na kuchangia katika uchumi wa mtu mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla. Aidha, Sekta hii inasimamiwa na Idara ya Maendeleo ya Michezo na taasisi zilizo chini yake ambazo ni Baraza la Michezo la Taifa (BMT) na Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya.

**3.2.4.1 Idara ya Maendeleo ya Michezo**

**197. Mheshimiwa *Spika,*** katika kipindi cha mwaka 2025/26 majukumu yaliyotekelezwa ni yafuatavyo:

**198. *Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeratibu kwa ufanisi michuano ya Mpira wa Miguu Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN 2024) pamoja na kuendelea na maandalizi ya Mashindano ya AFCON 2027. Mashindano ya CHAN ni kigezo ambacho Shirikisho la Soka Afrika (CAF) hutumia kama kipimo cha nchi kuwa mwenyeji wa mashindano ya AFCON. Mashindano hayo yamefanyika nchini kuanzia tarehe 02 hadi 30 Agosti, 2025 ambapo nchi za Tanzania, Kenya na Uganda zilikuwa wenyeji. Timu ya Taifa ya Tanzania *(Taifa Stars)* ilishiriki na kuonesha kiwango cha juu cha ushindani kwa kufanikiwa kufika hatua ya robo fainali, hatua inayodhihirisha kuimarika kwa soka letu la ndani. Aidha, kutokana na ubora wa maandalizi na usimamizi wa mashindano hayo CAF ilimtunuku tuzo ya heshima Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, jambo linaloendelea kuitangaza nchi yetu kimataifa kama mwenyeji mahiri wa matukio makubwa ya kimataifa ya michezo. Mafanikio haya ni matokeo ya jitihada za Serikali ya Awamu ya Sita (6) inayoongozwa na mwanamichezo nambari moja (1) Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye amekuwa na mapenzi makubwa na michezo hususan kuwekeza kwenye miundombinu ya michezo, kuwezesha kuijenga timu imara kupitia maandalizi bora, motisha kwa wachezaji na programu za kitaalamu kwa makocha na viongozi wa timu.

**199.** ***Mheshimiwa Spika,*** sambamba na mashindano hayo, Serikali imeendelea na maandalizi ya Mashindano ya Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON 2027) kwa kutekeleza kwa ufanisi majukumu mbalimbali hususan ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya michezo, barabara, hoteli na viwanja vya mazoezi katika miji wenyeji ya Dar es Salaam, Zanzibar na Arusha. Hatua hizi ni sehemu ya mkakati wa Serikali wa kuhakikisha nchi yetu inakuwa na miundombinu ya kisasa inayokidhi viwango vya kimataifa kwa ajili ya mashindano hayo makubwa barani Afrika. Kwa upande wa Jiji la Dar es Salaam, Wizara imeendelea kusimamia utekelezaji wa miradi ya ukarabati wa uwanja wa Benjamin Mkapa ambao umefikia asilimia 95 ya utekelezaji. Aidha, ukarabati wa viwanja vitatu (3) vya mazoezi vya Gymkhana, Meja Jenerali Isamuhyo na Shule ya Sheria umekamilika na ujenzi wa viwanja vitatu (3) vingine vya mazoezi vya Farasi, Leaders Club na Gymkhana II vipo katika hatua za awali.

**200.** ***Mheshimiwa Spika***, kwa upande wa Jiji la Arusha, Wizara imeendelea kusimamia ujenzi wa uwanja utakaotumika katika mashindano ya AFCON 2027 wenye uwezo wa kuchukua watazamaji 32,000 ambapo utekelezaji wake umefikia asilimia 77.5. Aidha, ujenzi wa kiwanja kimoja cha mazoezi kinachojengwa katika eneo la mradi umefikia asilimia 60. Sambamba na kiwanja hicho, Wizara imeainisha maeneo ya Mgambo, Magereza ya Kisongo na Engutoto kwa ajili ya ujenzi wa viwanja vitatu (3) vya mazoezi ikiwa ni sehemu ya kukamilisha mahitaji ya miundombinu kwa ajili ya mashindano ya AFCON 2027. Utekelezaji wa miradi hii unaendelea kuonesha dhamira thabiti ya Serikali katika kuhakikisha maandalizi ya AFCON 2027 yanakamilika kwa wakati, kwa ubora unaotakiwa na kwa kuzingatia viwango vya kimataifa. Kufanyika kwa mashindano haya nchini kutafungua fursa mbalimbali za biashara na kuitangaza Tanzania na vivutio vyake Kimataifa pamoja na kuongeza pato la Taifa kupitia michezo.

**201.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuhakikisha mashindano ya AFCON 2027 yanafanikiwa, Serikali kupitia Kamati ya Kitaifa ya Maandalizi

ya Mashindano iligawa majukumu kwa Wizara zote na Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo imeendelea kufanya ufuatliliaji wa utekelezaji wake. Napenda kutumia fursa hii kuipongeza kamati hiyo kwa utendaji wake chini ya Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pamoja na mradi wa uwanja, miundombinu saidizi imeendelea kujengwa ambayo ni barabara za Mateves – Bondeni yenye urefu wa kilomita 6.5 (kilomita 1.5 za njia nne na kilomita 5 za njia mbili) kutoka barabara kuu ya Arusha – Babati; barabara ya Lendita yenye urefu wa kilomita 2.75 kwa njia nne; barabara ya Essuri yenye urefu wa kilomita 2.45 kwa njia nne, zote zikitokea barabara kuu ya Arusha bypass; na kilomita 1.5 za barabara zitakazozunguka uwanja. Aidha, ujenzi wa miundombinu mingine muhimu ikiwemo umeme, maji na mawasiliano unaendelea. Katika hatua nyingine, kwa lengo la kupata thamani halisi ya uwekezaji unaofanywa na Serikali, umetolewa mwongozo wa maendelezo ya maeneo yote yanayozunguka uwanja wa Arusha.

**202.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuridhihirisha dhamira ya dhati ya Serikali kuhakikisha tunafanikisha mashindano ya AFCON 2027, tayari Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ameridhia na kutoa kiasi cha Dola za Marekani 30,000,000, sawa na shilingi 76,157,100,000 kama ada ya uandaaji wa mashindano husika. Hii ndiyo tafsiri halisi ya Dkt. Samia Suluhu Hassan kama mwanamichezo namba 1 nchini.

**203.** ***Mheshimiwa Spika***, sambamba na maandalizi ya miundombinu ya AFCON 2027, Serikali imeendelea kuwekeza katika maendeleo ya miundombinu mingine ya michezo nchini kwa kutekeleza miradi mikubwa ya kimkakati yenye lengo la kukuza vipaji na kuboresha huduma za michezo kwa wananchi. Miradi mingine ambayo inatekelezwa ni ujenzi wa Akademia ya Michezo katika Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya ambapo utekelezaji wake umefikia asilimia 49, ujenzi wa uwanja wa mpira wa miguu jijini Dodoma wenye uwezo wa kuchukua watu 32,500 ambao umefikia asilimia 5, ujenzi wa Kituo cha Mazoezi na Kupumzikia Wananchi Jijini Dodoma ambao umefikia asilimia 73.5, ujenzi wa Kituo cha Mazoezi na Kupumzikia Wananchi jijini

Dar es Salaam kilichofikia asilimia 49, ukarabati wa uwanja wa Uhuru ambao umefikia asilimia 70 na ujenzi wa miundombinu ya michezo katika shule teule saba (7) za michezo ambapo zabuni imetangazwa. Utekelezaji wa miradi hii unaonesha dhamira ya dhati ya Serikali ya kuendeleza sekta ya michezo kwa kuweka miundombinu thabiti kwa ajili ya ukuzaji wa vipaji.

**204.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuhakikisha mashindano ya AFCON 2027 yanafanikiwa, Wizara iliunda kamati tatu (3) za maandalizi. Kamati hizo ni Kamati ya Kitaifa ya Maandalizi inayoundwa na Mawaziri Wote na inaongozwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu ambayo jukumu lake ni kusimamia maandalizi ya mashindano zikiwemo kamati zote; Kamati ya Wataalamu inayoundwa na Makatibu Wakuu na kuongozwa na Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu. Jukumu lake likiwa ni kutoa ushauri wa kitaalamu kwa Kamati ya Kitaifa, na Kamati ya Maandalizi ya Ndani - *Local Organizing Committee – (LOC)* iliyoundwa na wadau wa michezo kutoka sekta za umma, binafsi, Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania na Zanzibar ambapo jukumu lake ni kutekeleza maelekezo kutoka Kamati ya Wataalamu na kutoa ushauri.

**205.** ***Mheshimiwa Spika***, kufuatia nchi yetu kuwa mwenyeji wa Mashindano ya AFCON 2027, Wizara imeendelea kuchukua tahadhari na hatua madhubuti za kuimarisha usalama katika michezo kwa kuratibu mkutano wa kimataifa kuhusu kupambana na ugaidi michezoni uliofanyika tarehe 4 Machi, 2026 jijini Dar es Salaam. Mkutano huo uliwashirikisha wadau 45 kutoka Umoja wa Mataifa kupitia Kitengo cha Usalama Michezoni na Kupambana na Ugaidi (UNOCT), Baraza la Michezo la Umoja wa Afrika (AUSC), Mwakilishi wa Kudumu wa Tanzania katika Umoja wa Mataifa New York nchini Marekani, Baraza la Michezo la Taifa (BMT), Jeshi la Wananchi Tanzania, Tume ya Nguvu za Atomu Tanzania, Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), Shirikisho la Mpira wa Miguu Zanzibar (ZFF), Kamati ya Olimpiki Tanzania (TOC), Jeshi la Polisi Tanzania, Idara ya Uhamiaji na Taasisi nyingine za ndani ya nchi. Lengo kuu la mkutano huo lilikuwa ni kuwakutanisha wadau wa sekta ya michezo nchini na wataalamu wa masuala ya usalama michezoni kutoka Mashirika

ya kimataifa ili kuweka mikakati ya pamoja, kubadilishana uzoefu, kujenga uelewa wa pamoja na kuweka mikakati madhubuti ya kuzuia na kukabiliana na vitisho vya ugaidi wakati wa mashindano ya AFCON 2027. Kupitia mkutano huo, Tanzania imeendelea kujiandaa kikamilifu kwa kuimarisha mifumo ya usalama, kuongeza uwezo wa rasilimali watu, na kuhakikisha kuwa nchi inakuwa salama na ya kuaminika wakati wote.

**206.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha ushiriki wa nchi katika majukwaa ya kimataifa na kukuza vipaji vya wanamichezo, Wizara kwa kushirikiana na Baraza la Michezo la Taifa (BMT) na Kamati ya Olimpiki Tanzania (TOC) imeendelea na uratibu wa ushiriki wa wachezaji wa Tanzania katika Michezo ya Jumuiya ya Madola itakayofanyika kuanzia tarehe 23 Julai hadi 2, Agosti 2026, jijini Glasgow, nchini Scotland. Uteuzi wa wanamichezo watakaoiwakilisha nchi umekamilika, ambapo jumla ya wanamichezo 11 wamechaguliwa kushiriki katika michezo ya riadha (5), ngumi (4), judo (1) na kuogelea (1). Aidha, kambi za maandalizi kwa wanamichezo hao zinaendelea na zimepangwa kwa kuzingatia hali ya hewa pamoja na mahitaji ya mchezo husika.

**207.** ***Mheshimiwa Spika***, kwa upande wa riadha, kambi zinafanyika mkoani Arusha; mchezo wa kuogelea kambi inaendelea nchini Afrika Kusini; na mchezo wa judo mazoezi yanaendelea Ukonga, jijini Dar es Salaam. Mara ya mwisho michezo hii kufanyika ilikuwa mwaka 2022 mjini Birmingham nchini Uingereza, ambapo Tanzania ilishiriki katika michezo ya ngumi, riadha na judo ikijizolea medali tatu (3) kutoka kwa mwanariadha Felix Simbu aliyeshinda medali ya Fedha baada ya kuibuka mshindi wa pili (2) wa mbio za marathon na mabondia Yusuf Changalawe na Kassim Mbundwike walioshinda medali za shaba. Serikali kupitia Wizara inaendelea kuweka mikakati stahiki ya kuhakikisha nchi inawakilishwa na wachezaji wengi zaidi ili tuweze kuongeza uwezekano wa kupata medali nyingi zaidi.

**208.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara katika kuendelea Kupambana na Matumizi ya Dawa na Mbinu Haramu Michezoni (*Anti-doping*) imeratibu uchukuaji wa sampuli 64 kwa wachezaji walioshiriki

mashindano ya CHAN 2024 kuanzia tarehe 02 – 30 Agosti, 2025 na kuziwasilisha katika maabara kwa uchunguzi wa kitaalamu, ambapo matokeo yalibainisha kuwa sampuli zote hazikuwa na viashiria vya matumizi ya dawa au mbinu haramu. Aidha, Wizara imeendelea kutekeleza jukumu hili kwa kuchukua sampuli za wanamichezo wa ngazi za kitaifa na kimataifa wanaoshiriki katika michezo mbalimbali hapa nchini, ikiwa ni sehemu ya kuhakikisha uzingatiaji wa misingi ya haki, uwazi na uadilifu katika michezo. Hatua hizi zinaendelea kuimarisha taswira ya Tanzania katika medani za michezo kimataifa na kulinda afya za wanamichezo.

**209.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuhakikisha tunawaongezea ujuzi wataalamu katika kupambana na dawa na mbinu haramu michezoni, Wizara imetoa mafunzo kwa watalaamu 200 na kuwawezesha wataalamu wanne (4) kuhudhuria vikao na mafunzo mbalimbali kitaifa na kimataifa ikiwemo kikao cha Wakala wa Dunia wa Kupambana na Matumizi ya Dawa na Mbinu Haramu Michezoni (WADA) kilichofanyika Busan Korea Kusini kuanzia tarehe 1 – 5 Desemba, 2025 kikiwa na washiriki takribani 1,500 kutoka Serikalini, Mashirika ya Kikanda na Kitaifa, Maabara za *Anti-doping*, watoa huduma, watafiti na wanahabari; kikao cha Kanda ya Tano cha kupambana na mbinu haramu michezoni kilichofanyika kwa njia ya mtandao tarehe 18 Desemba, 2025 kikiwa na washiriki 10 wakiwemo kutoka UNESCO, WUSM na Zanzibar; kikao cha kitaifa cha utekelezaji wa mkataba wa kimataifa wa udhibiti wa Matumizi ya Dawa na Mbinu Haramu Michezoni kilichofanyika mkoani Morogoro kuanzia tarehe 22 – 26 Septemba, 2025. Vilevile, Wizara imeratibu mafunzo ya kudhibiti Matumizi ya Dawa na Mbinu Haramu Michezoni kwa wataalamu 48 wa kinga na tiba michezoni yaliyofanyika tarehe 27 Desemba, 2025 katika uwanja wa Benjamin Mkapa na mafunzo ya Maafisa Udhibiti watatu (3) kutoka Tanzania Bara na Zanzibar yalifanyika kwa njia ya mtandao.

**210.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha Tanzania inaendelea kunufaika na fursa za diplomasia ya michezo, kwa mara ya pili Serikali imekuwa mwenyeji wa mkutano wa Pili wa Baraza la Mawaziri wa Michezo Afrika Kanda ya Nne (*AUSC Region IV*) uliofanyika tarehe 18 hadi 21 Agosti, 2025 Jijini Dar es Salaam.

Jumla ya nchi tisa (9) ambazo ni Tanzania, Kameruni, Komoro, Mauritius, Shelisheli, Rwanda, Kenya, Sudan Kusini na Uganda na wadau wa sekta ya michezo kutoka Baraza la Umoja wa Afrika – *African Union Sports Council* (AUSC) walishiriki. Katika mkutano huo, Waziri mwenye dhamana ya michezo Tanzania alichaguliwa kuwa Makamu Mwenyekiti wa Kanda hiyo jambo linaloendelea kuimarisha nafasi na ushawishi wa Tanzania katika uongozi wa michezo barani Afrika. Aidha, Tanzania ilifanikiwa kupata hadhi ya kuwa mwenyeji wa Sekretarieti ya Baraza la Michezo la Afrika Kanda ya Nne (*AUSC Region IV Secretariat)* kufuatia kusainiwa kwa Mkataba wa uenyeji hatua itakayowezesha nchi kunufaika zaidi na shughuli za michezo za kikanda, kuongeza ajira na utalii.

**211*. Mheshimiwa Spika,*** ikiwa ni hatua ya kuibua na kuendeleza vipaji vya watoto nchini, Serikali imeendelea kuratibu Mashindano ya Michezo ya UMISSETA na UMITASHUMTA kwa kushirikiana na Vyama na Mashirikisho ya Michezo. Serikali kupitia Wizara imeratibu na kushiriki mashindano ya UMITASHUMTA na UMISSETA kwa kushirikiana na OWM - TAMISEMI na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (WEST). Mashindano hayo yalifanyika mkoani Iringa kuanzia tarehe 7 – 30 Juni, 2025 yakihusisha jumla ya timu 28 kutoka Tanzania Bara na Visiwani. Jumla ya michezo 10 ilishindaniwa ambayo ni: Mpira wa Miguu, Mpira wa Mikono, Mpira wa Kikapu, Netiboli, Mpira wa goli, Riadha, Sanaa za Maonesho, Usafi, Nidhamu, Tenisi na Tenisi ya Mezani. Jumla ya wanafunzi 3,194 walishiriki, wakiwemo wavulana 1,611na wasichana 1,583 kutoka mikoa 26 ya Tanzania Bara na Visiwani pamoja na viongozi wa michezo na walimu 843. Serikali imeendelea kuwatumia wadau katika kulea vipaji vinavyopatikana kupitia mashindano hayo. Mashindano hayo yamekuwa na manufaa makubwa katika uibuaji wa vipaji ambapo Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF) likiwa ni wadau muhimu miongoni mwa wadau wakubwa wa kuendeleza vipaji, wanawachukua watoto waliofanya vizuri na kuwaendeleza katika vituo vyao vya michezo vya Kigamboni jijini Dar es Salaam na Mnyanjani Tanga. Aidha kukamilika kwa mradi wa ujenzi wa Shule teule 56 za michezo pamoja na Akademia ya Michezo chuoni Malya kutaongeza wigo wa kuendeleza/kulea vipaji hivyo.

**212.** ***Mheshimiwa Spika,*** sambamba na michezo iliyotajwa hapo juu, Serikali imeratibu michezo ya Shirikisho la Michezo ya Shule za Sekondari Afrika Mashariki (FEASSA) iliyofanyika Kakamega nchini Kenya ambapo jumla ya wanafunzi 4,199 walishiriki kutoka nchi sita (6) ambazo ni Burundi 37, Rwanda 261, na wanafunzi 18 kutoka Ivory Coast. Tanzania iliwakilishwa na wanafunzi 490, Kenya 1,815, Uganda 1,578. Michezo iliyoshindaniwa katika mashindano hayo ni; Kriketi, Mpira wa Goli, Mpira wa Miguu, Mpira wa Pete, Mpira wa Wavu, Mpira wa Besiboli, Mpira wa Mikono, Tenisi ya Meza, Tenisi na Riadha. Tanzania ilifanikiwa kushinda jumla ya medali 10, zikiwemo nne (4) za dhahabu, mbili (2) za fedha, na nne (4) za shaba. Katika kukuza na kuendeleza vipaji vinavyoibuliwa kupitia mashindano hayo, Serikali kupitia Wizara inashirikiana na vyama na mashirikisho ya michezo katika ufuatiliaji wa vipaji ili kuhakikisha wanamichezo wenye vipaji wanaendelezwa na kuunganishwa na timu mbalimbali pamoja na akademia za kitaifa na kimataifa.

**213.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kutambua mchango wa Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa katika kuibua na kuendeleza michezo nchini, Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo imechukua hatua za haraka kwa kuanza majadiliano na OWM– TAMISEMI ili kuhakikisha kuwa Halmashauri zote nchini zinajenga viwanja vya michezo pia maeneo yote yaliyotengwa kwa ajili ya shughuli za michezo yanalindwa, yanatunzwa na kuendelezwa kama ilivyokusudiwa. Hatua hii inalenga kuibua vipaji, kuzuia uvamizi wa maeneo husika na kuhakikisha yanatumika kwa malengo yaliyokusudiwa. Aidha, Serikali inaendelea kuhimiza ushiriki mpana wa sekta binafsi katika kuwekeza kwenye ujenzi wa miundombinu ya michezo.

**214.** ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na juhudi kubwa zinazoendelea kufanywa na Serikali katika ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya michezo nchini, Serikali kupitia Wizara imepata kibali cha kuanzisha Wakala wa Usimamizi wa Miundombinu ya Michezo nchini ujulikanao kama - *Sports Infrastructure Management Agency* (SIMA). Kuanzishwa kwa Wakala huu kutaongeza ufanisi katika utunzaji na uendeshaji wa miundombinu ya michezo iliyopo na inayoendelea kujengwa, sambamba na

kutoa miongozo ya kitaalamu kuhusu ujenzi, usimamizi na uendeshaji wa miundombinu hiyo kwa kuzingatia viwango bora vya kitaifa na kimataifa, pia kutoa ushauri wa kitaalamu kwa wadau wote wanaokusudia kuwekeza katika miundombinu ya michezo nchini. Aidha, kwa kuwa Serikali inaendelea kuwekeza rasilimali fedha kwa kiwango kikubwa katika sekta hii kwa matarajio ya kupata thamani halisi ya uwekezaji wake, Wakala huu utaweka mifumo madhubuti ya usimamizi na utunzaji wa miundombinu hiyo ili kuhakikisha ubora, uendelevu na uwekezaji wenye tija.

**215.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika jitihada za kuimarisha sekta ya michezo nchini, Wizara imefanikiwa kuandaa na kuratibu Kikao Kazi cha 16 cha Maofisa Maendeleo ya Michezo Tanzania kilichofanyika tarehe 28 - 31 Machi, 2026 jijini Arusha ambapo jumla ya wadau 147 walishiriki. Kikao hicho kilihusisha Maofisa Michezo kutoka ngazi ya Wizara, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa na wadau mbalimbali wa sekta ya michezo. Kikao hicho kilitumika kama jukwaa muhimu la kujengeana uwezo, kubadilishana uzoefu na kuimarisha uelewa wa pamoja kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Sekta ya michezo hususani katika ngazi za Halmashauri na Mikoa. Aidha, kupitia kikao hicho, washiriki walipata mafunzo kuhusu fursa zitokanazo na mashindano ya AFCON 2027 na jinsi ya kunufaika nazo.

**216.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha ustawi na afya za wanamichezo nchini, Serikali kupitia Wizara imeendelea kuchukua hatua madhubuti za kuratibu utoaji wa huduma za kinga na tiba michezoni ambapo kwa kipindi cha Julai, 2025 hadi Aprili 2026 jumla ya wanamichezo 771 walioshiriki katika michezo mbalimbali ya kitaifa na kimataifa walipatiwa huduma hizo. Huduma hizo zinalenga kuhakikisha wanamichezo wanapata huduma stahiki za afya kabla, wakati na baada ya mashindano na hivyo kuimarisha uchezaji wao, kulinda afya zao na kuongeza ushindani kwa ngazi ya taifa na kimataifa. Mbali na huduma ya kinga na tiba michezoni, Serikali pia imeendelea kuratibu mafunzo ya tiba na kinga michezoni kwa jumla ya watoa huduma wapatao 240 na wanamichezo 120 wa michezo ya Judo, Ngumi, Riadha na kriketi.

### 3.2.4.2 BARAZA LA MICHEZO LA TAIFA (BMT)

**217.** ***Mheshimiwa Spika***, Baraza la Michezo la Taifa (BMT) limeanzishwa chini ya Sheria ya Baraza la Michezo la Taifa Sura ya 49. Majukumu ya BMT ni pamoja na kuendeleza, kustawisha na kudhibiti aina zote za michezo ya ridhaa na kulipwa kwa kushirikiana na Vyama/Mashirikisho ya Michezo; kuhimiza na kutoa fursa za ushirikiano miongoni mwa Vyama vya Michezo; kuidhinisha mashindano na matamasha ya Kitaifa na Kimataifa yanayoandaliwa na Mashirikisho/Vyama vya Michezo na kuamsha ari ya wananchi kupenda aina zote za michezo. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Aprili 2026 majukumu yaliyotekelezwa na Serikali kupitia BMT yanabainishwa ifuatavyo:

**218.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imeendelea kuendeleza ushirikiano na mataifa mbalimbali katika sekta ya michezo. BMT kwa kushirikiana na taasisi ya ushirikiano wa Kimataifa ya Japani (JICA) limeratibu awamu ya saba ya mashindano ya Riadha kwa Wanawake "*Ladies First*" ambayo yalifanyika jijini Dar es Salaam kuanzia tarehe 28 - 30 Novemba, 2025. Jumla ya wanariadha wa kike 152 kutoka mikoa 31 ya Tanzania Bara na Zanzibar walihudhuria katika mashindano hayo. Mashindano hayo yamekuwa na mafanikio makubwa kwa kuzalisha wanariadha wawili wa kike ambao wameliwakilisha taifa katika mashindano mbalimbali ya kimataifa ikiwemo michezo ya Jumuiya ya Madola, michezo ya Afrika pamoja na Marathoni za kimataifa.

**219.** ***Mheshimiwa Spika,*** BMT imeendelea kutekeleza mipango mbalimbali ya kuhamasisha ushiriki wa watu wenye ulemavu katika michezo. Baraza kwa kushirikiana na Halmashauri ya Manispaa ya Temeke limeratibu tamasha la michezo kwa wanafunzi wenye ulemavu kupitia programu ya michezo kwa wote (Sports for all) ambapo jumla ya wanafunzi 2,000 walishiriki katika tamasha hilo. Vilevile, BMT kwa kushirikiana na Chama cha Mpira wa Meza kwa Watu wenye Ulemavu (Tanzania Para Table Tennis Association) waliendesha mafunzo kwa walimu 23 wa mchezo wa mpira wa meza kwa watu wenye ulemavu kwa lengo la kuongeza idadi ya wataalamu wa michezo ya watu wenye ulemavu.

**220. *Mheshimiwa Spika,*** BMT kwa kushirikiana na Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF) liliratibu mkutano wa Kamati ya Utendaji ya Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika (CAF) ambao ulifanyika tarehe 13 Februari, 2026 jijini Dar es Salaam. Mkutano huo uliwaleta pamoja viongozi 50 wa soka barani Afrika ukiwa na lengo la kujadili na kuweka mikakati ya kukuza vipaji, kuimarisha ushindani wa vilabu na timu za taifa, pamoja na kuongeza uwekezaji katika miundombinu ya mpira wa miguu. Tanzania kuwa mwenyeji wa mkutano huo ni kielelezo cha uwezo wa nchi yetu kuandaa mikutano mikubwa na umeongeza hadhi ya Tanzania katika ramani ya soka Afrika, hasa wakati Taifa linajiandaa na fainali za mashindano ya "Africa Cup of Nations 2027" (AFCON 2027). Kufanyika kwa mkutano huu nchini, umeifanya nchi yetu iendelee kuaminiwa kama kitovu cha maamuzi makubwa ya michezo barani Afrika.

**221. *Mheshimiwa Spika***, Serikali imeendelea kutambua na kuthamini mafanikio ya wanamichezo na timu za Taifa kwa kutoa tuzo kwa wanamichezo waliofanya vizuri katika mashindano mbalimbali ya kimataifa. Baraza la Michezo la Taifa linaendelea kutoa motisha na tuzo kwa wanamichezo waliofanya vizuri kwa msimu wa nne (4) mfululizo tangu mwaka 2022 zilipoanzishwa tuzo hizi na kuwa chachu ya mafanikio katika sekta ya michezo na kwa wanamichezo kwa ujumla. Aidha, kwa msimu wa 2024/25 tuzo zinatarajia kufanyika mwezi Mei 2026 jijini Dar es salaam.

**222. *Mheshimiwa Spika***, Serikali kupitia BMT imeanza ujenzi wa Kituo cha Mafunzi ya Michezo "*Sports Training Centre*" katika mji wa Babati mkoani Manyara. Serikali inatarajia kujenga vituo vya michezo katika kanda saba (7) ambazo ni Kanda ya Kaskazini, Kusini, Mashariki, Kati, Ziwa, Magharibi pamoja na Nyanda za Juu Kusini. Kwa awamu ya kwanza Serikali inaanza ujenzi katika Kanda ya Kaskazini katika Mkoa wa Manyara. Kazi zilizofanyika ni kulipa fidia ya eneo, hati miliki ya eneo na michoro imeandaliwa. BMT lililipa fidia ya eneo lenye ukubwa wa mita za mraba 54,896 kwa thamani ya Shilingi 137,240,000. Pia, Mshauri Elekezi amepatikana ambaye ni *Volumetric Architec Consultancy Ltd* na zabuni ya ujenzi imetangazwa.

**223. *Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Baraza la Michezo la Taifa (BMT) imeendelea kuwezesha ushiriki wa wanamichezo na timu za taifa katika mashindano ya kimataifa ambapo uwezeshaji huo umeleta mafanikio makubwa katika ushiriki wa wanamichezo wetu. Serikali inampongeza mwanariadha Alphonce Felix Simbu aliyefanikiwa kushinda medali ya dhahabu katika mashindano ya riadha ya Dunia yaliyofanyika Septemba 2025 jijini Tokyo, Japani, ikiwa ni medali ya kwanza ya dhahabu kwa Tanzania katika mashindano hayo tangu kupata uhuru, pia kwa kuibuka mshindi wa pili na kushinda medali ya fedha katika mashindano ya marathoni ya kimataifa yaliyofanyika tarehe 20 Aprili, 2026 Jijini Boston, Marekani. Pia, tunampongeza mwanariadha John Nahhay Wele aliyetwaa medali ya dhahabu katika mashindano ya nusu marathon yaliyofanyika tarehe 19 Aprili, 2026 nchini Poland. Vilevile, Serikali inazipongeza Timu ya Taifa ya mpira wa miguu "Taifa Stars" kwa kufika hatua ya 16 bora katika mashindano ya AFCON 2025 yaliyofanyika nchini Morocco na kufika hatua ya robo fainali ya mashindano ya CHAN 2024, Timu ya wanawake ya Futsal kwa kushiriki Kombe la Dunia 2025 nchini Ufilipino na kufika hatua ya makundi, "Twiga Stars" iliyotwaa ubingwa wa CECAFA Senior Women's Championship 2025 na kufuzu WAFCON 2026, pamoja na timu ya Amputee Football kwa kushiriki mashindano ya Afrika Mashariki na Kati nchini Burundi. Aidha, Wizara inatoa pongezi kwa timu ya Taifa ya ngumi kwa kushinda jumla ya medali 18 (dhahabu 1, fedha 4 na shaba 13) katika mashindano ya kanda ya tatu Afrika yaliyofanyika Kenya mwaka 2025; timu ya Kriketi U19 kwa kufuzu Kombe la Dunia la U19 2026 lililofanyika Namibia na Zimbabwe; timu ya mpira wa kikapu ya Dar City iliyoshiriki mashindano ya kikapu Afrika yaliyofanyika nchini Afrika Kusini na kufanikiwa kufuzu kucheza fainali ya mashindano hayo itakayofanyika nchini Rwanda Mei 2026; bondia Ibrahim Class alipigana na kuapata mikanda miwili ya WBC na WBO; bondia Lupakisyo Shoti alishinda mkanda wa IBO Afrika; Amani Bariki (Manichuga) alishinda mkanda wa WBC Intercontinental; Frank Shagembe alishinda mkanda wa WBO Afrika kwa uzito kg 90; Yusuph Changarawe ameshinda mkanda wa WBC Afrika; Halima Vunjabei alishinda mkanda wa PST, mafanikio hayo yanayoonesha maendeleo chanya ya michezo nchini.

**224. *Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia BMT kwa kushirikiana na Shirkisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF) liliratibu mkutano wa Kamati ya Utendaji ya Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika (CAF) ambao ulifanyika tarehe 13 Februari, 2026 jijini Dar es Salaam. Mkutano huo uliwaleta pamoja vigogo wa soka barani Afrika ukiwa na lengo la kujadili na kuweka mikakati ya kukuza vipaji, kuimarisha ushindani wa vilabu na timu za Taifa, pamoja na kuongeza uwekezaji katika miundombinu ya mpira wa miguu. Tanzania kuwa mwenyeji wa mkutano huo ni kielelezo cha uwezo wa nchi yetu kuandaa mikutano mikubwa na umeongezea hadhi ya Tanzania katika ramani ya soka Afrika hususan wakati mataifa yakijiandaa na fainali za AFCON 2027. Ujio wa viongozi hawa unaweka wazi kuwa nchi yetu inazidi kuaminiwa kama kitovu cha maamuzi makubwa ya michezo barani Afrika.

**225. *Mheshimiwa Spika,*** uwekezaji mkubwa unaofanywa na Serikali ya awamu ya sita katika sekta ya michezo umechochea ukuaji wa sekta hii na kuchachusha upatikanaji wa ajira kwa vijana wa kitanzania ndani na nje ya nchi. Wachezaji wa kitanzania 57 wamepata ajira za kulipwa katika nchi mbalimbali, katika vilabu vya mpira wa miguu kwa wanawake na wanaume, mpira wa kikapu, mpira wa miguu kwa watu wenye ulemavu, mchezo wa *softball*, mchezo wa kikapu na mchezo wa wavu.

**226. *Mheshimiwa Spika,*** kutokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia, Wizara kupitia BMT ipo kwenye hatua za ujenzi wa mfumo wa kukusanya mapato, kutoa vibali vya wachezaji pamoja na usajili wa vyama, vilabu pamoja na mashirikisho ya michezo unaoitwa "*Sports Intergrated Management Information System*" (SIMIS). Mfumo huu utaongeza ufanisi katika makusanyo ya mapato ya Serikali pamoja na kurahisisha mchakato wa usajili wa vyama vya michezo. Mfumo huu unajengwa na Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) na unatarajiwa kukamilika Julai 2027 kwa gharama ya shilingi 139,476,000. Mfumo upo kwenye hatua ya upembuzi yakinifu na utarahisisha utoaji wa vibali kwa njia ya mfumo ambao utaunganishwa na taasisi zingine ambazo zinahusika katika shughuli za michezo ili kurahisha huduma kwa wateja.

**227.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia BMT imeidhinisha na kutoa jumla ya vibali 304 sawa na asilimia 75.71 ya lengo la kutoa vibali 350 kwa wanamichezo mbalimbali pamoja na timu za Taifa kushiriki katika mashindano mbalimbali ya Kimataifa. Baraza linaendelea na kusimamia taratibu kwa mujibu wa sheria ili vyama na mashirikisho vifuate taratibu za upatikanaji wa vibali kwa ajili ya kuendesha matukio ya michezo. Vibali vilivyotolewa vinahusisha michezo ifuatayo:-

(a) Mabondia wa Ngumi za kulipwa vibali 56;
(b) Mapromota kuandaa mapambano ya ngumi za kulipwa vibali 31;
(c) Safari za Wanariadha kwenda nje ya nchi vibali 32;
(d) Kuandaa marathoni vibali 18;
(e) Wachezaji na wataalamu wa kigeni vibali 137;
(f) Matukio mengine ya michezo vibali 30; na
(g) Mabonanza vibali 23.

**228.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kutoa elimu kwa umma na kusajili vyama, Akademia, Mawakala, Mashirikisho, na Vilabu vya Michezo kwa kutumia mfumo wa kidigitali, ambapo katika kipindi cha kuanzia Julai 2025 hadi Aprili 2026 jumla ya vyama vya michezo 260 vimesajiliwa ambapo, vituo vya michezo ni 18, akademia 27, mawakala wa michezo 46, mashirikisho 27 na vilabu 142 vimesajiliwa sawa na asilimia 173 ya lengo la kusajili 150.

**229.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kufanya maandalizi ya timu ya Taifa ambayo itashiriki katika mashindano ya AFCON. Ushindani katika mashindano ya AFCON umeendelea kuongezeka kutokana na uwekezaji mkubwa unaofanywa na nchi mbalimbali katika maendeleo ya soka. Kwa kuzingatia kuwa Tanzania itakuwa mmoja ya wenyeji wa mashindano hayo, timu ya Taifa inatakiwa kufanya vizuri ili kulinda heshima ya nchi yetu. Wizara imeendelea kutekeleza Mpango Mkakati madhubuti wa maandalizi ya timu ya taifa unaolenga kuimarisha uwezo wa wachezaji, benchi la ufundi, na mifumo ya maandalizi ya timu kwa ujumla. Mpango huo ni pamoja na kumpata kocha mwenye uwezo wa kuiongoza timu hiyo, kuandaa kambi za muda mfupi kwa ajili ya kuwapa wachezaji uzoefu, kushiriki mechi za kirafiki za

kimataifa, kuimarisha mfumo wa utambuzi wa vipaji pamoja na kuongeza uungwaji mkono wa mashabiki kwa timu ya Taifa kwa kutengeneza jezi zenye ubora na mvuto zitakazovaliwa na wananchi.

**230.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika hatua ya kuimarisha dhana ya utawala bora Wizara kupitia BMT imeratibu na kusimamia chaguzi za vyama na mashirikisho ya michezo, pamoja na kusimamia utawala bora kwa vyama vya michezo kwa kuratibu vikao 21 vya vyama na mashirikisho ya michezo kwa lengo la kujadili masuala ya maendeleo ya michezo ikiwa ni pamoja na kutatua changamoto zinazowakabili. Jumla ya chaguzi 12 sawa na asilimia 300 ya lengo la mwaka zimeratibiwa. Chaguzi zilizosimamiwa na Baraza ni zifuatazo:-

(a) Uchaguzi Mkuu wa chama cha Waamuzi wa Ngumi za Kulipwa Tanzania (ATPBO) uliofanyika jijini Dar es Salaam tarehe 12 Julai, 2025;

(b) Uchaguzi wa Chama cha Mbio za Pikipiki Tanzania uliofanyika jijini Dar es Salaam tarehe 8 Novemba, 2025;

(c) Uchaguzi wa Shirikisho la Taekwondo Tanzania uliofanyika jijini Arusha terehe 15 Novemba, 2025;

(d) Uchaguzi wa Shirikisho la Mpira wa Wavu Tanzania uliofanyika tarehe 21 Desemba, 2025 jijini Dodoma;

(e) Uchaguzi wa Kamati ya Paralimpiki Tanzania (TPC) uliofanyika tarehe 25 Januari, 2026 jijini Dar es Salaam;

(f) Uchaguzi wa Chama cha Michezo ya Mashua Tanzania (TCA) uliofanyika tarehe 9 Februari, 2026 jijini Dar es Salaam;

(g) Uchaguzi wa Chama cha wanawake wa gofu (TLGU) uliofanyika tarehe 22 Februari, 2026 jijini Dar es Salaam;

(h) Uchaguzi wa Chama cha Netiboli Tanzania (CHANETA) uliofanyika tarehe 01 Februari, 2026 jijini Dodoma;

(i) Uchaguzi wa shirikisho la mpira wa kikapu Tanzania (TBF) uliofanyika tarehe 28 Februari, 2026 jijini Dodoma; na

(j) Uchaguzi wa Chama cha Judo Tanzania (JATA) uliofanyika tarehe 16 Januari, 2026 jijini Dar es Salaam.

**3.2.4.3 CHUO CHA MAENDELEO YA MICHEZO MALYA**

**231.** ***Mheshimiwa Spika,*** Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya ni chuo cha kati kilichosajiliwa mwaka 2010 na Baraza la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET) kwa usajili namba REG/PWF/019 na kupatiwa ithibati ya kutoa mafunzo. Chuo hiki ni taasisi muhimu ya Serikali katika kuendeleza taaluma ya michezo nchini na katika kutekeleza na kukuza sekta ya michezo ili iwe sehemu muhimu ya kukuza uchumi wa Taifa. Kupitia Chuo hiki, Serikali inalenga kuandaa wataalamu wa michezo watakaosaidia kuibua na kukuza vipaji, kuboresha usimamizi wa michezo na kuongeza mchango wa sekta hii katika ajira, afya ya jamii na maendeleo ya uchumi kwa ujumla. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi April 2026, Wizara kupitia Chuo imetekeleza majukumu yafuatavyo:

**232.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha rasilimaliwatu katika sekta ya michezo, Serikali kupitia Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya imeendelea kutoa mafunzo ya muda mrefu kwa wanachuo 416, sawa na asilimia 83 ya lengo la kutoa mafunzo kwa wanachuo 500. Mafunzo hayo yametolewa katika programu mbalimbali zikiwemo Astashahada na Stashahada ya Elimu ya Viungo kwa Michezo, Stashahada ya Utawala na Uongozi katika Michezo pamoja na Stashahada ya Ufundishaji wa Michezo. Kupitia programu hizi, Serikali inaendelea kuandaa wataalamu watakaosaidia kuibua na kukuza vipaji vya wanamichezo, kuimarisha usimamizi wa mashindano na kuongeza mchango wa sekta ya michezo katika kuchochea uchumi na ajira kwa vijana.

**233.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuwajengea uwezo na kuongeza ufanisi katika kusimamia na kuendeleza michezo nchini, Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya kimetoa mafunzo ya muda mfupi kwa wadau mbalimbali wa michezo. Jumla ya wadau 279

wamenufaika na mafunzo, wakiwemo viongozi wa vilabu na makocha 52, watoa huduma ya kwanza na madaktari wa timu 108, waamuzi 30, mawakala wa wachezaji 11 na waandishi wa habari za michezo 20. Mafunzo hayo yametolewa katika Nyanja za Usimamizi wa Michezo (Sports Management), usimamizi wa majeraha ya michezo na uhamasishaji wa udhibiti wa matumizi ya dawa zilizokatazwa michezoni, mafunzo ya Mikataba na Ustawi wa Wachezaji (Sports Agency Contract Management and Athlete Welfare) na mafunzo ya sheria za Michezo, mikataba na masuala ya maadili (sports law, contract and ethical issues). Mafunzo haya ni sehemu ya jitihada za Serikali kulinda maslahi ya wanamichezo na kuhakikisha sekta ya michezo inasimamiwa kwa weledi na uwazi.

**234.** ***Mheshimiwa Spika,*** Chuo kilitoa mafunzo kwa waongoza vituo vya mazoezi ya viungo *(Fitness and Gym Instructors)* 28 wa vituo 28 Nchini. Vilevile, mafunzo ya michezo mbalimbali ikiwemo mpira wa miguu, mikono, kikapu, wavu, goli na mchezo wa riadha yalifanyika katika Halmashauri ya Jiji la Arusha yakihusisha walimu 44 wa michezo kutoka shule za msingi na sekondari.

**235.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika dhamira ya dhati ya kuijenga Tanzania yenye vijana wenye ujuzi, ajira na mchango hai katika uchumi wa Taifa, Wizara imeendelea kuchukua hatua madhubuti kuhakikisha kuwa mitaala ya mafunzo inaendana kikamilifu na kasi ya mabadiliko ya sekta ya michezo duniani pamoja na mahitaji halisi ya soko la ajira. Kupitia Chuo husika, Serikali imefanya maboresho ya kimkakati katika mitaala ya programu za pamoja na *Sports Coaching*, katika ngazi ya tano na sita.

**236.** ***Mheshimiwa Spika,*** maboresho haya si ya kawaida, yamelenga kwa makusudi kabisa kuimarisha mafunzo kwa vitendo, kuongeza ubora wa ujuzi kwa wanafunzi wetu, na kuhakikisha kuwa wahitimu wanaandaliwa kuwa wataalamu mahiri, wabunifu na wenye uwezo wa kushindana katika soko la ajira la ndani na kimataifa. Hatua hii inaakisi dira ya Serikali ya kuhakikisha sekta ya michezo inakuwa chanzo cha ajira, kipato na fahari ya taifa letu. Tunajenga kizazi chenye maarifa, nidhamu na weledi kitakachoipeleka Tanzania mbele kupitia michezo.

**237.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuhakikisha mitaala ya mafunzo inaendana na mabadiliko ya sekta ya michezo Duniani na mahitaji ya soko la ajira, Wizara kupitia Chuo imefanya maboresho katika mitaala ya programu za Elimu ya Viungo kwa Michezo (Physical Education and Sports), Uongozi na Utawala wa Michezo pamoja na Ufundishaji wa Michezo (Sports Leadership and Management), katika ngazi ya tano na sita. Maboresho hayo yamelenga kwa makusudi kabisa kuimarisha mafunzo kwa vitendo, kuongeza ubora wa ujuzi kwa wanafunzi wetu, na kuhakikisha kuwa wahitimu wanaandaliwa kuwa wataalamu mahiri, wabunifu na wenye uwezo wa kushindana katika soko la ajira la ndani na kimataifa.

**238.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kupanua wigo wa programu za mafunzo ili kuendana na mwelekeo wa sasa wa maendeleo ya michezo duniani, Wizara kupitia Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya kwa kushirikiana na Baraza la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET) imeandaa mitaala mipya mitatu (3) ambayo itaanza kufundishwa mwaka wa masomo 2026/27. Mitaala hiyo ni Mtaala wa Usimamizi wa Michezo katika Jamii, Afya na Ustawi *(Community Sports, Health and Wellness Management)*, Uandishi wa Habari za Michezo *(Sports Journalism)*, Utalii wa Michezo *(Sports Tourism)* na Masoko ya Michezo na Ukarimu *(Sports Marketing and Hospitality Studies)*. Programu hizi zinalenga kuongeza thamani ya sekta ya michezo katika uchumi wa Taifa kwa kufungua fursa za ajira, ubunifu na uwekezaji katika michezo.

**239.** ***Mheshimiwa Spika***, Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya kimeendelea kuimarisha ushirikiano wa kimataifa katika maendeleo ya michezo kwa kuanzisha ushirikiano na taasisi 4 za kimataifa. Ushirikiano huu unalenga kubadilishana utaalamu, kufanya tafiti na kuendeleza elimu ya michezo. Katika hatua hiyo, Wizara imeanzisha ushirikiano na Taasisi ya *Yoga for Wellness Tanzania/Africa* ili kuendeleza programu za michezo kwa afya na ustawi wa jamii. Vilevile, majadiliano yanaendelea na Chuo Kikuu cha North Carolina nchini Marekani yenye lengo la kuboresha eneo la habari za michezo, Chuo Kikuu cha Michezo cha Scuber nchini Japan kwa ajili ya kubadilishana utaalamu wa michezo.

Hali kadhalika, majadiliano na *Norwegian School of Sports Sciences* yanaendelea kwa ajili ya kupata vifaa na mafunzo yatakayosaidia kukuza Akademia za Michezo.

**240.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuongeza ufanisi wa shughuli za michezo pamoja na kushughulikia changamoto ya uhaba wa wataalamu wa michezo katika shule za msingi, sekondari na taasisi zingine za umma, Wizara kupitia Chuo imeandaa andiko la mpango wa ushirikiano wa kitaasisi na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI pamoja na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa lengo la kuimarisha utoaji wa elimu ya michezo katika ngazi mbalimbali za elimu. Lengo kuu la ushirikiano huu ni kuimarisha mfumo wa utoaji wa elimu ya michezo katika ngazi zote za elimu, sambamba na kuweka mazingira wezeshi ya kitaasisi yatakayochochea ubunifu, utaalamu na ushindani. Kupitia mpango huu, Serikali inalenga kuibua, kulea na kukuza vipaji vya michezo kwa utaratibu endelevu, kuanzia ngazi ya shule hadi kufikia viwango vya juu vya kitaaluma kitaifa na kimataifa, hivyo kuchangia kikamilifu katika ajenda ya taifa ya kukuza ajira, afya na hadhi ya nchi katika medani za kimataifa.

**241.** ***Mheshimiwa Spika***, ili kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia, Serikali imekamilisha ukarabati wa madarasa matatu (3), jengo moja (1) la ofisi (utawala) pamoja na ujenzi wa jengo la hosteli la ghorofa nne (4) lenye uwezo wa kuchukua wanachuo 198. Kukamilika kwa miundombinu hii kunaongeza uwezo wa Chuo kudahili wanafunzi wengi zaidi na hivyo kuongeza idadi ya wataalamu wasio tia shaka katika tasnia ya michezo nchini. Aidha, Serikali imenunua magari mawili (2) likiwemo basi dogo la Chuo kwa ajili ya kurahisisha safari za mafunzo kwa vitendo kwa wanachuo pamoja na gari la Mkuu wa Chuo ili kuboresha ufanisi wa shughuli za kiutendaji. Hatua hizi zimeendelea kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia Chuoni.

**242.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuhakikisha vipaji vya michezo mbalimbali vinaibuliwa na kuendelezwa, Serikali inaendelea na ujenzi wa miundombinu ya Akademia ya Michezo ambao umefikia asilimia 49**.** Kupitia akademia hii, Serikali inalenga kuibua

na kukuza vipaji vya vijana, kuandaa wataalamu wa michezo watakaokidhi vigezo vya kitaifa na kimataifa ili kuifanya sekta ya michezo kuwa chanzo muhimu cha ajira, kipato na uchumi. Aidha, maendeleo ya akademia hii yatawezesha kuvutia mashindano na uwekezaji wa michezo kutoka ndani na nje ya nchi.

### 3.2.5 KUIMARISHA UTENDAJI WA WIZARA NA RASILIMALIWATU

**243.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuleta tija na ufanisi katika utekelezaji wa majukumu, Serikali kupitia Wizara inaendelea kutoa huduma ya usafiri kwa viongozi na watumishi ambapo Wizara imeimarisha sehemu ya usafiri kwa kuipatia vitendea kazi vipya na vya kutosha yakiwemo magari. Jumla ya magari 23 yameendelea kutumika na kuhudumiwa. Vilevile, Wizara imeendelea kulipa stahiki za viongozi na watumishi kwa kuzingatia Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo mbalimbali iliyowekwa na Serikali. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2026, Watumishi 50 wamelipwa gharama za likizo, watumishi sita (6) wamelipwa stahiki za uhamisho na watumishi watatu (3) wamelipwa stahiki za kusafirisha mizigo baada ya utumishi wao wa umma kukoma.

**244.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kusimamia upatikanaji wa huduma za ulinzi na usafi kwa ofisi za Wizara zilizopo Mtumba Dodoma na Eneo Changamani la Michezo Dar es Salaam. Huduma zote zinatolewa kwa kuzingatia miongozo mbalimbali ya Serikali. Sambamba na hilo, ili kuimarisha utaalamu na ujuzi, Wizara imeendelea kuratibu na kuwezesha watumishi kupata mafunzo ya muda mrefu na mfupi ndani na nje ya nchi ambapo jumla ya watumishi 51 wamehudhuria mafunzo hayo, kati ya hao wanaume ni 31 na wanawake ni 20. Kati yao watumishi 27 wanaendelea kupata mafunzo ya muda mrefu kwa idadi ya wanaume 16 na wanawake 11. Aidha, watumishi 24 wamehudhuria mafunzo ya muda mfupi ambapo wanaume ni 15 na wanawake ni tisa (9). Mafunzo hayo ni kwa ajili ya kuwajengea uwezo na kukidhi vigezo vya miundo mbalimbali ya kiutumishi.

**245.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inaendelea kuboresha mazingira ya utendaji kazi na kuwapatia watumishi vitendea kazi. Watumishi

wamehamia kwenye jengo jipya la wizara lenye nafasi ya kutosha na samani nzuri. Sambamba na hilo, mazingira ya kazi yameboreshwa kwa kuwapatia vifaa vya kisasa vinavyoendana na mabadiliko ya teknolojia zikiwemo kompyuta na printa. Katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Aprili 2026, Wizara imenunua kompyuta za mezani 55, kompyuta mpakato 30 na printa 10. Juhudi zote hizi zinalenga kuongeza ari ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara na kuongeza ufanisi.

**246.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inatambua kuwa mazingira bora ya utendaji kazi pamoja na ustawi wa watumishi, ni chachu ya kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu. Hivyo, Wizara inaendelea kuboresha mazingira ya utendaji kazi na ustawi wa watumishi. Kwani kwa kufanya hivyo, watumishi watakuwa na utulivu ambao utaongeza ari katika utekelezaji wa majukumu.

## 4.0 CHANGAMOTO ZILIZOJITOKEZA NA HATUA ZILIZOCHUKULIWA KUKABILIANA NAZO

**247.** ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na mafanikio yaliyopatikana mwaka 2025/26, changamoto katika utekelezaji wa majukumu hazikosekani. Changamoto hizo na hatua zilizochukuliwa na Serikali ni kama ifuatavyo:-

(i) Ufinyu wa bajeti ya Wizara hususan ya Matumizi Mengineyo (OC), unaosababisha kushindwa kutekeleza baadhi ya majukumu yake ikiwemo kufanya tafiti mbalimbali kuhusu utamaduni, mila na desturi za mtanzania, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbuku;

(ii) Kasi ya maendeleo ya sayansi na teknolojia na utandawazi inayosababisha upotoshwaji wa mila, desturi na maadili hususan kwa vijana na wasanii; na

(iii) Kuwepo kwa migogoro kwenye baadhi ya vyama na vilabu vya michezo hivyo kukwamisha maendeleo ya michezo.

**248.** ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na changamoto hizo, Serikali imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa kutumia njia

mbalimbali za kutatua changamoto hizo. Miongoni mwa njia ilizozitumia ni pamoja na:-

(i) Kuendelea kutafuta kikamilifu vyanzo vipya vya mapato kwa kupitia upya sheria na kanuni zinazosimamia sekta zilizo chini ya mamlaka yake;
(ii) Kuendelea kutoa elimu kwa vijana na wasanii kupitia njia mbalimbali ikiwemo semina, mikutano na warsha. Pia, mafunzo hutolewa kwa njia ya vyombo vya habari na mitandao ya kijamii; na

(iii) Serikali kupitia Baraza la Michezo la Taifa inaendelea kutoa elimu kwa wadau wa michezo kuhusu uzingativu wa sheria na taratibu kwa maendeleo ya sekta.

## 5.0 MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/27

**249** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha wa 2026/27, Wizara na Taasisi zake kwa kushirikiana na wadau itatekeleza majukumu mbalimbali kwa kuzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050; Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2026/27- 2030/31); Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (2025 - 2030); Maelekezo ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alipohutubia Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 14 Novemba, 2025; maelekezo ya Hotuba ya Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu Mwelekeo wa Kazi za Serikali kwa Mwaka 2026/27; Mpango Mkakati wa Wizara (2026/27 2030/31); Malengo ya Umoja wa Mataifa kuhusu Maendeleo Endelevu ya Mwaka 2030; na Sera, Sheria na Miongozo mbalimbali ya Sekta za Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo.

### a. SEKTA YA HABARI

#### i. IDARA YA HABARI - MAELEZO

**249.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara, kupitia Idara ya Habari – MAELEZO, katika mwaka wa fedha 2026/27 itaendelea kutekeleza

jukumu la kusimamia Sekta ya Habari ili kuhakikisha Watanzania wanapata taarifa sahihi na kwa wakati. Katika kutekeleza hilo, Wizara itaratibu na kuandaa mikutano ya Msemaji Mkuu wa Serikali kwa lengo la kuelezea utekelezaji wa miradi ya kimkakati, pamoja na kukusanya, kuchakata na kusambaza habari na makala kuhusu utendaji wa Serikali. Vilevile, Wizara itaratibu na kufanya tathmini ya utoaji wa taarifa za Serikali kwa umma, kwa lengo la kuhakikisha kuwa wananchi wanaendelea kupata taarifa sahihi, kwa wakati, kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Serikali. Aidha, Wizara itaratibu na kuandaa mikutano ya Wizara na taasisi za Serikali na waandishi wa habari, ili kuimarisha mawasiliano kati ya Serikali na vyombo vya habari.

**250. *Mheshimiwa Spika***, kadhalika, Wizara itaratibu kikao kazi cha mwaka cha Maofisa Habari wa Serikali pamoja na mkutano wa mwaka wa maendeleo ya Sekta ya Habari. Pia, itaendelea na jukumu la kuchapisha leseni za magazeti na majarida, kuchapisha Jarida la *NCHI YETU*, pamoja na kusambaza picha rasmi za Baba wa Taifa, Mwalimu Julius K. Nyerere. Sambamba na hayo, Wizara itaendelea kuratibu utambuzi wa akaunti za mitandao ya kijamii ya taasisi za Serikali, pamoja na kuratibu vyombo vya habari na waandishi wa habari wa ndani na nje ya nchi katika matukio mbalimbali ya kitaifa na ziara za viongozi. Hatua hizi zinalenga kuimarisha utoaji wa taarifa sahihi na kuongeza uwazi katika utekelezaji wa shughuli za Serikali.

## ii. SHIRIKA LA UTANGAZAJI TANZANIA (TBC)

**251. *Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka 2026/27, TBC imepanga kutekeleza majukumu yafuatayo; kuhakikisha upatikanaji wa maudhui ya redio (TBC Taifa, Bongo FM na TBC International), Televisheni (TBC1, TBC2, Tanzania Safari Chaneli na Televisheni ya Kiingereza), TBC mtandao, kurasa za mitandao ya Kijamii na redio za Kanda za TBC (TBC Dodoma na TBC Arusha); kuendelea kuhabarisha, kuelimisha na kuburudisha kwa kutangaza utekelezaji wa shughuli za kimkakati za Serikali, kurusha matangazo ya michuano ya mpira wa miguu kitaifa (NBC Premier League mechi 180) na kimataifa (AFCON mechi 64) na kushiriki kampeni za kimkakati za kuhabari zinazoendana na Dira ya Taifa

ya Maendeleo 2050 (Kampeni za mazingira (*Pika kijanja* na *Jicho la Mpita njia*) na Kampeni za utalii *(Slave Caravan*)); kurusha matangazo mubashara ya viongozi wakuu wa kitaifa na matukio yenye manufaa ya umma 500 pamoja na sherehe 15 za kitaifa; na kulipa stahiki za watumishi, upatikanaji wa vitendea kazi na mafunzo kwa watumishi 100 wa kada mbalimbali.

**iii. KAMPUNI YA MAGAZETI YA SERIKALI (TSN)**

**252.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2026/27, TSN imepanga kutekeleza majukumu yafuatayo; kuandaa na kuchapa makala maalumu za kuhabarisha umma juu ya michuano ya AFCON 2027; kuhabarisha na kuelimisha umma juu ya Mipango, miongozo, mikakati, sera na miradi ya kimkakati inayotekelezwa na Serikali; kuchapa na kusambaza nakala 1,909,752 za magazeti ya *Daily News* na HabariLEO; kukamilisha mradi wa ukarabati wa Studio ya kisasa ya kidigiti; kuandaa maudhui ya kidigitali na kusambaza kupitia chaneli ya *Dailynews Digital* na mitandao ya kijamii; kuandaa sheria ya kuanzishwa kwa TSN; na kuwezesha stahiki na kuendesha mafunzo ya muda mfupi kwa watumishi 130 na mafunzo ya muda mrefu kwa watumishi 18.

**iv. BODI YA ITHIBATI YA WAANDISHI WA HABARI**

**253.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2026/27, Bodi ya Ithibati ya Waandishi wa Habari itaendelea kutekeleza jukumu lake la kisheria kwa kutoa ithibati na vitambulisho 500 kwa waandishi wa habari kwa lengo la kuhakikisha kuwa waandishi wote wanatekeleza majukumu yao wakiwa na utambulisho rasmi wa kisheria na unaokidhi viwango vya taaluma na maadili; hatua hii itachangia kuongeza ufanisi katika utendaji wa sekta ya habari sambamba na kuimarisha na kuboresha ubora wa kanzidata ya waandishi wa habari nchini.

**254.** ***Mheshimiwa Spika***, Bodi ya Ithibati, imejipanga kuimarisha usimamizi wa uzingatiaji wa maadili ya taaluma ya uandishi wa habari kwa mujibu wa sheria na kanuni za maadili ya taaluma. Katika kutekeleza azma hiyo, Bodi itaboresha mifumo ya kupokea, kuchakata na kushughulikia malalamiko ili kuhakikisha kuwa haki

inatendeka kwa wakati, kwa uwazi na kwa kuzingatia misingi ya haki, usawa na uwajibikaji. Aidha, Bodi itaongeza matumizi ya mifumo ya kidijiti na kuimarisha ufuatiliaji wa mwenendo wa malalamiko ili kuongeza ufanisi, uwazi na imani ya wadau katika utekelezaji wa majukumu yake.

**255.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Bodi ya Ithibati, itaendelea kutoa elimu na mafunzo kwa umma na waandishi wa habari nchini kama sehemu ya kuimarisha taaluma na uelewa wa majukumu ya Bodi ya Ithibati; mafunzo haya yatatekelezwa kwa mtindo endelevu katika kanda tano (5) yakilenga kuwawezesha waandishi kuendana na mabadiliko ya teknolojia, kuzingatia maadili ya taaluma, na kuongeza ubora na weledi wa kazi zao. Aidha, Bodi itaongeza na kuimarisha ushirikiano na taasisi mbalimbali zikiwemo vyuo vikuu, mamlaka za usimamizi na wadau wa sekta ya habari ili kuhakikisha mafunzo yanayotolewa yanakuwa yenye tija, yanazingatia viwango vya kitaaluma, na yanakidhi mahitaji ya wakati pamoja na changamoto zinazoibuka katika mazingira ya kazi.

**256.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2026/2027, Bodi ya Ithibati, imepanga kufanya maboresho ya mfumo wa ithibati na usajili kwa ajili ya kanzidata ya waandishi wa habari nchini. Maboresho hayo yanalenga kuimarisha utambuzi wa waandishi wa habari, kuboresha taratibu za usajili ili ziwe rahisi, wazi na zenye ufanisi zaidi, pamoja na kuongeza usahihi wa taarifa zinazohifadhiwa katika kanzidata hiyo kwa madhumuni ya upangaji, ufuatiliaji na usimamizi bora wa taaluma.

**v. KAMATI YA MAUDHUI**

**257.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2026/27, Kamati ya Maudhui imepanga kuendelea kutoa elimu kwa watoa huduma za maudhui na imeandaa kitabu elekezi kuhusu Kanuni, Miongozo, Masharti ya Leseni na Maadili ya Uandishi na Utangazaji wa Habari. Vilevile, Kamati itaendelea kufuatilia uzingatiaji wa maadili ya utangazaji ili kuhakikisha watoa huduma wanatoa maudhui yanayokidhi Sheria, Kanuni na miongozo iliyopo kwa kuendelea kufanya vikao vya mashauriano na watoa

huduma, na wadau/taasisi nyingine za sekta ya Habari na Utangazaji. Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania, kupitia Kamati ya Maudhui, inatekeleza mfumo wa kushauriana na watoa huduma na kuwapa fursa ya kuondoa kasoro zinazojitokeza kabla ya kuchukua hatua za kiusimamizi.

## b. SEKTA YA MAENDELEO YA UTAMADUNI

### i. IDARA YA MAENDELEO YA UTAMADUNI

**258.** ***Mheshimiwa Spika,*** malengo yaliyopangwa kutekelezwa na Idara ya Maendeleo ya Utamaduni kwa mwaka 2026/27 ni kukamilisha uandishi wa Sera ya Utamaduni ya Mwaka 1997 Toleo la Mwaka 2026; kufuatilia utekelezaji wa Sera ya Utamaduni ya mwaka 1997 katika mikoa na mamlaka za Serikali za Mitaa; kuratibu Kampeni ya kitaifa ya kukabiliana na changamoto za mmomonyoko wa maadili nchini; kuandaa Kikao Kazi cha Sekta ya Utamaduni nchini; kuratibu Tamasha la Nne la Kitaifa la Utamaduni na Matamasha mengine matano (5) ya utamaduni yanayoandaliwa na wadau; kuratibu maendeleo na matumizi ya lugha ya Kiswahili kitaifa na kimataifa pamoja na kufanya tafiti za lugha, mila na desturi za jamii za kitanzania.

### ii. BARAZA LA KISWAHILI LA TAIFA (BAKITA)

**259.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2026/27, majukumu yaliyopangwa kutekelezwa ni kuratibu Maadhimisho ya Siku ya Lugha ya Kiswahili Duniani katika ngazi ya kitaifa na kikanda; kufanya Kongamano la Kimataifa la Kiswahili jijini Paris, Ufaransa; kusanifisha Istilahi za michezo (AFCON), Sheria na Mseto; kuendeleza Kongoo ya Kiswahili (KOKITA); kutoa elimu ya matumizi fasaha na sanifu ya lugha ya Kiswahili kwa kuandaa na kurusha hewani jumla ya vipindi 750 kupitia redio na televisheni; kutoa mafunzo ya kuimarisha stadi za kufundisha Kiswahili kwa wageni; na kutoa mafunzo ya msasa ya matumizi ya Kiswahili fasaha na sanifu kwa makundi maalumu.

**260.** ***Mheshimiwa Spika***, majukumu mengine ni pamoja na kuendesha mtihani wa kupima umahiri wa lugha ya Kiswahili kwa

wageni; kuendesha mafunzo ya Kiswahili kwa wageni; kufanya tafiti kwa lengo la kuongeza maneno kwenye Kongoo ya Kiswahili; kuendesha mafunzo kwa wakalimani; na kutoa huduma ya tafsiri kwa nyaraka 800 na kuthibisha kazi 3,000 zinazofanywa na mawakala wa Baraza.

**iii. KITUO CHA URITHI WA UKOMBOZI WA BARA LA AFRIKA**

**261.** ***Mheshimiwa Spika***, Kituo cha Urithi wa Ukombozi wa Afrika kitafanya ufuatiliaji wa uhifadhi katika maeneo 15 ya Ukombozi; na kuanzisha vituo saba (7) vya taarifa katika mikoa ya Morogoro, Mbeya, Dodoma, Lindi, Pwani, Iringa na Ruvuma kwa ajili ya kukuza utalii wa ukombozi, utafiti na elimu.

**c. SEKTA YA MAENDELEO YA SANAA**

**i. IDARA YA MAENDELEO YA SANAA**

**262.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2026/27, majukumu yaliyopangwa kutekelezwa na Idara ya Maendeleo ya Sanaa ni kusimamia maandalizi na uendeshaji wa mashindano ya 74 ya kimataifa ya Miss World 2027 yanayofungamanishwa na AFCON 2027 ili kupata manufaa makubwa ya kiuchumi; kufanya tathimini ya utekelezaji wa majukumu yanayotekelezwa na taasisi zilizo chini ya Idara ya Maendeleo ya Sanaa; kufuatilia utekelezaji wa Sera ya Utamaduni katika mikoa 10 ya Tanzania Bara; kuandaa Mkakati wa Maendeleo wa Sekta ya Sanaa; na kuratibu matamasha 3 ya kitaifa na 3 ya kimataifa ya Sanaa ikiwemo Serengeti Music Festival; kuibua na kukuza vipaji vya Sanaa; kuratibu tafiti za mchango wa sekta ya Sanaa kwenye Pato la Taifa; kusimamia hamasa ya ushiriki wa wananchi kwenye mashindano ya AFCON 2027 kupitia shughuli za Sanaa na burudani; na kufuatilia utekelezaji wa Miradi yaTaasisi za Sanaa.

**ii. BODI YA FILAMU TANZANIA**

**263.** ***Mheshimiwa* Spika**, katika mwaka wa fedha 2026/27, majukumu yatakayotekelezwa na Bodi ya Filamu ni kuwajengea uwezo wasanii 500 wa filamu na michezo ya kuigiza kupitia

programu mbalimbali; kusimamia maudhui ya filamu kwa kuhakiki na kupanga katika madaraja filamu na tamthilia 300; kusimamia maudhui ya filamu kwa kuhakiki na kupanga katika madaraja michezo sita (6) ya jukwaani; kuratibu Tamasha 1 la Tuzo za Filamu Tanzania (TAFFA) na kusimamia utekelezaji wa matamasha matano (5) yatakayoandaliwa na wadau; kusimamia utayarishaji wa filamu kwa kuchakata maombi na kutoa vibali 400 vya utayarishaji wa filamu; na kuimarisha urasimishaji wa biashara za filamu kwa kutoa leseni 450 na vitambulisho 350 vya wasanii wa filamu na Michezo ya Kuigiza.

**iii. BARAZA LA SANAA LA TAIFA (BASATA)**

**264.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2026/27, BASATA imepanga kutekeleza majukumu mbalimbali ikiwamo; kukuza na kuimarisha Sekta ya Sanaa ili iendelee kutengeneza fursa za ajira na kuchangia Pato la Taifa; kusimamia uzingatiaji wa Maadili katika shughuli za Sanaa kwa kutekeleza Miongozo nane (8) iliyoandaliwa na BASATA na kuandaa miongozo mitano (5); kuimarisha uhusiano na Wadau wa Sekta ya Sanaa wa ndani wanne (4) na wawili (2) nje ya nchi; kuimarisha kanzidata ya wasanii kwa kufanya utambuzi na usajili wa wasanii na wadau wa sanaa nchini 12,000; kuimarisha utumiaji wa mifumo ya TEHAMA katika kurahisisha utoaji na upatikanaji wa Huduma za Baraza; na kuandaa tuzo ya ubora wa kazi za sanaa.

**iv. OFISI YA HAKIMILIKI TANZANIA (COSOTA)**

**265.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha kuwa usimamizi wa Hakimiliki nchini unafanyika kwa ufanisi mkubwa Wizara kupitia COSOTA imepanga kutekeleza majukumu yafuatayo: kufanya mapitio ya Kanuni mbili (2) za Sheria ya hakimiliki na hakishiriki; kutoa leseni kwa Kampuni za Kukusanya na Kugawa Mirabaha (CMOs) katika madaraja manne (4) ya muziki, kazi za maandishi, kazi za vielelezo vya kusikia na kuona *(audiovisual)*, sanaa za maonesho na ufundi; kufanya usimamizi, ufuatiliaji na tathmini za utendaji wa CMOs kila robo mwaka, ikijumuisha ukusanyaji na ugawaji wa mirabaha kwa wanufaika; kutoa leseni 10 kwa watumiaji wa kazi za hakimiliki katika madaraja ambayo hayana

CMOs; kufanya programu nne (4) za uhamasishaji na uelimishaji kwa watumiaji na wamiliki wa hakimiliki; kufanya oparesheni nne (4) za kupambana na uharamia (piracy) dhidi ya kazi za sanaa na ubunifu; na kusajili kazi 2,000 za wamiliki wa kazi za ubunifu.

**266.** ***Mheshimiwa Spika,*** majukumu mengine yatakayotekelezwa ni: kukusanya tozo ya hakimiliki hadi kufikia shilingi bilioni 1.4 kwa mwaka; kuratibu utatuzi mbadala wa migogoro *(Alternative Dispute Resolution - ADR)* ya hakimiliki; kuimarisha uwezo na uendelevu wa kifedha wa taasisi kwa kuandaa na kutekeleza mkakati wa kuboresha mapato; kuandaa na kuboresha miongozo mitatu (3) ya ndani kwa ajili ya kuimarisha mifumo ya utendaji na kuboresha ufanisi; kufanya tafiti moja (1) inayohusiana na masuala ya hakimiliki kwa kushirikiana na vyuo vikuu na taasisi za utafiti; kujenga na kuimarisha mahusiano na ushirikiano na wadau wa tasnia ya sanaa na ubunifu ndani (Taasisi 5 – Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Tume ya Ushindani (FCC), Jeshi la Polisi na nje ya nchi (Mashiriki 6 - WIPO, ARIPO, CISAC, International Federation of Reproduction Rights Organization (IFRRO), International Federation of the Phonographic Industry (IFPI), African Continental Free Trade Area (AfCFTA); kuboresha mfumo wa usajili kidijiti Copyright Registration Management Information System (CRMIS); na kuanzisha Kanzidata ya Kitaifa ya Kazi za Ubunifu.

**v. TAASISI YA SANAA NA UTAMADUNI BAGAMOYO (TaSUBa)**

**267.** ***Mheshimiwa Spika***, kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2026/27, majukumu yatakayotekelezwa ni kudahili na kusajili wanafunzi 900 wa kozi ndefu na 350 wa kozi fupi; kuandaa mitaala mitatu (3) ya masomo ya Sanaa na Utamaduni; kuandaa Tamasha la 44 la Kimataifa la Sanaa na Utamaduni Bagamoyo; kutangaza shughuli na mazao yatokanayo na chuo kwa kufanya ziara kwa shule za sekondari 20 katika mikoa ya Dar es Salaam na Pwani; na kuendesha mafunzo ya kozi fupi kwa wanachuo 100 kwenye vituo vya Dar es Salaam na Songea.

## vi. MFUKO WA UTAMADUNI NA SANAA TANZANIA

**268.** ***Mheshimiwa Spika,*** malengo ya Mfuko wa Utamaduni na Sanaa kwa mwaka 2026/27 ni yafuatayo: kutoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 20 kwa wadau wa tasnia za habari, utamaduni na sanaa; kutangaza huduma zake kwa Wadau kupitia vipindi vya Televisheni, redio, machapisho ya magazeti, machapisho katika mitandao ya kijamii pamoja na vipeperushi; kuwakutanisha wadau wa utamaduni na sanaa pamoja kwa ajili ya kujengewa uwezo na kubadilishana uzoefu na kutatua changamoto za masoko ambapo utaandaa Mkutano Mkuu wa mwaka wa tatu (3) wa wadau wa mfuko na maonesho ya kimataifa ya kazi za utamaduni na sanaa; kuchochea urasimishaji wa kazi za kiutamaduni na Sanaa 11,000 ili zijiendeshe kibiashara, zikuze uchumi na kuzalisha ajira nchini; na kushirikiana na taasisi 5 za kimataifa na taasisi 10 za kitaifa katika kutekeleza shughuli mbalimbali kama mafunzo.

## d. SEKTA YA MAENDELEO YA MICHEZO

### i. IDARA YA MAENDELEO YA MICHEZO

**269.** ***Mheshimiwa Spika***, kuelekea mashindano ya AFCON 2027 yatakayofanyika kuanzia tarehe 19 Juni hadi 17 Julai, 2027, Wizara imejipanga kikamilifu kwa kushirikisha wadau wote kuhakikisha mashindano haya siyo tu yanafanyika bali yanaweka historia na alama isiyofutika kwa taifa letu. Tayari tunazo Kamati mbalimbali za uratibu kitaifa na katika hili nimshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye ni mwenyekiti wa Kamati Kuu ya Kitaifa na Waheshimiwa Mawaziri wote kwa ushiriki wao madhubuti.

**270.** ***Mheshimiwa Spika***, pamaoja na miundombinu iliyoelezewa hapo awali, tayari Serikali imewaunganisha pamoja wadau katika sekta za utalii na ukarimu hususan mighahawa, hoteli na huduma za malazi, huduma za usafiri na ushafirishaji (magari, treni, ndege na meli), maeneo ya starehe na burudani kwa mashabiki (fun zones), maboresho ya muonekano wa miji yetu, vivutio vya utalii (mbuga, fukwe, malikale n.k.), matibabu ya kibingwa, ulinzi na

usalama, uhamiaji n.k. Mkakati mahsusi wa hamasa kuelekea AFCON 2027 umeandaliwa ambapo utazinduliwa hivi karibuni na kuhakikisha kuwa kila mtanzania anakuwa sehemu ya mashindano haya kwa lengo lengo la kunufaika na fursa za AFCON na kutangaza nchi.

**271.** ***Mheshimiwa Spika***, kutokana na hayo yote tumeendelea kushirikiana na wadau na wanamichezo maarufu walioonekana kusaidia au kutoa mchango mkubwa kwa nchi zao na dunia katika soka. Na hapa niruhusu nimtambue mwanamichezo maarufu Didier Drogba ambaye ni mchezaji bora wa wakati wote na nahodha wa zamani wa timu ya taifa ya Ivory Coast. Pia, amewahi kutumikia vilabu vikubwa vya mpira wa miguu duniani vya Chelsea na Galatasaray na ni mmiliki wa klabu ya Phoenix Rising ya Marekani. Uwepo wake leo ni uthibitisho tosha wa namna gani Serikali imeamua kuitumia AFCON 2027 kuitangaza taswira ya Tanzania kimataifa.

**272.** ***Mheshimiwa Spika***, majukumu mengine ni: kuratibu na kushiriki mikutano na makongamano ya kitaifa na kimataifa ya michezo; kuratibu udhibiti wa matumizi ya dawa na mbinu haramu michezoni; kuratibu Michezo ya UMITASHUMTA, UMISSETA na FEASSA kwa kushirikiana na OWM-TAMISEMI na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia; kusimamia uendeshaji wa Wakala wa Usimamizi wa Miundombinu ya Michezo Nchini (SIMA); kuratibu kikao kazi cha Maafisa Michezo nchini; kusimamia na kuratibu utoaji wa huduma za kinga na tiba kwa wanamichezo 800 watakaoshiriki kwenye michezo mbalimbali ya kitaifa na kimataifa; kuratibu Michezo ya Jumuiya ya Madola; kuandaa siku ya michezo duniani; kuandaa kongamano la wadau wa michezo; na kuratibu ushirikiano wa michezo na nchi mbalimbali.

### ii. BARAZA LA MICHEZO LA TAIFA (BMT)

**273.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/27 majukumu yatakayotekelezwa ni pamoja na kuendelea kuwezesha na kuzigharamia timu 20 za taifa kushiriki mashindano mbalimbali ya Kimataifa; kuendelea kutoa mafunzo ya utaalamu wa michezo na usimamizi kwa wataalamu 500 ili kupata wataalamu wa

michezo nchini; kuendelea kusajili Vyama/Mashirikisho na vilabu vya michezo vipatavyo 200; kuratibu matamasha matatu (3) ya Michezo ya Wanawake; kuendelea kuhamasisha utawala bora katika vyama na mashirikisho ya michezo 45; kuratibu chaguzi 8 za vyama na mashirikisho ya michezo kuidhinisha vibali 400 vya matukio mbalimbali ya michezo; kuendelea kutoa tuzo kwa wanamichezo bora kwa michezo yote inayochezwa Tanzania; kuendelea kutoa elimu kwa umma na wadau 350 kushiriki katika michezo kupitia vyombo vya habari; kukamilisha ujenzi wa kituo cha michezo na mazoezi mkoani Manyara; na kukamilisha marekebisho ya sheria ya Baraza la Michezo la Taifa pamoja na kuboresha muundo wa Utumishi wa Baraza la Michezo la Taifa.

**iii. CHUO CHA MAENDELEO YA MICHEZO MALYA**

**274.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/27, majukumu yaliyopangwa kutekelezwa na Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya ni kutoa mafuzo ya muda mrefu kwa wanachuo 500 na muda mfupi kwa wadau wa michezo 700; kuongeza programu sita (6) mpya za mafunzo ya muda mrefu; kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia; kujenga mahusiano na vyuo sita (6) vya michezo vya ndani vitatu (3) na nje nchi vitatu (3); kukamilisha muundo wa Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya ili kuwa Taasisi ya elimu ya Michezo; na kuanzisha kambi ya michezo ya vijana kwa ajili ya kumbukumbu ya kudumu ya mchango wa AFCON 2027.

**iv. UTAWALA NA USIMAMIZI WA RASILIMALI WATU**

**275.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/27, malengo yatakayotekelezwa ni kuhakikisha stahiki mbalimbali za Watumishi 261 na Viongozi wa Wizara zinatolewa; kutoa huduma ya usafiri kwa Viongozi na Watumishi 261 wa Wizara; kuandaa na kusimamia utekelezaji wa mpango wa mafunzo wa Wizara; kusimamia mpango wa utekelezaji wa majukumu ya watumishi wa Wizara; kuboresha mazingira ya utendaji kazi kwa kuwapatia vitendea kazi Watumishi 261 wa Wizara; na kuandaa na kutekeleza Mpango Mkakati wa rasilimaliwatu.

## e. MIRADI YA MAENDELEO

**276.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali katika mradi wa Upanuzi wa usikivu wa TBC imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo; kufunga mitambo kwenye vituo (20) vya urushaji wa matangazo ya FM ya redio ambapo ujenzi wa majengo unaendelea; ununuzi wa haki na uandaaji wa maudhui ya Michuano ya Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON 2027); kuendelea na mradi wa kuhamisha maudhui zilizopo katika maktaba za TBC kutoka mfumo wa analojia kwenda kidijiti; kununua vitendea kazi ikiwemo magari 20 kwa ajili ya shughuli za utangazaji, kompyuta mpakato 300, kamera 50, vinasa sauti 50, FLY AWAY - 2, Ndege nyuki (Drone) sita (6), Live-U 13 na quantum 15 kwa ajili ya kuimarisha chaneli za kimkakati za TBC (TBC 2, Bongo FM, TBC mtandaoni, Tanzania Safari Chaneli na Televisheni ya Kiingereza) na redio za Kanda (TBC Arusha na TBC Dodoma) pamoja na kuongeza uwezo wa urushaji wa Matangazo Mbashara; kuendelea na Ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya TBC eneo la Vikonje jijini Dodoma.

**277.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mradi wa Ufungaji wa Mitambo Mipya ya Kisasa ya Uchapaji Serikali imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo; ukamilishaji wa ujenzi wa jengo la kiwanda cha uchapaji; ukamilishaji wa ufungaji wa Mitambo Mipya ya Kisasa ya Uchapaji; kuunganisha mifumo ya uendeshaji wa shughuli za uchapaji *(Digital Convergence);* ufungaji mtambo maalumu wa uchapaji wa kisasa wa Vitambulisho awamu II; ufungaji mitambo ya urejelezaji (recycling) kutokana na uzalishaji wa kiwanda kipya cha uchapaji; na kuimarisha ofisi za biashara kikanda.

**278.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali katika mradi wa Habari kwa umma imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo; kukusanya, kuchakata na kusambaza taarifa (habari) kuhusu miradi ya maendeleo inayotekelezwa na Serikali; kuandaa na kurusha vipindi (picha jongefu) vinavyoitangaza Tanzania, kuratibu na kuandaa mikutano ya Wanahabari na Mawaziri, Wakuu wa Mikoa; Taasisi na Wakurugenzi wa Halmashauri na Msemaji Mkuu wa Serikali kutangaza utekelezaji wa miradi ya maendeleo; kurusha matangazo mbashara (Livestreaming) ya miradi na matukio ya Serikali; kugharamia vipindi vya televisheni vya

kutangaza utekelezaji wa shughuli za Serikali na kuchapisha nakala 10,000 za Jarida la NCHI YETU.

**279.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali katika mradi wa ujenzi wa Makao Makuu ya Ukombozi wa Afrika, Kongwa imepanga kumtafuta Mshauri Elekezi kwa ajili ya upembuzi yakinifu; kumtafuta Mkandarasi wa mradi; na kuanza ujenzi.

**280.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali kupitia mradi wa Kuimarisha BAKITA na Kukuza Kiswahili Kikanda na Kimataifa imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo; kufanya usanifishaji mkubwa wa pili wa lugha ya Kiswahili; kufanya Maadhimisho ya sita (6) ya Siku ya Kiswahili Duniani (MASIKIDU); kuendeleza kongoo ya Taifa; kuandaa atlasi ya lugha za Tanzania; ubidhaishaji kwa kufungua vituo vya kufundisha Kiswahili kwa wageni; kutengeneza mifumo miwili ya Kiswahili (mfumo wa mauzo ya machapisho pamoja na mfumo wa tafsiri ya nyaraka); na kufanya maboresho ya darasa la kufundishia Kiswahili kwa wageni.

**281.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali katika kuendelea kutekeleza mradi wa ukarabati wa Chuo cha Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSUBa), imepanga: ununuzi wa vifaa vya kisasa vya kufundishia na kujifunzia; kuanza ujenzi wa jengo moja (1) la utawala; kuendelea na ujenzi wa uzio kuzunguka hosteli za wanachuo; kuanza ujenzi wa jengo moja la hosteli za wanachuo; kufanya ufungaji na uboreshaji wa mifumo ya TEHAMA; kuboresha vifaa na miundombinu ya Tamasha la Kimataifa la Sanaa na Utamaduni Bagamoyo; kuendela na ujenzi wa jengo moja la kutunzia vifaa *(warehouse);* kuendelea na ukarabati wa vifaa na miundombinu ya Taasisi; na kununua jenereta moja.

**282.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali katika mradi wa ujenzi wa Ukumbi wa Wazi wa Sanaa imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo; kufanya upembuzi yakinifu wa mradi; kuandaa michoro; kufanya ununuzi kwa ajili ya kumpata mkandarasi wa ujenzi wa eneo la Ilala Sharif Shamba; kutafuta eneo na kufanya upembuzi yakinifu kwa ajili ya ujenzi wa Makumbusho ya Taifa ya Sanaa *(National Art Gallery)* jijini Dodoma; kuendelea na maandalizi ya Atlasi ya Vifaa vya Muziki wa Asili wa Tanzania; na kuendelea na mapitio

na maboresho ya Mfumo wa AMIS pamoja na kutengeneza BASATA mobile APP.

**283.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mradi wa ujenzi wa Jumba Changamani la Filamu Serikali imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo; kufanya tathmini ya awali ya mradi *(preliminary assessment)*, kufanya upembuzi yakinifu *(feasibility study)* ili kubaini uhalisia wa kiuchumi, kiufundi na kijamii wa mradi. Mradi huu ni sehemu ya miradi iliyoombewa mkopo wa masharti nafuu kutoka benki ya EXIM ya Korea Kusini ambapo taratibu zitakapokamilika utekelezaji wake utaanza na unatarajiwa kugharimu takribani bilioni 150.

**284.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali kupitia Mfuko wa Utamaduni na Sanaa Tanzania imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo; kuendelea kutoa mikopo yenye masharti nafuu kwa wadau wa utamaduni na sanaa ambapo mikopo itakayotolewa itakuwa na thamani ya shilingi 20,000,000,000 kwa wasanii 8,000 na ajira zinazotarajiwa kuzalishwa ni 105,000; kuwajengea uwezo wadau wa utamaduni na sanaa 15,000 katika masuala yanayohusiana na elimu ya fedha, uwekezaji, masoko, TEHAMA na hifadhi ya jamii; kuendelea kutafuta fedha kutoka kwa wadau wa maendeleo ili kuwa na Mfuko endelevu; na kufanya ufuatiliaji na tathmini kwa wanufaika 200 wa Mfuko.

**285.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali itaendelea na uboreshaji wa Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya ambapo imepanga: kuanza ujenzi wa maktaba, maabara ya michezo, ujenzi wa madarasa, ujenzi wa jengo la utawala na nyumba kumi (10) za watumishi; kuendelea na ukarabati wa nyumba kumi (10) za watumishi; kukarabati viwanja vya michezo saba (7) ambavyo ni Mpira wa Miguu viwili (2), Netiboli kimoja (1), Mpira wa Mikono viwili (2) na Mpira wa Kikapu viwili (2); kuimarisha mfumo wa mawasiliano; na kuendelea na ufungaji wa huduma za maji, umeme na ulinzi.

**286.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali katika mradi wa Akademia ya Michezo katika Chuo cha Michezo imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo: kukamilisha ujenzi wa miundombinu ya akademia ya

michezo ikiwemo viwanja vya mpira wa miguu vitatu (3), netiboli viwili (2), kikapu viwili (2), wavu viwili(2), mikono kimoja (1), tenisi viwili (2), jengo moja la madarasa lenye vyumba vya madarasa nane (8), bwalo moja(1), na hosteli moja (1), na kuanza ujenzi wa bwawa la kuongelea na jengo la utawala.

**287.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Michezo umepanga kutekeleza shughuli zifuatazo: kugharamia uendeshaji wa mashindano ya AFCON 2027 katika vituo vya Dar es Salaam, Arusha na Zanzibar ikiwemo kugharamia timu ya Taifa, Kamati za uratibu za Kitaifa, uratibu wa mashindano na wajibu wa Tanzania kimkataba; kuratibu Mashindano ya Urembo ya Dunia (Miss World) kama sehemu ya matukio ya AFCON 2027; kuwezesha ushiriki wa timu na wanamichezo wa Kitanzania katika mashindano ya kimataifa; kuanza ujenzi wa ofisi ya makao makuu ya Baraza jijini Dodoma; kuanza ujenzi wa kituo cha michezo katika Mkoa wa Manyara.

**288.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mradi wa Eneo Changamani la Michezo Dar es Salaam Serikali imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo; kukamilisha maboresho ya eneo la kuchezea (pitch); kuboresha eneo la jukwaa la wageni mashuhuri (VVIP); kutoa na kuweka milango mipya katika ofisi zote zilizopo uwanjani; kuweka mfumo wa TEHAMA wa kuingia uwanjani; na kuweka milango mipya katika vyoo vya watazamaji katika Uwanja wa Benjamin Mkapa. Aidha, Serikali itakamilisha ukarabati wa uwanja wa uhuru kwa kufungua viti 1,446 katika eneo la jukwaa la VIP; kuendelea na upanuzi wa vyumba vya kubadilishia nguo vya wachezaji; kufunga taa mpya za Uwanja (Pitch lights); na kukamilisha marekebisho ya eneo la kuchezea (pitch). Kazi nyingine ni kukamilisha ujenzi wa viwanja vya mazoezi kwa ajili ya AFCON 2027 vya Gymkhana 2, Farasi na *Leaders Club*.

**289.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mradi wa ujenzi wa uwanja wa Mpira wa Miguu wa Arusha Serikali imepanga: kukamilisha ujenzi wa uwanja ikiwemo ujenzi wa eneo la kuchezea (pitch); kuweka Mfumo wa kudhibiti halijoto *(Heating Ventlation and Air Conditioning - HVAC)*; na kukamilisha viwanja vya mazoezi vya AFCON 2027 katika maeneo ya Magereza ya Kisongo, Engutoto

na Mgambo.

**290. *Mheshimiwa Spika,*** katika mradi wa ujenzi wa uwanja wa mpira wa Dodoma Serikali imepanga: kuanza ujenzi wa jengo kuu la uwanja wa michezo, ujenzi wa miundombinu saidizi itakayojumuisha huduma za maji, umeme, barabara na mtandao wa mawasiliano. Serikali itajenga viwanja viwili (2) vya mazoezi pamoja na jengo la Kituo cha Habari *(Media Centre)* katika eneo la mradi.

**291. *Mheshimiwa Spika,*** katika mradi wa ujenzi wa Vituo vya Mazoezi na Kupumzikia Wananchi (*Recreational Centres*) Dodoma na Dar es Salaam Serikali imepanga: kukamilisha ujenzi wa viwanja viwili (2) vya mpira wa miguu, mpira wa mikono (1), mpira wa kikapu (1), netiboli (1) na wavu (1); kukamilisha ujenzi wa majengo ya utawala, kubadilishia nguo na eneo la burudani linalojumuisha jiko, kaunta ya vinywaji na vizimba vya kupumzikia; ujenzi wa uzio; ujenzi wa bwawa la kuogelea; ujenzi wa eneo la maegesho ya magari; na upandaji wa miti eneo la bustani.

**292. *Mheshimiwa Spika,*** katika mradi wa Ujenzi na Uimarishaji wa Miundombinu ya Michezo katika shule saba (7) maalumu za michezo kati ya 56 Serikali imepanga: kuanza ujenzi wa viwanja wa mpira wa miguu, riadha, kikapu, tenisi, mpira wa mikono, mpira wa wavu na netiboli katika shule za sekondari Nanguruwe (Mtwara), Kicheba (Tanga), Bisheshe (Kagera), New Kiomboi (Singida), Dkt. Damasi Ndumbaro (Ruvuma), Ikwiriri (Pwani) na Sekondari Dodoma (Dodoma).

**293. *Mheshimiwa Spika***, katika mradi wa ujenzi wa Arena ya Michezo Serikali imepanga: kuandaa mahitaji ya mradi; michoro; na kumtafuta Mshauri Elekezi na Mkandarasi wa Mradi. Eneo la ujenzi wa mradi limepatikana ambapo ekari 12 zimetengwa katika eneo la Tanganyika Packers Kawe jijini Dar es Salaam. Mradi huu ni sehemu ya miradi iliyoombewa mkopo wa masharti nafuu kutoka benki ya EXIM ya Korea Kusini ambapo taratibu zitakapokamilika utekelezaji wake utaanza.

**294. *Mheshimiwa Spika,*** Serikali katika mradi wa Maendeleo ya

Taasisi imepanga kutekeleza shughuli zilifuatazo; kufuatilia na kutathmini programu na miradi inayotekelezwa chini ya Wizara; kuratibu Ofisi ya Kanda ya Sekretarieti ya Baraza la Michezo la Umoja wa Afrika Kanda ya IV; kuratibu usimamizi wa vihatarishi katika miradi inayotekelezwa na Wizara; uendeshaji wa Wakala wa Usimamizi wa Miundombinu ya Michezo (SIMA); kuratibu shughuli za Bodi ya Ithibati ya Waandishi wa Habari; kuimarisha mifumo ya ukusanyaji wa Mapato ya Wizara na taasisi zake; na kuwajengea uwezo watumishi kuhusu uandishi wa maandiko ya miradi, maandalizi ya bajeti na masuala ya usimamizi wa vihatarishi.

## 6.0 SHUKURANI

**295.** ***Mheshimiwa Spika****,* kabla ya kuhitimisha hotuba yangu, nitumie nafasi hii kuwashukuru wadau mbalimbali ambao kwa namna moja au nyingine wamechangia kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo. Ushirikiano na misaada yao ya kifedha, kiufundi na kitaalamu imekuwa nguzo ya mafanikio yaliyopatikana katika mwaka 2025/26. Wadau hao ni pamoja na nchi wahisani, mashirika mbalimbali ya kimataifa, taasisi za fedha, vyombo vya habari, taasisi za hiari zisizokuwa za kiserikali na mashirika ya kidini.

**296.** ***Mheshimiwa Spika*****,** kwa upande wa wadau siyo rahisi kuwataja wote kwa majina, nitawataja wachache nikianza na wadau wa ndani, ambao ni Kampuni za Azam Media; Multichoice Tanzania; Airtel Tanzania; Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), Benki ya NMB; Benki ya CRDB; Benki ya NBC; Tanzania National Parks (TANAPA); Mamlaka ya Hifadhi ya Bonde la Ngorongoro (NCA); Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA); Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF); na Makumbusho ya Taifa. Aidha, wadau wengine ni pamoja na Shirika la Bima la Taifa (NIC); Wakala wa Serikali Mtandao (eGA); Kituo cha Mikutano cha Kimataifa Arusha (AICC); Shirika la Culture and Development East Africa (CDEA); Taasisi ya Global Opportunity Youth Network (GOYN); Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA); Kampuni ya Startimes; Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS); Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF); Vituo vya Redio vya Clouds Media

Group, EFM; Mega FM; Wasafi; Crown Fm; Dodoma FM; Chamwino Arts Center; Vyama na Mashirikisho ya Sanaa; Mingle and Audience Agency; Jambo Group of Companies (JAMUKAYA); Kilimarathon; Sports Pesa; na 361 Degrees Africa Limited.

**297.** ***Mheshimiwa Spika,*** natambua mchango mkubwa wa Balozi zote za Tanzania katika mataifa mbalimbali; Serikali ya Mji wa Busan nchini Korea ya Kusini; Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Korea (KOICA); Bagamoyo Friendship Society (Ujerumani); Musicians for a Better Life (Ujerumani); Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO); Wamiliki wa Kampuni za Emirates; Jamhuri ya Watu wa China; Umoja wa Ulaya; Organisation of African Carribean Pacific States (OACPS); na Kituo cha Sanaa na Utamaduni cha Alliance Francaise.

**298.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mara nyingine tena ninamshukuru kwa dhati kabisa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa maono yake, maelekezo na miongozo yake katika utekelezaji wa majukumu ya sekta za Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo. Wizara hii tunakiri kuwa tunadaiwa matokeo, Mheshimiwa Rais amemaliza kazi yake. Nimhakikishie kuwa katika kipindi alichoniamini kusimamia majukumu haya sitomwangusha. Watanzania tuendelee kumwombea kwa Mwenyezi Mungu amjalie afya njema ili aendee kutuongoza vema.

**299.** ***Mheshimiwa Spika***, pia ninamshukuru Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa maelekezo na ushauri katika kuimarisha usimamizi wa shughuli za Sekta za Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo. Vile vile, ninampongeza na kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa miongozo na maelekezo yake yaliyowezesha kuboresha utendaji wa Wizara na Serikali kwa ujumla.

**300.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninawashukuru Viongozi wa dini wanaoendelea kuliombea taifa letu usiku na mchana libaki moja,

lenye mshikamano na amani. Niendelee kuwaomba wasichoke, tumlilie Mungu wetu kwa imani zetu aendelee kulifunika na kulinda Taifa la Tanzania dhidi ya maadui wa ndani na nje.

**301.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninakishukuru Chama cha Mapinduzi chini ya Mwenyekiti wake Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kunipendekeza kuwa mgombea na hatimaye kuchaguliwa kwa kura nyingi na wananchi kuwa Mbunge wa jimbo la Arusha Mjini. Ninaahidi kulipa imani hii kubwa kwa utumishi wenye matokeo chanya kwa taifa langu.

**302.** Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine niwashukuru wananchi wa Jimbo la Arusha mjini kwa ushirikiano wanaonipa katika kutekeleza mipango ya maendeleo ya jimbo letu. Arusha tulichelewa sana kutekeleza shughuli za msingi za maendeleo na sasa wananchi wameamua kuibadili sura ya Arusha kwa kufanya kazi. Nawashukuru sana Waheshimiwa madiwani wote wa Arusha wakiongozwa na Mheshimiwa Maximilian Iraghe, Mstahiki Meya.

**303.** ***Mheshimiwa Spika***, kufika kwangu hapa leo hii, wapo watu ambao Mwenyezi Mungu kwa kusudi lake aliwatumia katika namna moja au nyingine katika safari yangu. Namkumbuka na kumshukuru Marehemu Samwel Sitta, aliyekuwa Spika wa Bunge la Tisa kwa maelezi yake kwangu kisiasa na kunijenga nilivyo; Marehemu Reginald Mengi kwa maelezi yake kifamilia na elimu katika wakati nilioihitaji zaidi; Marehemu Bernard Membe, aliyekuwa mwalimu wangu nguli wa siasa na mikakati ndani ya Chama cha Mapinduzi; Mheshimiwa Harson Mwakyembe aliyekuwa Mbunge na Waziri pamoja na Mheshimiwa Victor Mwambalaswa aliyekuwa Mbunge kwa mchango wao mkubwa katika maisha yangu ya siasa.

**304.** ***Mheshimiwa Spika***, kipekee kabisa niwashukuru Mheshimiwa Hamis M. Mwinjuma (Mb.), Naibu Waziri Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo; Ndugu Gerson Msigwa, Katibu Mkuu na Ndugu Methusela Ntonda, Naibu Katibu Mkuu. Aidha, nawashukuru Wenyeviti wa Bodi za Taasisi, Wakurugenzi na Wakuu wa Vitengo, Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara; na wafanyakazi wote wa Wizara na Taasisi kwa kuendelea kutekeleza majukumu yao kwa weledi mkubwa hatua

iliyopelekea mafanikio makubwa tunayoyashuhudia hivi leo.

**305.** ***Mheshimiwa Spika***, niishukuru familia yangu, Hususan mke wangu kipenzi Maria Felix Massenge na watoto wetu wapendwa Keagan, Kenzel na Kenzlin. Hawa wamekuwa faraja kubwa kwangu kwanza kwa maombi yao, uvumilivu ninapokuwa katika majukumu ya kitaifa na usimamizi imara wa wajibu wao katika familia. Haya yamenipa moyo na faraja kuendelea mbele bila kuchoka wala kukata tamaa katika kulitumikia Taifa. Mwenyezi Mungu awabariki sana.

**307.** ***Mheshimiwa Spika***, napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwako binafsi, Naibu Spika, Wenyeviti wa Bunge na Waheshimiwa Wabunge na wananchi wote kwa kunisikiliza. Aidha, hotuba hii inapatikana kwenye tovuti ya Wizara ambayo ni *www.michezo.go.tz.*

## 7.0 HITIMISHO

**308.** ***Mheshimiwa Spika***, mwaka 2026/27, Wizara inatarajia kukusanya jumla ya **shilingi 1,058,000,000**. Vyanzo vya mapato hayo ni Vitambulisho vya Waandishi wa Habari, machapisho ya picha, mabango na majarida, usajili wa magazeti, ada ya mwaka ya magazeti, viingilio katika uwanja wa Benjamin Mkapa na Uhuru, ada za upangishaji na matangazo katika eneo changamani la michezo Dar es Salaam pamoja na ada za wanachuo kutoka Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya. Aidha, kwa upande wa Taasisi 12 zilizo chini ya Wizara kiasi kinachotarajiwa kukusanywa ni **shilingi 40,898,692,000**.

**309.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kutekeleza majukumu ya Wizara katika mwaka 2026/27 naomba Bunge lako Tukufu liridhie na kuidhinisha Bajeti ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa mwaka 2026/27 yenye jumla ya **Shilingi 525,327,857,000.** Kati ya bajeti hiyo **Shilingi 39,071,597,000** ni kwa ajili ya Mishahara; **Shilingi 28,065,472,000** ni Matumizi Mengineyo; na Miradi ya Maendeleo ni **Shilingi 458,190,778,000.**

**310.** ***Mheshimiwa Spika***, naomba kutoa hoja

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, ninaafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Makonda, hoja imeungwa mkono.

Sasa Waheshimiwa Wabunge, kura zimepigwa matokeo tayari, ninamkaribisha msimamizi mkuu wa uchaguzi atupe taarifa inayokuja.

Katibu.

**MATOKEO YA KURA**

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa taarifa ya kukamilika kwa zoezi la Uchaguzi wa Bunge wa Bunge la Afrika Mashariki; na kwa kuzingatia matakwa ya fasili ya 14(a) na (b) ya Nyongeza ya Tatu ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Msimamizi wa Uchaguzi amepewa wajibu ufuatao: -

(1) Kulijulisha Bunge kuhusu matokeo ya uchaguzi kwa kutaja kura zilizopigwa kwa kila mgombea; na

(2) Kutangaza washindi.

Mheshimiwa Spika, fasili ya 14(b) inasema aliyeshinda ni yule aliyepata kura nyingi katika kura zilizopigwa.

Waheshimiwa Wabunge, sasa katika uchaguzi uliokamilika hivi punde, matokeo ya uchaguzi ni kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, idadi ya Wabunge Kikatiba ni 404, idadi ya Wabunge waliopo kwa sasa ni 401, idadi ya Wabunge waliopiga kura ni 293, idadi ya kura zilizoharibika, hakuna.

Mheshimiwa Spika, Kundi A, kundi la wanawake, mgombea alikuwa ni Ndugu Fatma Abdallah Kange; idadi ya kura za

"Ndiyo" ni 223, kura za "Hapana" ni 70. Kwa hiyo, ninaomba kutumia fursa hii kuwatangazia kuwa Ndugu Fatma Abdallah Kange amechaguliwa kuwa Mbunge wa Bunge la Afrika Mashariki kwa kupata kura 223 sawa na 76.1%.

Mheshimiwa Spika, Kundi D wagombea wa Tanzania Bara. Wagombea walikuwa Ndugu Cossato David Chumi na Ndugu Kambarage Masato Wasira. Tukianza na Ndugu Cossato David Chumi, idadi ya kura za "Ndiyo" ni 289, kura za "Hapana" ni nne. Hivyo, ninapenda kumtangaza Ndugu Cossato Chumi kama mshindi wa Kiti cha Ubunge wa Afrika Mashariki kwa idadi ya kura 98.6%. Ndugu Kambarage Masato Wasira; kura za "Ndiyo" ni 284, "Hapana" ni tisa. Hivyo, Ndugu Kambarage ameshinda nafasi ya Ubunge wa Afrika Mashariki kwa idadi ya 96.9%.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Ahsante sana Msimamizi wa Uchaguzi. Matokeo rasmi ndiyo hayo. Wabunge wetu waliochaguliwa kuingia kwenye Bunge la Afrika Mashariki ni Ndugu Fatma Abdllah Kange, Ndugu Cossato David Chumi na Ndugu Kambarage Masato Wasira. Hili sasa ndiyo tangazo rasmi na ni Taarifa Rasmi ya Bunge iingie kwenye *Hansard,* kwamba hawa sasa ndio wawakilishi wetu kwenye Bunge hili la Afrika Mashariki.

Waheshimiwa Wabunge, sasa kabla sijawaita wagombea kuja kushukuru, Waheshimiwa wetu hawa, maana mwanzo tulitawambulisha kama ndugu, sasa ni Waheshimiwa Wabunge wa Bunge letu kutuwakilisha kwenye Bunge la Afrika Mashariki.

Sasa ninamwita Ndugu Fatma Abdallah Kange, Ndugu Cossato David Chumi na Ndugu Kambarage Masato Wasira, wote kwa pamoja waingie ndani. *(Makofi)*

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge Wateule wa Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki (EALA) Waliingia Ukumbini)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Fatma Abdallah Kange karibu, na hongera sana; Mheshimiwa Chumi karibu, na hongera sana; na

Mheshimiwa Wasira karibu, na hongera sana. Sasa kama mna mawili matatu ya kutoa shukrani, karibuni. Kwa lugha ya Kifaransa. Karibu Bi. Fatma tumia hata Kiswahili.

**MHE. FATMA A. KANGE:** Mheshimiwa Spika, *Asalam Aleikum,*

**WAHESHIMIWA WABUNGE:** Waaleikum Salaam.

**MHE. FATMA A. KANGE:** Tumsifu Yesu Kristo.

**WAHESHIMIWA WABUNGE:** Milele Amina.

**MHE. FATMA A. KANGE:** Bwana Yesu asifiwe.

**WAHESHIMIWA WABUNGE:** Amen.

**MHE. FATMA A. KANGE:** Kazi na Utu.

**WAHESHIMIWA WABUNGE:** Tunasonga mbele.

**MHE. FATMA A. KANGE:** Mheshimiwa Spika, kwa unyenyekevu na kwa heshima kubwa ninalishukuru Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniteua kwenda kushiriki katika Bunge la *East Africa* kwa uwakilishi wa wanawake Tanzania Bara. *(MAkofi)*

Mheshimiwa Spika, ninafanya kazi na wajasiriamali. 60% ya maisha yangu nimeitumia kwa wajasiriamali wa Tanzania. Ninajua kilio chao. Nikitokea katika taasisi tanzu kabisa iliyonifundisha kuhusu *SMEs Development (SIDO),* ikanipa *spirit* ya kuwa na nguvu katika kuiangalia sekta ndogo ya wajasiriamali nchini kwa jicho tofauti kabisa. Wajasiriamali wa Tanzania wamepata mwakilishi ambaye anaongea lugha yao katika Bunge hili. Kwa hiyo, kwa heshima hiyo, kwa niaba ya wajasiriamali ninawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mengi tutayatekeleza. Kilio chetu kilikuwa ni taarifa. Mimi nitakuwa mshusha taarifa na wananijua kwa makongamano, yanakuja. Ninamshukuru Mama Samia kwa jicho

lake kubwa la kuweza kututafuta watu ambao tumefanya kazi kwenye masoko na wajasiriamali. Mimi ninalishukuru Bunge hili na ahsanteni sana. Kazi na iendelee.

**SPIKA:** Mheshimiwa Chumi.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Spika, na Waheshimiwa Wabunge ahsanteni sana. Ninawashukuru sana na Mwenyezi Mungu awabariki sana. Ninakishukuru sana chama changu chini ya Mwenyekiti wa Chama na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kunithibitisha kupitia vikao mbalimbali mpaka leo hii kufikia katika jengo lenu Tukufu. Ninawashukru sana. Ni imani kubwa ambayo Chama cha Mapinduzi, Serikali na Bunge hili mmeionesha kwangu. Kwa hiyo, nimepewa imani na mimi wajibu wangu ni kuwalipa imani.

Mheshimiwa Spika, kwa uzoefu wangu kama mtumishi wa Serikali na baadaye kiongozi wa kisiasa, nitatumia uzoefu huo kuendelea kuifanya Tanzania kuwa sauti imara ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, kuendelea kuifanya Jumuiya ya Afrika Mashariki iendelee kufahamika miongoni mwa Watanzania waweze kujua fursa mbalimbali ambazo zinapatikana kutokana na kwamba sisi Tanzania tuko sehemu ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, wakati wa uchaguzi huu nimejifunza ambavyo baadhi ya wananchi wetu hawako *aware* sana kuhusu jumuiya. Wengine hata walikuwa wananiuliza; “na sisi tutapiga kura?” Kwa hiyo, ni wajibu wangu pia kuwaelimisha wananchi wetu kujua, kuendelea kuifahamu jumuiya, lakini kikubwa fursa mbalimbali za kibiashara na kiuwekezaji ndani ya eneo letu la Jumuiya ya Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninarudia tena, Mwenyezi Mungu awabariki sana, mwendelee kutuongoza, kutusimamia ili tukatekeleze haya ambayo leo tumeyazungumza humu ndani kwa ufanisi kwa manufaa ya Taifa letu, ahsanteni sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Kambarage.

**MHE. KAMBARAGE M. WASIRA:** Mheshimiwa Spika, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania!

**WABUNGE FULANI:** Kazi Iendelee!

**MHE. KAMBARAGE M. WASIRA:** Mheshimiwa Spika na ndugu zangu Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kipekee ninaomba nichukue nafasi hii kuwashukuru sana. Tumefanya kampeni, tumejieleza, wengi mmenishauri namna ya kufanya. Nimeona kama Wabunge mmekuwa ndugu zangu na nimeamini kwamba ninaweza nikawa Mbunge bora wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, mimi nimekuwa ninafanya biashara, kwa hiyo, ninaelewa changamoto za *private sector head-on* kwamba hizi ni changamoto na ninajua kuna fursa ambazo zipo ndani ya Afrika Mashariki. Mimi ninaomba niende kuwa kama kinara, niwe mwakilishi mzuri. Ninavyokwenda huko kuwakilisha nchi, niwe sauti ya Tanzania Afrika Mashariki, na pia niwe ninarudi kwenu kupata *feedback* na kushirikiana kuona namna nzuri tunavyoweza kuijenga hii jumuiya.

Mheshimiwa Spika, Taifa la Tanzania ni Taifa la pili kwa uchumi katika Afrika Mashariki, *potentially* tunaweza tukaongoza. Namna pekee ni pale ambapo unaamua kufanya kazi na watu kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii, kwa kuomba kura na kupewa nafasi na ridhaa. Tuko pamoja, na ahsanteni sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa, ninawashukuru sana. Sasa mnaweza mkaenda kuendelea na shughuli nyingine. *Sergeant At Arms,* njoo uwatoe.

Subiri kwanza *Sergeant*.

Waheshimiwa Wabunge, kuna migogoro mingi sana ndani ya Jumuiya hii. Kuna nchi bado zinagombana wenyewe kwa wenyewe. Nendeni mkasimamie maslahi mapana ya umoja wa jumuiya. Nendeni mkasimamie shughuli za biashara. Umoja wetu huu una *GDP* ya bilioni 440, tukishikamana zaidi *GDP* itakwenda juu na wananchi wetu watanufaika. *(Makofi)*

Ninawaomba sana kusimamia amani, uchumi na biashara katika mipaka yetu, ninawaomba sana. Ahsanteni sana na Mungu awape kila la heri. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ninaomba kumtambulisha Mheshimiwa Jumaa Aweso, ndio Kaimu Kiongozi Mkuu wa Serikali katika siku ya leo. *(Makofi)*

Sasa, ninamwita Mheshimiwa Paresso aje kumalizia awamu hii inayofuata. *(Makofi)*

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Cecilia D. Paresso) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaendelea, sasa ninamwita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo. *(Makofi)*

**MHE. CORNEL L. MAGEMBE – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ELIMU, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninaomba kuleta taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa mwaka wa fedha 2025/2026 pamoja na Maoni na Ushauri wa Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa mwaka 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya kwanza, utangulizi. Kwa mujibu wa Kanuni ya 121(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge za mwaka 2025, ninaomba kuwasilisha taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Fungu 96 kwa mwaka wa fedha 2025/2026 pamoja na maoni ya Kamati

kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa inayowasilishwa ni matokeo ya shughuli za Kamati kwa kipindi cha tarehe 9 hadi 29 Machi, 2026 kutokana na uchambuzi wa makadirio ya mapato na matumizi ya sekta zilizo chini ya Kamati hii. Ninaomba taarifa yote ya Kamati iingie kwenye *Hansard* kama ilivyowasilishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu hii inabainisha mtiririko wa maudhui pamoja na kuzingatia masharti ya Kanuni ya 145 ya Kanuni za Bunge kuhusu muundo wa taarifa yoyote ya Kamati inayowasilishwa Bungeni. Kwa maelezo hayo, taarifa hii imegawanyika katika sehemu tatu ambapo sehemu ya kwanza inatoa maelezo ya jumla na kuonyesha msingi, mbinu na wigo wa kazi ya Kamati katika kufanyia kazi makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya pili, inabainisha matokeo ya uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa bajeti kwa Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2025/2026 na uchambuzi wa makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/2027. Sehemu ya tatu inabainisha maoni na ushauri wa Kamati na kumalizia kwa hitimisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu msingi, mbinu na wigo wa lazi ya Kamati. Msingi wa Kamati kuchambua taarifa ya utekelezaji na Makadirio ya Bajeti ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Fungu 96 ni masharti ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 5(7)(g) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge kikisomwa pamoja na Kifungu cha 7(1)(a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge kinaipa Kamati hii jukumu la kushughulikia Bajeti ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo. Aidha, Kanuni ya 120(2) ya Kanuni za Bunge ilitaka makadirio haya yajadiliwe na Kamati kabla ya kuwasilishwa Bungeni leo hii. Ninaomba kulihakikishia Bunge lako kuwa masharti haya yalizingatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapema asubuhi ya leo taarifa hii iliwekwa Mezani kwa mujibu wa Kanuni ya 121(5) ya Kanuni za Bunge na sasa ninawasilisha taarifa hii kwa mujibu wa Kanuni ya 121(9) ya Kanuni za Bunge kama ilivyoelezwa hapo awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mbinu na njia zilizotumika kubainisha njia iliyotumiwa na Kamati kuifanyia kazi hoja hii, ni masharti ya Kanuni ya 145(a)(2) ya Kanuni za Bunge. Lengo lake ni kuiwezesha taarifa hii kuwa rejea madhubuti inayosaidia mjadala wa Bunge kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hii. Kwa kufanya hivyo, Kamati inajenga msingi wa uadilifu uliozingatiwa ili kupata maoni na ushauri wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbinu mbalimbali za uchambuzi zilijumuisha kupokea maelezo ya Waziri, kuhoji mambo yaliyojitokeza na kupokea majibu ya mtoa hoja. Uchambuzi wa majibu na mawasilisho ulifanyika kwa kufanya ulinganisho kimaudhui na uhalisia. Haya yote yamefanikisha kupatikana kwa taarifa hii ambayo inabainisha maoni na ushauri wa kufanyia kazi katika hoja inayohusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama inavyofahamika, lengo la taarifa hii ni kulipatia Bunge tathmini ya kina kwa misingi ya ushahidi kuhusu makadirio ya matumizi na mapato yaliyowasilishwa na mtoa hoja. Lengo ni kuongoza mjadala unaozingatia uwajibikaji wa kibajeti na kuhakikisha kuwa rasilimali za umma zinatengwa kwa kuzingatia vipaumbele vya Taifa na Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025 inayoeleza, ninaomba kunukuu: "Utamaduni, sanaa na michezo ni sekta muhimu katika kuchochea ukuaji wa uchumi endelevu kwa kuzalisha fursa za ajira, kuchochea mauzo ya bidhaa za kitamaduni ndani na nje ya nchi, kuvutia uwekezaji, kukuza utalii na kuitangaza nchi Kimataifa," ukurasa wa 35. Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa msingi huo, taarifa hii inahusu utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2025/2026 na

makadirio ya bajeti kwa mwaka wa fedha 2026/2027. Maudhui yake yanahusu utekelezaji wa miradi ya maendeleo, ukusanyaji wa maduhuli, upatikanaji wa fedha na uzingatiaji wa ushauri uliotolewa na Kamati wakati Bunge lilipopitisha bajeti ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine la maudhui ya taarifa hii linagusa makadirio ya ukusanyaji wa maduhuli, ulinganisho wa vipaumbele na bajeti inayoombwa kwa mwaka wa fedha 2026/2027. Kimsingi, maudhui ya sehemu hii ya taarifa yanalisaidia Bunge kuona namna taarifa ilivyozingatia taratibu za Kibunge ikiwemo dhana ya uchunguzi wa Kibunge kuzingatia ushahidi *(evidence-based scrutiny)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya pili ni uchambuzi wa utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Sehemu hii imefafanua mambo makuu mawili. Kwanza ni uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2025/2026 na pili ni uchambuzi wa makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/2027. Katika sehemu ya kwanza, maelezo yametolewa kuhusu uzingatiaji wa ushauri wa Kamati, uchambuzi wa mwenendo wa ukusanyaji wa maduhuli, utekelezaji wa miradi ya maendeleo na utekelezaji wa majukumu na mipango ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ukusanyaji wa maduhuli, Kamati ilichambua makusanyo ya maduhuli kwa Wizara kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo ililenga kukusanya maduhuli ya jumla ya shilingi 41,331,192,000. Hadi kufikia mwezi Februari, 2026, Wizara hii ilikuwa imekusanya shilingi 14,656,583,088.86 sawa na 35.46% ya malengo yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya uchambuzi yameweka bayana kuwa kuna uwezekano mdogo sana wa kufikia lengo la kukusanya ambapo kunaweza kuathiri utekelezaji wa Bajeti Kuu ya Serikali kwa kuwa makusanyo hayo ni sehemu ya mapato yanayozingatiwa katika bajeti ya matumizi kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa miradi ya maendeleo, Kamati ilikagua miradi mitatu ambayo ni sehemu ya miradi iliyotengewa fedha kwa mwaka 2025/2026. Mwenendo wa utekelezaji wa miradi hiyo unaendana na upatikanaji wa fedha. Hata hivyo, utekelezaji wa mradi namba 6505; ujenzi na ununuzi wa mitambo ya uchapaji wa magazeti ya Serikali *(TSN)* hauendelei kwa kasi inayokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, sehemu hii imefafanua kuhusu uchambuzi wa makadirio ya bajeti ya matumizi ya kawaida na uzingatiaji wa maoni na ushauri wa Kamati. Maelezo yaliyotolewa yameonyesha kuwa sehemu ya ushauri uliotolewa unaendelea kufanyiwa kazi, uzoefu wa mwaka wa fedha 2025/2026 umezingatiwa katika bajeti ya mwaka wa fedha 2026/2027 na upatikanaji wa fedha zilizoidhinishwa na Bunge unaendana na majukumu yaliyopangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kutoa taarifa kwamba maelezo kamili kuhusu sehemu ya pili pamoja na viambatanisho vinapatikana katika taarifa hii kuanzia ukurasa wa 6 - 19.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa makadirio ya mapato na matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027, maelezo ya jumla. Sehemu hii inafafanua mambo makuu matatu. Kwanza ni makadirio ya ukusanyaji wa maduhuli; pili, ni makadirio ya mapato kwa mwaka wa fedha 2026/2027; na tatu, ni makadirio ya matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa maeneo haya ulifanyika kwa kuzingatia mipango na majukumu ya msingi ya Wizara hii na hotuba ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan aliyoitoa Bungeni tarehe 14 Novemba, 2025. Vile vile, uchambuzi ulizingatia mwelekeo wa jumla wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 ambapo imeeleza malengo mahususi katika sekta ya habari, sekta ya utamaduni na sekta ya sanaa na michezo kama ifuatavyo: -

(i) *"Kuwa na sekta ya habari inayofanya kazi kwa uhuru, uwazi na inayochochea uwajibikaji, uhuru wa kujieleza na*

*upatikanaji sawa wa taarifa kama mhimili wa demokrasia hai. Aidha, katika muktadha huu vyombo vya habari huru na vinavyojitegemea ni nyenzo muhimu katika kuhakikisha utawala bora na uwajibikaji; (ukurasa wa 16)*

(ii) *Kutumia urithi wake wa kiutamaduni wenye utajiri mkubwa, sekta ya habari, ubunifu na michezo inayokua kwa kasi, pamoja na Kiswahili kama nyenzo ya diplomasia na lugha yenye manufaa kiuchumi inayopanuka na kutambulika Kimataifa. Hata hivyo, utamaduni utaongeza ushawishi wa Tanzania kupitia nyanja mbalimbali kwa kukuza Kiswahili kama nyenzo ya kidiplomasia na lugha yenye manufaa ya kiuchumi katika ushirikiano wa uwili, kikanda na Kimataifa; (ukurasa wa 28) na*

(iii) *Tanzania inalenga kuwa kitovu wa utamaduni, sanaa, ubunifu na michezo Barani Afrika ifikapo mwaka 2050 ikiwa na sekta zinazostawi katika muziki, filamu, mitindo na burudani. Kwa kukuza vipaji na kuweka mazingira wezeshi Tanzania itafungua milango ya ubunifu na ujasiriamali kwa vijana." (ukurasa wa 31).* Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa makadirio ya mapato, Kamati ilipokea taarifa kuhusu lengo la ukusanyaji wa maduhuli kwa mwaka wa fedha 2026/2027. Uchambuzi ulijikita zaidi katika lengo lililokuwa limewekwa kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Aidha, katika mwaka wa fedha 2026/2027, Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Fungu 96, inakadiriwa kukusanya maduhuli jumla ya shilingi 41,956,692,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa makadirio haya yameongezeka kwa shilingi 625,500,000,000 sawa na asilimia moja nukta tano moja ikilinganishwa na makadirio ya makusanyo kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ina maoni kwamba pamoja na kuwepo kwa ongezeko la ukusanyaji wa maduhuli Wizara iongeze ubunifu katika kuibua vyanzo vipya vya mapato. Aidha, umakini zaidi unahitajika katika maeneo mengine. Hii inatokana

na ukweli kwamba vyanzo vya mapato vimebaki kuwa vile vile kila mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu makadirio ya matumizi ya maendeleo, Kamati ilichambua jumla ya shilingi 458,190,780,000 kwa ajili ya kugharimia miradi ya maendeleo inayopangwa kutekelezwa na Wizara kwa mwaka wa fedha 2026/2027. Uchambuzi huo umefanyika kwa ulinganisho na mwaka wa fedha wa 2025/2026. Matokeo ya uchambuzi yameonesha kuwa fedha za utekelezaji wa miradi ya maendeleo hazijaongezeka kwa mwaka 2026/2027 ikilinganishwa na mwaka 2025/2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kutenga fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kwa kiasi kikubwa fedha hizo zitasaidia kukamilisha ujenzi wa miundombinu bora ya michezo Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kutoa taarifa kwamba maelezo kamili kuhusu uchambuzi wa makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/2027 yanapatikana katika taarifa hii kuanzia ukurasa wa 20 hadi ukurasa wa 30.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya tatu ni maoni, ushauri na hitimisho. Kuhusu maoni, baada ya uchambuzi ninaomba kutoa maoni ya Kamati kwa kuzingatia matokeo ya uchambuzi. Maoni haya yanajenga msingi wa ushauri nitakaoutoa. Maoni hayo ni kama ifuatavyo: -

(i) Kutokupatikana kwa fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya mradi wa ujenzi na ununuzi wa mitambo ya kisasa ya uchapaji *TSN* ni jambo linaloweza kuathiri ukamilishaji wa mradi huu na pengine kusababisha hasara kwa Serikali;

(ii) Kuendelea kutenga bajeti na kutoa fedha kwa wakati kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa viwanja vitatu vya mazoezi katika Mkoa wa Dar es Salaam na viwanja vitano vilivyopo mkoani Arusha ni jambo linaloweza kufanikisha maandalizi madhubuti ya *AFCON* 2027. Aidha, pamoja na kutumika wakati wa mashindano ya mpira wa miguu kwa timu za Taifa za

wanaume Afrika, yaani *AFCON* 2027, vitasaidia kupunguza utegemezi wa viwanja vya Benjamin Mkapa.

(iii) Kupungua kwa wigo wa ukusanyaji wa mapato ya tozo kwa Bodi ya Filamu Tanzania kunakosababishwa na kupungua kwa idadi ya uandaaji wa filamu kutokana na mabadiliko ya soko la filamu pamoja na kukua kwa teknolojia, kunadhoofisha ukusanyaji wa maduhuli kwa taarifa hiyo;

(iv) Ufinyu wa bajeti kwa ajili ya ujenzi wa *arena* ya Sanaa na michezo unakwamisha uwezekano wa kuongeza fursa za ajira, kukuza uchumi, kuitangaza Tanzania Kimataifa, kukuza vipaji vya vijana, kuimarisha umoja na kuboresha afya;

(v) Kutokuwepo kwa mpango wa Wizara kukamilisha mchakato wa vazi la Taifa kunafifisha azma ya Serikali kuweka utambulisho wa Taifa kupitia mavazi;

(vi) Kutokamilika kwa ujenzi wa miundombinu ya barabara zinazoelekea ndani na nje ya Uwanja wa Arusha kutaathiri mwenendo mzima na ucheleweshaji wa maandalizi ya mashindano ya *AFCON 2027*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na maoni yalivyoelezwa hapo juu, Kamati ilizingatia ipasavyo maoni hayo na kuyatumia kama msingi wa ushauri ufuatao: -

(i) Serikali iendelee kutoa fedha za mradi wa ujenzi na ununuzi wa mitambo ya kisasa ya uchapaji *(TSN)* kwa kiwango kilichokusudiwa ili kukamilisha mradi huo kwa wakati, na kuipunguzia hasara zinazoweza kuzuilika;

(ii) Serikali ikamilishe ujenzi wa viwanja vitatu vya mazoezi katika Mkoa wa Dar es Salaam na viwanja vitano vilivyopo mkoani Arusha kwa wakati ili Tanzania iweze kukidhi vigezo vya kuandaa Mashindano ya Mpira wa Miguu kwa Timu za Taifa za Wanaume Afrika *(AFCON 2027);*

(iii) Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo iboreshe namna ya kuongeza wigo wa ukusanyaji wa mapato ya Bodi ya Filamu Tanzania kwa kuendana na maendeleo ya dunia kurahisisha mawasiliano, kuboresha ubunifu na kuongeza ufanisi katika uzalishaji na usambazaji wa taarifa na kazi za wasanii;

(iv) Serikali iongeze bajeti kwa ajili ya ujenzi wa *arena* ya Sanaa za Michezo kwa kuwa kukamilika kwa utekelezaji wa mradi huu kutaongeza fursa za ajira, kukuza uchumi, kuitangaza Tanzania Kimataifa, kukuza vipaji vya vijana, kuimarisha umoja na kuboresha afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri huu unaendana na mwelekeo alioutoa Mheshimiwa Rais wakati wa Hotuba yake alipozindua Bunge la Kumi na Tatu, ninanukuu: "Tunaendelea na maandalizi ya ujenzi wa *studio* ya kisasa ya filamu ili kupandisha thamani ya kazi za wacheza filamu wetu hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutajenga ukumbi wa kisasa wa maonesho ili kuwawezesha wasanii wetu kufanya matamasha ya Kimataifa na kuvutia wasanii wa nje wakubwa kufanya matamasha nchini. Tunataka sanaa, filamu na muziki zitengeneze ajira na kuchangia uchumi wa Taifa, ukurasa wa 22 – 23" mwisho wa kunukuu;

(v) Serikali ifufue na kukamilisha mchakato wa upatikanaji wa vazi la Taifa ili kuimarisha utambulisho wa Taifa, kukuza umoja wa Kitaifa, kukuza uchumi, ajira pamoja na kuhifadhi na kuendeleza utamaduni wa Mtanzania;

(vi) Serikali iongeze kasi ya ujenzi wa miundombinu ya barabara za ndani na nje ya Uwanja wa Arusha ili kukamilisha maandalizi ya mashindano ya *AFCON 2027*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, ninachukua fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi kwa ajili ya kuwasilisha Taarifa hii. Aidha, ninawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge, ya Elimu, Utamaduni na Michezo ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha kukamilisha kwa taarifa hii.

Ninaomba majina yao kama yalivyoorodheshwa katika Taarifa hii yaingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati, ninapenda kumshukuru Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo Mheshimiwa Paul Christian Makonda, Naibu Waziri Mheshimiwa Hamis Mohamed Mwinjuma, Katibu Mkuu wa Wizara hii Ndugu Gerson Patnas Msigwa na Naibu Katibu Mkuu Ndugu Methusela Steven Ntonda pamoja na Watendaji wengine wa Wizara kwa ushirikiano mkubwa waliyoipa Kamati katika kutekeleza majukumu yake na kwa usimamizi mzuri wa majukumu ya Wizara kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya kipekee, ninapenda kuwashukuru Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge wakiongozwa na Katibu wa Bunge, Ndugu Baraka Ildephonce Leonard kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake vyema katika wakati wote ilipokutana na hata wakati wa utayarishaji wa Taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo haya, sasa ninaliomba Bunge lako Tukufu lipokee Taarifa hii ili lijadili na likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja na ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**4 MEI, 2026**

## TAARIFA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

*(Kwa mujibu wa Kanuni ya 121(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2025)*

## SEHEMU YA KWANZA

### 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 121 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2025, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo (**Fungu 96**) kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027. Taarifa inayowasilishwa ni matokeo ya shughuli za Kamati kwa kipindi cha tarehe 09 hadi 27 Machi, 2026 kutokana na uchambuzi wa makadirio ya mapato na Matumizi ya Sekta zilizo chini ya Kamati hii.

### 1.2 Muundo wa Taarifa

**Mheshimiwa Spika**, sehemu hii inabainisha mtiririko wa maudhui pamoja na kuzingatia masharti ya Kanuni ya 145 ya Kanuni za Bunge, kuhusu muundo wa Taarifa yoyote ya Kamati inayowasilishwa Bungeni. Lengo ni kuliwezesha Bunge kufuatilia mtiririko wa taarifa na kuonesha taarifa inavyozingatia masharti ya Kanuni za Bunge kuhusu muundo wa Taarifa. Kwa maelezo hayo, Taarifa hii imegawanyika katika sehumu kuu tatu ambazo ni:

(i) Sehemu ya **Kwanza** inatoa maelezo ya jumla na kuonesha Msingi, Mbinu na Wigo wa Kazi ya Kamati katika kufanyia kazi makadirio ya mapato na Matumizi ya Wizara hii.

(ii) Sehemu ya **Pili** inabainisha matokeo ya uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Wizara hii kwa Mwaka wa fedha 2025/2026 na uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

(iii) Sehemu ya **Tatu** inabainisha Maoni na Ushauri wa Kamati na kumalizia kwa hitimisho.

## 1.3 Msingi, Mbinu na Wigo wa Kazi ya Kamati

### 1.3.1 Msingi

**Mheshimiwa Spika,** msingi wa Kamati kuchambua taarifa ya Utekelezaji na Makadirio ya Bajeti ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo **(Fungu 96)** ni masharti ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2025. Kifungu cha 5 (7) (g) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, kikisomwa kwa pamoja na Kifungu cha 7 (1) (a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, kinaipa Kamati hii jukumu la kushughulikia Bajeti ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo. Aidha, Kanuni ya 120 (2) ya Kanuni za Bunge ilitaka makadirio haya yajadiliwe na Kamati kabla ya kuwasilishwa Bungeni leo. Naomba kulihakikishia Bunge hili kuwa masharti hayo yalitimizwa.

**Mheshimiwa Spika**, mapema asubuhi ya leo, taarifa hii iliwekwa mezani kwa mujibu wa Kanuni ya 121 (5) ya Kanuni za Bunge. Na sasa, nawasilisha taarifa hii kwa mujibu wa Kanuni ya 121 (9) ya Kanuni za Bunge kama nilivyoeleza hapo awali.

### 1.3.2 Mbinu na Njia Zilizotumika

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebainisha njia zilizotumika kufanyia kazi hoja hii kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 145 (a) (iii) ya Kanuni za Bunge. Lengo ni kuiwezesha Taarifa hii kuwa rejea madhubuti, inayosaidia mjadala wa Bunge kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara. Kwa kufanya hivyo, Kamati inajenga msingi wa uadilifu uliozingatiwa ili kupata maoni na ushauri wake.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilitumia mbinu mbalimbali za uchambuzi zikiwemo kupokea maelezo ya Waziri, kuhoji mambo yaliyojitokeza na kupokea majibu ya mtoa hoja. Uchambuzi wa majibu na mawasilisho ulifanyika kwa kufanya ulinganisho kimaudhui na uhalisia. Haya yote yamefanikisha kupatikana kwa taarifa hii ambayo inabainisha maoni na ushauri wa kufanyiwa kazi katika hoja hii inayohusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo.

### 1.3.3 Wigo wa Kazi

**Mheshimiwa Spika,** madhumuni ya Taarifa hii ni kulipatia Bunge tathmini ya Kibunge kwa misingi ya ushahidi kuhusu makadirio ya matumizi na mapato yaliyowasilishwa na Mtoa hoja. Lengo ni kuongoza mjadala unaozingatia uwajibikaji wa kibajeti na kuhakikisha kuwa rasilimali za umma zinatengwa kwa kuzingatia vipaumbele vya kitaifa na Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025 inayoeleza; **nanukuu:**

*"Utamaduni, sanaa na michezo ni sekta muhimu katika kuchochea ukuaji wa uchumi endelevu kwa kuzalisha fursa za ajira, kuchochea mauzo ya bidhaa za kitamaduni ndani na nje ya nchi, kuvutia uwekezaji, kukuza utalii na kuitangaza nchi kimataifa."* (uk. 35). **Mwisho wa kunukuu.**

**Mheshimiwa Spika**, kimsingi Taarifa hii inagusa utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2025/2026 na Makadirio ya bajeti kwa mwaka wa fedha 2026/2027. Maudhui yake yanahusu utekelezaji wa miradi ya maendeleo, ukusanyaji wa maduhuli, upatikanaji wa fedha na uzingatiaji wa ushauri uliotolewa na Kamati wakati Bunge lilipopitisha bajeti ya Wizara hii. Eneo lingine la maudhui ya Taarifa hii linagusa makadirio ya ukusanyaji wa maduhuli, ulinganisho wa vipaumbele na bajeti inayoombwa kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

## 1.4 Majumuisho ya Sehemu

**Mheshimiwa Spika,** kwa ujumla sehemu ya Kwanza inaonesha ombi la kuiwasilisha rasmi Taarifa hii katika majadiliano ya Bunge,

muundo unavyozingatia masharti ya Kanuni ya 145 ya Kanuni za Bunge na kubainisha msingi wa Kamati kufanyia kazi makadirio ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo. Maelezo haya yamewekwa kwa muktadha na msingi wa maudhui ya Taarifa. Kwa kufanya hivyo, sehemu hiyo inalisaidia Bunge kuona nmna taarifa ilivyozingatia taratibu za Kibunge ikiwemo dhana ya uchunguzi wa Kibunge kuzingatia Ushahidi *(Evidence based scrutiny)*.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 UCHAMBUZI WA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

### 2.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, sehemu ya pili ya Taarifa hii inatoa maelezo kamili kuhusu mambo yote yaliyochambuliwa na Kamati. Sehemu hii itakuwa na maelezo kuhusu mambo makuu mawili. Mambo hayo ni: -

(i) Uchambuzi wa Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026; na

(ii) Uchambuzi wa makadirio ya mapato na matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi huo ulifanyika kwa ulinganisho kama ilivyoelekeza Kanuni ya 120 (1) na (2) za Kanuni za Bunge. Ni uchambuzi unaojenga msingi wa maoni na ushauri wa Kamati.

### 2.2 Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji

**Mheshimiwa Spika**, ili kukidhi masharti ya Kanuni za Bunge, tarehe 26 Machi, 2026, Kamati ilipokea taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2025/2026 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/2027. Lengo lilikuwa ni kuliwezesha Bunge kulinganisha dhamira yake wakati wa kupitisha bajeti na matokeo. Aidha, uchambuzi wa makadirio

ya bajeti kwa mwaka wa fedha 2026/2027 ulilenga kuliwezesha Bunge kupitisha bajeti ya Wizara hii kwa namna yenye mchango unaolingana na ahadi waliyopewa wananchi kupitia Ilani ya CCM iliyorejewa.

**Mheshimiwa Spika**, kwa madhumuni hayo, sehemu hii inatoa matokeo ya uchambuzi wa mambo matano ambayo ni:-

(i) Uzingatiaji wa Ushauri wa Kamati;
(ii) Utekelezaji wa Kazi zilizopangwa;
(iii) Ukusanyaji wa Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026;
(iv) Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo; na
(v) Mwenendo wa Upatikanaji wa Fedha za Bajeti.

### 2.2.1 Uzingatiaji wa Ushauri wa Kamati

**Mheshimiwa Spika**, sehemu hii ya Taarifa inatoa mrejesho na fursa kwa Bunge na Umma kufahamu kiwango cha Serikali kuzingatia ushauri uliotolewa Bungeni kuhusu matumizi ya rasilimali za umma. Kwa kufanya hivyo, taarifa hii inapima dhamira ya Serikali katika kutekeleza vipaumbele vilivyoainishwa kwa ufanisi uliokusudiwa na Bunge kukidhi matarajio ya wananchi.

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa uchambuzi wa Bajeti ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Kamati ilitoa maoni na ushauri kuhusu mambo mbalimbali kwa lengo la kuboresha utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii. Naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba kwa sehemu kubwa ushauri wa Kamati ulizingatiwa na sehemu nyingine, utekelezaji wake ni endelevu kama inavyobainishwa katika **Kiambatisho Na. 2.**

**Mheshimiwa Spika,** mfano wa ushauri uliozingatiwa unahusu jukumu la Serikali kuendelea kutenga bajeti kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa Uwanja wa Arusha. Ushauri huu ulilenga kufanikisha na kukamilisha utekelezaji wa mradi huu kama ilivyokusudiwa na pia kuongeza chachu ya utalii na kuwa kituo muhimu katika Mashindano ya Mataifa ya Afrika (AFCON).

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa iliyotolewa kwenye Kamati inaonesha kwamba katika mwaka wa fedha 2024/2025, Serikali ilitenga na kutoa kiasi cha **shilingi 153,161,763,553.50** kwa ajili ya ujenzi wa uwanja wa Arusha. Ili kuhakikisha inakamilisha maandalizi ya kuwa mwenyeji wa mashindano ya AFCON 2027, kwa kushirikiana na nchi za Kenya na Uganda, kwa mwaka wa fedha 2025/2026, imetenga jumla ya **shilingi 162,976,682,000.00** kwa ajili ya mradi wa ujenzi wa uwanja wa Arusha. Hadi Februari 2026, Serikali imetoa jumla ya **shilingi 106,742,579,088** sawa na **asilimia 65.5** ya bajeti iliyotengwa. Aidha, hadi Februari 2026 ujenzi wa uwanja umefikia **asilimia 75** na jumla ya **shilingi 256,208,264,022.55** zimetolewa, sawa na **asilimia 73.8** ya gharama ya mradi. Hata hivyo, katika mwaka wa fedha 2026/2027 Wizara imeendelea kutenga bajeti kwa ajili ya Ujenzi wa eneo Changamani la Michezo Arusha kiasi cha **shilingi 125,653,212,000.**

**Mheshimiwa Spika,** Vilevile ushauri wa kuandaa mikakati ya kuboresha viwanja vingine vyenye hadhi ya kuendesha mashindano ya kitaifa na kimataifa ili kupunguza mfululizo wa matumizi ya Uwanja wa Benjamin Mkapa ulizingatiwa ambapo serikali imeendelea na ukarabati na ujenzi wa viwanja vipya vya michezo.

**Mheshimiwa Spika,** mfano wa viwanja hivyo vilivyokarabatiwa ili kukidhi vigezo ni uwanja wa Uhuru, Meja Jenerali Isamuhyo, Gymkana na uwanja wa shule ya Sheria (Law school). Vile vile, Serikali imeanza ujenzi wa viwanja vitatu (3) vya Farasi, Gymkana Annex na Leaders Club. Katika hatua nyingine, Serikali inajenga viwanja vitano (5) vya mazoezi jijini Arusha katika eneo la Magereza, Kisongo, Uwanja wa Mgambo, eneo la Police Field Force na Engutoto. Viwanja hivi vitatumika wakati wa Mashindano ya Mpira wa Miguu kwa timu za Taifa za Wanaume Afrika (AFCON 2027).

**Mheshimiwa Spika**, upo pia ushauri wa Kamati ambao uzingatiaji wake haujakamilika. Ushauri huo ulihusu yafuatayo:-

(a) Kuongeza wigo wa ukusanyaji wa Mapato ya Tozo za Hakimiliki kwa kuongeza vifaa vinavyotozwa Tozo hii hasa vya Kidijitali;

(b) Fedha kwa ajili ya ujenzi na ununuzi wa mitambo ya uchapaji kutolewa kabla ya tarehe 01 Julai, 2025; na

(c) Ujenzi wa Jengo la Kiwanda cha Uchapishaji ili kupunguza gharama za uendeshaji na utunzaji wa mitambo katika maghala ya Taasisi nyingine.

**Mheshimiwa Spika,** ushauri wa Kamati ulijengwa kwa misingi halisi inayostahili kupewa uzito wake. Kamati ina maoni kwamba, kutokuzingatia ushauri wake ni jambo linaloweza kutatiza azma ya kutimiza matarajio ya wananchi. Aidha, mtiririko wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ulichangia kutozingatiwa ipasavyo kwa baadhi ya ushauri uliotolewa.

### 2.2.2 Ukusanyaji wa Maduhuli

**Mheshimiwa Spika**, lengo la uchambuzi wa taarifa za makusanyo ya maduhuli kwa Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo ni kuliwezesha Bunge kubaini iwapo lengo la makusanyo lililoidhinishwa na Bunge limefikiwa. Hata hivyo, uchambuzi huu unaliweka Bunge katika nafasi ya kutoa uzoefu unaopatikana kwa mwaka wa fedha 2025/2026 na kubaini uhalisia unavyostahili kwa mwaka wa fedha 2026/2027. Kamati ilifanya uchambuzi kwa kuzingatia masuala yafuatayo:-

(i) Kiasi kilichokusanywa ikilinganishwa na lengo la makusanyo; na

(ii) Ulinganisho wa kipindi kama hicho kwa mwaka wa fedha 2025/2026

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2025/2026, Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo ililenga kukusanya maduhuli ya jumla ya **Shilingi 41,331,192,000.** Hadi kufikia Mwezi Februari 2026, Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo

ilikuwa imekusanya **Shilingi 14,656,583,088.86** sawa na asilimia **35.46** ya malengo yaliyokusudiwa. Mchanganuo wa fedha hizo ni kama inavyoonekana katika Jedwali Na 1.

**Jedwali Na 1: Ukusanyaji wa Maduhuli kwa Mwaka 2025/2026 - Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo**

| UKUSANYAJI WA MADUHULI FUNGU 96 KWA MWAKA 2025/2026 | | | |
|---|---|---|---|
| **CHANZO** | **MAKADIRIO** | **MAKUSANYO** | **ASILIMIA** |
| Idara na Vitengo Wizarani | 1,036,000,000 | 661,373,423 | **63.8** |
| Taasisi | | 13,995,209,665.86 | **34.7** |
| **JUMLA** | 40,295,192,000<br>**41,331,192,000** | **14,656,583,088.86** | **35.46** |

**Chanzo:** *Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kuhusu Mwelekeo wa Bajeti kwa Mwaka 2025/2026*

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa data kwenye jedwali hilo, unabainika katika chati duara *(pie chart)* ili kurahisisha ulinganisho uliokusudiwa kwenye Kanuni ya 120 (2) ya Kanuni za Bunge. Picha halisi ya uchambuzi huo inaonekana katika Chati Na. 1

**Chati Na. 1: Ukusanyaji wa Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 - Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo**




**Chanzo:** *Usanifu wa Kamati kutoka kwenye Jedwali Na, 1 la Taarifa hii*

**Mheshimiwa Spika,** taswira iliyojitokeza inaonesha kwamba: -

(i) Mwenendo wa Jumla wa makusanyo hadi kufikia Mwezi Februari, 2026 ni **asilimia 35.46** ambayo ni pungufu ya nusu ilihali kipindi cha utekelezaji kimevuka nusu mwaka;

(ii) Uwiano wa makusanyo kwa lengo umekuwa hafifu zaidi katika Taasisi zilizo chini ya Wizara kuliko Idara na Vitengo vilivyoko Wizarani. Wakati Idara na Vitengo vya Wizara vimefikia **asilimia 63.8** ya lengo, Taasisi zimefikia **asilimia 34.7** ya lengo.

(iii) Kwa ujumla mwenendo wa makusanyo kwa baadhi ya taasisi ni hafifu zaidi. Mathalani Bodi ya Filamu Tanzania imekusanya **asilimia 27** ya lengo la makusanyo yake.

**Mheshimiwa Spika,** kwa ujumla Kamati imebaini kwamba uwiano wa lengo la makusanyo kati ya Wizara na taasisi zake ulitofautiana na uwiano wa makusanyo halisi kati ya Wizara na taasisi. Ufafanuzi umeonesha kwamba, wakati wa makadirio ya Wizara ilitarajiwa kukusanya **asilimia 2.50** ya lengo la makusanyo ya Wizara na taasisi zake. Katika utekelezaji Wizara imekusanya **asilimia 4.51** ya jumla ya makusanyo ya Wizara na taasisi zake.

**Mheshimiwa Spika,** kwa uwiano huo, lengo la makusanyo kwenye taasisi za Wizara linahitaji kuangaliwa vizuri. Aidha, utaratibu na utekelezaji wa makusanyo kwa ujumla unahitaji kufanyiwa tathmini ipasavyo.

**Mheshimiwa Spika**, matokeo ya uchambuzi huu yameweka bayana kuwa kuna uwezekano mdogo sana wa kufikia lengo la makusanyo ambapo kunaweza kuathiri utekelezaji wa Bajeti Kuu ya Serikali kwa kuwa makusanyo hayo ni sehemu ya mapato yaliyozingatiwa katika bajeti ya matumizi kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

**Mheshimiwa Spika,** mwenendo kwa ujumla wa makusanyo katika baadhi ya taasisi zilizo chini ya Wizara hii hauoneshi uwezekano

wa kukamilika kwa lengo. Mathalani, makusanyo kwa Bodi ya Filamu Tanzania hadi kufikia mwezi Februari, 2026 ni **asilimia 27** tu. Hali hii ni ishara kuwa makusanyo ya jumla ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2025/2026 yanaweza yasifikie malengo ifikapo tarehe 30 Juni, 2026.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilihoji sababu za makusanyo duni ya maduhuli kwa baadhi ya taasisi na kuchangia pengo la ufikiaji wa lengo. Kamati ilijulishwa kwamba, kupungua kwa idadi ya waandaaji wa filamu kutokana na mabadiliko ya soko la filamu pamoja na kukua kwa teknolojia kumesababisha waandaaji wengi kuandaa na kurusha filamu kupitia program tumizi (App) kwa kutumia vifaa rahisi zikiwemo simu janja kunasababisha wengi kutokufuata taratibu zilizowekwa na Serikali na hivyo kumeikosesha Bodi ya Filamu Tanzania mapato yaliyolengwa.

**Mheshimiwa Spika**, sababu nyingine ni Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA) kuondolewa kwa baadhi ya vyanzo vya mapato ambavyo vilikuwa na mchango mkubwa kwenye makusanyo kama vile Ada za kumbi za starehe na burudani pamoja na Ada za matukio ya kazi za Sanaa ambazo zilikuwa zimekadiriwa kukusanywa shilingi **755,000,000**.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na sababu hizo ni ukweli usiopingika kwamba mabadiliko ya Teknolojia ni jambo lisiloepukika katika sekta ya habari, sekta ya sanaa, sekta ya michezo na sekta ya utamaduni jambo linalohitaji kuendana na maendeleo ya dunia, kurahisisha mawasiliano, kuboresha ubunifu na kuongeza ufanisi katika uzalishaji na usambazaji wa taarifa na kazi za kisanii.

### 2.2.3 Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 120(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilifanya ziara katika Mikoa ya Arusha na Dar es Salaam. Kamati ilikagua miradi mitatu ambayo ni sehemu ya miradi iliyotengewa fedha kwa mwaka 2025/2026. Naomba kubainisha kuwa Kamati ilipokea taarifa ya upatikanaji wa fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo na

kuchambua utekelezaji wa miradi hiyo. Ufafanuzi zaidi kuhusu Miradi unaambatishwa pamoja na Taarifa hii **(Kiambatisho Na1).**

**Mheshimiwa Spika,** matokeo ya jumla ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo yanaonesha kama ifuatavyo:

(i) Kiasi cha fedha kilichopokelewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya Maendeleo ni **asilimia 63.2** ya bajeti yote.

(ii) Kwa ujumla, upatikanaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mitatu iliyokaguliwa umefikia wastani wa **asilimia 72.89**

(iii) Mwenendo wa Utekelezaji wa miradi hiyo unaendana na upatikanaji wa fedha. Hata hivyo, Utekelezaji wa **Mradi Na. 6505**, Ujenzi na Ununuzi wa Mitambo ya Uchapaji wa Magazeti ya Serikali hauendelei kwa kasi iliyokusudiwa.

### 2.2.4 Utekelezaji wa Kazi Zilizopangwa

**Mheshimiwa Spika,** tarehe 26 Machi, 2026 Kamati ilipokea na kuchambua Taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026. Wakati wa uchambuzi Kamati ilizingatia vipaumbele vya Wizara na kufanya tathmini ya hali halisi ya utekelezaji wa kazi zilizopangwa ikilinganishwa na Bajeti iliyopitishwa na Bunge. Uchambuzi ulionesha kuwa mipango na majukumu yaliendana na upatikanaji wa fedha kwa mwaka unaohusika.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi ulionesha kuwa majukumu na mipango ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2025/2026 yapo katika hatua nzuri za utekelezaji. Kwa mfano, Wizara ilikuwa imepanga kuratibu maandalizi ya Michuano ya CHAN 2024 na AFCON 2027. Serikali ilieleza kwamba katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Februari, 2026 Wizara imeratibu maandalizi ya mashindano ya Mpira wa Miguu Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN 2024) kwa mafanikio makubwa. Mashindano haya yalifanyika kuanzia 02 hadi 30 Agosti, 2025 kwa kushirikiana na nchi za Kenya na Uganda.

**Mheshimiwa Spika,** Timu ya Taifa ya Tanzania (Taifa Stars) ilishiriki katika mashindano haya kwa mara ya tatu na kupata mafanikio makubwa ambapo ilifika hatua ya robo fainali. Tanzania ilipokea tuzo ya heshima kutoka Shirikisho la Mpira wa Miguu Barani Afrika (CAF) kwa kufanya vizuri katika maandalizi na uratibu wa mashindano hayo.

**Mheshimiwa Spika,** vilevile Wizara imeendelea na maandalizi ya Mashindano ya Mpira wa Miguu kwa timu za Taifa za Wanaume Afrika (AFCON 2027) kwa kutekeleza majukumu mbalimbali hususan ujenzi na ukarabati wa miundombinu itakayotumika katika mashindano hayo ikiwemo ukarabati wa Uwanja wa Benjamin Mkapa ambao umefikia asilimia **95**, ukarabati wa Uwanja wa Uhuru ambao umefikia asilimia **70**, na viwanja vya mazoezi vya Uwanja wa Gymkhana, Meja Jenerali Isamuhyo na Shule ya Sheria vimekamilika.

**Mheshimiwa Spika,** ujenzi wa viwanja vingine vya mazoezi kwa ajili ya AFCON 2027 ambavyo ni Farasi, Leaders Club na Gymkhana 2 vya Jijini Dar es Salaam vipo katika hatua za awali za ujenzi ambapo mkandarasi amekabidhiwa eneo. Vilevile, katika Jiji la Arusha, Wizara inaendelea kusimamia ujenzi wa Uwanja mkubwa wa michezo utakaokuwa na uwezo wa kubeba mashabiki 32,000 ambao umefikia asilimia **75.** Kwa upande wa viwanja vya mazoezi Wizara imeainisha maeneo ya Mgambo, Magereza, Kisongo na Engutoto.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilijulishwa zaidi kuhusu mikakati ya kupeleka Kiswahili Kimataifa kwa kufungua vituo vya Kufundisha Kiswahili kwa wageni katika nchi 10. Serikali ilieleza kwamba katika kuendeleza na kueneza Kiswahili Kimataifa jumla ya vituo vitatu (3) katika nchi mbili (2) vilifunguliwa kwa kushirikiana na Ubalozi wa Tanzania nchini Afrika Kusini ambapo imesajili vituo viwili (2) vya kufundishia Kiswahili kwa wageni katika Jiji la Johannesburg. Vituo hivyo ni Kiswahili Centre of Excellence South Africa (KCESA) na Tanzania Kiswahili Cultural Centre ambavyo vinamilikiwa na Watanzania waishio Afrika Kusini. Aidha, kituo kimoja cha Imani Languages Academy kinachomilikiwa na Mtanzania kimesajiliwa nchini Japan.

### 2.2.5 Mwenendo wa Upatikanaji wa Fedha za Bajeti

**Mheshimiwa Spika,** ufanisi wa utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo unategemea mwenendo wa upatikanaji wa fedha kutoka Hazina kama ilivyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu. Kwa kuzingatia hilo, Kamati ilipokea na kuchambua mwenendo wa upatikanaji wa fedha kwa **Fungu 96** kama ilivyoelezwa na mtoa hoja. Kwa mwaka wa Fedha 2025/2026, Wizara hii iliidhinishiwa jumla ya **shilingi 61,469,285,000** sawa na **asilimia 11.82** kwa ajili ya matumizi ya Kawaida na jumla ya **shilingi 458,190,778,000** sawa na **asilimia 88.17** kwa ajili ya matumizi ya Miradi ya Maendeleo. Uchambuzi ulibainisha yafuatayo:

(i) Kiasi cha fedha kilichoidhinishwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida ya Wizara hii asilimia **11.82** ya Bajeti yote ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2025/2026 ililenga matumizi ya kawaida, lakini fedha iliyopatikana kwa ajili ya matumizi ya kawaida ni asilimia **11.70**. Uwiano huo hautofautiani na mtazamo uliokuwepo wakati wa kupitisha bajeti.

(ii) Kiasi cha bajeti ya matumizi ya kawaida kilichotengwa kwa matumizi mengineyo ni asilimia **45.6,** lakini kiasi cha fedha za matumizi ya kawaida kilichopatikana kwa ajili ya matumizi mengineyo ni asilimia **43.14** ya bajeti ya matumizi ya kawaida. Uwiano huu hautofautiani sana.

(iii) Kati ya fedha hizo **Shilingi 28,065,472,000** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo, **Shilingi 33,403,813,000** ni kwa ajili ya mishahara na **Shilingi 458,190,778,000** kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** Mwenendo huo wa upatikanaji wa fedha unaonekana katika **Jedwali Na.2**

**Jedwali Na. 2: Mwenendo wa Upatikanaji wa Fedha za Matumizi ya Kawaida na Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026**

| UPATIKANAJI WA FEDHA FUNGU 96 MWAKA 2025/2026 | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **MATUMIZI** | | **KILICHOIDHINISHWA** | **KILICHOPOKELEWA** | **ASILIMIA** |
| **KAWAIDA** | MISHAHARA | 33,403,813,000 | 21,852,172,806.12 | **65.4** |
| | OC | 28,065,472,000 | 16,583,499,387.28 | **59.1** |
| **MAENDELEO** | NDANI | 458,190,778,000 | 289,878,498,984.34 | **63.3** |
| **JUMLA BAJETI** | | **519,660,073,000** | **328,314,171,177.74** | **63.2** |

**Chanzo:** *Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kuhusu Mwelekeo wa Bajeti kwa Mwaka 2025/2026*

**Chati Na. 2: Mwenendo wa Upatikanaji wa Fedha za matumizi ya Kawaida na Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026**




**Chanzo:** *Usanifu wa Kamati kutoka kwenye Taarifa za Randama ya Wizara kwa Mwaka 2025/2026*

2.3 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027

**Mheshimiwa Spika**, ili kuzingatia masharti ya Kanuni ya 120 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilichambua na kujadili Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa kuzingatia kazi zilizopangwa kutekelezwa kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

Wakati wa uchambuzi, Kamati ilijielekeza katika maeneo yafuatayo:-

(i) Makadirio ya ukusanyaji wa Maduhuli;
(ii) Makadirio ya Mapato kwa mwaka wa fedha 2026/2027; na
(iii) Makadirio ya Matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa maeneo hayo ulifanyika kwa kuzingatia mipango na majukumu ya msingi ya Wizara hii na hotuba ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan aliyoitoa Bungeni tarehe 14 Novemba, 2025. Vilevile, uchambuzi ulizingatia mwelekeo wa Jumla wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050, ambapo imeeleza malengo mahususi katika Sekta ya Habari, Sekta ya Utamaduni na Sekta ya Sanaa na Michezo kama ifuatavyo:

(i) *"Kuwa na sekta ya habari inayofanya kazi kwa uhuru, uwazi na inayochochea uwajibikaji, uhuru wa kujieleza na upatikanaji sawa wa taarifa kama mhimili wa demokrasia hai. Aidha, katika muktadha huu, vyombo vya habari huru na vinavyojitegemea ni nyenzo muhimu katika kuhakikisha utawala bora na uwajibikaji; (uk.16)*

(ii) *Kutumia urithi wake wa kiutamaduni wenye utajiri mkubwa, sekta ya sanaa, ubunifu na michezo inayokua kwa kasi pamoja na Kiswahili kama nyenzo ya diplomasia na lugha yenye manufaa ya kiuchumi inayopanuka na kutambulika kimataifa. Hata hivyo, utamaduni utaongeza ushawishi wa Tanzania kupitia nyanja mbalimbali kwa kukuza Kiswahili kama nyenzo ya kidiplomasia na lugha yenye manufaa ya kiuchumi katika ushirikiano wa uwili, kikanda na kimataifa; (uk.28) na*

(iii) *Tanzania inalenga kuwa kitovu cha utamaduni, sanaa bunifu na michezo barani Afrika ifikapo mwaka 2050, ikiwa na sekta zinazostawi katika muziki, filamu, mitindo, na burudani. Kwa kukuza vipaji na kuweka mazingira wezeshi, Tanzania itafungua milango ya ubunifu na ujasiriamali kwa vijana." (uk.61)* **mwisho wa kunukuu.**

**Mheshimiwa Spika,** misingi hiyo ya uchambuzi imezingatiwa kwa sababu inatoa mwelekeo rasmi wa sera, vipaumbele, na malengo ya maendeleo ya Taifa kwa kila sekta. Kwa sababu hiyo, mgawanyo na matumizi ya fedha za umma unaongozwa na ahadi, mipango na vipaumbele ambavyo Bunge linapaswa kujielekeza.

### 2.3.1 Makadirio ya Mapato

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokea taarifa kuhusu lengo la ukusanyaji wa maduhuli kwa mwaka wa fedha 2026/2027. Uchambuzi ulijikita zaidi katika lengo lililokuwa limewekwa kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Aidha, katika mwaka wa fedha 2026/2027 Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo **Fungu 96** inakadiriwa kukusanya maduhuli jumla ya **Shilingi 41,956,692,000.** Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa makadirio haya yameongezeka kwa shilingi **625,500,000** sawa na asilimia **1.51** ikilinganishwa na makadirio ya makusanyo kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Uchanganuzi wa makadirio hayo unaonekana katika **Jedwali Na. 3** na **Chati Na. 3**.

**Jedwali Na. 3: Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa Mwaka 2025/2026 na Mwaka 2026/2027**

| ULINGANISHO WA UKUSANYAJI WA MADUHULI (FUNGU 96) 2025/2026 NA 2026/2027 | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **CHANZO** | **2025/2026** | **2026/2027** | **ONGEZEKO/UPUNGUFU** | **% YA ONGEZEKO /UPUNGUFU** |
| **Idara na Vitengo Wizarani** | 1,036,000,000 | 1,058,000,000 | 22,000,000 | 2.1 |
| **Taasisi** | 40,295,192,000 | 40,898,692,000 | 603,500,000 | 1.5 |
| **JUMLA** | **41,331,192,000** | **41,956,692,000** | **625,500,000** | **1.51** |

**Chanzo:** *Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kuhusu Mwelekeo wa Bajeti kwa Mwaka 2026/2027*

**Chati Na. 3: Ulinganisho wa Ukusanyaji wa Maduhuli Fungu 96 2025/2026 na 2026/2027**




**Chanzo:** Usanifu wa Kamati kutoka kwenye Taarifa za Randama ya Wizara kwa Mwaka 2026/2027

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa makadirio hayo umeonesha kama ifuatavyo:-

(i) Makadirio ya makusanyo chini ya Wizara na taasisi zake kwa mwaka wa fedha 2026/2027, yameongezeka kwa **asilimia 1.51** ikilinganishwa na lengo la makusanyo kwa mwaka wa fedha 2025/2026;

(ii) Makadirio ya Makusanyo kwa Idara na Vitengo vya Wizara kwa mwaka wa fedha 2026/2027 yameongezeka kwa **asilimia 2.1** ikilinganishwa na makadirio hayo kwa mwaka wa fedha 2025/2026; na

(iii) Makadirio ya makusanyo kwa taasisi zilizo chini ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2026/2027 yameongezeka kwa **asilimia 1.5.**

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa makadirio ya mapato kwa mwaka wa fedha 2026/2027 ulilinganishwa na utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2025/2026 kwa lengo la kuzingatia uzoefu uliopatikana. Uchambuzi umeonesha mambo yafuatayo:-

(i) Ongezeko la **asilimia 1.51** katika makadirio ya mapato haliendani na uzoefu unaojitokeza katika Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa fedha 2025/2026. Kwa uzoefu uliopita, hadi kufikia zaidi ya nusu ya kipindi cha utekelezaji, ukusanyaji ulikuwa chini kwa **asilimia 35.46,** jambo

lililoashiria kuwa lengo halina mwelekeo wa kutimia. Hali hii inaonesha kwamba lengo linalowekwa kwa mwaka wa fedha 2026/2027 linastahili kupungua badala ya kuongezeka.

(ii) Ongezeko la **asilimia 2.1** la makusanyo kwa Idara na Vitengo vya Wizara katika mwaka wa fedha 2026/2027 ni halisi kwani lina uwezekano wa kufikiwa.

(iii) Ongezeko la **asilimia 1.5** katika makadirio ya mapato kwa taasisi zilizo chini ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2026/2027, haliendani na uzoefu uliopatikana wakati wa utekelezaji kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Taarifa ya utekelezaji ilionesha kwamba, hadi kufikia mwezi Februari, 2026, ukusanyaji wa mapato ya taasisi ulifikia **asilimia 34.7** ya lengo, kiwango ambacho kinaashiria kuwa hakitomudu ongezeko la makadirio linalopendekezwa.

(iv) Uwiano wa makadirio ya mapato kati ya Wizara na taasisi zake kwa mwaka wa fedha 2026/2027, hauendani na uwiano uliopatikana wakati wa utekelezaji wa bajeti kwa mwaka 2025/2026. Taarifa ya utekelezaji ilionesha kuwa katika ukusanyaji, Taasisi zilikusanya **asilimia 34.7** ya makusanyo yote na Wizara ilikusanya **asilimia 63.8** ya makusanyo yote. Makadirio kwa mwaka 2026/2027 yanaonesha kuwa makadirio ya mapato ya taasisi ni **asilimia 97.47** ya jumla ya makadirio yote kwa **Fungu 96**.

**Mheshimiwa Spika,** mantiki ya Kanuni ya 120 (2) ya Kanuni za Bunge ni kuliwezesha Bunge kutumia uzoefu uliopatikana wakati wa utekelezaji ili kujadili bajeti kwa mwaka wa fedha unaofuata. Uzoefu uliopatikana kwa mwaka wa fedha 2025/2026 unaonesha kuwa uwiano wa uwezo wa Wizara katika makusanyo na taasisi zake ni **asilimia 63.8** kwa Wizara na **asilimia 34.7** kwa taasisi zake. Makadirio yasiyozingatia uwiano huo yanaashiria kupatikana kwa vyanzo vipya vya mapato kwenye taasisi zilizo chini ya Wizara hii.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi zaidi wa Kamati umeonesha kuwa karibu vyanzo vyote vya mapato kwa mwaka wa fedha ulioisha ndivyo vinavyoendelea kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

Tafsiri ya matokeo hayo inaashiria kuhitajika kwa tathmini ya lengo la mapato kwa **Fungu 96.** Kamati ina maoni kwamba, pamoja na kuwepo kwa ongezeko la ukusanyaji wa maduhuli, Wizara inahitaji kuongeza ubunifu katika kuibua vyanzo vipya vya mapato.

### 2.3.2 Makadirio ya Matumizi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilichambua makadirio ya jumla ya **Shilingi 458,190,788,000** kwa ajili ya kugharamia Miradi ya Maendeleo inayopangwa kutekelezwa na Wizara kwa mwaka wa fedha 2026/2027. Uchambuzi huo umefanyika kwa ulinganisho na mwaka wa fedha wa 2025/2026. Matokeo ya uchambuzi yameonesha kuwa:-

(i) Makadirio ya bajeti hii ya miradi ya maendeleo hayajaongezeka kwa mwaka 2026/2027 ikilinganishwa na mwaka 2025/2026. Kamati imebaini kuwa Wizara hii haina miradi mipya na ratiba ya utekelezaji wa miradi ya awali haiongezi bajeti ya maendeleo.

(ii) Kwa ujumla Bajeti ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo imeongezeka kwa **asilimia 1.09** bila ongezeko lolote katika bajeti ya miradi ya maendeleo. Kwa takwimu hizi uendeshaji wa Wizara umeongezewa bajeti kiasi na miradi ya maendeleo itaendelea kama ilivyokuwa.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ina maoni kuwa, kuendelea kutenga fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo kutasaidia kukamilisha ujenzi wa miundombinu bora ya michezo Tanzania. Aidha, Kamati imefanya ulinganisho wa Bajeti ya miradi ya maendeleo, mishahara na matumizi mengineyo chini ya Wizara hii kwa Mwaka 2025/2026 na 2026/2027. Uchambuzi huo unaonekana katika **Jedwali Na. 4 na Chati Na. 4.**

**Jedwali Na. 4: Ulinganisho wa Bajeti ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa Miradi ya Maendeleo, Mishahara na Matumizi Mengineyo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 na 2026/2027**

| ULINGANISHO WA BAJETI 2025/2026 NA 2026/2027 (FUNGU 96) | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **MATUMIZI** | | **2025/2026** | **2026/2027** | **ONGEZEKO/ UPUNGUFU** | **% YA ONGEZEKO /UPUNGUFU** |
| **KAWAIDA** | MISHAHARA | 33,403,813,000 | 39,071,597,000 | 5,667,784,000 | 17 |
| | OC | 28,065,472,000 | 28,065,472,000 | 0 | 0 |
| **MAENDELEO** | NDANI | 458,190,778,000 | 458,190,788,000 | 0 | 0 |
| **JUMLA BAJETI** | **JUMLA KUU** | **519,660,073,000** | **525,327,857,000** | **5,667,784,000** | **1.09** |

**Chanzo:** *Randama ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kuhusu Mwelekeo wa Bajeti kwa Mwaka 2026/2027*

**Chati Na. 4: Ulinganisho wa Bajeti 2025/2026 na 2026/2027 (Fungu 96)**




**Chanzo:** *Usanifu wa Kamati kutoka kwenye Taarifa za Randama ya Wizara kwa Mwaka 2026/2027*

### 2.3.3 Makadirio ya Matumizi ya Kawaida

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilichambua makadirio ya bajeti ya matumizi ya kawaida kwa mwaka wa fedha 2026/2027 kwa kulinganisha na mwaka wa fedha 2025/2026. Matokeo ya uchambuzi yameonesha mambo yafuatayo:-

(i) Makadirio ya matumizi ya kawaida yameongezeka kwa **asilimia 14.82** ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2025/2026;

(ii) Ongezeko la Bajeti ya mishahara kwa Wizara hii limeongezeka kwa **asilimia 17** ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2025/2026;

(iii) Bajeti ya matumizi ya uendeshaji yaani matumizi mengineyo haijaongezeka ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2025/2026;

(iv) Bajeti ya matumizi mengineyo kwa mwaka 2026/2027 ni sawa na **asilimia 5.34** ya jumla ya bajeti ya Wizara hii. Uwiano huo unatofautiana na mwaka wa fedha 2025/2026, ambapo bajeti ya matumizi mengineyo ni **asilimia 5.4** ya jumla ya bajeti ya Wizara.

### 2.4 Majumuisho ya Sehemu ya Pili

**Mheshimiwa Spika**, sehemu hii imefafanua uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji kwa mwaka wa fedha 2025/2026 na kuonesha makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2026/2027. Mambo makuu matatu yamejitokeza kama ifuatavyo:

(i) Upangaji wa lengo la makusanyo umebainika kuhitaji tathmini kwa kutumia uzoefu uliopatikana kwa mwaka wa fedha 2025/2026;

(ii) Utekelezaji wa kazi zilizopangwa na Wizara ulizingatia majukumu ya msingi ya Wizara na uliendana na upatikanaji wa fedha kwa mwaka wa fedha 2025/2026;

(iii) Makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/2027 yanawezesha Wizara hii kuendelea na utekelezaji wa majukumu yake; na

(iv) Mipango ya Wizara na vipaumbele kwa mwaka wa fedha 2026/2027 imezingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2025/2030.

**4 MEI, 2026**

**SEHEMU YA TATU**

## 3.0 MAONI, USHAURI NA HITIMISHO
### 3.1 Maoni

**Mheshimiwa Spika**, baada ya uchambuzi, naomba kutoa maoni ya Kamati kwa kuzingatia matokeo ya uchambuzi. Maoni haya yanajenga msingi wa ushauri nitakaoutoa. Maoni hayo ni kama ifuatavyo:-

(i) Kutokupatikana kwa fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya Mradi wa Ujenzi na Ununuzi wa Mitambo ya Kisasa ya Uchapaji *(TSN)* ni jambo linaloweza kuathiri ukamilishaji wa mradi huo na pengine kusababisha hasara kwa Serikali.

(ii) Kuendelea kutenga bajeti na kutoa fedha kwa wakati kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa viwanja vitatu (3) vya mazoezi katika Mkoa wa Dar es Salaam na viwanja vitano (5) vilivyopo mkoani Arusha ni jambo linaloweza kufanikisha maandalizi madhubuti ya AFCON 2027. Aidha, pamoja na kutumika wakati wa Mashindano ya Mpira wa Miguu kwa timu za Taifa za Wanaume Afrika (AFCON 2027), vitasaidia kupunguza utegemezi wa Uwanja wa Benjamin Mkapa.

(iii) Kupungua kwa wigo wa ukusanyaji wa Mapato ya Tozo kwa Bodi ya Filamu Tanzania kunakosababishwa na kupungua kwa idadi ya waandaji wa filamu kutokana na mabadiliko ya soko la filamu pamoja na kukua kwa teknolojia kunadhoofisha ukusanyaji wa maduhuli kwa taasisi hiyo.

(iv) Ufinyu wa bajeti kwa ajili ya ujenzi wa Arena ya Sanaa na Michezo unakwamisha uwezekano wa kuongeza fursa za ajira, kukuza uchumi, kuitangaza Tanzania kimataifa, kukuza vipaji vya vijana, kuimarisha umoja na kuboresha afya.

(v) Kutokuwepo kwa mpango wa Wizara kukamilisha mchakato wa vazi la Taifa kunafifisha azma ya Serikali kuweka utambulisho wa Taifa kupitia mavazi.

(vi) Kutokukamilika kwa ujenzi wa miundombinu ya barabara zinazoelekea ndani na nje ya Uwanja wa Arusha kutaathiri mwenendo mzima na uchelewashaji wa maandalizi ya Mashindano ya AFCON 2027.

### 3.2 Ushauri

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na maoni yalivyoelezwa hapo juu, Kamati ilizingatia ipasavyo maoni hayo na kuyatumia kama msingi wa ushauri ufuatao:-

(i) Serikali iendelee kutoa fedha za Mradi wa Ujenzi na Ununuzi wa Mitambo ya Kisasa ya Uchapaji *(TSN)* kwa kiwango kilichokusudiwa ili kukamilisha mradi huo kwa wakati na kuipunguzia hasara zinazoweza kuzuilika.

(ii) Serikali ikamilishe ujenzi wa viwanja vitatu (3) vya mazoezi katika Mkoa wa Dar es Salaam na viwanja vitano (5) vilivyopo mkoani Arusha kwa wakati ili Tanzania iweze kukidhi vigezo vya kuandaa Mashindano ya Mpira wa Miguu kwa timu za Taifa za Wanaume Afrika (AFCON 2027).

(iii) Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo iboreshe na kuongeza wigo wa ukusanyaji wa mapato ya Bodi ya Filamu Tanzania kwa kuendana na maendeleo ya dunia, kurahisisha mawasiliano, kuboresha ubunifu na kuongeza ufanisi katika uzalishaji na usambazaji wa taarifa na kazi za wasanii.

(iv) Serikali iongeze bajeti kwa ajili ya ujenzi wa Arena ya sanaa na michezo kwa kuwa kukamilika kwa utekelezaji wa mradi huu kutaongeza fursa za ajira, kukuza uchumi, kuitangaza Tanzania kimataifa, kukuza vipaji vya vijana, kuimarisha umoja na kuboresha afya. Ushauri huu unaendana na mwelekeo alioutoa Mheshimiwa Rais wakati wa Hotuba yake akilizindua Bunge la 13:

**Nanukuu,** *"Tunaendelea na maandalizi ya ujenzi wa studio ya kisasa ya filamu ili kupandisha thamani ya kazi za wacheza filamu wetu hapa nchini. Tutajenga ukumbi wa kisasa wa*

*maonyesho ili kuwawezesha wasanii wetu kufanya matamasha ya kimataifa, na kuvutia wasanii wa nje wakubwa kufanya matamasha nchini. Tunataka sanaa, filamu na muziki zitengeneze ajira na kuchangia uchumi wa Taifa." (uk.22-23)* **mwisho wa kunukuu.**

(v) Serikali ifufue na kukamilisha mchakato wa upatikanaji wa vazi la Taifa ili kuimarisha utambulisho wa Taifa, kukuza umoja wa kitaifa, kukuza uchumi, ajira pamoja na kuhifadhi na kuendeleza utamaduni wa Mtanzania.

(vi) Serikali iongeze kasi ya ujenzi wa miundombinu ya barabara za ndani na nje ya Uwanja wa Arusha ili kukamilisha maandalizi ya Mashindano ya AFCON 2027.

### 3.3 Hitimisho

**Mheshimiwa Spika**, nachukua fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi kwa ajili ya kuwasilisha Taarifa hii. Aidha, nawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha kukamilika kwa taarifa hii. Naomba majina yao kama yalivyoorodheshwa katika Taarifa hii yaingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)*:-

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Husna Juma Sekiboko, Mb | - Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Cornel Lucas Magembe, Mb | -M/Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Hamis Shabani Taletale, Mb | - Mjumbe |
| 4. | Mhe. Asha Ramadhan Baraka, Mb | - Mjumbe |
| 5. | Mhe. Asha Juma Feruzi, Mb | - Mjumbe |
| 6. | Mhe. Regina Henry Mikenze, Mb | - Mjumbe |
| 7. | Mhe. Asha Juma Kombo, Mb | - Mjumbe |
| 8. | Mhe. Dkt. Christine Christopher Mnzava, Mb | - Mjumbe |
| 9. | Mhe. Yumna Mmanga Omar, Mb | - Mjumbe |
| 10. | Mhe. Kijakazi Yunus Mohamed, Mb | - Mjumbe |
| 11. | Mhe. Mohamed Abdulla Makame, Mb | - Mjumbe |
| 12. | Mhe. Mabula Johnson Magangila, Mb | - Mjumbe |
| 13. | Mhe. Fagason Aron Nkingwa, Mb | - Mjumbe |
| 14. | Mhe. Juma Abdalla Juma, Mb | - Mjumbe |

15. Mhe. Bakari Shingo Bakari, Mb - Mjumbe
16. Mhe. Onesmo Merdson Mnkondya, Mb - Mjumbe
17. Mhe. Baraka Ulimboka Mwamengo, Mb - Mjumbe
18. Mhe. Isaya Moses Mngurumi, Mb - Mjumbe
19. Mhe. Dkt. Mashaka Doto Biteko, Mb - Mjumbe
20. Mhe. Kassim Amar Mbaraka, Mb - Mjumbe

**Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati napenda kumshukuru – Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo Mhe. Paul Christian Makonda (Mb), Naibu Waziri - Mhe. Hamis Mohamed Mwinjuma (Mb), Katibu Mkuu wa Wizara hii Ndg. Gerson Partinus Msigwa, Naibu Katibu Mkuu Ndg. Methusela Stephen Ntonda, pamoja na Watendaji wengine wa Wizara kwa ushirikiano mkubwa walioipa Kamati katika kutekeleza majukumu yake na kwa usimamizi mzuri wa majukumu ya Wizara kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya kipekee napenda kuwashukuru watumishi wote wa Ofisi ya Bunge wakiongozwa na Katibu wa Bunge *Ndg. Baraka Ildephonce Leonard,* kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake vema katika wakati wote ilipokutana na hata wakati wa utayarishaji wa taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu lipokee Taarifa hii ili lijadili na likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 kama yalivyowasilishwa na Mtoa Hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

Husna Juma Sekiboko, Mb

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ELIMU, UTAMADUNI NA MICHEZO**
04 Mei, 2026

**MWENYEKITI:** Tunakushukuru Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti kwa uwasilishaji wa Taarifa ya Kamati.

Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea, ninaomba kuleta matangazo ya wageni walioko ukumbini na tunaanza na wageni wa Mheshimiwa Paul Christian Makonda, Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo ambaye ni Ndugu Victor Mwambalaswa, Mbunge Mstaafu, Ndugu Yasmin Razak Bashir, Wakala wa Didier Drogba na Ndugu Ronald Japont, Msaidizi wa Didier Drogba. *(Makofi)*

Wageni wengine wa Mheshimiwa Waziri ni Wajumbe wa Bodi za Taasisi za Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo na Wajumbe wa Kamati ya Maudhui. *(Makofi)*

Tunao wageni wengine ambao ni Menejimenti ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo na Wakuu wa Taasisi zake, Viongozi wa Vyama, Taasisi za Habari na Vyombo vya Habari. *(Makofi)*

Tunao pia wageni wengine wa Mheshimiwa Waziri ni Taasisi za Kifedha nchini za *NMB*, *CRDB* na *NBC*. *(Makofi)*

Tunao Wajumbe wa Kamati ya Siasa ya Mkoa na Wilaya ya Arusha, Waheshimiwa Madiwani wa Jiji la Arusha na pia Viongozi wa Dini na Mila kutoka Arusha. *(Makofi)*

Tunao wadau wa Kampuni ya Magazeti ya Serikali, Bodi ya Filamu Tanzania, Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika, Mawakala wa Tafsiri wa Baraza la Kiswahili na Viongozi wa Chama cha Maafisa Utamaduni Tanzania. *(Makofi)*

Tunao pia Watendaji Ofisi ya Mbunge wa Arusha Mjini, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Arusha na Wadau wa Masuala ya Utalii. *(Makofi)*

Tunao viongozi wa vyombo vya kurusha maudhui *DSTV* na *Azam TV*. *(Makofi)*

Tunao pia Viongozi wa Mashirikisho ya Sanaa, Wasanii, Wasimamizi wa Wasanii na Watayarishaji wa Muziki, Filamu, Tamthiliya na Ucheshi. *(Makofi)*

Tunao Wasanii Wakongwe wa Muziki wa Bongo Fleva, wapo pia wanufaika wa Mfuko wa Utamaduni na Sanaa kutoka *Maasai Market Arusha*. *(Makofi)*

Tunao wadau wa Hakimiliki, Balozi wa Ofisi ya Hakimiliki Tanzania na Kiongozi wa Serikali ya Wanafunzi ya Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao mabondia waliofanya vizuri katika Mashindano ya Kitaifa na Kimataifa, hongereni sana mabondia wetu. *(Makofi)*

Tunayo Timu ya Mpira wa Kikapu ya *Dar City*. *(Makofi)*

Tunao pia wawakilishi wa wanafunzi wanaosoma Shahada ya Uandishi wa Habari na Uhusiano wa Umma katika Chuo Kikuu cha Dodoma *(UDOM)*. *(Makofi)*

Tunao Viongozi wa Mashindano ya Ulimbwende na Washindi wa Ulimbwende katika mashindano mbalimbali. *(Makofi)*

Karibuni wageni wetu wote ambao ni wageni wa Mheshimiwa Waziri wetu wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo na hasa Viongozi wetu wa Kamati ya Siasa wanaotoka Mkoa wa Arusha ukizingatia nami Mwenyekiti pia ni Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Arusha, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo ambao ni wageni 15 kutoka Jukwaa la Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi Jijini Dodoma. Karibuni sana wageni wetu wote hapa Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, na sasa tunaingia kwenye uchangiaji. Tunaanza na Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko, ajiandae Mheshimiwa Ahmed Juma Ngwali.

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa fursa ya kuwa mchangiaji wa kwanza katika bajeti hii ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo. Ninatumia fursa hii kwa haraka haraka kumshukuru na

kumpongeza sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa ambayo ameifanya katika kuleta mageuzi makubwa katika Sekta ya Michezo nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, utakubaliana nami kwamba katika kipindi cha Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, tumeona mabadiliko makubwa, na leo tumeshuhudia washindi wengi, mabingwa wengi wa michezo, tuzo nyingi zinakuja nchini. Hii siyo siri nyingine, bali siri anayo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kuwawezesha wanamichezo nchini na kutoa fursa kubwa kwa wanamichezo kuonesha vipaji vyao na mwisho wa siku kutuletea tuzo mbalimbali. Tunawapongeza na tunamshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inayohusika na masuala ya michezo, Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake amesema ni *soft power*. Ni *soft power* kwa sababu gani? Kwa sababu ni nguvu inayopeleka ushawishi kwa wananchi wake hasa katika kutumia nyenzo laini huku tunazungumzia sanaa, burudani, michezo, mambo yote ambayo yanamfanya mwananchi kuelewa vizuri dhana na mambo mbalimbali yanayowasilishwa kwake na Serikali yake kwa sababu hii ni *soft power*. Ni *soft power* kwa sababu inaleta ushawishi mkubwa katika jamii na katika nchi kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatumia fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutuletea Waziri mwenye uwezo wa kuleta ushawishi Kitaifa, ushawishi Kimataifa, Ndugu yangu Mheshimiwa Paul Christian Makonda. Tunampongeza kwa sababu, sote tumeshuhudia katika kipindi kifupi ametengeneza nchi yetu katika maeneo mbalimbali yanayohusiana na Habari, Utamaduni na Michezo kuwa *headline* Kimataifa. Tumeshuhudia mambo mengi, tunampongeza sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Hamis Mwinjuma almaarufu Mwana FA, amekuwa nyenzo kubwa. Nami ninapenda kusema, nimekuwepo kwenye

Kamati inayosimamia Sekta hii ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa kipindi chote cha maisha ndani ya Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeshuhudia Waheshimiwa Mawaziri wengi na Waheshimiwa Manaibu Mawaziri wengi wamepita katika Wizara hii, lakini nataka kusema kwa dhati ya moyo wangu, Waheshimiwa Mawaziri hawa, Mwana FA na Mheshimiwa Makonda wamefanya kazi ambayo wanaifanya Wizara hii sasa isionekane kama ni Wizara ya mchezo mchezo, ionekane ni Wizara ya Michezo, Habari, Utamaduni, Sanaa, ni Wizara ambayo sasa imekuwa na mvuto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka ya nyuma, wakati huo tulikuwa tunazungumzia bajeti ya Wizara hii ikiwa na shilingi bilioni 35, shilingi bilioni 32, shilingi bilioni 33 pekee, leo tuna bajeti tunayokwenda kuipitisha ya shilingi bilioni 525 na zaidi. Haya ni mapinduzi makubwa. Nami ninaamini Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan hakuidhinisha tu fedha hizi nyingi, alikuwa anajua wapo watu wa kwenda kusimamia na kuleta tija inayokubalika, nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati ninaingia Bungeni hapa 2020/2021, tulikuta bajeti ya shilingi bilioni 35 na kwa kweli ilikuwa ni bajeti inavunja moyo, na kwa kweli ilikuwa ni Wizara ambayo haina mvuto kwa sababu utaenda kufanya nini na bajeti ya shilingi bilioni 35? Unakuta sehemu kubwa ilikuwa ni mishahara ya watumishi, ni mambo madogo madogo, lakini leo tuna miradi ya maendeleo. Miradi ya maendeleo tunazungumzia ujenzi wa viwanja mbalimbali ndani ya Mji wa Dodoma, ndani ya Jiji la Arusha, ndani ya Jiji la Dar es Salaam, vinajengwa viwanja vikubwa vizuri vyenye uwezo wa kufanya mashindano ya Kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunafurahia kwamba mashindano mengi ya Kimataifa ikiwemo Michuano ya Mpira wa Miguu Afrika *(AFCON)* inakuja kufanyika Tanzania ni kwa sababu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameamua kuwekeza fedha nyingi za kutosha katika ujenzi wa miundombinu katika ujenzi wa viwanja vya michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli, kama Kamati, tunamshukuru na tunampongeza sana Mheshimiwa Rais wetu na tunawapongeza wataalamu wote wakiongozwa na Katibu Mkuu Ndugu yangu Msigwa, anafanya kazi nzuri, kubwa, Msemaji Mkuu wa Serikali, tunawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho wa siku tunatamani kuona maandalizi ambayo tumeelezwa kuhusiana na michuano ya *AFCON*, iende ikafanyike kwa vitendo. Hatutaki kuona kigugumizi katika kutolewa fedha zinazokwenda kwenye maandalizi ya *AFCON*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatamani kuona nchi yetu, na sekta zote zinazohusika na masuala ya maadalizi ya *AFCON*, zione hili ndiyo jukumu namba moja, ndiyo kipaumbele kwa sasa cha Taifa ili kuhakikisha kwamba nchi yetu inakwenda kuandika historia mpya katika dunia kwa kuwa wenyeji wa michuano ya *AFCON*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mambo ni mengi, tukizungumzia michezo, tumezoea kuzungumzia michezo ya *football* kwa sababu ndiyo mchezo ambao namba moja unaopendwa katika nchi yetu na pengine katika dunia kwa ujumla; lakini wapo wadau ambao wameamua kuiibua michezo mingine, na sasa inaanza kutuletea heshima ya Kimataifa, kama vile Mpira wa Kikapu *(Basket Ball)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ninataka kusema, kuna wadau, kuna Watanzania wenzetu wamewekeza nguvu kubwa katika kutengeneza timu. Leo ninaiona hapa *Dar City,* timu ambayo imeenda *South Africa* kushiriki mashindano ya Mpira wa Kikapu Afrika na imeweza kufuzu kuingia kwenye robo fainali na sasa wanakwenda kuiwakilisha nchi Kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nimeitaja *Dar City,* hatuna viwanja vya kutosha kwa ajili ya michezo ya Basketi, hatuna viwanja *indoors* kwa ajili ya michezo ya *volleyball*, hatuna viwanja vya kutosha katika michezo mingine. Ili tuweze kuendelea kuunga mkono jitihada za Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan za

kuongeza maendeleo makubwa katika mapinduzi ya michezo, ni lazima Bunge hili tukubaliane kwamba kuna ulazima wa Serikali kufanya ujenzi wa viwanja vya michezo nchini hasa ile michezo ambayo tayari wenzetu wameiibua, na tayari imeleta mvuto na inaleta tuzo na heshima kubwa kwa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuzungumza eneo lingine, nalo ni habari. Tumezoea kuona na ninataka kuwapongeza sana Waandishi wa Habari na Wanahabari kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na Waheshimiwa wabunge wote mtakubaliana nami, hivi karibuni pameibuka wimbi la Wanahabari wa kujitegemea. Nawaita wa kujitegemea kwa sababu, katika vikao vyetu vya Kamati, tulijaribu kudodosa kujua hawa walitokea wapi? Ninalozungumzia hapa, ukienda kwenye ziara majimboni, wako vijana wanakuja na *microphone*, zina nembo ya chombo fulani cha habari, ukimwuliza unatoka chombo gani? Hataki kusema kwa sababu ana hiyo nembo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, wenye chombo chao hawamtambui na muda mwingine hahudumiwi, hana posho, hana mshahara. Yeye amepewa *microphone* tu anazunguka nayo kutafuta habari wewe ambaye utakuwa na hiyo habari utawajibika kumpa posho ya kujikimu ili hiyo habari yako aitoe *positive*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama umeshindwa kumhudumia siku hiyo maana yake anaweza kuamua chochote cha kuandika juu yako, ndiyo maana tumeona wimbi la habari zinazoenea kwenye mitandao ya kijamii, zinazoendelea hata kwa baadhi ya magazeti na baadhi ya vyombo kama *TV*, ni habari ambazo zinakinzana na maadili ya uandishi wa habari, lakini zingine zinachochea mazingira yasiyokuwa sahihi na mwisho wa siku zinaleta taharuki kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe sasa Wizara kwa sababu wameshakuja na utaratibu wa ithibati na kwa sababu sasa waandishi wote wanapaswa kuwa kwenye ithibati wawe na sifa

zile ambazo zinakubalika kwa mujibu wa taratibu za Habari, basi wasimamie wale wote ambao wanaandika habari, wale wote ambao wanatafuta habari wahudumiwe na vyombo vyao wawe na ajira ikiwa ni za mkataba…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa muda wako umekwisha.

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ikiwa ni za kudumu, lakini ajira hizo ziweze kuwasaidia kumudu maisha na siyo kuhemea wakati wanapokwenda kutafuta taarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninashukuru sana, ninaunga mkono hoja na ninawatakia kila kheri katika utekelezaji wa bajeti. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ahsante. Nilimtaja Mheshimiwa Ahmed Juma Ngwali na ajiandae Mheshimiwa Hamisi Shabani Taletale.

**MHE. AHMED JUMA NGWALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikushukuru, lakini nimshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ameniwezesha leo kuwepo hapa na kuchangia katika Hotuba hii. Pia nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa ambayo anaifanya na ya uhakika na kwa hakika ametuheshimisha. Ninawapongeza Mawaziri wote kwa kuteuliwa na wanafanya kazi zao vizuri na kwa uhakika kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru tena kwa kunipa nafasi hii kuchangia katika hoja hii muhimu inayohusu sekta ya michezo na maendeleo ya michezo hususan, nitaongelea soka. Hoja yangu ni moja na ipo eneo moja la udhibiti wa fedha hapo ndiyo hoja yangu ilipo, udhibiti wa fedha katika michezo hiyo ndiyo hoja yangu mwanzo mpaka mwisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika kwamba katika siku za karibuni soka letu la Tanzania limeonesha ukuaji unaovutia hususan katika mafanikio ya baadhi ya vilabu vyetu

katika mashindano ya kimataifa na kuwavutia zaidi, kuleta hamasa zaidi kwa washabiki pamoja na wawekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio hayo yanayoonekana, ninapenda kuwasilisha hoja yangu kwamba ukuaji huo hauna misingi imara na haujaegemezwa kitaasisi na kifedha, jambo ambalo linahatarisha uimara wa michezo yetu siku zijazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo wa *club licensing* ni mfumo ambao umeanzishwa na *FIFA* na kutekelezwa na *CAF* katika ngazi ya bara kwa lengo la kuweka utawala wa kifedha katika mpira na haki katika mpira wa miguu, lakini kwa bahati mbaya sana katika utekelezaji wake hapa nchini kuna mapungufu yafuatayo:- *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, kuna mapungufu ya uwiano baina ya mapato na matumizi. Kuna kitu tunaita *break even requirement,* hakuna hicho kitu na siyo kwamba sijui kuna Kamati ya Fedha. Kamati ya Fedha ipo ndani ya *TFF* ambayo inakagua hesabu za wakandarasi wa timu pamoja na mikataba, lakini shida iliyopo ni kwamba hii Kamati inafanya kazi yake kiutendaji zaidi siyo *strategic financial management*. Kwa hiyo, inakagua tu, ikishakagua inatazama mikataba kama imepikwa ama hesabu zimepikwa na inapeleka mbele na tunaendelea; hakuna ukaguzi huru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushahidi wa hoja yangu ni kwa mujibu wa taarifa iliyowasilishwa katika Mikutano Mikuu ya Mwaka 2023/2024 katika vilabu vyetu vikubwa vya Simba na Yanga ambayo imeonesha hakuna uwiano kati ya mapato na matumizi. Kwa mfano, ninaomba ninukuu Klabu ya Yanga iliripoti mapato ya takribani shilingi bilioni 21.2 dhidi ya matumizi ya bilioni 23.3 sawa na hasara ya shilingi bilioni 1.1. Wakati Simba iliripoti mapato ya shilingi bilioni 14.5 dhidi ya matumizi ya shilingi bilioni 19.3, sawa na hasara ya shilingi bilioni 4.8. Kwa hiyo, hakuna uwiano kati ya mapato na matumizi, lakini hatuna Uhakika hayo mapato je, yapo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii Kamati iliyokuwepo ndiyo maana huku mbele ninakuja kupendekeza tuwe na *independence financial control body* ambayo itakuwa na *mandatory* ya kukagua hizo fedha. Je, ni kweli hayo mapato yapo? Zimetumiwa? Hii hasara inakwenda kwa nani kifedha? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo inashangaza tuna klabu ya Yanga ambayo imeanzishwa mwaka 1935 na Simba 1936, lakini wakiondoka wafadhili katika vilabu hivyo, vilabu vyenye miaka karibu mia wakiondoka wafadhili katika vilabu hivyo vinashindwa kulipa mshahara wa mwezi mmoja wa wachezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa una taasisi ambayo ipo miaka 100 inashindwa kulipa mshahara wa mwezi mmoja wa wachezaji. Kwa hivyo, tunafurahia mpira, lakini kwenye ukweli hasa na sasa duniani hapa tunatumia tu *club licensing* lakini *Europe* tayari *UEFA* tayari wameanza kutumia *financial fair play* muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha ambazo siyo za mpira haziruhusiwi kuingia ndani ya mpira wa miguu. Maana yake hakuna fedha za wafadhili zitakazoingia ndani ya mpira kwa mujibu wa *financial fair play* na hii *club licensing* ni takwa la *FIFA*. Kwa hivyo, hata *financial fair play* inakuja kuchukua nafasi ya *club licensing* na hiyo itafanya vilabu vyetu vishindwe kushindana katika mashindano ya kimataifa na hata mashindano ya ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, athari za kukosekana kwa udhibiti wa fedha katika soka letu ni nyingi. Kwanza ni kuendelea kumtegemea mfadhili mmoja ambapo akiondoka basi *club* inaweza kudondoka ama kupotea kabisa. Tuna mifano mingi, Zanzibar sisi tulikuwa tuna vilabu vingi sana tulikuwa na Malindi chini ya Mfadhili Mkuu Naushad imepotea. Tulikuwa na Kikwajuni imepotea, tulikuwa tuna *Sports* Simba chini ya Abraham Msoma imepotea; timu zote zimepotea. Tulikuwa na Shangani chini ya Mohamed Raza, timu zimepotea kabisa sasa zimebakiwa timu za vigosi pekey ake. Kwa hivyo, hizi timu pendwa bila kuweka utaratibu mzuri wa fedha zinaweza nazo pia kupotea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, kukosekana kwa ushindani wa haki, bila udhibiti wa fedha (uwiano wa mapato na matumizi) ushindani wa haki hauwezi kupatikana. Kwa hivyo, niharakishe kwa sababu ya kengele nipendekeze sasa. Ninapendekeza kuanzisha mkakati ambao utawezesha vilabu kujitegemea badala ya kutegemea mfadhili mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tuwe na mkakati maalumu wa kuhakikisha kwamba vilabu vitajitegemea na kwa sababu mifumo inayokuja duniani maana yake sasa hivi watu wamekwenda mbali zaidi ya *financial fair play,* kuna *FSR* tayari wameanza imetoka 2022. Kwa hiyo, sasa ni muhimu sana kuanzisha taratibu mifumo ya kifedha katika *club licensing* ili itakapokuja *financial fair play* iwe tumejitayarisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipendekeze kuwe na mfumo wa uwazi wa mapato na matumizi yaani *quarterly* siyo ripoti ya fedha itoke mwaka mpaka mwaka, hapana. Kila robo ya mwaka tupate ripoti na hizo ripoti ziwekwe wazi kwa sababu hatuwezi kuruhusu fedha holela zikaingia katika mpira wetu lazima fedha za mpira zitokane na mpira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mtu anataka kuwekeza ama mfadhili anataka kuwekeza awekeze kwenye miundombinu, awekeze kwenye mambo mengine na hasara kwa mujibu wa *financial fair play* hatujafika huko, lakini tunazungumza huko hiyo inakuja hasara inabebwa na mfadhili kwa kuwekeza katika miundombinu siyo tena aikopeshe *club*. Sasa hizi *Club* za Simba na Yanga mpaka leo jamani zinashindwa kulipa mshahara wa mwezi mmoja eti wafadhili wameondoka, tunakwenda wapi? Achilia mbali na *club* nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuimarisha huu Mfumo wa *Club Licensing* pia kwa kuongeza vigezo vya kifedha kuanzia ufuatiliaji endelevu katika matumizi ya vilabu. Kama nilivyosema awali, mimi ni mmoja ambaye *almost* sikubali kwamba matumizi haya ni sahihi, haya mapato ni sahihi na haya madeni ni sahihi kwa sababu hatuna *Independent Financial Control Body* ya kutuambia kwamba kweli haya matumzi yaliyotumika ni sahihi.

Kama nilivyosema ipo *operational* tu inakagua tu ile hesabu halafu inatupa taarifa, lakini sitaki kuamini maana nikisema ninaamini nitakuwa mwongo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine kuanzishwa kwa mfumo wa mpito wa udhibiti wa fedha utakaowezesha vilabu vyetu kujijenga kiuchumi hatua kwa hatua. Maana yake tukisema leo tuige mfumo wa *financial fair play* maana yake ni nini? Vilabu vyote hivi vitaanguka kwa sababu vilabu hivi havina *asset,* havina *liquidity,* havina chochote maana yake…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ahsante kwa mchango wako, muda wako umekwisha.

**MHE. AHMED JUMA NGWALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nilimtaja Mheshimiwa Hamisi Shabani Taletale, ajiandae Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi.

**MHE. HAMISI S. TALETALE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza kabisa ninamshukuru Mwenyezi Mungu *Azza wajalla* kwa kunipa nguvu ya kuweza kuchangia siku ya leo. Niipongeze Wizara ya Michezo, ninaona leo Wizara imemwaga watu wa kimataifa, hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze pia Mheshimiwa Rais kwa kile anachokifanya, sisi tunamwita ndiyo mwanamichezo namba moja nchini. Kabla ya wote niwashukuru sana wananchi wenzangu wa Morogoro Kusini Mashariki kwa kuniamini na kunileta hapa na kusema maneno yanayohusu Mkoa wetu wa Morogoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudi kwenye hotuba ya bajeti aliyoizungumza Waziri Mheshimiwa Makonda. Kiukweli Mheshimiwa Waziri amesoma Hotuba ambayo tukiitazama Wizara vizuri tunaona Wizara inakwenda kutengeneza mabadiliko, lakini

niongee jambo moja, mimi ni Mjumbe kwenye Kamati ya Elimu, Utamaduni na Michezo, vijana huko nje wanalia na *arena*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ni siku ambayo nina mtihani, Mheshimiwa Rais ameniletea Mawaziri wote washikaji zangu. Yule mchungaji mshikaji wangu, yule Mwana-*hip hop* ni mshikaji wangu lakini leo nitaondoka na shilingi yao kwa maslahi ya vijana wa nchi hii. Hatuwezi kila siku tunazungumza *arena,* halafu Waziri amesimama hapa amemaliza maneno yake yote sijaona akizungumza bajeti ya *arena*, sijaona hatima ya vijana hawa ambao wanaolalamika huko nje kwamba tunahitaji *arena*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais ametoka kifua mbele amesema ametupatia *arena,* Waziri amesimama hapa hajasema lolote. Ndugu yangu, Mheshimiwa Makonda leo kama mama anamwombea dua nyumbani mshahara wake ninaondoka nao. Mshahara wake ninaondoka nao Mwana-FA hatuwezi kukaa vijana wanataka *sports arena*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaona mfano, amezungumza Mheshimiwa Mwenyekiti wetu wa Kamati hapa kuhusu ndugu zetu wale wa *Dar City* wana-*hustle,* wanakwenda kufanya mazoezi Zanzibar wale. Yule ndugu yetu Mzenji anapambana kama laiti tungekuwa na *sports arena* wale wangefanyia hapo, lakini leo Mzenji anaungaunga anakwenda kulipa nje, anatoa wachezaji nje ya nchi, lakini viwanja havina kiwango. Mheshimiwa Rais ameleta pesa hatuoni hivyo *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi tulikuwepo na Mawaziri wote hawa wawili tukiangalia ngumi pale kwa ndugu yetu Mafia, ule uwanja wachezaji wakicheza katikati wanateleza kwa sababu mvua ilinyesha. Hebu fikiria tungekuwa na *sports arena* ingekuwa hivyo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa leo hii ninazungumza mimi ndiyo mtu wa kwanza, ndugu zangu watanisamehe, Taifa kwanza undugu baadaye. Ninataka kuona utaratibu wa *sports arena*

kujengwa. Ninataka azungumze asimame na atupe na ushahidi, vijana wamechoka. Mimi ni Mswahili sana unajua mimi, nikikuzungumza Uswahili mimi ni Mswahili mpaka chenji inabaki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninavyozungumza hivyo, msimu huu ni msimu wa mvua, watu wanapigia Masheikh mvua zisinyeshe ndiyo watu wapigane ngumi pale. Alikuwepo Mheshimiwa Waziri mchana jua kali, dakika mbili jua kali haiwezekani haya mambo mvua inyeshe burudani ziendelee na ili ziendelee lazima tufuate kile alichokisema Mheshimiwa Rais. Mheshimiwa Rais ametoka huko Korea ametuletea pesa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunajua na tunafahamu mwezi mmoja uliopita kuna mtu aliuliza humu swali Mheshimiwa Waziri naye akaelezea, pesa tunajua ipo *more than four hundred billions* tumeletewa kwa ajili ya *sports arena.* Mheshimiwa Waziri hii pesa hajazungumza anaipeleka wapi? Anataka iende wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa siwezi kuwa yaani mkaguzi wa hesabu za Kiserikali nikawa ninataka kuzuia hela yenu la hasha! Mimi ninazuia mshahara wako, leo jua wazi Mama Maria huko nyumbani na Mama Malika huko nyumbani wajue wazi leo hapa wanaume wao wanaondoka bila mshahara. Mimi ninaondoka na mishahara yao kwa maslahi ya vijana wa nchi hii. Hatuwezi kuwa tunazungumzia Bajeti ya Michezo kila siku, ninajua watu wengi watazungumzia kuhusu *AFCON,* lakini nisipozungumzia kuhusu *sports arena* watasahau, wakae wakijua leo mshahara hawapati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Michezo ni Wizara ambayo inalinda amani ya nchi hii. Sisi wakazi wa Morogoro, Mkoa kwa ujumla sisi ndio wenye burudani ya ukweli. Wachezaji wa mpira wanatoka kwetu na wachezaji wa ngumi wanatoka kwetu pia.  Nikisema hapa, kwenye bajeti ya Mheshimiwa Waziri hakuna hata iliyozungumzia kwenye hii *AFCON* kutakuwa kuna uwanja wa mazoezi pale Morogoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme, hasira zangu za kukosa uwanja Morogoro ninazipeleka kwenye kukosa *arena*. Ninazungumza mshahara wa Mheshimiwa…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa muda wako umekwisha, ahsante kwa mchango wako.

**MHE. HAMISI S. TALETALE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimalizie kwa kuwapongeza, lakini mishahara yao leo ninaondoka nayo. Ahsante sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ahsante kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, ajiandae Mheshimiwa Clayton Revocatus Chipando.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kutoa mchango wangu kwenye bajeti ya Wizara hii. Nianze kwanza kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuwa mwanamichezo namba moja na kwa kuwa katika hii Awamu ya Sita kwa kweli tumeona mafanikio makubwa sana katika sekta zote za michezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee nimpongeze sana Waziri mwenye dhamana ya michezo ndugu yangu Mheshimiwa Paul Christian Makonda kwa kazi kubwa na nzuri sana ambayo anaifanya yeye pamoja na Naibu Waziri, ndugu yangu Mheshimiwa Hamis Mwinjuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu yetu Mheshimiwa Makonda kwa kweli amefanya kazi kubwa, hata utambulisho wa leo wa wageni waliongia ndani ya Bunge unaweza ukatoa ushuhuda kwamba angalau kwa kiasi kikubwa amekusanya sekta zote zinazohusika katika michezo, kwa maana ya kwamba anatambua. Mimi ninavyomfahamu ni mtu wa mambo magumu ambayo wengine wanashindwa, yeye huwa anayamudu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaamini kuwepo kwake katika Wizara hii ni jambo ambalo Mheshimiwa Rais amemwona kwa jicho la kipekee. Tunaamini Wizara hii inahitaji sana ushirikishwaji wa sekta binafsi na leo pia, amewatambua wadau kadhaa wa sekta binafsi ambao wako ndani ya jengo hili. Ninamwomba Waziri aendelee kutoa ushirikiano, hata hizi *arena* anazozungumza Mheshimiwa Babu Tale ninaamini kwamba, Sekta Binafsi ikishikirishwa inavyopaswa wanaweza wakajenga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo kuna wenzetu wa sanaa, hasa hizi za uchongaji wa vinyago, ususi na kadhalika, ninatamani na wenyewe mwakani tuwaone wakiwa humu ndani. Hata wale Wasukuma wanaocheza ile michezo ya kuchezea chatu, siyo vibaya na wenyewe pia, wakawakumbuka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nielekee sasa kwenye Mashindano ya *AFCON* kwa Mwaka wa 2027. Ninatambua jitihada za Serikali katika maandalizi ya michezo ya *AFCON* mwakani, lakini pamoja na maelezo ya Mheshimiwa Waziri wakati anasoma hotuba yake, bado ninataka kuiona Serikali ikiwa pamoja katika jambo hili. Jambo hili siyo la Wizara ya Michezo pekee, jambo hili linaihusu Serikali yote kwa ujumla wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatambua Mheshimiwa Waziri Mkuu ofisi yake ndiyo inayoratibu, lakini ninatamani kuona kwenye kila Wizara tutakayopitisha bajeti yake hapa, angalau kwa kiwango fulani, tuone *component* inayotaja *AFCON*. Haitapendeza huko mbele ya safari Wizara zikianza kuambiwa ziwajibike pale, watasema hawana kifungu. Kwa hiyo, ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, hili jambo libebwe na Serikali kwa umoja wake, kwa ujumla wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa kuna Sekta ya Utalii, itahusika kwa kiwango kikubwa. Wizara ya Mambo ya Ndani, hawa ndiyo wanaotoa vibali vya watu wa Uhamiaji. Tusingependa kuona wageni wanakuja kwenye nchi yetu wananza kuambiwa *deferred Visa* miezi miwili, mitatu kabla, hiyo haiwezekani. Hapa tunatengeneza utalii, lakini tunatengeneza jambo lenye heshima

kwa nchi kwa hiyo, watu wa Uhamiaji waandaliwe kisaikolojia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Maji, Ndugu yangu Mheshimiwa Aweso yuko hapa, tusingetamani kuona wakati ule kuna kiangazi wanaanza kutupa hadithi, maji na yenyewe yapatikane wakati wote wa michezo hii. TAMISEMI, Uchukuzi na Nishati, wote hawa ni wadau muhimu katika eneo hili kwa hiyo, tunaomba, Serikali, tushikane kwa pamoja tuhakikishe kwamba, michezo hii inafanikiwa. Ninamwomba Mheshimiwa Waziri, sisi hapa Tanzania tumeandaa Mashindano ya *African Football League,* ambayo Mwaka 2023 yalizinduliwa hapa katika Uwanja wa Benjamin Mkapa Dar es Salaam, Simba akicheza dhidi ya Klabu ya Al Ahly.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwaka 2024 tukaandaa tena Mashindano ya *CHAN*, ambayo ufunguzi umefanyika katika nchi yetu. Ninamwomba Waziri kwa ushawishi wake, kwa mikakati yako, ahakikishe kwamba, Mungu anapojalia *AFCON* fainali ichezwe katika Nchi yetu ya Tanzania. Hapa tutahakikisha kwamba, tunapata wageni mashuhuri, wachezaji wakubwa wote watakuja ile siku ya fainali, lakini pia, itakuwa *motivation* kwa timu yetu ya Taifa kuhakikisha kwamba, katika hatua za awali inapambana hadi kufika ngazi hiyo ya fainali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni kuhusu utamaduni. Nimemsikia Mheshimiwa Waziri jana akiwa na watu, watengeneza maudhui, amezungumza vizuri sana namna ya kulinda utamaduni wetu. Kupitia Mfuko uleule wa utamaduni, ni vizuri pia, akaziwezesha *media* zetu, kama *AZAM, TBC, Channel 10* na zenyewe pia, ziweze kununua maudhui ya hawa wasanii ambao wanayatengeneza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona watengeneza filamu, tumewawekea kwenye Mfuko wa Filamu. Wanaweza wakapata fedha, kwa ajili ya kukopeshwa kutengeneza maudhui. Wakitengeneza haya maudhui wanamuuzia nani? Sasa hivi soko limejifunga, mnunuzi ni mmoja peke yake. Kwa hiyo, ni busara pia, tuwezeshe hivi vyombo vingine vya habari viweze kushindana

katika kununua maudhui, ili watu hawa waweze kupata pesa ya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana kulikuwa na Mechi ya Ligi Kuu ya Soka Tanzania Bara. Kwa kweli, tunafarijika kuona kwamba, sasa ma-*referees* kutoka nje wanatenda haki na mchezo unaonekana, yale mambo ya mbeleko hayapo. Jana limefungwa goli bora kabisa ambalo, kama siyo *AZAM TV* kuwepo hewani, sijui kama miaka ijayo tungewezaje kushuhudia goli la kisasa namna ile. *(Makofi)*

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shangazi, kuna Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Joseph Musukuma.

**TAARIFA**

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza sana mzungumzaji, anazungumza vizuri, lakini nataka kumwambia kwa faida ya wengi aende akaangalie kwenye *television* leo mchana, akiwa amepumzika vizuri. Lile goli analolisema bora ni *clear offside*. Ahsante. *(Kicheko/Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shangazi, unaipokea Taarifa hiyo?

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa hiyo ninaipokea. Ndiyo maana ninawapongeza *AZAM TV* kwa sababu, lile goli lingefungwa bila kuwepo kwa *TV* hata Mheshimiwa Musukuma sijui siku za usoni angekuja kuwahadithia nini wananchi wake? *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana, tumekuwa na utamaduni wa kutoa uraia kwa watu ambao wala hawana sifa, lakini huyu aliyefunga goli jana, kwanza anajua kuongea Kiswahili

vizuri. Ameshaisaidia Simba kwenda robo fainali mara mbili kupitia miguu yake. Hawa ndiyo aina ya watu ambao wanapaswa kupewa uraia wa heshima katika Taifa letu. Siyo tunawapa uraia watu ambao wakiingia dakika tano wanacheza *foul* wanatolewa nje… *(Makofi)*

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na ninaunga mkono hoja. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shangazi muda wake umekwisha. Tunakushukuru kwa mchango wako.

Nilimtaja Mheshimiwa Clayton Revocatus Chipando. Ajiandae Mheshimiwa Festo Richard Sanga.

**MHE. CLAYTON R. CHIPANDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika Wizara hii, ambayo inahusiana kabisa na kazi niliyokuwa ninaifanya kabla sijawa Mbunge wa Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa ninaomba kuwapongeza viongozi wote ambao wanaiongoza Wizara hii, akiwemo Waziri, Ndugu yangu, Mheshimiwa Paul Makonda. Sina mashaka hata kidogo na uwezo wa Mheshimiwa Paul Makonda na ninampongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kumpa nafasi katika Wizara hii inayohusiana na michezo kwa sababu, michezo anaijua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina uhakika 100%, Wizara hii ndiyo itakuwa Wizara bora kuliko Wizara zote ambazo zimetangulia huko nyuma. Kiongozi huyu, Waziri huyu, Mheshimiwa Paul Makonda, anakwenda kufanya maajabu katika nchi yetu ya

Tanzania. Yapo mambo machache, ambayo na mimi nitampa, ili aendenayo yaweze kusaidia na kuboresha kazi anayoenda kuifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza ni, kuhusiana na muziki na wasanii. Wasanii wa Nchi hii ya Tanzania wanakusanya pesa kidogo sana za mirabaha kuliko zile ambazo wanastahili kupata. Sehemu nyingi ambazo wanapaswa kupata pesa hawazipati kwa sababu, Wizara kupitia watu ambao wanafanya makusanyo hawayafikii hayo maeneo na zile pesa zinapotea bure. Hii imesababisha wasanii wamekuwa na hali mbaya sana kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii, ninakwambia tu Mheshimiwa Waziri, ametangaza mikopo kwa wasanii. Ukienda kuchungulia pale utagundua kuna wasanii wengi alitegemea wataenda kuchukua mikopo, lakini wamekosa kwa sababu, baadhi ya vigezo wameshindwa kuvitimiza, ikiwemo nyumba. Mimi nimepata shilingi milioni 200, lakini nimeweka ghorofa langu. *(Makofi)*

**MHE. KHADIJA S. TAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Clayton Chipando, kuna Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Khadija Taya.

**TAARIFA**

**MHE. KHADIJA S. TAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nimpe Taarifa mzungumzaji kwa ushahidi kabisa, hata mimi kwa muda wote niliokaa hapa Bungeni sijapokea mrabaha wangu, kwa hiyo, anachokizungumza ni sahihi kabisa. Tunaomba Mheshimiwa Waziri asisitize hilo katika bajeti hii. Ninashukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. CLAYTON R. CHIPANDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, unilindie muda.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Clayton Chipando, unaipokea Taarifa hiyo?

**MHE. CLAYTON R. CHIPANDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeipokea Taarifa ya dada yangu, Mheshimiwa Keisha. Tunapokuwa tunatetea haki na pesa za wasanii kwa pamoja tunakuwa tunapiga *collabo*. Siyo mbaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wasanii wa nchi hii walipaswa kuwa matajiri sana kwa sababu, Kiswahili kinasikika sehemu nyingi sasa hivi duniani. Ukiangalia kiuhalisia sehemu nyingi ambazo walipaswa kupata pesa maskini ya Mungu, hawapati pesa zao na hicho kidogo kinacholetwa namna kinavyokatwakatwa! Maana ninasikia sasa hivi hawakusanyi tena wale Maafisa wa Serikali, kuna wakala ambaye anakusanya, naye anakata *percent* yake, kisha analeta Serikalini. Baada ya hapo, kidogo kinachogawiwa kwa wasanii hawa wanashindwa kujikimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana vigezo vilivyowekwa na benki vimeshindwa kuwapa nafasi wao kuweza kukopa. Ninaomba sana Mheshimiwa Waziri akipata muda kaa na wale *top five* au *top 10* wasanii wa Nchi hii ya Tanzania; 100% wamesaini mikataba ya kujilipua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikataba yao hata ukitokea ugomvi kati yao wao na yule mtu, ambaye wamesaini naye, hauwezi kuuingilia hapa Tanzania, inabidi uende *Mauritius*. Wamejilipua, wamewekewa sharti gumu, wakawekewa hela mbele, wamesaini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ikitokea mgogoro kati ya msanii na mtu anayesambaza ngoma na nyimbo zao, wamekubaliana kwamba, ugomvi huo uende ukaamuliwe *Mauritius*. Tanzania utapita juu juu, utaangalia, lakini hautaugusa huo mkataba kwa hiyo, akae nao wote, wasanii wote *top 10*, ninadhani anawajua; akina Diamond Platinums, Ali Kiba, Harmonize, nani! Kaanao watampa hiyo siri. Ninaomba akae nao aone namna ya kuweza kuwasaidia wasanii wetu, ili waache.

Unakuta msanii anaombaomba wakati walikuwa na nafasi ya kuweza kupata pesa nyingi katika nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine nimeona katika bajeti hii wamegusia suala la singeli. Ni kweli, watu wengi tulikuwa tunaona Singeli ni kama mziki wa kihuni hivi, lakini kiuhalisia kwenye nchi yoyote ikilia Singeli unaiona Tanzania, kwa hiyo, tumegoma. Mwisho wa siku tukubaliane kwamba, Singeli inaenda kututambulisha kama muziki wetu Watanzania, Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, nimeona bajeti imeombwa hapa, zaidi ya shilingi bilioni 500 na kitu. Pesa nyingi ninaona zinawekwa kwenye kutengeneza barabara, viwanja, kuweka mazingira mazuri; tunashukuru sana, lakini ninataka nimwambie Mheshimiwa Waziri kwamba, viwanja havichezi pale ndani. Kama hatutawekeza kwenye Timu ya Taifa na tukapeleka wazee walewale, itakuwa ndiyo aibu ya kwanza kukutananayo katika mechi ya kwanza ya ufunguzi na Rais yuko pale tunapigwa tatu, hata refa abebeje hawezi kutupa penati tatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninataka kumpa ushauri Mheshimiwa Waziri. Bado muda tunao, twende tutafute vijana, hata akitaka sisi hapa tuko, Wabunge wenzake, tutamsaidia kwenye *angle* moja. Tupe kazi kila Mbunge kwenye jimbo lake amletee vijana wawili kiboko kabisa, awakusanye pale Dar es Salaam. Tuko Wabunge hapa zaidi ya 270 na kitu, tukimletea vijana wawili au watatu atapata vijana 800. Mwambie Mzee Gamondi, kama yupo! *Where is Mr. Gamondi*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, angenisikia na yeye. Wakusanyie vijana 800 pale, amwambie katika hawa vijana 800 ambao nimewaleta kutoka kwenye kila jimbo, ninaomba upate wachezaji 25 ambao wataenda kushambulia pale. Vinginevyo, akipeleka wazee ndiyo ataona namna ambavyo anakwenda kupata aibu mbele ya Mheshimiwa Rais, ndugu yangu. Mimi Waziri ni jamaa yangu, lazima nisimame naye kwa hiyo, tutaaibika wote pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshauri Waziri tutafute vijana katika shule, tutafute vijana katika majimbo. Sisi Wabunge kariziki kapo kidogo, tunao uwezo wa kumsaidia hata kuwasafirisha hao vijana kwa pesa zetu tuwalete Dar es Salaam, wakusanyike pale awachuje. Lazima atushirikishe sisi kwa sababu, akiwapa Maafisa Michezo wataona dili limeingia kwenye kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Wabunge tunapenda sifa, kwa hiyo, lazima tutamletea watu ambao watatuletea sifa kwenye majimbo yetu. Atupe nafasi tumsaidie, hii kazi haiwezi yeye mwenyewe ndugu yangu. Atupe nafasi tumsaidie tupate timu yenye vijana. Akipeleka wazee akili inataka kupiga, mwili unakataa kabisa, viungo vimeshaenda, viungo viko *old*. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua mataifa mengine wanakuja hapa wana hasira, hawatatuhurumia eti kwa sababu, sisi ndiyo tumeandaa haya mashindano. Tutapigwa kama ng'ombe na mimi hiyo sitakubali na itazidi kutupa ugumu sisi ambao tunahamasisha wananchi waende wakaishabikie Timu ya Taifa. Tusifikiri watu hawaipendi Timu ya Taifa, ila wanaogopa vipigo. Wakienda pale wanaona kabisa yaani ninaenda kushabikia, lakini kipigo nitakachokutana nacho kitanirudisha na uchungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Muda wako umekwisha.

**MHE. CLAYTON R. CHIPANDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *yes*. Dakika moja ya mwisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, ninaunga mkono hoja. Ninaomba tuwape hela hawa mabwana tuwapime. Huu ni mwaka wao wa kwanza. Mimi na Mheshimiwa Makonda ni wapya katika Bunge hili, hebu tumwone makeke yake. Nina

uhakika kwa 100% hata angekuwa Diwani huyu bwana angeng'ara hivihivi kwa sababu, uwezo…

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako.

**MHE. CLAYTON R. CHIPANDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nilimtaja Mheshimiwa Festo Richard Sanga. Tutamalizia na Mheshimiwa Dkt. Christina Christopher Mnzava.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Jambo la kwanza, ninapenda kuipongeza Wizara pamoja na kamati kwa maoni na bajeti ambayo wameisoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza Waziri, kaka yangu Mheshimiwa Paul Christian Makonda, kwa kazi kubwa anayoifanya, lakini pia, Binamu, Mwana-FA ninampongeza kwa kazi kubwa, ambayo wanaifanya. *Home boy,* ndugu yangu, Katibu Mkuu wa Wizara ya Michezo, Gerson Msigwa, pia, ninawapongeza kwa kazi ambayo wammeifanya kuhakikisha kwamba, Wizara inaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunazungumza bajeti ya michezo, ambayo inaenda kwenye shilingi bilioni 525 kama sikosei. Wakati ninaingia hapa Mwaka 2020 bajeti ilikuwa shilingi bilioni 35 tu, shilingi bilioni 32 tena na pointi. Tafsiri yake ni kwamba, kuna *revolution*, kuna mapinduzi kwenye michezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ambaye amekuwa ni mdau namba moja kwenye ku-*support*, kuunga mkono, sekta ya michezo. Hii tunaiona kabisa Mheshimiwa Waziri, ni moja kati ya Wizara ambazo sasa wanaingia kwenye rekodi. Hela ya maendeleo ni kubwa kuliko hela ya matumizi. Ninampongeza sana Mheshimiwa Makonda, kwamba, hili linaonesha wao wamejikita kwenye kazi na wanakwenda kulifanya hili jambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuna mashaka na Mheshimiwa Makonda kwa sababu, amejibainisha kwamba, ni Waziri ambaye hapendi tu kusifiwa. Yaani hata kama watu wanamchukia, aache wamchukie, lakini anasimamia msimamo wake. Kwa hiyo, tunaamini hata kwenye hili la michezo watu watamchukia, watu watamfurahia, lakini yeye asonge mbele, kwa ajili ya maslahi mapana ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza kubwa ambalo ninatamani kuchangia ni kwenye suala la *AFCON*. Tunajiandaa na *AFCON,* lakini suala la *AFCON* Mwaka 2027, Waheshimiwa Wabunge, hili jambo siyo la Wizara ya Michezo peke yake, hili ni suala ambalo linahusisha Wizara zote. Linahusisha Wizara ya TAMISEMI, linahusisha Wizara ya Maliasili, linahusisha Wizara ya *TANESCO* kwa maana ya Nishati, Wizara tofauti tofauti. Tusiache msalaba huu, tukamwachia Mheshimiwa Makonda peke yake, tutaaibika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, atajenga viwanja, lakini kama barabara hazipitiki kuelekea kwenye hayo maeneo tutakuwa tumemkwamisha Mheshimiwa Makonda, tutakuwa tumekwamisha nchi, tutatukuwa tumekwamisha Serikali yetu. Kwa hiyo, ninawaomba Mawaziri wote wanaohusika na sekta mbalimbali tuifanikishe *AFCON* kuleta heshima ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais ametoa fedha nyingi sana kulipia hili jambo. Lazima kila Waziri aone huu ni mzigo wake, siyo mzigo wa Mheshimiwa Makonda peke yake kwa sababu, tukiacha Sekta ya Michezo peke yake, kuna wagonjwa watatokea, lazima hospitali ziwe bora, kwa hiyo, lazima Sekta ya Wizara ya Afya iingie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili ni, tunahitaji pia, utalii kuanzia *airport* kwa madereva *taxi* na maeneo yote ya hoteli kuwe na *diplomatic hospitality* kwa wageni ambao watakuja kwenye *AFCON*. Haya tunatamani Wizara zote ziweze kuhusika. Hilo ninatamani sana Mheshimiwa Waziri afanye namna jinsi ya kuendelea kuongea na Wizara nyingine, ili waweze kulifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine Mheshimiwa Waziri ninataka kumshauri ni, yeye ni mdau wa vijana, ni mdau wa maendeleo ya michezo. Ninatamani Wizara yake waanzishe Mfuko wa Vifaa vya Michezo Shuleni, Mfuko wa Vifaa vya Michezo Shuleni. Sisi hapa Wabunge karibu kila sekondari, kila shule ya msingi, wanatuomba vifaa vya michezo. Aandike historia, waanzishe Mfuko, hii fedha ni ndogo sana kuhakikisha kila shule ya msingi, kila sekondari ina vifaa vya michezo, ina mipira, ina jezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii inaweza kugawa bure sekondari zote za Serikali wakaondoa mzigo ambao, sisi kama Wabunge, tumekuwa tunaupata. Hiyo hoja Mheshimiwa Waziri akiisimamia atafanya mabadiliko ya ajabu sana kwenye michezo kwa sababu, kuna vijana wako shule za msingi hawajawahi kuona kiatu, hajawahi kuona mpira. Mheshimiwa Makonda afanye hayo mabadiliko kwake, kama Waziri. Ninamshauri kwamba, aweke Mfuko wa Maendeleo ya Vifaa vya Michezo Shuleni; shule za msingi na sekondari, ili watoto wetu kila mwaka wapewe vifaa kutoka Wizara ya Michezo, kwa ajili ya maendeleo ya michezo shule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ninataka kumuunga mkono Mheshimiwa Waziri ni kwenye *media,* habari. Jana nimeona akizungumza na Watanzania, lazima tukubaliane, tunapojenga nchi yetu kuna mambo lazima tuweke uelekeo wa pamoja. Waziri ameonesha uelekeo, *content creators*, waandishi wa habari ndiyo wanahitaji uhuru wa habari kwenye nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli wanahitaji wafanye mazingira salama, lakini maudhui wanayotengeneza yasiende kupotosha maadili ya nchi yetu, lazima kama nchi tukatae kabisa moja kwa moja. Mheshimiwa Waziri, kuna *content creators*, kuna waandishi wa habari, kuna watu maarufu, wanapotosha maadili na utamaduni wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunamwomba Waziri, kama ambavyo wamefanya kwenye ithibati kuchuja ambao hawana *standards* za uandishi wa habari, twende tukasimamie hili kwa pamoja. Tusimwachie Mheshimiwa Mama Gwajima peke yake,

mtu wa Maendeleo ya Jamii. Kwa watu ambao kwa sababu tu ya umaarufu, nenda Rwanda pale, huwezi kupata umaarufu wa kijingajinga, lazima upate umaarufu kwa kitu bora unachokifanya kwenye Taifa lako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapata umaarufu kwa kutangaza vitendo vya hovyo na vya ajabu ambavyo vinavunja maadili yetu! Tunamwomba Waziri alisimamie hilo, lakini siyo wewe tu pamoja na Jeshi la Polisi kwa maana ya Wizara ya Mambo ya Ndani lazima ikuunge mkono, tunapokwenda kwenye *ultimatum* ya maadili ya nchi lazima Watanzania tukubaliane, siyo suala la kwamba Waziri anabana, mbona anatuingilia! Hakuna wa kukuingilia kwenye suala la maadili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la maadili ni mustakabali wa nchi, suala la maadili ni usalama wa nchi, suala la maadili ni suala ambalo linahusisha Taifa letu miaka 30, miaka 100 ijayo, hili siyo suala la kwamba aaah Waziri anatuingilia, hakuna. Mheshimiwa Waziri, asonge mbele, awabane kadri anavyoweza kuwabana. Watu wa *TCRA*, watu wa Polisi wafanye kazi kuhakikisha kwamba tunalinda heshima ya nchi yetu. *Content* tunazozalisha kwenye jamii ziwe ni *content* zenye maadili na zinazobeba sifa la Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, ninamwomba na ninamsihi, amelizungumza Babu Tale ni suala la *arena*. Ukisoma kwenye Ilani ya CCM wanasema, katika kukuza na kuendeleza sanaa za michezo nchini, Serikali ya CCM itachukua hatua zifuatazo, namba 11 inasema, kujenga kituo kikubwa cha burudani kwa ajili ya maonesho ya kazi za sanaa na burudani nyingine za kitaifa na kimataifa. Mheshimiwa Waziri, anaweza kukubali kwamba, mkono wa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan ni mkono wa baraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepata hapa maandalizi ya ma-*Miss* Tanzania tunaenda kufanya, tumepata hapa, tunaona *basketball* inakua, tunaona *football* inakua, tunaona riadha inakua, tunaona muziki unakua, lazima tuwe na *arena*. Mheshimiwa Waziri, hatuna *option* nyingine lazima tuwe na

ukumbi mkubwa, ambao *arena* si tu, tunaangalia katika kufanikisha hayo matukio bali tunaangalia katika kukusanya mapato na katika kutangaza utalii wa nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ukienda *Kigali arena* watu jinsi ambavyo kila mara matukio yanafanyika ni vyema nchi yetu ikaenda kwenye hili jambo. Nimhakikishie Waziri kwamba, akilifanya hili ataleta heshima kwenye Taifa, ataleta heshima kwa Serikali ya Chama Cha Mapinduzi na zaidi utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi kama ambavyo imeahidi kwa wananchi lazima tuwe na *arena* na lazima tulisimamie hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Christian Paul Makonda, nikutakie kila la heri, lakini zaidi kuna maslahi ya wachezaji, lazima kama Serikali imetangaza kima cha chini cha mishahara ya wafanyakazi, kwa mfano kwenye *football* wachezaji wengi wana changamoto ya maslahi, mishahara yao ni midogo, lazima tu-*set standard* kwamba kwa *level* hii tuliyoifikia, ndani ya ligi kuu kuna watu wanapokea shilingi milioni 80, kuna watu wanapokea shilingi milioni 50 na ndani ya ligi kuu kuna watu wanapokea shilingi laki tatu, laki mbili, laki nne na milioni moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tu-*set standard* ya mishahara angalau kuanzia kima fulani kwenda juu ili kuzuia rushwa, lakini pia upangaji wa matokeo. Kwa hiyo, ni vyema tukalisimamia hilo ili kuleta usawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho na zaidi nikutakie kila la heri, ninaiunga mkono bajeti, ninawatakia kila la heri kama mwanamichezo na niwaambie Watanzania michezo ni *passion*, michezo ni *passion* siyo kila mmoja anaweza kuwa mwanamichezo. Mwanamichezo namba moja Tanzania mwenye *passion* ni Dkt. Samia Suluhu Hassan, tumeona akifanya kwenye *football*, tumeona akifanya kwenye ngumi, tumeona akifanya kwenye ma-*miss* kila eneo, basi tuwaunge mkono bajeti hii iweze kufanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Nilimtaja mchangiaji wa mwisho kwa mchana wa leo ambaye ni Mheshimiwa Dkt. Christina Christopher Mnzava.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili kuweza kuchangia katika Wizara hii ambayo ni Wizara muhimu sana kwa burudani, lakini kwa kujenga afya zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa kibali cha kusimama na kuchangia, lakini pia ninampongeza sana Dkt. Samia Suluhu Hassan, kinara namba moja wa michezo Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini ninasema ni kinara namba moja? Ukiangalia kwenye Ilani ya Chama Cha Mapinduzi, michezo imepewa kipaumbele, lakini haitoshi Dkt. Samia Suluhu Hassan, ameweza kutoa fedha zaidi ya shilingi trilioni 1.2 kwa ajili ya uwezeshaji wa timu za Taifa, lakini ujenzi wa miundombinu pamoja na uwekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Dkt. Samia Suluhu Hassan, amedhamiria kuwekeza katika michezo. Ukiangalia tuna mashindano ya *AFCON* kila mtu anayaongelea na kila Mtanzania anatamani tuweze kufanikisha kwa kiwango kikubwa. Tumeona viwanja ambavyo vinajengwa, Arusha kiwanja kinajengwa, Dar es Salaam viwanja vinakarabatiwa, Dodoma kuna uwanja unajengwa lakini kuna viwanja 11 ambavyo vitakuwa ni viwanja vya mazoezi. Arusha vipo vitano, Dar es Salaam vipo sita na vyote vipo katika hatua mbalimbali ya kukamilisha, hiyo yote ni dhamira safi ya kuhakikisha kwamba Tanzania inashiriki kikamilifu mashindano ya *AFCON*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyotangulia kusema msemaji aliyetangulia, pamoja na kwamba jukumu hili ni la Wizara ya Sanaa, Utamaduni na Michezo, lakini ninaona jukumu hili ni mtambuka. Kuna barabara ambazo zitapitiwa kutoka eneo moja kwenda uwanjani. Mfano kwa Arusha, kwa *plan* iliyopo tunaona kuna barabara kama nne za kuingia na kutoka katika ule uwanja.

Mheshimiwa Waziri, anapokuja kuhitimisha nitapenda kujua ni hatua gani ambazo zimekwisha kufikiwa kuhusu miundombinu ya pale Arusha ili kuwezesha ule uwanja kuwa katika hali ambayo tunaitarajia, ni hatua gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, fedha zimetoka au wana utaratibu gani, wanao mpango gani kuhakikisha kwamba inapofika uwanja unakabidhiwa miundombinu yote ile ambayo ipo kwenye ramani imeweza kukamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo haitoshi, tunajua Watanzania wengi tunapenda *football*, mimi mwenyewe ninapenda *football*, tumeona juzi kwenye mashindano ya Muungano vijana wetu wa Simba, walivyotufurahisha wakatufuta machozi, lakini tumeona jinsi ambavyo tunahitaji matumizi ya *VAR* ili huu udanganyifu unaofanyika fanyika mara nyingi huu wa wapinzani wetu kupata magoli ambayo hawakustahili kuyapata uweze kwisha. Katika viwanja vinavyojengwa ninaamini *VAR* itakuwepo kwa sababu ni viwanja vya kimataifa ni viwanja ambavyo vinakidhi matakwa ya kimataifa ya *FIFA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na *football,* lakini tuna *basket*, tuna riadha tunafanya vizuri, kuna walimbwende tumeona Tanzania imesaini mkataba kwamba wataandaa mashindano miaka mitatu mfululizo ya walimbwende. Hii ni fursa kwetu ya kiuchumi, hii ni fursa kwetu ya uwekezaji lakini haitoshi tunahitaji kuwa na viwanja vingi zaidi. Mbali na *football* lakini tunahitaji kuwa na viwanja vya *netball*, tunahitaji kuwa na viwanja vya *basket*, tunahitaji kuwa na viwanja vya riadha vizuri vya kisasa, hii yote itakamilika iwapo Ilani ya Chama Cha Mapinduzi itakapotekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona kwenye Ilani kuna ujenzi wa *arena*...

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mweyekiti, Taarifa.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *arena* ni muhimu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava, kuna taarifa kutoka kwa Profesa Shemdoe.

**TAARIFA**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kumpa taarifa Mheshimiwa Mbunge kwamba, kule Arusha ambako ametaja, tumesaini mikataba ya barabara nne zinazoelekea kwenye uwanja mkubwa wa *AFCON*. Ujenzi wa barabara zile *mobilization* imeshaanza kufanyika. Kwa hiyo tuna uhakika wa 100% kwamba mpaka mwezi Aprili mwakani barabara hizi zitakuwa zimekamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kutoa taarifa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava, unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipokea taarifa hiyo na ninafarijika sana kuona kwamba Serikali yetu ni sikivu, yale ambayo tunayashauri yanatekelezwa kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kwenye suala zima la *arena* tunahitaji kuwa na uwanja, tunahitaji kuwa na *arena* kubwa ya kimataifa. Tukiangalia wenzetu majirani zetu *South Africa*, mimi ni mdau wa *basket*, mimi ni mdau wa *netball*, ni mdau wa *golf*. Tulikwenda South Africa baadhi ya Wajumbe hapa wa Kamati ya Utamaduni na Michezo, tumeona jinsi ambavyo wamewekeza, tumeona jinsi ambavyo wanaingiza mapato kwenye michezo hasa *basket*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mwekezaji Tanzania mwenye *Dar City* amejitolea kuwekeza mamilioni ya fedha, amesajili wachezaji kutoka nje, amepeleka timu kwa mara ya kwanza

kwenye mashindano ya Afrika na timu yetu ya *Dar City*, imefuzu kwenda kwenye hatua nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatakiwa sisi kama Watanzania, wao kama Serikali wahakikishe wanawatia moyo wawekezaji kwa kuwajengea viwanja vyenye hadhi. Tunawatia moyo wawekezaji kwa kujenga *arena*, tutaingiza mapato, lakini tutahamasisha, tukumbuke kwamba vijana wengi wanapenda *football*, wanapenda *basket*. Michezo ni ajira, michezo ni afya, michezo ni burudani, tukiwekeza katika *arena* kama walivyofanya wenzetu wa Rwanda ni hakika kabisa *basketball* itakua, ni hakika kabisa michezo mingi itapata wafuasi wengi, tutapata wachezaji wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba anapokuja ku-*wind up* Waziri, atueleze mpango ambao umeshafikiwa au mpango ambao upo wa kuhakikisha kwamba Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya kujenga *arena* unafanikiwa. Wapo kwenye hatua zipi, wana mpango gani, watajenga lini, nini kimefanyika, ninafikiri wakinipa hayo majibu tutakuwa tumekosha mioyo ya Watanzania ambao wanapenda michezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho siyo kwa umuhimu, ninampongeza sana Waziri kwa ubunifu, kuleta wachezaji wa kimataifa, tulikuwa tunamwona mchezaji Drogba, kutoka nje tunamwona kwenye *TV*, leo tunamwona *live,* tuna-*shake hands*. Tumewaona wachezaji wengi ambao wamefanya vizuri, walioshindana kwenye riadha, lakini kuna ma-*miss* wapo hapa, hii yote ni kutufanya Watanzania ambao sisi Wabunge tunawawakilisha, kwamba, tupo karibu na wanamichezo ambao wanatuwakilisha kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana kaka yangu, Makonda pamoja na Mwinjuma aendelee kuchapa kazi. Watendaji wa Wizara hii kwa kweli wanafanya kazi nzuri. Ninaomba jambo moja la mwisho, tunafanya mambo mazuri na kwa sababu sekta hii ina mambo ya habari, watangaze mazuri ambayo yanafanyika, viwanja vinajengwa, mambo mazuri yanafanyika.

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa mchango wako Mheshimiwa, muda wako umekwisha.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo mazuri yanafanyika, tunaomba watangaze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa uchangiaji kwa mchana wa leo na watakaoanza kuchangia jioni atakuwa ni Mheshimiwa Suleiman Mohamed Rashid, Mheshimiwa Zainab Abdallah Issa, Mheshimiwa Kijakazi Yunus Mohamed na orodha itaendelea.

Waheshimiwa Wabunge, naomba nilete kwenu matangazo ya wageni waliopo Bungeni. Tunaanza na wageni wa Mheshimiwa Waziri Mkuu, ambao ni Walimu 150 wa shule za Sekondari za Amali nchini walioshiriki mafunzo ya kujifunza ujuzi wa kidijitali nchini India. Karibuni sana Walimu na hongera kwa kuhitimu mafunzo hayo, nina imani itakuwa tija kwa wanafunzi wetu hapa nchini. *(Makofi)*

Wapo pia wageni wengine wa Mheshimiwa Paul Christian Makonda, Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo ambao ni Waandishi wa Habari na wachambuzi wa michezo. Wapo pia viongozi wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania *(TFF)* na Shirikisho la Riadha Tanzania. Karibuni. *(Makofi)*

Wapo Mameneja wa Mabondia na Viongozi wa Kamisheni ya Kusimamia Ngumi za Kulipwa Tanzania. Karibuni sana wageni wetu wote mliotembelea Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri wetu Paul Christian Makonda, anaomba Wabunge ambao mtapenda kupiga picha na mgeni wetu basi tukutane pale nje.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema haya, ninasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja jioni.

*(Saa 7.12 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)*

*Mwenyekiti (Mhe. Deodatus P. Mwanyika) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae.
Katibu.

**NDG. MICHAEL CHIKOKOTO, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea sasa na majadiliano. Nimwite sasa, Mheshimiwa Suleiman Mohamed Rashid, atafuatiwa na Mheshimiwa Zainab Abdallah Issa na Mheshimiwa Kijakazi Yunus Mohamed ajiandae.

**MHE. SULEIMAN MOHAMED RASHID:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi jioni ya leo kwa mchangiaji namba moja wa Wizara hii ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, niungane na wenzangu walionitangulia kwa kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii, Mheshimiwa Naibu Waziri, kaka yangu Hamis Mohamed Mwijuma, Katibu Mkuu, pamoja na watendaji wote wa Wizara hii ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo. Kipekee niendelee kuwashukuru sana wadau mbalimbali wa sekta ya habari, sekta ya michezo, sekta ya sanaa pamoja na sekta ya utamaduni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnamo tarehe 27 Septemba, 2023, Mkutano Mkuu wa Chama cha Mpira Afrika uliofanya mkutano wake jijini Cairo Nchini Misri, ulithibitisha na kuidhinisha kwamba Tanzania atakuwa ni mwenyeji wa mashindano ya *AFCON* yatakayofanyika 2027. Kama hiyo haitoshi mashindano haya ya *AFCON* mwakani yatakuwa ya uhai wa miaka 70, tangu kuasisiwa kwake mwaka 1957, Nchini Sudan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hiyo haitoshi kati ya nchi wanachama 54, ni nchi 18 tu ambazo zimepata fursa ya kuwa wenyeji wa mashindano haya ya *AFCON* tangu kuasisiwa kwake mwaka 1957. Katika hili, niungane na wenzangu waliotangulia kwa kuendelea kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan. Tunapokuwa tunampongeza ni kwa sababu ya utashi wake, kwa yale yote ambayo ameweza kuyafanya ndani ya Taifa letu kwenye sekta hii ya michezo hasa mpira wa miguu ni kumbukumbu tosha, ya kwamba yeye ni mwanamichezo namba moja na yupo tayari kuona matokeo chanya yanaendelea kupatikana ndani ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Mheshimiwa Rais anahutubia Bunge letu hili la Kumi na Tatu, moja ya dhana kubwa ambayo aliweza kuizungumza ni suala la michezo ni uchumi; na hii tunaona katika hotuba yake kwenye ukurasa ya 35. Hivyo ninakiri, kwamba mashindano ya *AFCON* si tu mashindano ya mpira wa miguu, bali ni fursa kubwa ya kiuchumi, kibiashara na maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uchumi kuna dhana inaitwa *multiplier effect,* ambayo inaelezea jinsi ongezeko la matumizi au uwekezaji mmoja unavyoweza kusababisha ongezeko kubwa zaidi la mapato ya shughuli za kiuchumi kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mashindano ya *AFCON* ya 2025 ambayo yaliyofanyika Nchini Morocco, *multiplier effect* ambayo iliweza kupatikana ni 1.82, ikiwa na maana gani? Ikiwa na maana kwamba uwekezaji uliofanywa kwa ajili ya mashindano yale, faida yake ilikuwa ni 82%. Kwa mfano, uwekezaji ambao ulifanyika

dola milioni 100, baada ya mzunguko wote, fedha ambayo ilipatikana ni dola milioni 182, ikiwa na maana dola milioni 82 ni faida ya uwekezaji ule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa tovuti ya *Morocco World News*, faida ya uchumi na biashara kwa Nchi ya Morocco ambayo ilipatikana katika mashindano yale ya *AFCON* ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, mapato ya moja kwa moja yalifikia zaidi ya bilioni ya 1.5 *Euro*. Si hivyo tu, matumizi ya wageni yaliongezeka kwa 190%. Isitoshe, watalii waliweza kuongezeka kati ya 600,000 hadi 1,000,000; pia kuongezeka kwa umaarufu wa soka katika Nchi ya Morocco; na mwisho kuvutia kwa wawekezaji wengi katika sekta mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu, ninataka niweze kuishauri Serikali namna ambavyo tutaendelea kufaidika na mashindano haya ya *AFCON*, mashindano ambayo tumeletewa na Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan, yaweze kuwa na tija ya kifaida na uchumi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu, kwenye suala la miundombinu; ni lazima twende tukaimarishe miundombinu yetu ya viwanja vya mpira na katika hapa sizungumzii viwanja ambavyo vimeteuliwa kwa ajili ya mashindano haya, kwamba ni viwanja vitatu; Dar es Salaam, Arusha na Zanzibar; ninachozungumzia ni namna gani ambavyo tutaweza ku-*host* timu nyingine za ziada ambazo zitakuwa ziko tayari kufunga kambi ndani ya Nchi yetu ya Tanzania. Kadri tutakavyokuwa na viwanja vya kutosha, vyenye hadhi ya *CAF* na *FIFA*, itakuwa ni rahisi kwetu kuweza kuwavutia timu nyingine kufunga kambi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nishauri tu, kupitia balozi zetu tulizoko katika mataifa mbalimbali ya Afrika, tutumie *forum* hili kuweza kuelezea namna ambavyo Taifa letu tumewekeza zaidi kwenye viwanja vingine vya ziada, ambavyo viwe ni chachu ya mataifa mengine kuweza kufika ndani ya nchi yetu, kuweza

kufunga kambi na kujitayarisha na mashindano haya hata kama hawajapangiwa ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nilitaka nishauri ni kwenye kuimarisha sekta ya utalii. Hapa nilitaka nielezee kuweza kuimarisha hadhi za hoteli na pia katika huduma. Ninafahamu miongoni mwa viwango ambavyo tunavitumia, kwamba kila eneo ambalo linachezewa mashindano haya ya *AFCON*, angalau tuwe na hoteli yenye hadhi ya nyota tano, au zaidi ya tano, zaidi ya sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nishauri tutoke nje ya *box;* kadri ambavyo tutakuwa na hoteli nyingi zaidi zenye hadhi ya nyota tano tutakuwa na fursa ya kukaribisha wageni wengi zaidi. Nimetoa takwimu ambazo zinaonyesha namna ambavyo Morocco waliweza kupata wageni wengi zaidi. Kama tutaweza kutumia vizuri fursa hii kuweza kuungana na wadau mbalimbali wa sekta ya utalii, tutaona kwamba maeneo yetu katika nchi yetu yataweza kuimarika na kupata faida kwa wananchi wetu wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye sekta hiyo ya utalii pia kuna suala zima la huduma. Tunapaswa kulazimisha, kwamba ni lazima tuweze kutoa huduma iliyo bora. Tunaweza kuwa na hoteli nzuri, tuna vivutio vizuri, lakini kama tutashindwa kuimarisha utoaji wetu wa huduma ukawa bora yawezekana kwamba mgeni akashindwa kuvutiwa kukaa zaidi Nchini Tanzania kwa sababu ya huduma ambazo zimetolewa. Kwa hiyo nishauri kwamba Serikali ione haja ya kuona wanawekeza na kusimamia katika suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuhusiana na kuwawezesha wafanyabiashara wadogo. Wakati tunachangia hapa Ofisi ya Rais, Maendeleo ya Vijana tulizungumza suala la uwezeshaji. Ipo neema ambayo Mheshimiwa Rais ametuletea kutokana na mashindano haya, tuone namna gani ambavyo tunaweza kuwawezesha vijana wetu, akina mama tuweze kuwawezesha, lakini isitoshe tuweze kuwatengea maeneo maalum ambayo yatakuwa yanatambulikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa wale wageni ambao watapata fursa ya kuja Tanzania kwenye mashindano haya, basi pale ambapo watakuwa wanahitaji bidhaa, wanahitaji huduma, wataweza kujua ni maeneo gani ambayo wataweza kupata huduma hizo. Kwenye hili, vyombo vyetu pamoja na taasisi zetu ziweze kushirikiana namna ambavyo tutaweza ku-*brand* bidhaa zetu. Namna tutakavyo-*brand* bidhaa zetu itasaidia bidhaa zetu kuwa na ubora zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo ninataka nishauri Serikali ni kuhusiana na usafiri. Tunaweza tukafikiria, yawezekana kwamba tuna viwanja ambavyo tumeweza kujenga, lakini kukawa na usumbufu namna ambavyo wapenzi wa mchezo wa mpira wa miguu watakavyoweza kufika katika viwanja hivi. Tutengeneze njia maalum; pia si kutengeneza njia maalum tu, tunaweza pia tukawa na utaratibu maalum wa kuzisimamia njia hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muda ambao mashindano yetu yanapokwenda kuanza kunakuwepo na *escort* maalum ambayo inamwezesha shabiki kutoka sehemu moja kuweza kufika uwanjani kwa urahisi zaidi. Tukiweza kufanya hivyo tutaweza kuonyesha ukarimu wetu kama Watanzania na tutaweza kufaidika kama Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuhusiana na suala la kuboresha taarifa za maeneo. Yapo baadhi ya maeneo yetu ya kimkakati, bado hayasomi kwenye mitandao. Niombe sana Serikali kushirikiana na Wizara husika ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kuona maeneo haya tunaweza tukayasajili. Unaweza ukatumia *Uber* pamoja na mitandao mingine kutafuta eneo, lakini inashindikana ni kwa sababu kwamba maeneo yetu haliwezi kusoma. Kwa hiyo niombe sana Serikali waone haja ya kuimarisha eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye ushauri wangu pia, la mwisho kabisa kwenye suala la ushirikiano. Tumekuwa mashuhuda, mwaka 2022 wakati tunajiandaa na sensa nchi yetu imekuwa ikifanya kazi hiyo kwa ushirikiano wa pande zote mbili,

kwa upande wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, lakini upande pia wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tumekuwa tukishuhudia kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu anakuwa ni Mwenyekiti na Makamu wa Pili anakuwa ni Mwenyekiti Mwenza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna haja kwamba kwenye eneo hili wakati tunajitayarisha na mashindano haya ya *AFCON;* na bahati nzuri moja ya vipaumbele ambavyo ameonyesha Mheshimiwa Waziri kwenye hotuba yake miongoni mwa vipaumbele tisa, kipaumbele namba mbili kilikuwa ni suala hili la mashindano ya *AFCON*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiweza kutengeneza mfumo wa kushirikiana baina ya Serikali zetu hizi mbili, tukawa na utaratibu wa vikao vyetu katika ngazi ya Wizara, ngazi ya Makatibu Wakuu, na pia katika ngazi ya sekta itaweza kusaidia kuweza kufanya maamuzi ya haraka na kuweza kufikia malengo ya *AFCON* haya kama zilivyo ndoto za Mheshimiwa Rais za kuona mashindano kuwa haya yanaleta tija ya kibiashara pamoja na kiuchumi wa Tanzania na kwa wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mwere, mimi naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja juu ya mia moja.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nilimwita Mheshimiwa Zainab Abdallah Issa, Mheshimiwa Kijakazi Yunus Mohamed na Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud wajiandae.

**MHE. ZAINAB ABDALLAH ISSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii kuchangia katika bajeti ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo. Ninaomba nianze na nukuu ambayo ni maarufu kule Spain; wanasema, "*No se acaba hasta que se acaba*" wakimaanisha, "*It's not over until it's over*". Yaani haiishi mpaka iishe na hii inadhihirika kwa viongozi wetu wa Wizara ya Sanaa, Utamaduni na Michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri nimepata heshima ya kufanya kazi na Mheshimiwa Makonda toka akiwa Rais wa

*TAHLISO*, Mheshimiwa Hamis Mwinjuma Mwana FA nikiwa pale Mkuu wa Wilaya Muheza, na kaka yangu Gerson Msigwa toka akiwa habari maelezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka niwaambie ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge na Watanzania, kwanza viongozi hawa ni watu ambao hawakubali kushindwa; lakini pili wakilianza jambo watahakikisha linafika mwisho; tatu na likifika mwisho lazima liwe na matokeo Chanya; nne ni watu ambao hata jambo dogo wanali-*magnify* linakuwa jambo kubwa. Kwa lugha ya Kiingereza tunasema ni *master of branding.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tumeshuhudia Wizara yetu tumeona kwa mara ya kwanza kwenye historia ya Bunge hili kupata ugeni mzito wa nyota nguli wa zamani wa Timu ya Taifa ya Ivory Coast na mchezaji nguli *striker* wa timu ya klabu ya Chelsea, Didier Drogba, ambaye amewahi kupata tuzo ya mchezaji bora Barani Afrika mara mbili, mwaka 2006 na mwaka 2009. Hongera sana kwa Mheshimiwa Waziri na timu nzima ya Wizara, sisi vijana wenzao tunajivunia uchapakazi wao; na tunaamini kupitia safu hii Wizara hii inaenda kuleta mageuzi makubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee nisiwe mchoyo wa fadhila, ninaomba nichukue fursa hii kumshukuru sana sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; kwanza kwa kuendelea kutuamini vijana na kutupa nafasi muhimu za juu kabisa za maamuzi ya Taifa letu. Tunaambiwa vijana ni Taifa la kesho, lakini vijana ni Taifa la leo na tumewaona vijana wenzetu wetu, hii leo wakifanya mambo makubwa na ya kutolewa mfano. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kutuamini vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais, kupitia Wizara hii mwaka 2023, bajeti ya Wizara hii ilikuwa bilioni 35; lakini leo tunaenda kupitisha bajeti ya bilioni 525, ongezeko la zaidi ya 700%. Haijawahi kutokea kwenye historia ya nchi hii. Hakika Mheshimiwa Rais ni mwanamichezo *champion* namba moja kwenye masuala ya sanaa na michezo Nchini Tanzania, tunamshukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unamshukuru pia tMheshimiwa Rais, ninadhani kwenye historia ya Afrika Tanzania ndiyo inakuwa nchi ya kwanza kuanzisha Mfuko wa Sanaa na Utamaduni, kwa mara ya kwanza Afrika tunakuwa na Mfuko huu. Kupitia Mfuko huu tumepata taarifa kupitia bajeti ya Mheshimiwa Makonda hapa, kwamba vijana waliopatiwa mafunzo ni zaidi ya 931 na miradi ambayo imetekelezwa kupitia Mfuko huu ni zaidi ya miradi 724 yenye thamani ya zaidi ya bilioni 12.4. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa mageuzi haya makubwa sana aliyoyafanya ndani ya muda mfupi katika Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa kuliko yote, ndani ya miaka michache ya uongozi wa Dkt. Samia tumefanya marekebisho ya sheria mbili kubwa ambazo zinainua sanaa, vipaji na wabunifu wa Taifa hili. Kwanza Sheria Na.7 ya Mwaka 1999 ambayo imefanyiwa marekebisho mwaka 2022. Sheria inayohusu hakimiliki na hakishiriki ambayo inatoa fursa kuwa *collective management organization (CMOs);* ambapo badala ya ofisi za hakimiliki kukusanya na kugawa mirabaha, sasa hivi kazi hiyo inafanywa na makampuni ya wasanii wenyewe hapa Tanzania. Haya ni mabadiliko makubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumefanya mabadiliko ya sheria ya tano ya fedha ya mwaka 1999, ambayo imefanyiwa marekebisho mwaka 2022; ambayo imeanzisha tozo mpya ya *copyright levy* ambayo ni asilimia 1.5 ambayo inatolewa kwa wale wote wanaoingiza vifaa vya sanaa ndani ya nchi. Fedha hii haijawahi kuwepo huko nyuma, lakini sasa hivi fedha hii inakusanywa na *TRA* na asilimia 60 ya fedha hii inaenda kuwasaidia wasanii na wabunifu wa Taifa hili. Tunashukuru sana Mheshimiwa Rais kwa mabadiliko haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa kubwa kubwa kuliko yote, tunampongeza Mheshimiwa Rais na tumeona Shirikisho la Soka Barani Afrika limempa tuzo ya heshima Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuwa *Champion* wa michezo si tu Tanzania lakini Afrika; na tumepata heshima ya kuwa wenyeji wa *AFCON* mwaka 2027. Tunampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa sababu

hii ni mara ya kwanza kwenye historia ya michuano tangu 1957, sisi Tanzania na wenzetu wa jirani kwa maana ya Kenya na Uganda kuwa wenyeji wa michuano hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, michuano hii mwaka 2019, Egypt baada tu ya michuano hii ya *AFCON* waliweza kuingiza milioni *83 US Dollars.* Mwaka 2021 Cameroon waliweza kuingiza *150 million dollars.* Wenzetu wa Ivory Coast mwaka 2023 waliweza kuingiza *400 million dollars.* Mwaka jana wenzetu wa Morocco wameingiza *1.17 billion dollars* na kutoa ajira kwa zaidi ya vijana laki moja. Ni lazima tujipange kama Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sana Ofisi ya Waziri Mkuu, kwanza tuwe na *proper coordination* kwenye Wizara zote mtambuka. Kwa sababu *AFCON* sio tu ya Wizara ya Sanaa, Utamaduni na Michezo, *AFCON* ni ya Watanzania na sekta zote lazima ziwajibike kuhakikisha jambo hili linafanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tumeshaambiwa viwanja vitakavyotumika kwenye *AFCON;* Benjamini Mkapa watu elfu 60, Dkt. Samia Suluhu Hassan Stadium kule Arusha watu elfu 30, Zanzibar Fumba Stadium watu elfu 36,500; lakini je, tumejipangaje kwa upande wa miundombinu ya barabara, ya maji, ya umeme? Tumejipangaje kuhakikisha kwamba vijana wetu wanapata ajira? Tumejipanga kutengeneza ajira ngapi? Je, *direct visitor expenses* tumejipanga kwa kiasi gani?

*Mheshimiwa Mwenyekiti, Tourism packages* pia tumejipanga kwa kiasi gani? Eneo la *branding* na *merchandise* tumejipanga kiasi gani? Sisi kama Taifa tunajivunia nini? Leo sisi ndiyo nchi pekee tunaozalisha *Tanzanite*, Wizara ya Madini imejipangaje kuhakikisha tuna-*brand Tanzanite* kupitia *AFCON*? Sisi kule Zanzibar tuna mavazi yetu, tumejipangaje ku-*integrate* masuala ya utamaduni kuhakikisha kwamba tunaitangaza nchi yetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sana tunahitaji Wizara zote zi-*team up* kwenye jambo hili na tuachane na *business as usual* twende kwenye *business unusual*. Kwa pamoja ninaamini tukiwa

kama timu moja tunaenda kuharakisha uchumi kupitia *AFCON* 2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuhitimisha, niseme kwamba Nelson Mandela aliwahi kusema, "*it always seems impossible until it's done*". Waende, tuna imani kubwa nao na Mwenyezi Mungu awasimamie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Nilimwita Mheshimiwa Kijakazi Yunus Mohamed, Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud atafuatia, Mheshimiwa Asha Ramadhani Baraka ajiande.

**MHE. KIJAKAZI Y. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo ukizingatia kwamba hii kwangu ni Wizara muhimu sana kwa sababu mimi ni mwanahabari. Niko hapa lakini nimetokana na tasnia ya habari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, ninaomba kwanza nianze kumpongeza Dkt. Samia Suluhu Hassan na kama mwanahabari, nimshukuru sana kwa sababu wote tutakumbuka, wakati anaingia madarakani Mheshimiwa Rais alionesha dhahiri shahiri kwamba yeye ni muumini wa uhuru wa vyombo vya habari. Alipoingia tu madarakani, aliruhusu baadhi ya vyombo vya habari ambavyo vilikuwa vimefungiwa viweze kuruhusiwa ama kuachiwa ili viendelee kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitazama hii ilikuwa ni hatua kubwa sana hususan kwetu wanahabari na wadau habari. Hata hivyo, hatua hii Mheshimiwa Rais, wote mtakumbuka na msipokumbuka ninaomba niwakumbushe kwamba ilisababisha kutupigisha hatua, wakati anaingia madarakani Mheshimiwa Rais tulikuwa nafasi ya 143 katika nchi ambazo zinazingatia uhuru wa vyombo vya habari, mpaka kufikia nafasi ya 95 mwaka 2024/2025. Tulilinganishwa na nchi takribani 180. Kwa hiyo, ni hatua kubwa

sana hususan kwetu sisi wanahabari na wadau wa tasnia ya habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba pia nichukue nafasi hii kuwapongeza kwanza Waziri Mheshimiwa Paul Makonda, wote tunafahamu kwamba uwezo wake ni mkubwa. Amefanya kazi katika nafasi mbalimbali kwa umahiri mkubwa. Ndugu yangu Zainab, wifi yangu pale ameeleza kwamba, Mheshimiwa Makonda akiwa na jambo lake, akitaka liwe, atalipambania mpaka kuhakikisha kwamba linakuwa. Kwa hiyo, sisi wanahabari tuna imani kubwa na yeye, tunamwamini na tunamtegemea kwamba atatutoa sehemu tulipo kwenda sehemu kubwa zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikimzungumzia Mheshimiwa Naibu Waziri, Hamisi Mwinjuma maarufu kama Mwana FA, wote tunafahamu amefanya kazi kubwa kuanzia awamu iliyopita, kitendo cha Mheshimiwa Rais kuendelea kumwamini kuwa katika Wizara hii, maana yake ni kwamba kuna kazi kubwa ambayo ameifanya kiasi Mheshimiwa Rais amemwamini na anaamini kwamba ataendelea kufanya kazi nzuri akishirikiana na kijana mwenzake Mheshimiwa Paul Makonda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katibu Mkuu wa Wizara hii ambaye ndiye Msemaji Mkuu wa Serikali tunaiona kazi yake. Tunajua anafanya kazi kubwa na niseme kwamba sisi wanahabari tunatambua mchango wake na tunaona thamani ambayo anatupatia sisi wanahabari kwa kupewa kazi na kuitenda kwa zaidi inawezekana ya matumaini yetu sisi ambao tunamtazama. Tunampongeza, lakini nipongeze watendaji wote ambao wanafanya kazi kumsaidia Mheshimiwa Waziri kwenye Wizara hii pamoja na viongozi wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nijikite kuzungumzia kwenye sekta ya habari. Sekta ya habari moja kati ya changamoto ambazo tunakabiliana nazo ni hali ya kiuchumi na uzuri ni kwamba Serikali inalitambua hili kwamba vyombo vya habari vinapitia hali mbaya ya kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati mbaya sana, sekta ya habari ndiyo sekta ambayo inatoa huduma, halafu baadaye ndipo inakuja kulipwa. Tofauti na huduma zingine utaenda dukani, utapewa huduma, utalipia, utaondoka, lakini sekta hii unatakiwa utoe huduma, halafu usubiri baada ya miezi miwili, mitatu uende kufuatilia madeni. Madeni hayo yamekuwa yakichukua mpaka miaka miwili, miaka mitatu mpaka mitano, vyombo vya habari vinaendelea ku-*struggle* havilipwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati mbaya sana pamoja na wao kutolipwa huduma ambayo wameitoa wanapaswa kuendelea kulipa mishahara, wanapaswa kuendelea kulipa kodi, wanapaswa kuendelea kulipia minara na huduma nyinginezo na hakuna huruma ambayo wanapewa kwamba tunajua hamjalipwa, mwendelee na huduma yenu bila kulipia kodi au kulipa mishahara. Pia, hakuna mfanyakazi ambaye ataelewa kwamba taasisi yangu haijalipwa, kwa hiyo niendelee kufanya kazi bila kulipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni tatizo kubwa sana ambalo linatusababisha kuendelea kuzorotesha tasnia hii ya habari na kusababisha weledi kwenye vyombo vya habari kuendelea kuporomoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakumbuka katika awamu iliyopita wakati Mheshimiwa Nape Moses Nnauye akiwa Waziri wa Habari, aliunda Kamati ambayo iliongozwa na Mzee wangu ambaye ninamheshimu sana Mzee Tido Mhando ambaye ni nguli kwenye tasnia ya habari. Kamati ile iliundwa kwa ajili ya kwenda kufuatilia masuala mbalimbali kwenye vyombo vya habari, ikiwemo uchumi kwenye vyombo vya habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ile ilileta ripoti ambayo ninakumbuka tarehe 18 Juni, 2024 alikabidhiwa Mheshimiwa Rais. Moja ya changamoto ilikuwa ni madeni ambayo vyombo vya habari vinadai Serikali pamoja na taasisi binafsi. Mheshimiwa Rais aliagiza pesa hizi zilipwe mpaka itakapofika 24 Disemba, 2024. Kwa masikitiko makubwa bado vipo vyombo vya habari

ambavyo havijalipwa, zipo taasisi ambazo mpaka leo bado hazijalipa madeni hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa kuongezea Jukwaa la Wahariri lilikusanya *invoice* na risiti kwa sababu Serikali ilitaka uthibitisho wa kuonesha kwamba vyombo hivi vya habari vinadai. Zile risiti na *invoice* zilikabidhiwa kwa Serikali, lakini mpaka sasa bado pesa hazijalipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Mheshimiwa Waziri, ninatambua kwamba anao uwezo wa kulisimamia hili, aende akasimamie ahakikishe pesa zinalipwa. Katika hili nimshukuru na kumpongeza sana Profesa Shemdoe, kwa sababu Serikali ni moja ya sekta ambazo zinadaiwa, sekta za Serikali. Wakati ule Profesa Shemdoe akiwa Katibu Mkuu *TAMISEMI* alilifuatilia kwa umahiri sana jambo hili…

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bulaya, Taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpe taarifa mwandishi mwenzangu, mdogo wangu kwa mchango wake mzuri. Kuchelewa kulipwa kwa vyombo vya habari kunaathiri kuchelewa kulipwa kwa mishahara ya waandishi wa habari na vilevile, inachelewesha pia michango ya makato ambayo inaenda kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, ambayo mwisho wake inawagharimu sana waandishi wa habari wanapomaliza muda wao kupata stahiki zao na mafao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa ninamwongezea mwandishi mwenzangu, mdogo wangu katika mchango wake mzuri. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kijakazi Mohamed, unapokea taarifa hiyo.

**MHE. KIJAKAZI Y. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, nimepokea na nitumie nafasi hii kumshukuru sana dada yangu Mheshimiwa Ester Bulaya, amekuwa mpiganaji mkubwa wa kupigania sekta ya habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, nilikuwa naelekea huko; kama alivyosema dada yangu Mheshimiwa Ester Bulaya, athari za vyombo vya habari kutolipwa zinaenda kuathiri moja kwa moja waandishi wa habari, ambao leo hii unakutana na mwandishi wa habari ana hali ngumu kutokana na kutolipwa mshahara, hali iliyotokana na vyombo vya habari kutolipwa pesa zao za matangazo kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa sababu ya muda nilikuwa nina mengi hapo ya kuendelea, lakini kwa kuheshimu muda, nimwombe Mheshimiwa Waziri aende akalisimamie hili. Tuna imani naye, tunajua anaweza, tunajua ana uwezo wa kulibeba hili, waandishi wa habari waende wakapate maslahi yao, ili weledi kwenye uandishi wa habari uendelee kupanda na uendelee kuzingatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa masikitiko, ninaunga mkono hoja, kwa sababu muda haukutosha. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nilimwita Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud, Mheshimiwa Asha Ramadhani Baraka atafuata na Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay ajiandae.

**MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa hii nafasi. Kwanza kabisa nichukue fursa hii adhimu kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara hii kwa usimamizi wao mzuri wanaoufanya kutekeleza majukumu yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuchukua nafasi hii kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa juhudi kubwa anazofanya kuhakikisha Wizara yake na sekta zake zote zinafanya kazi na zinafikia mafanikio makubwa katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri ameelezea kwamba kutakuwa na Kituo cha Harakati za Ukombozi Kusini mwa Afrika au Afrika kwa ujumla. Ninashauri katika tafiti zitakazofanyika na kule Zanzibar zifanyike tafiti kwa sababu, kuna maeneo tumeshayagundua mfano, kama Gana, Fumba na kuna maeneo mengine zaidi yapo ambayo yameshiriki. Kwa sasa mratibu pale yupo lakini hana ofisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninauelekeza sasa mchango wangu kwenye Baraza la Kiswahili la Taifa na lugha ya Kiswahili kwa ujumla wake. Kwanza kabisa, *BAKITA* ina mjumbe mmoja tu kutoka upande wa pili wa Muungano na huku kunaamuliwa mambo mazito ya kitaifa na nchi. Ninapendekeza waongezeke wajumbe angalau basi wawe wawili au wakati wa kufanya maamuzi basi waalikwe na wengine waongeze idadi ili wafikie maamuzi muafaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kiswahili ni ajira, ni bidhaa ni rasilimali. Kiswahili chetu duniani kinajulikana kwamba ni lugha nyepesi unayoweza kujifunza kwa haraka kuiandika, kuiongea na kuisoma. Lugha hii imekuwa nyepesi kwa sababu ambazo kila nikichangia ninazisema. Kiswahili kimetohoa maneno mengi kutoka lugha mbalimbali duniani, Kiingereza, Kiarabu, Kihindi, Kigujarati, Kipunjabi, Kireno, Kijerumani, Kiajemi, Kigiriki na lugha nyinginezo *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana sasa tukapata maneno ambayo kuyatumia inakuwa rahisi kwa sababu inafungana na lugha nyingine kwa maana ya kuzitohoa. Mfano, hifadhi, amin, kalamu ni Kiarabu. Karakana, pesa, tamasha ni Kihindi. Gereza ni Kireno, ninatoa mifano kama hivyo, kwa sababu yetu imetohoa lugha nyingi duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo sasa hoja yangu ni kwamba, tuendelee kuwa na lugha nyepesi inayoweza kufundishika kwa urahisi, kuzungumzika kwa urahisi. Badala ya Kiswahili kuwa chepesi, sasa kinakuwa kigumu. Hata Waswahili wenyewe sasa kuna baadhi ya maneno hawayajui na hawayatumii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna baadhi ya maneno yamo kwenye Kiswahili na kamusi zetu za Kiswahili, lakini yanapotea hayazungumzwi. Kazi yao sasa Baraza hili la Kiswahili, kuyatafuta yale maneno yanayopotea ambayo hayazungumzwi, yazungumzwe. Badala ya kuleta maneno mengine mapya na tunasema istilahi zinvyotafutwa ziangalie lahaja za Kiswahili, hilo neno halipo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama neno lipo kwenye lahaja zetu za Kiswahili kuna haja gani ya kuingiza maneno magumu? Mfamo, kifaa kimeundwa mwaka jana na kimepewa jina, sasa sisi hilo jina tunalitoa wapi la Kiswahili wakati kile ni kipya! Mbona tunatumia neno "Kidijiti" sasa kwa nini televisheni iwe runinga? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo ninakusudia kusema kwamba kuna maneno yanaingiliana hata katika lugha nyingine (yale maneno yanatumika kwa lugha tatu mpaka lugha nne). Soko Kiarabu, soko Kiswahili, soko Kihindi. Madrasa Kiarabu, madrasa Kihindi, madrasa Kiswahili. Sasa kuna haja gani ya kuingiza maneno magumu kwa sababu sasa hivi watu wanaona Kiswahili kinakuwa kigumu. Hofu yangu kwamba Kiswahili chetu, tusije tukaunda lugha ndani ya lugha. Tubaki na Kiswahili chetu cha asili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiendelea Kiswahili chetu kimestawishwa duniani kwa nyanja mbalimbali, ikiwemo nyanja ya uandishi, utunzi, riwaya lakini pia nyanja ya utangazaji. Kiswahili hiki kwa nyanja ya utangazaji ndiyo kinachozungumzwa huko duniani, ndicho walichokipata. Mfano, kwenye *Radio Prague - Czechoslovakia* alikuwepo mtangazaji Ramadhani Ally na Abdallah Hamid. Wamekitangaza Kiswahili huko duniani. *Radio Beijing,* Profesa Haroub Othman alitangaza huko na Kiswahili hicho ndiyo kinachozungumzwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Radio Japan* na *Radio Mosmar* ziko nyingi na hao watangazaji niliwataja wengi kwenye hotuba zangu za nyuma. Ninachosema kuna maneno yaliyopotea na yanayoenda kupotea na yanaendelea kupotea. Mfano neno

“Matlaba” halitumiki lakini ni neno la Kiswahili sanifu. Neno “Hidaya” hidaya si jina peke yake, hidaya ni zawadi, zaidi ya zawadi kwa maana ya zawadi maalum mahususi. Ni zawadi ya kutunukiwa ndiyo hidaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiendelea na mchango wangu, Kiswahili kiendelee kutumika kama kinavyotumika huko duniani sasa hivi na wataalam na vijana wetu wale wa Kiswahili waongezewe uwezo wa kumudu lugha mbalimbali zaidi ya mbili mpaka tatu, zikiwemo lugha za kiafrika ambazo tuko wengi sisi waafrika. Si lugha zile za kigeni lakini lugha za Mataifa ya Afrika zinazozungumzwa kwenye mataifa mbalimbali. Pia kuna haja ya kuwafundisha wataalam wetu wakafundishe, tukamate hili soko la ajira, kwa sababu baada ya muda itafika wale waliofundishwa Kiswahili sasa hivi katika nchi mbalimbali ndiyo watakamata hilo soko na sisi tutabaki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu wale walimu mfano, Profesa Mohamed na Profesa Abdallah walikwenda Makerere na Kenya kusomesha Kiswahili. Wataalam wale sasa hivi ndiyo wameshika soko la Afrika Magharibi na Afrika ya Kati, sisi Tanzania hatupo. Ninasisitiza uwezo, kuwe na haja maalum ya kuongeza uwezo kwa vijana wetu kwa lugha ya Kiswahili, kuwaongezea uwezo ili wamudu soko la ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania iwe ndiyo kinara wa lugha ya Kiswahili, ndiyo muasisi na ndiyo mwanzilishi. Kwa sababu kuna lugha sasa hivi zinazungumzwa, Kiswahili kimeanzia nchi fulani, kimeishia nchi fulani. Kiswahili ni cha Tanzania na tuoneshe kwamba lugha ni yetu, tuithamini, tuiheshimu na tuisambaze duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia, kwa kuwa hii ni Wizara ya Utamaduni na ninapenda kusema mambo yafuatayo:

Mola wetu utubarikie, ibariki nchi yetu,
Neema tuzidishie, na baraka nchini mwetu,
Nuru utung’arishie, hii Tanzania yetu,
Amani utudumishie, utulivu wa nchi yetu,

Mabaya utuepushie, na hasadi kwa nchi yetu,
Na pia utulindie, wote viongozi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud. Nilimwita Mheshimiwa Asha Ramadhani Baraka, Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay atafuatia na Mheshimiwa Baraka Ambindwile Ulimboka ajiandae.

**MHE. ASHA R. BARAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu, pia namshukuru Rais wangu, Mama Samia Suluhu Hassan kwa juhudi kubwa na nzuri sana anazozifanya katika kuendeleza sanaa hapa nchini Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishukuru Wizara yangu ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa kazi nzuri sana wanayoifanya, lakini ninaendelea kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa juhudi zake. Juzi kama mnavyoona alitoa salamu kupitia Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo Hamisi Mwinjuma alimaarufu Mwana FA kwenda kuwatembelea wanamuziki wa dansi wakongwe Mzee Zahiri Ally Zorro pamoja na Mzee Bichuka na kuwafariji, kwa sababu wapo katika hali mbaya na wapo bado vitandani wanapigania hali yao ya maisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitazungumzia sana upande wa muziki wa dansi, *BSS*, *film, boxing,* riadha, *netball* na *basketball* pamoja na *football* na *AFCON*. Kwanza nitoe pongezi kwa Waziri, Mheshimiwa Paul Makonda kwa kazi ngumu anayoifanya, kutembelea viwanja vyote vya *AFCON* pamoja na Katibu Mkuu, Msigwa pamoja na Mwana FA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakwenda kwenye muziki wa dansi. Pamoja na bajeti na hotuba nzuri ya Mheshimiwa Makonda sijamwona akizungumzia muziki wa dansi kwa ukaribu kabisa, hata hivyo sitamwondolea shilingi kama Mheshimiwa Babu Tale. Kwa sababu yeye ndiyo kwanza ameshika Wizara hii katika kipindi

kichache sana na kazi inaonekana ni kubwa sana. Kwa hiyo, ninaendelea kumpongeza tu, ninajua haya atayafanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, muziki wa dansi uko katika hali mbaya; unachechemea, dansi zinapigwa na muziki wa dansi huwa nyimbo zake hazifutiki, ni nyimbo ambazo hata miaka 100 na zaidi ya 100 bado zinaendelea kupendwa, kama mpaka sasa hivi tunasikiliza muziki wa Luambo Makiadi, tunasikiliza nyimbo za Mbaraka Mwishehe na wengine waliotangulia mbele ya haki ambao ni Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, muziki wa dansi sasa hivi unachechemea wasanii wanapiga kwa kiingilio cha bia na hata ukiwaambia utoze kiingilio kwa sababu hauna kumbi maalumu wenye kumbi wanakwambia sisi tunawalipa, sisi hii ni shughuli yetu, burudani yetu na ni maamuzi yetu. Wapo wanamuziki wanapiga katika hali mbaya mpaka bendi inalipwa shilingi 300,000 au 400,000 ukiangalia hiyo bendi ina wanamuziki takribani 40 mpaka 30, hali inakuwa ngumu wanawezaje kugawana shilingi 300,000. Kwa hiyo, hapo kama Wizara tunaomba wafanye kitu kuinusuru dansi na taarabu zipo katika hali mbaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata ukiangalia kwenye hizi shughuli muhimu za kitaifa muziki wa dansi hauitwi kwenye sherehe zozote za kitaifa. Zamani ilikuwa muziki wa dansi kama hivi leo amekuja Rais wa Kenya utakuta Msondo wako pale wanapiga, lakini sasa hivi hawaitwi, Sikinde wako pale na bendi nyingine *TOT Band* wako pale, unaona lakini haziitwi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba tu Wizara ifanye uwiano kwa sababu hawa wote hata muziki wa dansi ina wasanii ambao ni vijana siyo tu wakongwe ni vijana. Ukongwe ni kwamba zile bendi ziko muda mrefu majina yake. Kwa mfano ukiangalia Msondo, Msondo ni jina tu ukiangalia wanamuziki wanaofanya kazi pale wengi wao ni watoto wa wasanii, lakini ni vijana hata Sikinde vilevile ni vijana. Kwa hiyo, ukongwe ni umri wa jina wa miaka kwenye shughuli hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka kuiongelea *BSS*: *BSS* imeanza mwaka 2006 ambapo ukiangalia ni taasisi ambayo inaongozwa na Rita Paulsen, ni mwanamke jasiri ambaye anaibua vipaji vya wasanii kutoka mikoani na mpaka sasa hivi anaingia Afrika Mashariki (Kenya na Uganda) ili kuimarisha uhusiano wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, *BSS* ndiyo iliyomtoa mwanamuziki mkongwe kwenye Bongo Fleva anaitwa Msechu. Ninaomba Wizara iwaangalie kwa karibu, iangalie jinsi gani ya kuweza kuisaidia *BSS* ambayo inajipambania yenyewe na mpaka sasa hivi tunaweza kupata kupitia *Azam TV* ambao wamewasaidia *BSS* waweze kuonesha kazi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaongelea pia kuhusu *Film*. Sasa hivi *film* inafanya kazi nzuri sana, inafanya kazi nzuri sana kupitia *Azam TV* kupitia *TV* nyingine. Kwa mfano kuna huyu dada anaitwa Lamata, Lamata anafanya kazi nzuri sana kwenye *film* pia inatakiwa Serikali imwone na imsaidie. Kuna kikundi kingine kinaitwa Juakali na vikundi vingine ambavyo nimevisahau.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niweze pia kuzungumzia *boxing*. Ninaona *boxing* inakuja juu sana kwa kasi. Kuna mtu anaitwa *Mafia Boxing* yuko pale Magomeni Sokoni amechukua *flow* nzima katengeneza ofisi. Mheshimiwa Waziri Paul Makonda, ikimpendeza kwenye *AFCON* watu waende pale kufanya mazoezi, kwa sababu kuna *gym* kubwa sana ya kisasa, kuna vifaa vya kisasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi mwenyewe binafsi nimeenda kutembelea pale. Kwa hiyo, ninaomba Wizara yetu iweze kupitia pale katika *Mafia Boxing* na ndiyo inatoa changamoto kwenye *boxing* mpaka sasa hivi *boxing* zimekuwa na tija zimekuwa ni nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninazungumzia riadha; ambayo ilikuwa inatuwakilisha vizuri sana na inaendelea kutuwakilisha vizuri. Hata hivyo, tukienda kwenye riadha tunaenda katika mashindano ya Olimpiki na mengine. Hapa nilikuwa ni mkimbiaji

wa mita 100, Wabunge hawajui, nilikuwa ninakimbia sana na ni mkimbiza Mwenge wa Olimpiki kwa mara ya kwanza, ulivyotembea Tanzania 2008 nilikimbiza Mwenge wa Olimpiki na ninao kama zawadi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kwa mashindano haya ya Olimpiki ninaomba tuwe na kambi kama zilivyokuwa zamani tunaweka kambi Arusha pale kwa ajili ya mashindano ya Olimpiki na yalikuwa yanagharamiwa na Wizara ili kuiokoa kuifanya riadha ifanye vizuri katika mashindano ya kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaongelea *basketball*; *basketball* tuna ufinyu wa viwanja vya *basketball* ukiondoa labda kile kiwanja ambacho kipo pale Dar es Salaam ambacho wanafanyia *Dar City*, kulikuwa kuna viwanja vingine ambavyo ni vya Serikali *(Indoor Stadium)*. *Indoor Stadium* ni uwanja ambao ulikuwa unatumika kwa *Netball, Tennessee*, *Basketball*, *Baji Menton*, *Volleyball*, Ngumi na kadhalika. Nikisema ngumu ni zile za *amateur* ambazo washiriki wengi wa ngumi za *amateur* ndiyo wanatuwakilisha katika Olimpiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba hivyo viwanja viweze kufanyiwa kazi virekebishwe, viwe vizuri vya kisasa kama tunavyopigana na viwanja vya *AFCON*, lakini wasisahau kupigania kiwanja cha *Indoor Stadium* ambacho kitapakana na Kiwanja cha *AFCON* cha Mkapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa niongelee pia uhaba wa viwanja vya burudani. Kuna viwanja vya burudani zamani pale tulikuwa tunafanya burudani *Leaders Club*. Ule uwanja wa *Leaders Club* una hali mbaya na ni uwanja wa Serikali. Utasaidia kuwafanya wanamuziki waendelee kufanya miziki yao hasa *bonanza* zinapokuwa zinashughulika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kiwanja kingine ...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, muda wako umekwisha.

**MHE. ASHA R. BARAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, dakika moja ninamalizia, *Zakhem* pamoja na...

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Nilimwita Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay, Mheshimiwa Baraka Ambindwile Ulimboka atafuatia na Mheshimiwa Asia Abdulkarim Halamga ajiandae.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi kuchangia mada hii iliyo mezani. Kwanza nichukue nafasi hii kwa namna ya pekee sana kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa rehema zake mbalimbali, lakini kwa Taifa letu pia na mimi binafsi. Kwa namna ya pekee Mwenyezi Mungu ameturehemu baraka zake kama nchi na tumepata ustawi mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na muda ninaomba pia nimpongeze sana Mheshimiwa Rais na kumshukuru kwa namna ya pekee kwa kuisimamia Sekta hii ya Michezo na nafasi hii kubwa sana kwa Taifa letu. Mheshimiwa Rais niungane na Wabunge wenzangu wote kwa jinsi alivyoisaidia hii Sekta ya Michezo katika nchi yetu na kwa mafanikio makubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee kama siyo kipindi hiki Tanzania itajitokeza kwenye nyanda za kimataifa na kuona ulimwengu wa michezo kwa dunia nzima, hatutapata wasaa mwingine. Nina mashaka kwa sababu kwa muda mrefu katika nchi yetu michezo haijafanya vizuri kama kipindi hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee nimpongeze pia Mheshimiwa Waziri Paul Christian Makonda pamoja na Naibu Waziri na Wizara nzima kwa ujumla. Hongera sana kwa kipindi hiki katika kazi kubwa waliyoifanya kwa Wizara hii na kwa hotuba yake leo hii asubuhi na sasa hivi jioni tunapochangia. Kila Mbunge

aliposimama ameona mchango wa Wizara hii na Sekta hii imeheshimishwa kwa kadri ilivyotarajiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na muda pia nichukue nafasi hii kutoa pongezi kwa Kamati yetu ya Bunge kwa kazi kubwa iliyofanya ya kuchakata taarifa hii na hatimaye kufikishwa kwetu sisi tukipata wasaa wa kuichangia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kwa namna ya pekee pia nipongeze Chama Cha Mapinduzi ambapo ni Mbunge kiwa Awamu ya Tatu kupitia chama hicho kwa kweli chama chetu kimefanya kazi kubwa katika Ilani ya miaka 10 iliyopita na katika Ilani ya sasa bado tuemeendelea kuwapa Watanzania imani kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wizara hii nina mchango mdogo sana. Kwanza kwa namna ya pekee niiombe Wizara itazame upya, Mheshimiwa Waziri kalenda yetu itoke kwenye vijiji ama kwenye mitaa ije juu mpaka ngazi ya Taifa. Kule kuna rasilimali nyingi sana ya vijana wanashindwa namna ya kufika kwenye hizi ngazi ili wadau wa michezo waweze kuwaona na waweze kupata ajira na vipaji vyao vitambulike kwa fani mbalimbali katika utamaduni, sanaa na michezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli tuna vijana wengi na mimi kama Mbunge wa Jimbo la Mbulu Mjini ninamhakikishia kwamba kwa miaka yangu 10 nimeendesha kombe la jimbo kwa gharama yangu mimi binafsi na mpaka wakati ninakosa mgeni wa kuja kufunga, lakini gharama ni kubwa sana ya kuendesha michezo nchini. Wizara itazame upya muundo wa kupata wadau watakaoweza kusaidia hii Sekta ya Michezo kwa ngazi zile za chini ukiacha hizi za vilabu kwa sababu hizi tayari zimeshafanikiwa kwa kiasi kikubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini ninazungumza hivi? Katika ngazi za shule kuna michezo ya ngazi za sekondari na msingi sasa hivi zinaendelea. Wale vijana wakimaliza shule baadaye wanashindwa sasa namna ya kuungana na wale wenzao ambao wapo kwenye ngazi za Taifa na ngazi za mikoa. Kwa hiyo,

kalenda nyingi za michezo kwa ngazi ya michezo ya mipira na hata michezo ya riadha inaishia kwenye ngazi za wilaya ama ngazi za kata na vijana hawa hawapati nafasi ya kwenda mbele zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, rai yangu kwa Wizara na kwako Mheshimiwa Waziri. Kama Wabunge tunakupongeza sana ulipoanza kushika nafasi hii hatukuwa tumeamini tunakwenda kwa kasi hii ambayo Rais aliitamani na aliiandaa kwa muda mrefu. Hata wakati anagombea Ubunge mimi nilikuwa Mbulu Mjini wadau wengi niliwaambia Mheshimiwa Paul Makonda angebaki kuwa *RC* wa Arusha lakini kwa bahati nzuri kumbe aliletwa na Mwenyezi Mungu kwenye nafasi hii kwa makusudi makubwa sana. Hongera sana kwa nafasi hiyo ambayo Rais amekuamini na Watanzania wamepata imani kubwa sana kwake kwa jinsi ambayo anaisimamia Wizara na waandamizi wengine wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya kipekee nizungumzie changamoto ya ukosefu wa makocha. Yaani katika ngazi za wilaya hata Maafisa Michezo tunaowateua mimi ninadhani wakati fulani tutazame kwa sababu hizi ni fani ambazo zinahitaji baadhi ya watu wenye vipaji na elimu waliyonayo. Kwa mfano kwa Maafisa Michezo pamoja na ukosefu wa Makocha katika ngazi za Wilaya bado tuna changamoto kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara itazame upya tunafanyaje ili wale vijana wa ngazi za chini ikiwezekana pengine hata kocha mmoja kwenye ngazi ya wilaya kwa walimu tulionao ambao wamesomea fani hiyo atasaidia hiyo halmashauri aliyopo na vijana na fani mbalimbali zilizopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee kama hatutakuwa na utaratibu wa kutazama vyanzo vya kuendesha michezo ama fani hizi, iwe *Marathon* ama iwe michezo ya mipira kwa kutazama tu wajitegemee jamani kwa kijana wa kijijini kutafuta jezi tu ya viatu pamoja na jezi nyingine hizo kwa fani mbalimbali ni gharama kubwa sana hawataweza. Tutazame

maeneo ambayo tukapata wadau watakao-*support* michezo ili tuweze kufanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee pia na eneo hili la kama tutaweza tutazame rasilimali tulizonazo. Ninawaalika Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, sasa hivi mwezi Agosti, aje kufunga kombe langu atashangaa yanayofanyika na rasilimali iliyoko Mbulu Mjini, hapo ndipo atatambua kwa sababu mara nyingi nilipoandaa kila mgeni aliyekuja alikuwa ananiambia, uliwezaje. Tuna rasilimali nyingi kila wilaya, kila halmashauri, kila mkoa kupitia vijana tulionao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa namna gani tunawaunganisha, akija kufunga hayo mashindano ya kombe la jimbo atafanya kikao cha wadau wa michezo pale Mbulu Mjini, lakini pia atafanya kazi nyingine ya kutembelea uwanja wa *Nyerere Stadium* ambao kabla ya mwaka 2000 ulikuwa unatumiwa na wachezaji wa timu mbalimbali Kanda ya Kati na Kanda ya Ziwa, wakija kucheza Mbulu kwa ajili ya hali ya hewa nzuri, milima na hali ya hewa nzuri ya watu kuweza kukimbia na kucheza. Sisi tuko juu ya Bonde la Ufa, kwa namna ya pekee aje ajionee, lakini pia akifanya matukio hayo atakuwa ametujenga sana na ameiendeleza Mbulu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee pia tutazame fursa zilizopo. Hizi fursa ambazo zipo za *AFCON* iwe ni kielelezo kwetu sisi. Kama nchi tukitumia vizuri vijana wetu hatutorudi nyuma na michezo yetu haitorudi nyuma. Ninaamini kabisa ni nyakati sahihi na muda sahihi wa sisi kutoboa kama nchi kwenda kwenye ulimwengu mwingine wa michezo na tasnia nyingine ya michezo kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na muda ninaomba niendelee pia kutoa mchango mwingine wa kuzungumzia ngazi za Kamati zetu za Mikoa. Mheshimiwa Waziri tuna Kamati za Mikoa lakini hazina rejea, hazina ajenda, hazina kalenda hakuna mpango kazi. Kamati hizi zikipewa utaratibu wa mpango kazi, zikipewa utaratibu wa kuanzisha na kusimamia tasnia hii ya

michezo kwa namna ya pekee hatutakuwa tunaanzisha michezo ngazi za chini, ngazi za wilaya na hatimaye hazifiki mahali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima kwenye mchujo kuna watakaokwenda kwenye ngazi za Taifa na Kimataifa. Mfano huu uko kule Mbulu, vijana walioanza kwenye kombe la Jimbo mwaka 2015 wale wa riadha, sasa hivi wako kwenye riadha ngazi za kimataifa na wananiombea ndiyo maana ninaendelea kuwa Mbunge. Wanasema kazi kubwa uliyoifanya umetufikisha kwenye ulimwengu wa kimataifa tunakushukuru sana kwa gharama na utaratibu wote uliouhangaikia. Tukiwa na utaratibu huu wa kuwatafuta vijana kutoka ngazi hizo za chini tukaja kwenye ngazi zetu hizi za kata baadaye wilaya, baadaye mkoa, wale waliopanda juu wanapata ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuandae pia mazingira vijana wa ngazi za chini au michezo kwa ngazi ya chini iwe tasnia yoyote ipate basi namna ya kukusanya fedha, badala ya wanaokusanya fedha au michango wa kiingilio iwe ni ngazi za Taifa na pengine kwenye timu za kanda, ama timu za daraja la pili na la tatu. Kule chini tukiwa na viwanja vizuri tukiendeleza hivyo viwanja kwa namna ya pekee, ninaamini hata zile timu zitapata mapato na zitaweza kujiendeleza na kufanikiwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishukuru Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan katika mwaka huu wa fedha unaoisha na ule mwaka mwingine uliokwisha, katika miaka miaka hii miwili imepeleka pesa nyingi sana katika shule ya Sekondari ya Chifu Sarwatt kujenga uwanja wa michezo na kuiteua ile shule kuwa shule ya michezo kwa ngazi ya Wilaya ya Mbulu na Mkoa wa Manyara. Ni nafasi kubwa sana kwa sababu Mbulu tuna rasilimali, hali ya hewa inaruhusu, lakini pia tuna historia ya michezo kwa hiyo, tuna vijana wengi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mchango wangu huu ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ninaomba tuendelee na ratiba. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nilimwita Mheshimiwa Baraka Ambindwile Ulimboka, atafuatiwa na Mheshimiwa Asia Abdulkarim Halamga na Mheshimiwa Asha Juma Kombo ajiandae.

**MHE. BARAKA A. U. MWAMENGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nianze kumshukuru Mungu aliyetuwezesha siku ya leo kuwa wazima na wenye afya njema. Nimpongeze Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jinsi ambavyo amepandisha bajeti ya Wizara hii kutoka bilioni 35 mpaka sasa hivi tunazungumzia zaidi ya bilioni 500.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiki ni kitendo cha kupandisha bajeti hii...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ulimboka, *Hansard* zetu zikae vizuri aliye kwenye kiti ni Mwenyekiti.

**MHE. BARAKA A. U. MWAMENGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kulingana na bajeti hii ilivyopandishwa, sisi tunachukua nafasi hii kuipongeza sana Serikali na kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia, kwa kuwa ameanza kuona Wizara hii sasa kuwa inaenda kubadilika kuwa Wizara ya Michezo au kuwa Wizara ya kawaida na kwenda kuwa Wizara ya kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii pia kumpongeza ndugu yangu Waziri pamoja na Naibu Waziri pamoja Katibu Mkuu wa Wizara hii kwa jinsi ambavyo wanaendesha na jinsi ambavyo wanakimbizana na Wizara hii kama inavyoitwa Wizara ya hekaheka ni kweli imepata Waziri mwenye hekaheka kwelikweli. Ninaomba nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa jinsi ambavyo amekuwa akikimbizana na hekaheka hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia katika *International Finance Corporation*, inaonyesha kuwa utamaduni na michezo inaweza ikachangia pato la Taifa mpaka kufikia asilimia tano mpaka saba, lakini nchi yetu mpaka sasa hivi katika Wizara hii tunachangia chini ya asilimia moja. Kwa hiyo, ninaamini kupitia

ongezeko hili la bajeti, sasa baada ya miaka 10 mpaka 15, tunaenda kubadilika kwenda kuwa hii Wizara siyo ya burudani pekee yake bali inaenda kuwa Wizara ya uchumi pia kwa nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan mwanamichezo namba moja ameonesha hilo kwa kuwekeza fedha nyingi kwenye Wizara hii. Tunaamini kupitia hili tunaenda kwenda kuongeza uchumi wetu kupitia Wizara hii. Nimpongeze sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan mwanamichezo namba moja kwa jinsi ambavyo anakwenda na Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii pia mwaka huu tuna jambo letu kubwa ambalo tunasema ni jambo la kitaifa. Unapozungumzia *AFCON* tunazungumzia maendeleo makubwa kwenye hii Wizara ya Michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Kamati, tunaomba tu Wizara hii isiachiwe mzigo wa kuwa ni Wizara ya Michezo pekee yake. Badala yake Serikali ibebe jambo hili kama jambo la kitaifa, kama jambo la wote, kama jambo la Wizara zote; Wizara zote mtambuka ziweke nguvu kubwa ili kuchangia jambo hili la *AFCON* liende kwa kukamilika na kwa ufanisi mkubwa. Badala ya kuwa michezo peke yake, basi tuwaongeze vijana wetu wapate uchumi, nchi ipate mapato makubwa kulingana na michezo hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaamini kupitia Waziri, kupitia Naibu Waziri, kupitia mwanamichezo namba moja Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, tunaenda kutengeneza uchumi huo kupitia michezo hii. Niungane na wenzangu kama walivyosema kuwa kama tutaipatia Wizara hii yale waliyoyaomba, ninaamini kabisa tunaenda kufanikiwa kuifanya Wizara hii kuchangia uchumi wa Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nizungumzie jambo moja, niiombe Serikali kupitia Wizara hii, kuna jengo ambalo linajengwa pale kwenye *TSN*, lile jengo limeombewa fedha miaka mingi na jengo hili halijakamilika. Niiombe Serikali itoe fedha kwa

ajili ya jengo lile, kwa sababu linaenda kuimarisha uandishi wa habari, uhariri wa habari na mapato ambayo yatatokana na *TSN*. *TSN* pale hela zilizowekwa ni nyingi, tunaiomba Serikali itoe fedha ili lile jengo likamilike na lifanye kazi zake vizuri ili Mheshimiwa Makonda na Naibu Waziri waendelee kuwa ni wazee wa hekaheka kama tunavyowaita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni jambo linalohusu Maafisa wa Mendeleo ya Jamii, Maafisa Maendeleo ya Michezo na Maafisa Maendeleo Utamaduni waliopo katika ngazi za wilaya zetu. Wale watu wako chini ya TAMISEMI, lakini ukiona mambo ambayo wanayafanya kwenye maendeleo ya michezo, bado yanakuwa yapo nyuma nyuma kwa sababu hawana uwezo wa ku-*plan* kile ambacho wamekisema na kitu kilichopangwa na Wizara kwenda kukipandikiza katika ngazi ya chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe kupitia Wizara hii ya michezo, wale watu wahamishwe kutoka kule TAMISEMI waje kwenye Wizara ya hekaheka ili Mheshimiwa Makonda aweze kwenda ngazi ya chini, ngazi ya halmashauri. Ngazi ya halmashauri kule michezo ipo mingi, lakini imelala kwa sababu wale watu wapo chini ya TAMISEMI. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tungeomba kuwa, angalau kwa kuanzia tuwahamishe watu wa michezo waje ngazi ya Wizara ili hekaheka zile ziende mpaka kwenye halmashauri, ziende kwenye kata na ziende kwenye vijiji. Changamoto kubwa walizonazo kule chini zitakuwa zinatatuliwa moja kwa moja na Wizara na baada ya hapo tutamlaumu sasa Mheshimiwa wa hekaheka, Mheshimiwa Makonda ili aende sambamba na yale anayoyasema yaende kwenye kata na kwenye vijiji vyetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Mzee wa hekaheka Mheshimiwa Makonda tuwatakie kila la kheri. Tunaamini Wizara iko mikono salama, mwanamichezo namba moja Mheshimiwa Dkt. Samia, tunaomba katika hili tumuunge mkono na tumuunge mkono Mheshimiwa Makonda na Naibu Waziri pamoja na Katibu

Mkuu wa Wizara hii ili *AFCON* ya mwaka huu iende kwa *standard* ambayo tunaitegemea…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. BARAKA A. U. MWAMENGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa mchango. Ninamwita sasa Mheshimiwa Asia Abdukarim Halamga, atafuatiwa na Mheshimiwa Asha Juma Kombo na Mheshimiwa Dotto Jasson Bahemu ajiandae

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia bajeti ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa mwaka wa fedha 2026/2027. Awali ya yote nichukue nafasi hii kumshukuru mwenyezi Mungu kwa kutupatia uzima na afya na kufikia siku ya leo kuweza kuipitisha bajeti hii muhimu kwa maendeleo ya vijana wa Taifa letu, lakini Watanzania wote kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kumshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa mchango wake mkubwa na wa kihistoria katika kuhakikisha kwamba ameendelea kuisukuma Wizara hii ya Habari, Utamaduni Sanaa na Michezo na kuendelea kuhakikisha kwamba inakuwa ni sehemu ya kutoa ajira kwa vijana wa Kitanzania, lakini wananchi wa Kitanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakika kwa sasa upele umempata mkunaji, na mkunaji mwenyewe ni Mheshimiwa Paul Christian Makonda, Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo. Pia, akisaidiwa na Naibu Waziri wake. Bila kusahau, nichukue nafasi hii kumpongeza Katibu Mkuu wa Wizara, Naibu Katibu Mkuu, pamoja na watumishi wote wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa kazi kubwa ambazo wanazifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nianze kutoa mchango wangu. Wizara hii imefanya kazi kubwa sana, kwanza kuendelea

kutengeza mazingira rafiki ya kuendelea kuhakikisha, inatoa fursa mbalimbali ikiwemo kuwasaidia vijana, akina mama na wananchi wa Kitanzania na hususan wale ambao wanahusika na maudhui mbalimbali ya kutengeneza filamu. Nichukue nafasi hii kuipongeza sana Serikali, hususan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuhakikisha kwamba, wasanii sasa wanaweza kupata mikopo ili kuweza kuendeleza kazi zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kazi hii kubwa na nzuri ambayo imefanyika, nipende kutoa mchango wangu na kuishauri Serikali kwamba fedha hizi ambazo wenzetu wa filamu wanakopeshwa ili ziweze kuwa na tija, tuombe Wizara iende mbali zaidi kwa kuhakikisha kwamba inatafuta masoko ili mkopo huu wasanii waliouchukua uweze kuwa na soko la uhakika la kuuza kazi zao, ili waweze kurejesha fedha na ziweze kuwasaidia Watanzania wengine na kuendelea kukuza soko la filamu. Pia, kuhakikisha kwamba fedha hizi zinaendelea kukuza suala la sanaa na utamaduni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze sana Serikali kupitia Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kutengeneza mazingira bora na rafiki, hatimaye leo tunashuhudia ulimwengu unakuja hapa kupitia *AFCON* mwaka 2027. Jambo hili ni kubwa katika nchi yetu ni jambo ambalo linakuja kuitangaza Tanzania zaidi, lakini pia ni jambo ambalo linakuja kutuletea fursa za kiuchumi kwa Serikali, lakini pia kwa mwananchi mmoja mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutumia fursa hiyo, niipongeze Serikali kwa kuanza kujiandaa kwa kuanza kutengeneza mazingira rafiki na bora ya kuwekeza katika 2027 kupitia *AFCON*. Niombe sasa, pamoja na kazi hii nzuri ambayo imefanyika, msafiri siku zote hukaa stendi na hapa Mheshimiwa Waziri ninaomba anisikilize vizuri. Sisi Wanahanang tumekaa stendi tayari na kwa sababu tunatambua kwamba *AFCON* ni kitu kikubwa, tayari tumetenga zaidi ekari 10.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ekari hizo 10 tumeshazizungushia ukuta kupitia fedha za halmashauri,

tumeshaongea na Waziri Aweso hapa, ameshatupatia mitambo ya kuchimba kisima kwenye uwanja wetu. Hapa nimwombe Mheshimiwa Waziri kupitia *AFCON* tunatamani sana mchezo wa riadha Tanzania, ni moja ya michezo ambao unalitambulisha Taifa letu katika ulimwengu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Wanahanang kama ambavyo nimetangulia kusema kwamba tayari tumeshakaa stendi ili kupokea fursa hii ya *AFCON*. Pale tayari tumeshajenga ukuta na ndani ya ule ukuta wa uwanja wetu tumejenga ndani yake viwanja vitano vikiwemo vya *volleyball*, *basketball* tumeweka mpaka *swimming pool* na michezo mingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha hotuba yake, aniambie sasa ni lini tutakwenda Hanang akashuhudie kazi hii kubwa ambayo tumeifanya kupitia fedha za halmashauri na yeye kama Wizara ili aje atushike mkono viwanja vile viwe na tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mchezo wa riadha Wilaya ya Hanang imekuwa ni chanzo cha historia cha wachezaji, wakimbiaji wa riadha katika Taifa letu, tuone sasa na sisi Wanahanang tunatamani kuwa ni kitovu na kituo cha kunyanyua mchezo wa riadha Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunao wazee wetu ambao wamekuwa ni kielelezo cha historia ya mchezo wa riadha katika Taifa letu, imepeperusha Taifa letu la Tanzania huko duniani. Yupo Mzee wetu anaitwa Filbert Bayi, yupo Gidamis Shahanga, yupo Emanuel Giniki kijana anyefanya vizuri sana; yupo Francis Naali, yupo Alfredo Shahanga na yupo Geway Suja. Mfano hapa nikimwongelea Emmanuel Dinday, ametoka kufanya vizuri sana kwenye mashindano yaliyofanyika Nchini Korea. Watanzania hawa wamekuwa kinara wameshika nafasi ya tatu, mwingine kashika nafasi ya kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu wa mwisho kwenye suala la riadha; tunavyo viwanja Tanzania, tunavyo viwanja mpaka vya shule, tuone sasa viwanja ambavyo vinatumika kwa

ajili ya *football* viweze kutengenezewa miundombinu mizuri kwa ajili ya kucheza mchezo wa riadha. Mchezo wa riadha umekuwa ni kielelezo kwa Tanzania huko duniani. Ninataka kuendelea kuona sasa mchezo huu haumilikiwi na watu binafsi mchezo huu upatiwe vifaa, mchezo huu uendelee kuwa kinara cha kuibua vijana wengine wa Kitanzania, na niendelee kusisitiza, kitovu cha wana riadha kiko Hanang.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nimwombe sana Mheshimiwa Waziri aiangalie Hanang kama kitovu cha kuendelea kuhakikisha kwamba tunalitambulisha Taifa kwenye riadha huko duniani na kuendelea kupata heshima kubwa ambayo wenzetu wameendelea kutuletea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kuchukua nafasi hii kuipongeza sana Serikali kwa kuendelea kufanya vizuri. Suala la *AFCON* ni jambo kubwa katika nchi yetu. Hapa tunaendelea kuiomba Serikali, Wizara nyingine za kisekta zijipange siyo michezo peke yake. Tunahitaji barabara, maji, umeme wa uhakika, Wizara ya Maliasili na Wizara nyingine zote za kisekta, lazima tusukume suala la *AFCON* liwe ni kielelezo kikubwa katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamwomba sana Waziri wa fedha, jambo hili ni jambo ambalo linakwenda kuitambulisha zaidi Tanzania duniani. Kwa hiyo, tunaiomba sana Wizara ya Fedha ijiwekeze kikamilifu ili wageni wanapokuja hapa waondoke na kielelezo kizuri cha Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe sana Waziri, tukienda kwenye mikutano, ama mbio za mwenge, ama vitu kadhalika huko vijijini kitu cha kwanza kinachofanyika ni kuleta wasanii wakati tukio husika likiwa linasubiriwa. Suala la usanii na utamaduni wetu, tuombe sasa Maafisa Utamaduni katika ngazi za wilaya, wasanii wale wachanga wa huko chini wasitumike kipindi cha mwenge na baada ya mwenge kupita shughuli inakuwa imekwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sana tuinue kule chini kwa Maafisa Utamaduni kuwe na mashindano hata ya Kitaifa

ambayo yataanzia ngazi ya wilaya, mkoa hadi Taifa ili kuweza kuhakikisha kwamba, mbina zinachezwa vizuri, ngoma za Kinyaturu zinachezwa vizuri, Kibarbaig na makabila yote katika Taifa letu...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** ... waweze kupata fursa ya kujiona kwamba na wao Wizara ya Michezo inaendelea kufanya vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kusema kwamba ninaiunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia moja kwa kazi kubwa anayoifanya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, lakini viongozi wa Wizara ya Habari, Utamaduni Sanaa na Michezo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nilimwita Mheshimiwa Asha Juma Kombo, atafuatiwa na Mheshimiwa Dotto Jasson Bahemu na Mheshimiwa Onesmo Merdson Mnkondya ajiandae

**MHE. ASHA JUMA KOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa na nafasi hii adhimu kwa upande wangu ili niweze kuchangia hotuba hii ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo. Awali ya yote, ninapenda nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya na uzima na hatua ya kuweza kuwa miongoni mwa Wabunge wa Bunge hili la Kumi na Tatu na kuweza kusimama hapa mbele yako ili niweze kuliwakilisha Jimbo langu la Mfenesini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila kusahau kwa heshima zote ninapenda niwapongeze viongozi wangu wakuu, kwa kuanza na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi yake nzuri anayoifanya na kwa upande wa Zanzibar Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi kwa kazi yake ya mfululizo anayoifanya ya kuibadilisha Zanzibar na kuwa Zanzibar mpya. Ninawaambia kazi wanayoifanya ni ya kutukuka na inatupa heshima, kwa hivyo ninawaambia ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nafasi ya kipekee ninapenda kuwashukuru sana wapigakura wangu wa Jimbo la Mfenesini na wananchi wote kwa ujumla kwa kunichagua kwa kura za kishindo na kuona ninafaa kuwa mwakilishi wao wa kuweza kuleta zile changamoto zote zinazotukabili Jimbo letu la Mfenesini. Ninawaambia kwa heshima zote kwamba sitawaangusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda vilevile kuwashukuru wana-CCM wote kwa ujumla na wananchi wote mpaka wapinzani kwa kukiona Chama Cha Mapinduzi kinafaa kwa imani kubwa kilichoonesha na kwamba kinaweza kulivusha Taifa hili na kuleta maendeleo ya kishindo. Kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Mfenesini, ninapenda kuipongeza sana Wizara hii ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa kazi nzuri wanayoifanya na kuwasilisha hotuba iliyosheheni maono na matumaini kwa wananchi wetu wa Tanzania, ili kuweza kulivusha Taifa hili liwe lenye maendeleo ya haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda vilevile, kumpongeza Waziri Makonda na Naibu wake kwa ukakamavu waliokuwa nao, na kwa vile nilikuwa mjumbe wa Kamati hii ya Elimu nimeona kwa macho yangu mambo wanayoyasimamia, *speed* wanayoenda nayo ni kubwa sana na yenye matumaini, ninawaambia hongereni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na imani kubwa waliyonayo wananchi wangu wa Jimbo la Mfenesini kwa viongozi wao na kwa Waziri na Naibu wa Wizara hii ya Habari, Utamaduni na Sanaa, kwa vile wameona wana vijana wenzao, Mheshimiwa Paul Makonda na Mheshimiwa Mwinjuma, wamepata nguvu na kuona sasa katika uwanja huu wa michezo kwamba, shida imekuwa historia. Kwa niaba yao, wamenituma niwawasilishie, ama nitoe historia ama utayari tulionao jimboni kwetu katika kujikita katika michezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka hivi sasa tumejitahidi kuchekecha ama kufanya mashindano katika timu zetu 12 tulizonazo ndani ya Jimbo la Mfenesini ambazo zimesajiliwa na *ZFF* kwa kule Zanzibar. Tumefanya *competition* hiyo ya kutafuta timu

ya Jimbo la Mfenesini. Mashindano ambayo yalisimamiwa na viongozi kutoka *ZFF* katika kuchagua timu ya watu 25, ambayo itaweza kulivusha Jimbo la Mfenesini na hatimaye Tanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatukuishia hapo katika kuchekecha na kupata hiyo timu ambayo tunaiamini kwa baadaye inaweza ikalivusha Jimbo la Mfenesini. Tumetoa mafunzo pia kwa watu wetu 19, mafunzo ya ukocha katika timu hii ya watu 19, wakiwemo walimu wa michezo wa skuli saba za Jimbo la Mfenesini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumefanya hivi kwa makusudi, kwa kuona kwamba walimu hivi sasa umefika muda wasisome somo hili la michezo kwa mazoea, wasome kwa weledi na kujiamini ili waweze kuwafundisha watoto michezo, wawe watoto bora katika michezo, waibue vipaji, waendeleze vipaji kwa kujiamini na hatimaye Taifa lione faida inayopatikana kupitia walimu hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la kutoa mafunzo haya ya ukocha ni kuwawezesha wanafunzi wetu kushiriki katika michezo ya UMITASHUMTA, UMISSETA, elimu bila ya malipo na hatimaye *Olympic* Mungu akitujalia, kwa lengo la kuipata ushindi Taifa letu kwa nyanja hii ya michezo. Wamenituma niombe Wizara hii kama kuna neno lolote la kusema kwa kupitia Waziri Makonda, aweze kusema neno kama itakuwa kama kuna mpango wowote, ama *plan* yoyote iliyopangwa kwa ajili ya ku-*support* yale majimbo ambayo tayari yameshaanza kujikita katika michezo na kupenya hadi katika shule za msingi na sekondari tuweze kuipata fursa hiyo kwa kutambua kwamba michezo ni gharama na gharama kubwa ambayo sisi kama Wabunge hatutoweza kuimudu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, tunaiomba Serikali kwa kupitia Wizara hii, ikiwezekana itutafutie ufadhili ili waweze kutu-*support* katika ndoto yetu ya kuwa na *sports academy* ya kuweza kuwakuza watoto wetu katika michezo kitaalam kuanzia katika *age* ya miaka 19. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kabisa, ningemwomba Waziri Mheshimiwa Makonda akipata nafasi na kama ikimpendeza aje atutembelee Jimbo la Mfenesini, akutane na wanamichezo ili wazidi kuhamasika katika kujikita zaidi katika michezo. Tunafanya hivi kwa makusudi nikiwa kama kiongozi, ili kuituliza jamii yetu ya Jimbo la Mfenesini na hasa vijana wasiweze kuingia katika wimbi hatari la dawa za kulevya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja ya Bajeti ya Wizara hii ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nilimwita Mheshimiwa Dotto Jasson Bahemu, atafuatiwa na Mheshimiwa Onesmo Merdson Mnkondya na Mheshimiwa Fadhili Ally Liwaka, ajiandae.

**MHE. DOTTO J. BAHEMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika Wizara yetu ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo. Mwanzo kabisa kabla sijaanza kuchangia naomba nikutaarifu kwamba, mimi pia, ni mwanahabari. Nimetoka chumba cha habari kwenda kugombea Ubunge kwa hiyo, nimetoka kwenye habari nikaenda kwenye Ubunge moja kwa moja kwa hiyo, masuala yote ambayo yanahusu habari, hata kama siyafahamu kwa kina sana, lakini angalau ninajua vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nianze kwanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Waziri amekuwa ni mbunifu katika maeneo mbalimbali ambayo amekuwa akipita na mimi binafsi nimefanya naye kazi akiwa Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni, nimefanya naye kazi akiwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam. Baada ya pale akaenda benchi tukapotezana kidogo kwa sababu, nilikuwa na kazi yeye hakuwa na kazi. Akatoka akawa Katibu Mwenezi wa Chama Cha Mapinduzi, nimefanya naye kazi, lakini vilevile sasa hivi ambapo pia, ni Mheshimiwa Waziri ninashukuru kwamba, nafanya naye kazi nikiwa Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi chote ambacho nimefanya naye kazi, nimeshuhudia jinsi gani ambavyo ni mbunifu. Sisi vijana ambao tulikuwa tunamsaidia katika kutekeleza baadhi ya vitu ambavyo alikuwa anavifanya tunamshukuru kwamba, tulikuwa tunakaa na mtu ambaye unaona anawaza vitu kwa namna ya kipekee, namna kitofauti na hata sisi tunafurahi sana kwenda kutekeleza yale mambo ambayo anakuwa ametuomba twende tukayafanye. Kwa hiyo, ninampongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kusema hivyo, ninajua akiwepo Mheshimiwa Waziri Paul Makonda, Mheshimiwa, Naibu Waziri, Hamis Mwinjuma, ambaye naye katika eneo la sanaa amefanya vizuri kwa kipindi cha muda mrefu pamoja na kwamba, anaonekana bado ni kijana mdogo, lakini kwa sanaa ni *legend* kwa hapa Tanzania. Vilevile wanaye Katibu Mkuu, ambaye anaifahamu vizuri sana sekta na Taaluma ya Habari, ambaye amekuwa ni mwanahabari mwenzetu, ambaye ametokea pia, Chumba cha Habari; mpaka hapa alipo amefika kwa kupitia katika Taaluma ya Habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaamini kwa utatu huu wakisaidiwa na watu wengine wanaosaidia katika Wizara. Ninaamini Wizara yetu sisi, kama wanahabari, itakwenda mbele zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nimesikiliza michango tangu asubuhi. Niseme ni kwa bahati nzuri au bahati mbaya kwamba, Wizara yetu ni kubwa, ina habari, utamaduni, sanaa na michezo vilevile, lakini Waheshimiwa Wabunge wengi wamezungumza sana upande wa, aidha sanaa au michezo. Sasa sisi ambao ni wachache, wanahabari, ninaomba angalau tupate nafasi hii kuzungumzia kidogo kwenye sekta ya habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan. Wakati anaingia madarakani sisi ambao tulikuwa ni waandishi wa habari tuliona ni kwa namna gani ambavyo taaluma ile ilibadilika na tukatoka

katika kipindi ambacho tulikuwa tunafanya kazi katika mazingira magumu na tukaenda katika kipindi ambacho tulikuwa tunafanya kazi katika mazingira ambayo ni rafiki sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumetoka katika kipindi ambacho tulikuwa tunaitwa kwenda kutoa maelezo unaamini kwamba, ninaenda kufungwa pingu, ninaenda kufungiwa, lakini tukaenda katika kipindi ambacho ukiitwa kwenda kutoa maelezo *TCRA*, unaenda kupongezwa kwa kazi nzuri, ambayo umeifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni mabadiliko makubwa sana ambayo yamefanywa na Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan. Ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge kuna watangazaji wengi sana ambao mlikuwa mnawasikia katika kipindi cha nyuma, ambao sasa hivi inawezekana hamuwasikii; wapo ambao wametoka kwenye taaluma zao ama kwenye hii kazi kwa sababu mbalimbali, lakini wapo ambao wametoka kwa kulazimika kutoka kulingana na Sheria ambayo ilitungwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ile siyo mbaya ni nzuri na sisi, kama Waandishi wa Habari, tunaipongeza kwa sababu, inatengeneza mazingira ya taaluma yetu ya habari kwenda kuheshimika siku za usoni. Leo ninavyozungumza ninaamini baada ya miaka mitano ijayo mwandishi wa habari atakuwa akisimama akizungumza anaonekana kweli mtu amezungumza, ambaye ana kazi yake ambayo inaeleweka kwa sababu ya ile sheria, ambayo inakwenda kutulinda sisi waandishi wa habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati ambapo wameingia katika kipindi hiki ninawashukuru sana. Waziri amezungumza vizuri kwamba, wale waandishi wa habari wenzetu ambao sasa hivi hawapo kwa sababu ya matakwa ya kisheria ya kutokuwa na ithibati, ni kwa namna gani ambavyo atakwenda kuona siku za usoni watarudi kujiunga na sisi, ili waendelee kufanya kazi wapate vipato na waweze kuendesha familia zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tuwe na namna ya kutengeneza mazingira ya kwenda kuwasaidia kwa sababu, wale ambao wametoka siyo muda mrefu kuna waandishi wamefanya

kazi kwa miaka mingi, lakini sasa hivi hatuko nao. Waziri amezungumza vizuri kwamba, wanatengeneza utaratibu wa kwenda kuwasaidia, kwenda kuwarudisha katika ajira zao baada ya kuwa wamewatengenezea utaratibu mzuri wa kwenda kuwapa ithibati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tangazo lile lilivyotoka kuna waandishi ambao walilazimika kutoka kwenye ajira zao, vyombo vyao vikawaondoa kwamba, waende sasa wakapambane, kwa ajili ya kutafuta ile ithibati kwa hiyo, wakatolewa kwenye *payroll* na mikataba yao ikasitishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi Waziri anavyozungumza kwamba, wanaenda kutengeneza mazingira mazuri ya kwenda kutafuta namna ya kuwarudisha lazima pia, wakumbuke kwamba, zile ajira walizokuwanazo huku nyuma sasa hivi hazipo tena. Kwa hiyo, watakapotafuta namna ya kwenda kuwapa ithibati, Mheshimiwa Waziri tunajua Waziri na wasaidizi wake wote ni wabunifu, basi watafute namna ya kuwasaidia wale wengine ambao sasa hivi wako benchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna watu ambao wamefanya kazi miaka 30, miaka 25, wengine hawana taaluma ya uandishi wa Habari, lakini wana taaluma nyingine. Watafute namna ya kuwasaidia kwenda kulinda zile ajira zao ambazo zimepotea. Sote tunaamini Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ni kipenzi cha wanahabari na angependa kuona hakuna ajira ya Mtanzania yeyote ambayo inapotea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapotuona sisi waandishi wa habari tunavaa vizuri, tunapendeza, tunajipenda sana na huwa tunakaa hata sehemu ambazo wanakaa watu wa juu, tunakaa meza moja, lakini haimaanishi kwamba, tuna maisha mazuri, kama waliyonayo wale ambao tunakaa nao meza moja. Waandishi wa habari hali zetu ni ngumu sana kiuchumi kulingana na zile sehemu ambazo tunafanyia kazi. Vyombo vya habari ambavyo tunavifanyia kazi hali zao za kiuchumi ni mbaya sana kwa sababu mbalimbali, lakini moja ya sababu kubwa ambayo

tunaizungumza ni, vyombo vyetu vya habari havijatengenezewa mazingira mazuri ya kufanya biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile ambavyo vimetengenezewa mazingira mazuri ya kufanya biashara vinakopwa na Serikali, lakini Serikali hiyo hiyo inachelewa sana kwenda kulipa yale madeni. Kwa bahati mbaya, ukichelewa kulipa chombo cha habari madeni *TRA* hatajua kwamba, unaidai Serikali, umechelewa kulipa, *NSSF* hatajua kwamba, unaidai Serikali umechelewa kulipa, yeye atakuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wewe ambaye unamiliki chombo cha habari ni lazima utengeneze mazingira ya kuilipa Serikali, lakini katika mazingira ya kuilipa Serikali ambaye utamdanganya ni mwandishi wa Habari, yule ambaye umemwajiri kwa hiyo, atakaa mwezi wa kwanza, mwezi wa pili, mwezi wa tatu hajalipwa. Kwa hiyo, ninakuomba Mheshimiwa Waziri, wakati wa nyuma kidogo kuna kamati iliundwa, ambayo ilikuwa mahususi, kwa ajili ya kupitia uchumi wa vyombo vya habari na kwenda kutoa mapendekezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ile kamati ilimaliza kazi yake na yale mapendekezo yalitolewa. Tunamwomba Mheshimiwa Waziri arudi kule Wizarani akaombe taarifa ya ile kamati, ambayo ililetwa. Akaangalie ni vitu gani ambavyo vilikuwa vimeandikwa ama vilikuwa vimependekezwa katika ile kamati, ili aende akaifanyie kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miongoni mwa mambo ambayo yalipendekezwa ni kwenda kulipa madeni ya vyombo vya habari ambavyo vinadai, lakini vilevile vyombo vya habari kwenda kukopeshwa mikopo rafiki, mikopo ambayo haina ugumu kuipata, ambayo itakuwa na riba nafuu, ili vyombo vya habari vikope viende kufanya kazi na wananchi, sisi Watanzania waandishi wa habari tuweze kulipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana Mheshimiwa Waziri. Kama ambavyo Waziri amepambana amepata shilingi bilioni 20, kwa ajili ya kuwakopesha watengeneza maudhui,

anashindwa nini kutafuta fedha nyingine, kwa ajili ya kwenda kutafuta mikopo ya kuvikopesha vyombo vya Habari?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu, hivi vyombo vya habari ndivyo ambavyo vinakwenda kufanya au vinakwenda kuelezea yale mazuri ambayo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameyafanya. Wanafanya kwa uzalendo wao, lakini tunatengeneza mazingira ya kuvidhibiti vyombo vya habari vya ndani, wakati huo tunasahau kwamba, kuna vyombo vya habari vya nje ambavyo vinaweza vikatufikia kirahisi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano tu ni vurugu zilizotokea wakati wa uchaguzi. Vyombo vya habari vya ndani tunashukuru walikuwa wazalendo wakakaa upande wa Taifa, lakini ukija kuangalia kuna vyombo vya habari vya nje ambavyo ndivyo vilileta taarifa ambazo ni za uongo, ambapo tumetengeneza mazingira ya kuwadhibiti hawa ambao watakuwa wazalendo, lakini wale wengine ambao watakuja kuleta taarifa za uongo hatuna *access* ya kuweza kuwadhibiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwomba Mheshimiwa Waziri, yeye amekuwa ni rafiki wa wanahabari, Mwana-FA, Mheshimiwa Naibu Waziri, amekuwa ni rafiki wa wanahabari na Katibu Mkuu ni mwanahabari mwenzetu kwa kipindi cha muda mrefu. Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, alivyoingia watu ambao aliwatengenezea mazingira ya kunyosha vitu haraka haraka walikuwa ni waandishi wa Habari kwa hiyo, tunaamini hata haya mambo mengine hawawezi kushindwa kwenda kuyafanya. Tunaamini, muda siyo mrefu basi angalau hata sisi wanahabari tutakuwa tunashukuru kwamba, maisha yetu yanakwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia ninaomba nitoe pendekezo moja la mwisho kabisa. Vyombo vya habari vya kielektroniki, kwa maana ya televisheni na redio, wao wanawajibika kwenye Kamati ya Maudhui ya TRA...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, muda wako umekwisha.

**MHE. DOTTO J. BAHEMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuunga mkono moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nilimwita Mheshimiwa Onesmo Merdson Mnkondya, atafuatiwa na Mheshimiwa Fadhili Ally Liwaka na Mheshimiwa Elibariki Immanuel Kingu, ajiandae.

**MHE. ONESMO M. MNKONDYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia Hotuba yetu hii ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo. Kwanza ninaipongeza Wizara, chini ya Mheshimiwa Paul Makonda Christian na Naibu wake, kaka yangu, Mheshimiwa Mwana-FA. Utendaji wao hao watu tunaufahamu, kazi zao zinasema na usimamizi wao ni mkubwa kwenye Wizara hii kwa hiyo, hilo tuwapongeze sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza pia, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuwa mdau namba moja wa michezo kwenye Taifa letu. Kwa kweli, Mheshimiwa Rais wetu anatukosha moyo sisi, kama vijana, anafanya kazi nzuri na ndiyo maana kwenye Wizara hii ameleta vijana wachapakazi, vijana nguli kabisa, Mheshimiwa Makonda; sisi Watanzania tuna imani na wewe sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati ninataka kuchangia hotuba hii tunaye Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Elimu, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mheshimiwa Husna Sekiboko, kwa kweli naye ninampa pongezi zake. Anaweza mama huyu, ametusimamia vizuri, kama Kamati, wameona wakija kwenye Kamati namna ambavyo anatuongoza vyema, kwa ajili ya kuwashauri kwenye Wizara yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza pia, Makamu Mwenyekiti wake kwa kazi nzuri na Kamati yote kwa ujumla kwa kazi ambayo tulikuwa nayo tulipokuwa tunakaa nao vikao. Tunakwenda kupokea *AFCON* na *AFCON* hii inakwenda kuandika historia kwa Taifa letu. Kwa kweli, Mheshimiwa Rais Samia pamoja

na Wizara yetu hii mmekuwa kielelezo ndiyo maana tunakwenda kupokea mashindano haya makubwa Barani Afrika. Si kwa bahati mbaya ni kwa sababu, tumeonesha namna gani Tanzania tumekuwa wana michezo wazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kupitia namna wanavyoisimamia Wizara hii. Kaka yangu Mwana-FA alikuwepo toka mwanzo, ameisimamia Wizara hii akiwa na Mawaziri wengine kwa hiyo, tunakwenda kujivunia kupokea mashindano makubwa ambayo yanakwenda kuwa chachu kwa maendeleo ya Taifa letu kwenye sekta mbalimbali. Kwa kweli, tunakwenda kuwa na kitu cha tofauti kwenye Taifa letu, kwa mara ya kwanza 2027 mambo yanakwenda kuwa *bam bam* Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nishauri kidogo kwenye Wizara hii. Mheshimiwa Makonda, kwanza tunaomba sana kwenye nafasi hii, kama Waziri, ameingia hapo tuna imani kwamba, hili Vazi la Taifa ambalo umekuwa ni wimbo anakwenda kukamilisha mchakato huu, usiishie njiani. Tunatamani anapoondoka kwenye Wizara hii atuambie amekamilisha Vazi la Watanzania ambalo wanalisubiri kwa hamu kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ninatamani nishauri, nimeona namna ambavyo Wizara hii imefanya kazi kubwa, hasa kwenye viwanja ambavyo tumeenda kuvitembelea Arusha pale, amefanya kazi kubwa sana. Uwanja wa Uhuru maboresho ni makubwa mno, shamba la bibi, Uwanja wa Mkapa maboresho ni makubwa, viwanja vya mazoezi tumeona namna ambavyo Serikali yetu inawekeza kwenye michezo. Kwa kweli, kwa hapa ninampongeza Mheshimiwa Rais Samia ameamua kwelikweli Taifa letu liwe la michezo, Tanzania ni nchi ya wanamichezo, vijana tunajivunia sana hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tunapiga kelele juu ya viwanja, Mheshimiwa Waziri Simba na Yanga tumeona jana wanacheza pale Jenerali Isamuyo; kwa kweli, hivi vilabu vimekuwa vikubwa, ifike mahali Wizara kaeni na Simba na Yanga wajenge viwanja vyao. Hivi vilabu ni vikubwa sana Barani Afrika, kuendelea kutegemea hivi, kwa mfano tunapeleka mashabiki

kwenye uwanja ambao unapokea mashabiki 10,000 wakati siku zote tunajaza uwanja mashabiki 60,000 tumewapeleka kule, si sawa! Wajenge viwanja vyao hawa, Simba na Yanga wasiwaache...

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ester Bulaya, Taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kumpa Taarifa Mheshimiwa kwa mchango wake mzuri. Labda hapa aseme Simba, sisi Yanga tayari tumeanza mkakati wetu wa ujenzi wa uwanja na tunajenga Jangwani. Tayari tumekaa kwenye Mkutano Mkuu tumepitisha, tumepata na mtu ambaye anajenga.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mnkondya, unaipokea Taarifa hiyo kutoka kwa Mheshimiwa Bulaya?

**MHE. ONESMO M. MNKONDYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipokea, ninawapongeza kama kweli wameanza kujenga. Sasa na Simba tuanze kuona wanaanza kujenga uwanja wao, tena uwanja wa kisasa, lakini wakati ninampongeza Mheshimiwa Waziri na namna ambavyo unakwenda kupokea mashindano haya ya *AFCON,* ninaomba niseme kwa niaba ya Wanasongwe tena hapa…

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. ONESMO M. MNKONDYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wanaotoa Taarifa walinde muda wangu.

**MWENYEKITI:** Hebu subiri. Mheshimiwa Sanga, Taarifa.

## TAARIFA

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninatoa Taarifa, hoja ya mzungumzaji ni nzito na ninaweka wazi kwamba, Simba walianza kuwa na uwanja pale Bunju, kuliko timu yoyote. Kwa hiyo, hoja yake ijikite kwenye ile timu ambayo hadi sasa haina uwanja, lakini kwa Azam, Singida na Simba ni vilabu vya mfano kwamba, vina viwanja vyao, lakini kwa, hiyo timu nyingine ambayo ilikoswakoswa jana, labda iwe ndiyo hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mnkondya.

**MHE. ONESMO M. MNKONDYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipokea, lakini tulinde muda wangu. Hata kama wameanza kujenga Bunju ni muda mrefu sana Simba na mimi ni Mwanasimba, hatuna uwezo wa kupeleka mashindano tukacheze kule, hata ligi kuu, tunacheza viwanja vingine. Kwa hiyo, msimamo wangu uko palepale Simba tujenge uwanja wetu, uwanja bora ambao tunaweza tukaenda kupeleka mashindano makubwa huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nizungumze juu ya Wanasongwe. Tanzania hii Mheshimiwa Paul Makonda anaweza kwenda mkoa wowote na wasimdai uwanja wa mpira, lakini Mkoa wa Songwe kwa kweli, tutamdai. Mimi ni mdau namba moja wa michezo na maendeleo Mkoa wa Songwe na nimekuwa ninaunganisha vijana kupitia Mashindano ya *MOSE Super Cup,* maana yake *Mnkondya Onesmo Combine* au *Unity,* lengo ni kuhamasisha Mkoa wa Songwe tupate timu ligi kuu, lakini pia, Mkoa wa Songwe tupate uwanja, hatuna uwanja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Mheshimiwa Waziri nimemwomba kwamba, atukumbuke Mkoa wa Songwe tupate uwanja. Akija Mbeya, akienda Katavi, akienda Iringa, akienda Njombe, akienda Morogoro, akienda Dar es Salaam, Arusha na kwingine wanavyo viwanja, Songwe tu tumebaki. Vijana wanamwamini Mheshimiwa Rais na tuna imani, tunaomba Songwe watuangalie tupate uwanja wa michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kule Songwe tuna vivutio vingi, tuna kivutio cha kimondo Kata ya Mlangali, wanakifahamu kimondo cha Mbozi. Tuna kivutio cha maji moto Kata ya Nanyara, wanakifahamu. Tuna kivutio cha makaa ya mawe. Tunatamani sasa michezo Mkoa wa Songwe iwalete wawekezaji, iwalete wageni kuja kuangalia hivi vivutio, nini kitawaleta, ni pamoja na michezo mkoa huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Songwe ni lango kuu la *SADC,* tunapokea Mataifa kupitia mlango wa biashara, pamoja na njia ya usafiri. Tunapokea Zambia, Malawi, Congo, South Africa na Zimbabwe, Mataifa matano, lakini haya Mataifa yakifika kule hatuna uwanja! Tunaweza tukavutia wageni hao, wakifika hapa wanapumzika kuangalia soka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niseme, wakati Songwe inazaliwa miaka 10 sasa; tunapoomba mpira, tunapoomba uwanja wa michezo kwenye mkoa wetu na kama mdau namba moja, ninaomba Mheshimiwa Waziri anishike mkono kijana wako. Anishike mkono anipe hata uwanja wa mazoezi wa kuanzia, vijana wetu wapate ajira pale, akinamama wafanye biashara, Mkoa wa Songwe uchangamke. Simba na Yanga wanapokwenda kucheza, mara nyingi wanacheza kulekule Katavi…

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. ONESMO M. MNKONDYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wanapita pale, wanaanza kufanya mazoezi kule. Zambia wanaacha kufanya kwenye mkoa wetu, kwenye Taifa letu, walete mapato kwenye nchi yetu. Ninamwomba sana Waziri anishike mkono, kama mdau wa michezo namba moja Mkoa wa Songwe, Wanasongwe tupate uwanja angalau hata wa mazoezi. Ninaamini atakuja Mkoa wa Songwe kama nilivyomwomba, atakuja ajionee mwenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na ninapenda kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, ninakushukuru sana. Nilimwita Mheshimiwa Fadhili Ally Liwaka, atafuatiwa na Mheshimiwa Elibariki Emmanuel Kingu na Naibu Waziri, Mheshimiwa Hamis Mohamed Mwinjuma, ajiandae.

**MHE. FADHILI A. LIWAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa siku hii tena ya baraka, niungane na Wabunge wenzangu, kwanza kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii, kaka yangu na ndugu yetu Mheshimiwa Paul Christian Makonda kwa kazi kubwa ambayo ameanza nayo kwenye Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri atakubaliana nami kwamba juu ya namna ya kutekeleza wajibu kwa Mheshimiwa Paul Makonda siyo jambo lenye mashaka hata kidogo, unachotakiwa kufanya ni kumpa kazi tu jinsi ya kupendezesha kazi, kuifanya ivutie na kuifanya iwe bora hilo ni jukumu ambalo amekuwa akilionyesha kila wakati alipopata nafasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana pia Mheshimiwa Naibu Waziri Ndugu yetu Mwinjuma kwa kazi nzuri ya kumsaidia Waziri, lakini kwa kuendelea kuaminiwa na kutimiza wajibu wake vizuri kwenye eneo hili la Wizara ya Utamaduni, Habari, Sanaa na Michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nina maeneo mawili ya kuchangia. Eneo la kwanza ni juu ya uboreshaji na ukuzaji wa vipaji katika maeneo mbalimbali nchini ikiwemo Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo wakati Baba Levo anachangia hapa ndani ilikuwa kama anazungumza jambo ambalo linachekesha, lakini ni ukweli usiopingika kwamba tunahitaji vipaji kutoka kwenye ngazi ya Majimbo, Halmashauri na Mikoa yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nyenzo ya kufikia hatua hiyo sisi kama nchi tunayo na kwa bahati nzuri sana Wizara hii imepata Waziri mwenye uthubutu, mwenye kujaribu, mwenye kufanya,

mwenye kuamua, hana uwoga, anaweza kuingia kwenye jambo lolote akalifanyia kazi kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri zetu zina uwezo wa kumiliki viwanja vya michezo. Kila Halmashauri nchi hii ina uwezo wa kutenga fedha na kujenga viwanja vya kisasa vyenye *level* inayofanana na *KMC* ambayo imejengwa pale Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefurahi kwenye hotuba Mheshimiwa Waziri ameweka wazi nia ya kuzungumza na Wizara ya Ofisi Waziri Mkuu, TAMISEMI ili kuweza kuwa na makubaliano ya kufanya jitihada ya kutenga fedha ili kuweza kupata viwanja kwenye Halmashauri zetu.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Taarifa.

**MHE. FADHILI A. LIWAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka niungane na Mheshimiwa Waziri kwenye jambo lake na ninataka nishauri kama Bunge lako litaona inafaa, kama vile tulivyokuwa tumewaza na kuwafikiria vijana katika asilimia zao, wanawake katika asilimia zao na walemavu katika asilimia zao. Ni wakati wetu sasa kama Taifa kufikiria eneo la michezo katika asilimia kupitia pato la halmashauri na jambo hili lililetwa hapa Bungeni tuje tulijadili na tukubaliane na ikibidi tuweke sheria maalum itakayosukuma kila halmashauri nchini kutenga fedha kwa ajili ya kukuza michezo na kuendeleza maeneo ya michezo mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, michezo ni biashara, michezo ni uchumi. Leo wakati tunahangaika kulitazama Taifa juu ya viwanja, Mheshimiwa Mbunge ametoka kuzungumza hapa anaombwa kuungwa mkono, nina ushahidi na nimeshiriki ujenzi wa kiwanja kwenye Halmashauri wakati ninatumikia Wilaya ya Ruangwa. Uwanja wa Kassim Majaliwa ulijengwa kwa uthubutu wa Halmashauri kupitia makato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri wakinikubalia mimi ninataka niwahakikishie viwanja nchi hii vinaweza kujengwa kila Halmashauri. Jambo lake ni moja tu aende na hii ninataka

niiweke vizuri waielewe na dunia ielewe. Aende kwenye ofisi za Chama Cha Mapinduzi, wana vijana wanao uwezo wa kujitolea wakakaa kambi wakafanya kazi wakashiriki tukamaliza kupata viwanja. Ruangwa ni mfano wa jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna sababu ya kupata viwanja ili michezo yetu ikue. Tunayo sababu ya kupata viwanja ili tupate wachezaji wazuri. Tunayo sababu ya kupata viwanja ili tukuze uchumi wa Halmashauri na twende katika *level* inayofanana na dunia ya sasa kwenye eneo la *sports*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninafikiri sambamba na jitihada zetu za ndani, lakini hili ni takwa la ndani kabisa katika programu za Afrika kupitia *AU. African Union Framework* inaweka wazi kabisa kwamba ni sharti la msingi katika kila Halmashauri na Serikali za mitaa kuwa na maeneo ya kuchezea michezo mbalimbali ikiwemo viwanja vya mpira. Hili ndiyo lilikuwa eneo langu la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili, ninaomba nichangie kuhusiana na filamu. Waziri atakubaliana nami kwamba filamu zinatangaza nchi. Filamu zinakuza uchumi. Filamu zinatoa ajira. Leo hii kuna watu wanaijua Ikulu wa Marekani siyo kwamba wamefika. Kuna watu wanaijua India siyo kwamba wamefika. Kuna watu wanaingilia *Hong Kong*, wanaijua *Philippines* na nchi zingine kadha wa kadha ambazo zimewekeza vizuri kwenye filamu. Sababu ni moja tu. Nchi zao zimetoa fursa ya kutosha na kuwapa uhuru wasanii kuweza kutengeneza filamu bora na zenye *quality* ya hali ya juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka niweke rekodi yangu sawasawa. Ninachangia mchango huu na kutoa ushauri huu nikiwa ninafahamu kabisa yako masuala ya kiusalama, ulinzi wa matumizi ya nembo, vifaa vya kijeshi na mavazi ya majeshi mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa nchi yetu haitafuti wasanii wakubwa tunao tayari. Kwa sasa nchi yetu haitafuti maudhui mazuri ya kucheza, tayari yapo. Watu kama kina Jacobo

Stephen, Vincent Kigosi, Clam Vevo na wengine wengi hawa akina Lamata wamefanya kazi kubwa ya kuisogeza filamu kutoka chini kuwa filamu ya kimataifa. Kwa nini hatupati soko la kutosha katika maeneo mengine kama *Netflix* na chaneli zingine kubwa kubwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu ni moja, tumekuwa na ugumu wa matumizi ya vifaa vyenye uhalisia ikiwemo sare za kijeshi, silaha za kutengeneza zinazofaa kwa filamu, pamoja na maeneo mbalimbali yanayofaa kutumika kwa ajili ya kuchezea filamu zenye uhalisia ikiwemo mahakama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ombi langu kwa nchi yangu tuone sasa huu ni wakati wa kuwafungulia wasanii, tukiwa tumeweka vigezo na kuwekea masharti ya msingi yatakayosimamia masuala ya usalama kwa kulinda hivi vitu nilivyovisema hapa ikiwemo mavazi watakayoyatumia, maeneo watakayotumia na silaha watakazozionesha katika filamu zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunatamani wasanii wetu wanapokwenda Ghana, Serikali isimame wajue kuna msanii ameingia kwa sababu ya umashuhuri aliouonesha kwenye kazi ya sanaa. Leo hii tunatamani wasanii wetu wanapokwenda kwenye tuzo tuwe na uhakika wa kushinda tuzo kubwa na iwezekane. Leo tunatamani wasanii wetu wanapokwenda kwenye mashindano ya filamu waingie kwenye *category* zinazotosha na tuweze kupeperusha bendera ya nchi yetu vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa unyenyekevu mkubwa sana na mimi ninaweza kubeba dhamana ya wasanii hawa, nimefuatilia kazi zao nimeziona na nimetazama misingi waliojiwekea kwenye kujenga ukubwa wa filamu zetu kwa sasa inatosha kabisa kuwapa imani ya kutumia rasilimali za kijeshi, kutumia rasilimali za kiusalama, kutumia majengo ya Serikali na kutengeneza *movie* za uhalisia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nikupe tu mfano mmoja. Mheshimiwa Rais wakati anazindua Bunge letu na anatuhutubia hapa, aliweka wazi kwenye hotuba yake kwamba anakwenda

kufungua studio itakayosaidia uzalishaji wa filamu bora. *Studio* hizi ndimo zinakozaliwa haya mambo yote ninayoyasema hapa. Nimwombe sana Waziri katika jambo na kuomba alicheze kwa akili kubwa na kutuachia alama ni upatikanaji wa studio ya uzalishaji wa filamu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukipata *studio* tutapata filamu bora. Tukipata *studio* tutaweza kutumia haya mavazi niliyoyaomba, silaha nilizozisema na maeneo ambayo tunaona kwamba yana ugumu katika upatikanaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, filamu zetu kwa sasa zimepiga hatua kubwa sana. Wasanii wetu wamepiga hatua kubwa sana. Tunatamani kuchochea pato la nchi hii liweze kuwa kubwa na eneo la filamu na sanaa liwe ni chachu kubwa ya uzalishaji kama yalivyo mataifa mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kuomba tena kwamba eneo la sanaa ni eneo mtambuka, eneo hili tunalitumia vizuri. Moja kuleta umoja wa kitaifa, sanaa inaleta mshikamano. Sanaa inatatua changamoto ya mambo magumu ambayo yanafikirika kwa shida, sanaa inaleta mataifa mengi pamoja na kutengeneza utambulisho wa Taifa letu. Lazima tuilinde sanaa, tuienzi sanaa, tuipende sanaa na tuipe nafasi ya kuweza kuonekana katika ulimwengu wa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninakushukuru kwa nafasi na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nilimwita Mheshimiwa Elibariki Immanuel Kingu atafuatiwa na Mheshimiwa Hamis Mohamed Mwinjuma.

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, neno la Bwana kutoka Kitabu cha Kutoka 35:30 - 36 linasema: "Ndipo Bwana akamwambia Musa tazama nimekuchagua nimekuchagulia Bezaleli mwana wa Uri, mwana wa Huri wa kabila la Yuda. Naye amemjaza Roho ya Mungu pamoja na ustadi na uwezo na ujuzi katika aina zote za ufundi ili kubuni michoro ya

kupendeza katika ufundi wa dhahabu, fedha na shaba kuchonga vito na kuvitia mahali kufanya ufundi kwa mbao na kujishughulisha na aina zote za ufundi. Tena basi nimemteua Oholiabu mwana wa Ahisamaki wa kabila la Dani ili kumsaidia huyo niliyemteua". *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mbunge ninayetokana na Chama Cha Mapinduzi, lakini mimi ni Mbunge ambaye nimesoma kwa kodi za wanyonge walipakodi wa Taifa hili. Mimi ni Mbunge ambaye kwa neema ya Chama hiki Cha Mapinduzi na Bunge hili nimeweza kupata *exposure* kubwa duniani katika kulitumikia Taifa kwa sababu ya kodi za Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nimwambie hii ni mara yangu ya kwanza kusimama kuchangia kwenye bajeti ya Wizara hii toka nimekuwa Mbunge kwa miaka 10. Ninataka niseme kwa dhati ya moyo wangu, Waziri yeyote anayefanya kazi ya kumsaidia Rais Samia, Waziri yeyote anayefanya kazi ya kuleta ndoto za kutimiza Ilani ya Chama kilichotupa ridhaa ya kuwatumikia Watanzania, *from the bottom of my heart*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninajua Mawaziri wengi wanafanya kazi hiyo wakiwemo akina Mavunde vijana, wakiwemo akina Deo na leo tuko kwenye Wizara ya kaka yangu Makonda na Mwana-FA. Ninataka niseme kwa dhati ya moyo wangu, kaka yangu Makonda pamoja na Mwana-FA nimewachagulieni fungu la Kutoka nikimnukuu mtumishi wa Mungu Musa yeye na msaidizi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninataka niseme kwa dhati ya moyo wangu mimi ni Mbunge ninayeamini katika matokeo na ubunifu. Kwa muda toka umekamata mikoba kutoka kwa Mzee wangu Kabudi, Baba na Kiongozi wangu, ninataka nimpongeze Mheshimiwa Makonda *from the bottom of my heart*. Kwanza kwa namna ambavyo ameweza kuonyesha ya kwamba nini maana ya thamani ya Wizara hii muhimu ambayo kama tukiamua kuitengenezea mikakati, Wizara hii pekee yake ina uwezo wa kuchangia mpaka asilimia saba mpaka tisa ya bajeti ya pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu ninataka niwaambie mimi siwezi kuwa chawa, mimi ni kijana msomi, siyo tu msomi, ninasema kwa neema ya Bwana, mimi Chuo Kikuu nilipeleza pointi mbili kupata *First Class* na kwenye *Masters* nimepata *First Class*, siwezi kuwa chawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni kijana ambaye ninalipenda Taifa langu na ni mzalendo kwa nchi yangu. Kiongozi yeyote akifanya mambo mazuri nitasimama hapa nitapongeza. Kiongozi yeyote akizingua kwa maslahi ya kutokutekeleza Ilani ya Chama changu, nitamchana hapa awe Waziri wa rangi yoyote nitamwambia mchana kweupe, ndiyo wajibu wa Mbunge wa Chama Cha Mapinduzi kwenye Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Makonda ninakupongeza kwa sababu wewe ni kijana unayefanya uthubutu na ninataka nimtie moyo, ushauri wangu wa kwanza achukue karatasi na kalamu twende kazini. Kwanza, tutakapomaliza bajeti hii ninajua alikuwa hajajipanga kaka yangu Makonda aende akaanzishe kitu kinaitwa *National Sport Organization Fund*. Ninataka nimwambie *fund* hii ndiyo imesaidia mataifa makubwa duniani kuweza ku-*finance* shughuli zote zinazo emerge za kimichezo katika mataifa yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwa mataifa kama *Canada*, *China*, *Australia* na watu wataniambia unatoa mfano kwa mataifa yaliyokwenda kiuchumi, ninatoa mifano kwa mataifa yaliyofanikiwa kwenye michezo ambayo ni *model* ya sisi Tanzania kuiga. *Fund* hii Mheshimiwa Makonda atakapoianzisha, ninataka nimhakikishie yatakapokuja mashindano makubwa ya kitaifa na kimataifa wanamichezo watakapopata kazi ya kwenda kushindana kukimbia riadha duniani, hawatahangaika kuanza kuitana tumtafute sijui Bakhresa sijui nani, *fund* hii itawa-*fund* Watanzania kushiriki shughuli zote za michezo duniani na Taifa letu litaweza kupata *prosperity*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nimwambie, Fadhili ameniwahi, Katibu Msaidizi, ninataka nizungumzie suala pia la

*early specialization*, mimi peke yangu mwezi uliopita nime-*finance* vifaa vya michezo vya zaidi ya milioni 22 kwenye Jimbo langu kwa sekondari zote. Je, ni nani yupo kwenye Halmashauri anayefanya kazi ya kuchukua *data* na *logistics*, shule fulani kuna mtoto ana kipaji fulani kwa *database* nchi nzima ili waweze kuendelezwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Makonda aende akaanzishe *database* ya nchi ya kuchukua *statistics* za *early talent* zote za nchi nzima, hii alama atakwenda kuiacha, Rais Samia atamkumbuka, Watanzania watamkumbuka kwa *legacy* ya kazi atakayokwenda kuiacha kwenye Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu ninalotaka kushauri kwa kaka yangu Makonda. Kwanza, ninataka nipongeze sana hiki ambacho amekuja nacho kwenye bajeti yake. Ndugu zangu Wabunge wenzangu nataka niwaambie Taifa hili sisi ndiyo tumekomboa Msumbiji, Namibia, South Africa. Sisi tumemwaga damu Zambia kuhakikisha tunawaunganisha, tumefanya kazi Uganda na mataifa yote yaliyo Kusini mwa Bara la Afrika, Baba yangu Kabudi anaijua hiyo historia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo kitendo cha Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan Mama wa watu jamani hebu tuwe wakweli jamani ndugu zangu Wabunge, kwa kitendo hiki cha kuamua kujenga *center* ya ukombozi ya ukumbusho wa Bara la Afrika, ninaomba Wabunge wa Chama Cha Mapinduzi na upinzani tukiunge mkono, tumtie moyo Rais wetu, jambo hili Rais alilokwenda kulifanya. Ninataka niwaambieni haya ya *instability* yanayoendelea kwenye Mataifa ya Afrika, Tanzania sisi tulionesha mfano, akina Mzee Mangula walilala Msumbiji kuikomboa Msumbiji. Wapo wakina Mzee Kabudi wanajua historia ya Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Makonda kaka yangu hekta 240 ambazo Serikali imezitenga sisi tutamuidhinishia bajeti, waende wakajenge kituo cha heshima kitakachomfanya Baba wa Taifa hayati Julius Kambarage Nyerere ajue kazi aliyoifanya ya ukombozi wa bara la Afrika, yeye na watangulizi wake akina Nelson Mandela, akina Kwame Nkrumah, Patrice Lumumba nenda mkaweke historia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *center* hii, ninamshauri kaka yangu Mheshimiwa Makonda isiwe *center* tu ya kimfano wa kitalii, lakini kaka yangu akafungue vituo kwenye mataifa yote tuliyoyakomboa ya Afrika, watoto wafundishwe, tupate watalii na wageni wa kuja kutembelea *centre* hiyo kwa manufaa ya Taifa letu. Ninampongeza sana kwa hilo na ninamtia moyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kuna jambo lingine mimi linaniumiza moyo na ninamjua jana na juzi nimesikia akilitaja ni jambo la maadili ya watoto wa Kitanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kaka yangu Mwanyika, jambo la maadili ya watoto wa Kitanzania, ninataka nikuambie na nilieleze Bunge lako Tukufu, sisi kama Wabunge wa Chama Cha Mapinduzi tunaotokana na wengi wananchi waliotuleta hapa Bungeni tusipopaza sauti zetu, wakatusikia wale waliotuchagua kwamba tunataka kuwa na Taifa la namna gani katika kutunza na kuhifadhi maadili ya Mtanzania, makaburi yetu yatakuja kuhukumiwa, Mungu siku ya mwisho atakapokuja na parapanda na mwaliko wa ufufuo atakuja kutuuliza maswali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mambo yanaendelea kwenye mitandao ya kijamii, watu wanakuja na *content* zenye maudhui ya kushabikia mambo ya ushoga kwenye Taifa letu. Sisi kama viongozi kuna baadhi ya watu wanashabikia mambo haya. hawajui hatari tunayotaka kulitumbukiza Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unakuta mtu kwenye mitandao ya kijamii kwenye *Instagram*, kwenye *Facebook*, kwenye *Twitter* anajiita kwamba yeye anafanya mapenzi ya jinsia moja na watu wanashabikia tunatengeneza Taifa la namna gani? Tunataka kurithisha watoto wetu nini kwenye Taifa hili? Mama Gwajima Dorothy ninakupongeza sana mama yangu, nimekuona namna gani unatumia muda wako mwingi kuwaelemeisha Watanzania juu ya misingi ya kutunza maadili ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nitoe rai. Mheshimiwa Makonda ninajua alisimama kidete kupambana na mambo ya madawa ya kulevya na Mungu wa Isaka, Ibrahim na Yakobo

hajawahi kumwacha kumpa ulinzi. Ninamwomba kaka yangu na Naibu wake na amepata Naibu mchapakazi, kijana mtulivu na mzalendo. Washirikiane na Mwana-FA, ninamjua mwana-FA nimekaa naye katika Bunge miaka mingi, waende wakahakikishe misingi, tamaduni, desturi na mila za Taifa la Mwalimu Nyerere tunaziacha na kuzirithisha kwa watoto na vizazi vinavyokuja ili tuweze kulilinda Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho lakini si kwa umuhimu, ninataka nimtie moyo Rais Samia Suluhu Hassan...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Muda wako umekwisha, lakini dakika mbili malizia.

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nimtie moyo Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa hiki kinachokuja cha *AFCON*, lakini bado tunalo Bunge la Dunia na Makonda matukio haya mengi yanakwenda kutendeka kwenye Mkoa wake, ninawaomba Watanzania waimarishe amani na utulivu, waendelee kulipenda Taifa lenu, waendelee kuwa wamoja, waendelee kusimamia misingi ya upendo na mshikamano, tuweze kumsaidia Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan amalize vyema kipindi chake cha uongozi. Mungu awabariki. Mungu Ibariki Afrika. Mungu ibariki Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Elibariki Immanuel Kingu, ahsante sana kwa mchango wako. Nilimwita Mheshimiwa Naibu Waziri Hamis Mohamed Mwinjuma. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Ninakushukuru na ninakiri kwamba kuongea baada ya watu kama Mheshimiwa Kingu siyo mchezo. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kama anavyosema Mwalimu wangu Profesa Kabudi kwa ruzuku ya uhai na afya njema iliyotuwezesha kukutana siku ya leo ya tarehe 4 Mei, 2026 kupokea bajeti ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, iliyosomwa na Mheshimiwa Waziri Ndugu yangu MheshimiwaPaul Makonda kuijadili na kama italiridhia Bunge lako Tukufu kuipitisha na kuturuhusu tukafanye utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata ningepewa dakika tatu jambo moja ambalo ningeshindwa kuliacha kulisema katika muda wangu mfupi huo ni kumshukuru Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan na ninajua tunamshukuru Rais kila wakati, lakini ukweli ni kwamba Rais anafanya vitu vingi ambavyo itatuchukua pengine siku nzima kumwongelea yeye na ukubwa wa mambo anayoyafanya kwa nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo matatu ambayo leo ninataka kumshukuru Rais; kwanza, ni jinsi anavyoifanya kazi aliyokabidhiwa na Watanzania kwa nguvu na akili zake zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni la kibinafsi. Nina watoto wawili wa kike, Malika na Ayana. Kwa jinsi Mheshimiwa Rais anavyoifanya kazi ya kuiongoza nchi hii anawaondolea mipaka watoto wetu wa kike ambao ni wajukuu zake, ya kwamba watoto wa kike wanaweza kufanya kazi yoyote ile wanayotaka duniani. Kwa hivyo tunamshukuru. Nichukue fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kutusaidia kulea wajukuu zake wa kike kwa vitendo; ahsante sana Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, hili ni la kibinafsi. Ninataka kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kunipa fursa ya kuwahudumia Watanzania wenzangu. Miaka mitatu na ushee sasa nimekuwa Naibu Waziri kwenye Wizara hii. Ninakiri kwamba ninafahamu ya kwamba ninakaa kwenye Wizara hii kwa utashi na matakwa binafsi ya Mheshimiwa Rais, akinipa fursa ya kuwahudumia Watanzania wenzangu; na kwa hili ninamshukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitoka kwetu Muheza nikiomba ridhaa ya wananchi wenzangu wa Muheza kuwatumikia na kuwawakilisha wao; Mheshimiwa Rais akaona ninaweza kumsaidia na akanikasimia madaraka haya kama Naibu Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo ili nimsaidie kufanya kazi nchi nzima. Hili ni deni kubwa na namna pekee ambayo ninaamini kwamba ninaweza kulilipa ni kufanya kazi hii kwa akili na nguvu zangu zote na kuwa mwaminifu kwa Mheshimiwa Rais; na deni hili nitakwenda nalo kaburini. Ahsante sana Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwashukuru pia wenzangu pale Wizarani. Mheshimiwa Waziri ndugu yangu Paul Christian Makonda ambaye alimpokea mzee wangu Profesa Kabudi, kabla yake Mwalimu wangu Damas Ndumbaro, kabla yake mama Pindi Hazara Chana; na wenzangu wengine pale, kama vile Katibu Mkuu ndugu yangu Gerson Msigwa, Naibu Katibu Mkuu Methusela Ntonda, Wakurugenzi na Wakuu wa Idara kwa ushirikiano mkubwa wanaotupa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tuna Waziri ambaye ni *hands on eyes on*. Niwaambie Waheshimiwa Wabunge kazini kwangu kuna kazi kweli kweli; lakini bado tunaifanya kazi hii kwa utashi mkubwa kama ambavyo tumeaminiwa nayo kwa Mheshimiwa Rais na kuifanya kwa ajili ya Watanzania wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisiache kuwashukuru wananchi wenzangu wa Muheza kwa kuendelea kuniamini na kunipa ushirikiano wa hali ya juu. Wanajua kwamba wanaye mwakilishi, na mimi ni mwenzao na ninaendelea kuifanya kazi yao kwa uwezo wangu wote kwa jinsi ambavyo Mungu amenijalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nijibu hoja chache tu ambazo zimeletwa kwetu na Waheshimiwa wa Wabunge tangu asubuhi ya leo wakati walipokuwa wakichangia hoja ya Mheshimiwa Waziri Paul Makonda, ya jinsi ambavyo wangependa na wangeshauri vile inavyofaa wizara yetu kuendeshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikiri, kwamba kumsaidia kazi Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan ni kazi nzuri na kazi rahisi kwa sababu ya utashi na maono yake; anasaidia kufanya kazi yako kuwa nyepesi; na hicho ndicho ambacho kuwa amekifanya katika miaka yote mitatu ambayo nimekuwa katika Wizara hii. Hata unaweza kuona ushahidi kwa Waheshimiwa Wabunge na Waheshimiwa Mawaziri wa Wizara zote nyingine ambao wakija hapa wanaelezea jinsi ambavyo utashi wa Mheshimiwa Rais umekuwa ukiwarahisishia kazi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeingia kwenye Wizara hii mwaka 2023 bajeti ya Wizara hii ilikuwa bilioni 33. Hivi tunavyoongea Mheshimiwa Waziri ameomba bajeti ya bilioni 525 ongezeko la 1500%. Sisemi kwamba halijawahi kutokea, lakini silikumbuki. Huu ni utashi wa Mheshimiwa Rais na hivyo tunamwita mwanamichezo namba moja kwa sababu ya huu uwekezaji ambao amekuwa akiufanya kwenye nyanja za utamaduni, sanaa, michezo na hata habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sasa nijielekeze kwenye hoja chache ambazo ziliIetwa na Waheshimiwa Wabunge wakati wakichangia hoja hii, kabla sijamwachia Mheshimiwa Waziri kujimwayamwaya na kumalizia zilizobaki. Ninaomba nijibu hoja za Mheshimiwa Husna Sekiboko Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge, ambaye amekuwa akitusaidia sana, yeye na Kamati yake, kutusimamia kutupa maelekezo na miongozo na kufanya kazi yetu iwe rahisi. Yeye alitoa pongezi nyingi kwa Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa uwekezaji mkubwa ambao umekuwa ukifanyika katika Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ambalo tumelishika na tumeliandika chini na tutakwenda kulifanyia kazi ni kuhakikisha kuwa hakuna kigugumizi kwenye utoaji wa fedha za maandalizi ya michuano ya *AFCON*. Hii kwa sasa ni ajenda namba moja. Nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo, ya kwamba tunalifahamu na tunasisitizana humu ndani kwenye Serikali, Wizara zote ambazo kwa namna moja ama nyingine zina kitu cha kufanya kwenye *AFCON* kuhakikisha hakuna kigugumizi kwenye

utoaji wa fedha na miradi yote inayohusiana na *AFCON* inatekelezwa kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali kadhalika alizungumzia uwekezaji kwenye miundobinu ya michezo mingine, kama vile mpira wa kikapu. Ni kweli, kwamba tuna timu kama Dar *City* ya ndugu yangu Musa, ambayo imekuwa na uwekezaji wa mtu binafsi na ambayo imefanya vizuri na imeitoa kimasomaso nchi yetu. Ukweli ni kwamba hata mradi wa viwanja changamani ule wa Dar es Salaam, miongoni mwa miradi inayotekelezwa pale ni uwanja wa ndani ambao unakwenda kuchezwa michezo kama *basketball*. Hali kadhalika ujenzi wa *arena* ambao Mheshimiwa Waziri ameniambia atakuja kuizungumzia ni jambo ambalo limelenga kuhakikisha kwamba tunapata maeneo ya kufanya michezo yote ambayo inatakiwa kuchezwa ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye upande wa Mheshimiwa Clayton Chipando (Baba Levo), moja ya mambo aliyasema ambayo ningependa nimemwomba Mheshimiwa Waziri nilijibu mimi ni kuhusiana na uwekezaji kwenye timu. Kwamba tusiweke tusiwekeze tu kwenye miundobinu kwa ajili ya *AFCON,* lakini pia tuhakikishe kwamba tunawekeza kwenye timu tusije tukatia aibu wakati wa mashindano haya. Ukweli ni kwamba tunafahamu; mashindano haya tunaandaa katika kutokea *angle* mbili. Ya kwanza ni kuhakikisha kwamba tunakuwa waandaaji wazuri kama *host country,* lakini la pili ni kuhakikisha kuwa tunakuwa washiriki wazuri hali kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata leo mchana wakati tumepata *break* hapa nilikuwa mmoja wa watu tuliopoteza muda mwingi kuzungumza kuhusu mpira ni kocha wa Timu ya Taifa ndugu yangu Miguel Gamondi. Tulikuwa tunaongelea d*evelopment* ya mpira wa miguu, namna ambavyo tunaweza kupata wachezaji kutoka chini; tunaweza pamoja na mambo mengine kuhakikisha wachezaji wa ndani wanapata nafasi kwenye nafasi zote na kuimarisha timu yetu ya Taifa. Kwa hiyo hili tunalijua tunafahamu kwamba tuna vitu viwili vya kuandaa; tuandae mashindano yenyewe na pia tuandae timu yetu ya Taifa ili tusije tukatia aibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwingine ambaye ningependa kujibu hoja zake ni mama yangu, Mheshimiwa Khadija Aboud. Wakati anainuka kuchangia nilimwambia Mheshimiwa Waziri hapa, mama wa Kiswahili. Kama ningekuwa nina-*bet* ningemwambia Mheshimiwa Waziri tuweke hela, asipochangia kuhusu Kiswahili nitakulipa; na kweli akaja akazungumza mchango mzito kabisa kuhusiana na masuala ya Kiswahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, amesema mambo mengi, lakini miongoni mwa mambo aliyoyasema ni kuhusiana na kwanza ushiriki wa Zanzibar kwenye maamuzi yanayohusu BAKITA. Tumechukua ushauri wake na tutaufanyia kazi. Hali kadhalika kuhusiana na ugumu wa maneno mapya ambayo yanatengenezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli ni kwamba mimi binafsi ninapata shida sana kuhusiana na maneno haya ambayo BAKITA wamekaa kama Kamati na kuamua neno hili litumike kwa jambo fulani. Neno meza kwa mfano halina uhusiano na kitu meza; na neno meza ni neno la Kireno. Hatukukaa tukaamua kwamba neno hili kwa sababu linatumika Kireno sisi tukae chini tutunge neno letu. Maneno yote yanatoka kiasilia kwenye lugha na yale ambayo yanakuwa rahisi kutumika yanarasimishwa na kuendelea kutumika kama maneno rasmi ya lugha hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kiingereza kimekuwa kikubwa kwa sababu ya kukopa maneno kutoka kwenye lugha nyingine kama Kijerumani, Kifaransa na Kilatino. Kiswahili hali kadhalika kimetoa maneno kutoka kwenye Kiarabu, Kireno, Kiingereza na kadhalika. Hivyo Mheshimiwa Waziri ameagiza kwamba tukae na wenzetu wa BAKITA tujadiliane namna ambavyo maneno yatakayokubalika kurasimishwa kutumika kwenye lugha ya Kiswahili yawe maneno rafiki yanayoweza kukubalika na kuingia kwenye maneno ambayo yanatumika kikawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hili tutalifanyia kazi; na nimwahidi Mheshimiwa Aboud, kwanza ahsante sana kwa kugamaa na Kiswahili kila wakati, kuhakikisha anatoa mchango na anakisimamia kweli kweli. Tunaona na tunashukuru kwa

mchango wake mzuri na sisi tutafanya yale ambayo ameyashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninajua muda wangu umekwisha. Niombe Waheshimiwa Wabunge watupitishie bajeti hii ili twende tukafanye kazi ambayo tumekabidhiwa na Mheshimiwa Rais na ambayo Wabunge wamekuwa wakiisimamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Naibu Waziri. Nimwite sasa mtoa hoja aje kuhitimisha hoja yake, Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Christian Paul Makonda.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa uongozi wako mahiri na kutupa nafasi nyingine ya kusikiliza michango ya Waheshimiwa Wabunge. Takriban Waheshimiwa Wabunge 20 ndiyo waliochangia na Mheshimiwa Mbunge mmoja aliyechangia kwa maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote ninaendelea kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutupa uhai tena katika kipindi hiki na kutupa nafasi pia kushiriki katika kujenga Taifa letu kupitia Wizara yetu ya Habari, Michezo, Sanaa na Utamaduni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote kuanzia walioanza kuchangia asubuhi hadi waliomalizia leo jioni. Michango yao yote tumeipokea kwa moyo wa unyenyekevu tukiamini ndiyo msingi mzuri wa kujenga ustawi mpana zaidi wa Wizara yetu kwa malengo ya kuwahudumia wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii pia kumshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu na ufafanuzi mzuri alioutoa kwenye baadhi ya michango ya Waheshimiwa Wabunge ambao michango mingine tutaweza kuleta majibu yao

kwa njia ya maandishi kutokana na muda tutakaokuwa nao hivi leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo ninaendelea kushukuru na nilifurahi sana, nimemwona kaka yangu Nape amepambana kuwahi, lakini bahati mbaya hakuchangia. Ni miongoni mwa watu ambao walikuwa wanafuatilia kusikia mchango wake nikijua kwamba kwanza ni kaka wa wengi lakini pia akapata nafasi ya kuhudumu katika Wizara yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni matarajio yetu kwamba kaka zangu hawa, yeye Mheshimiwa Ndumbaro pamoja na mzee wetu Kabudi na kaka yangu Innocent Bashungwa wataendelea kutupa ushirikiano mkubwa, akiwemo na dada yangu Pindi Chana, ili kuhakikisha kwamba yale waliyotamani kuyafanya kwenye Wizara ambayo ninayo yanaendelea kufanyika na kuleta mapinduzi makubwa zaidi katika huduma ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, michango yote iliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge ninatamani kuigawa katika makundi manne. Kundi la kwanza ni kundi la michezo. Mheshimiwa Naibu Waziri amegusia katika maandalizi tuliyoayo kwa timu yetu ya Taifa. Hapa kipekee tumetaja katika hotuba yetu namna gani Dkt. Samia Suluhu Hassan tunamtambua kuwa mchezaji namba moja wa Taifa letu kwa namna ambavyo anafanya kazi kubwa ya kutuwezesha kuifanya kazi ya Wizara yetu kuwa rahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ametuwezesha katika makundi yote ya michezo kwa kututengenezea kwanza miundobinu kuruhusu sera na sheria na kanuni na kutuwezesha kwa kifedha. Nitatoa tu mfano, tunafahamu matokeo mazuri yaliyopatikana kwa timu yetu ya Taifa, Taifa *Star* katika mashindano ya *AFCON* kule nchini Morocco kwa kocha tuliyekuwa naye aliyefanya kazi kwa muda mfupi Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa ridhaa yake akiwa ni mchezaji namba moja katika Taifa hili, alikubali kumlipa mshahara kutoka kwenye fedha zake binafsi ili kuhakikisha kwamba Gamondi anaendelea kuwa kocha wa timu yetu ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kocha huyu kuwepo kwake kwetu kumeturuhusu kupitia ushirikiano wa *BMT* wakishirikiana na *TFF;* kuhakikisha kwamba tunatoa fursa kwa watoto wa kitanzania walioko ndani ya nchi na walioko nje ya nchi wawe sehemu ya timu yetu ya Taifa kwenye maandalizi ya *AFCON* 2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kukujulisha wewe pamoja na Bunge lako Tukufu kwamba, tayari tuna vijana wa Kitanzania zaidi ya 60 waliopatikana duniani kote ambao wako tayari kurudi Tanzania kuipigania heshima ya nchi yao kwenye mapambano ya *AFCON* 2027. Tumempa nafasi kubwa Mheshimiwa Gamundi na timu yake nzima ya ufundi wafanye kazi ya kuchagua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaelewa, kwamba iko tamaa au shauku kubwa ya kwamba angalau kila jimbo liwe na mtu wa kuwakilisha; lakini sisi tumekubaliana kama Wizara tutayarudisha tena Mashindano ya Taifa *Cup*. Mashindano ambayo yataibua vipaji vya vijana kutoka katika ngazi ya chini. Walioko kwenye mitaa yetu, walioko kwenye kata zetu, walioko kwenye wilaya zetu watashiriki, na kupitia Taifa *Cup* tutapata nafasi nzuri ya kuwaona wachezaji wakubwa wazuri ambao watakuja kuchezea kwenye vilabulia vitu vikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa tumruhusu Gamondi na timu yake ya ufundi waendelee kuwatafuta na kuwatambua vijana wenye vipaji ili asuke kikosi kizuri kitakachoweza kufanya kazi nzuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo Mheshimiwa Dkt. Samia hajatoa tu fedha kwa ajili ya ujenzi wa uwanja. Tumemsikia Waziri wetu wa TAMISEMI katika upande wa barabara za *TARURA,* lakini pia angekuwepo Waziri wetu wa Ujenzi Mheshimiwa Ulega angetaja pia. Pale pale Arusha tayari tumeshasaini mkataba na tayari wananchi wanalipwa fidia ili kupisha mkandarasi afanye kazi kwa ajili ya ujenzi wa barabara zinazoelekea kwenye eneo husika la uwanja wetu; na ndivyo inavyofanyika pia katika maeneo ya upande wa Zanzibar katika viwanja vile vya Fumba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee tena katika upande huu wa michezo. Tumebaini jambo moja kubwa na Waheshimiwa Wabunge watakuwa mashahidi. 95% ya Walimu wa Michezo walioko shule za msingi na sekondari hawana *basic* ya michezo yenyewe. Wamechaguliwa kutokana na *interest* zao tu. Wanakuangalia wanakuona wewe mwili wako kama hivi wa Elibariki Kingu unaonekana kama kijana hivi mtanashati wanasema, hivi wewe unapenda michezo? Anasema ndiyo ninapenda Simba na Yanga. Anamwambia basi wewe utakuwa mwalimu wa michezo. Kwa hiyo tuna upungufu wa walimu wa michezo katika shule za msingi na sekondari zaidi ya walimu 10,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hivyo tuna upungufu wa marefa na makocha. Kwa hiyo sisi kama Wizara tumekubaliana na ninaomba kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri wetu wa TAMISEMI na Mheshimiwa Waziri wetu wa Elimu, tumekubaliana kuendesha *program* mbili, tatu ndani ya kipindi kifupi tuweze kupata matokeo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tumekubaliana kuunda timu ya pamoja ya Wizara ya Elimu, Wizara ya TAMISEMI na Wizara yetu ya Michezo kupitia Chuo chetu cha Malya kuhakikisha kwamba tunatengeneza *program* za muda mfupi na za muda mrefu kwa ajili ya kuwabadilisha walimu wetu hawa wa michezo wawe na *knowledge* ya michezo wanaposimamia michezo katika shule za msingi na sekondari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili tulilokubaliana ya kwamba kwa sababu vyuo vya ualimu vinawapa nafasi walimu kujifunza na sisi tuweke mitaala yetu pale, mwalimu anayetaka kujifunza michezo basi aruhusiwe ku-*opt* michezo ili akitoka pale atambulike kuwa mwalimu wa michezo, anaporudi katika majukumu yake anapopangiwa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo letu hili pia linaenda hadi kwenye upande wa marefa na makocha. Kwa hiyo timu za Wizara zetu tatu TAMISEMI Wizara ya elimu na Wizara yetu ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Mchezo tunaendelea kufanya kwa

pamoja ili tuweze kutengeneza si tu timu ya kushindana *AFCON* 2027, bali tutengeneze timu na vijana wenye uwezo tutakaokuja kuwauza pia si kwenye Vilabu vya Simba na Yanga tu bali na kwa vilabu vingine huko duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili eneo la michezo yako mambo mengi. Ningependa kueleza kwa kina, lakini kwa sababu ya muda hautoshi ninaomba niwaambie Waheshimiwa Wabunge, kwamba, Serikali ya Dkt. Samia chini ya Wizara ninayoisimamia tumejiandaa kikamilifu kui-*surprise* dunia kwa maandalizi ya *AFCON*, 2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mashindano yaliyofanyika Nchini Misri *(Egypt)*, tulivyokwenda Cairo, nilipata bahati nikiwa Mkuu wa Mkoa, lakini mashindano yaliyofanyika Ivory *Coost,* kupitia Wizara yetu hata Naibu amepata nafasi ya kushiriki; mashindano yaliyofanyika Morocco mimi nimepata nafasi ya kushiriki kama Naibu na nimeshiriki kama Waziri nimejifunza na kujua mbinu zao. Ninaomba muwe na imani na Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, tunakwenda kui-*surprise* hii dunia. Hawataamini watakachokuja kukutana nacho hapa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazo ajenda za kitaifa ambazo tunatamani Mwenyezi Mungu akituwezesha tuzitimize. Kwa mfano, kupitia Waziri wetu Mkuu tumemwomba turejeshe mashirika yote yaliyoko nchini, zaidi ya 306, yawe na timu zao kama ilivyokuwa miaka ya nyuma. Bandari walikuwa na timu, Reli walikuwa na timu, Sigara walikuwa na timu. Tayari Mheshimiwa Waziri Mkuu amekwishatoa maelekezo kwa mashirika yote kuanza kutafuta timu ili waweze kutengeneza fursa hizi za kuuza vipaji vya watoto wetu wa hapa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, hili ninalisema kwa sauti ya chini kabisa kwa sababu liko kwenye maombi. Tumekubaliana kutengeneza mkakati wa ku-*support* Waheshimiwa Wabunge wanaohangaika kuendesha ligi kwenye majimbo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kumshirikisha Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ameridhia na tayari tunao mkakati, tunamalizia *design* ya jezi pamoja na mipira ili Mheshimiwa Dkt. Samia aje azindue mashindano ya kwenye majimbo yatakayowawezesha Waheshimiwa Wabunge kuwa na vifaa vya michezo katika maeneo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, michezo kwetu sisi siyo burudani tu, michezo ni fursa ya kuwatoa vijana wa Kitanzania walio na vipaji ambao mwisho wa siku wameamua kuendesha pikipiki na kubeba maguta wakati ni watu maarufu kuliko hata akina Drogba, tunaowaleta hapa kwenye ukumbi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo matumaini makubwa ya kwamba kupitia Taifa *Cup,* kupitia mashindano ya kwenye majimbo, na kupitia Muungano tutaendelea kulea vipaji vya watoto wa Kitanzania na hatimaye Taifa letu kuuza vijana kwenye mataifa makubwa duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba uniruhusu. Nimemsikiliza kaka yangu na rafiki yangu mpendwa daktari Tale Tale. Wakati ninamsikiliza nikaona shauku aliyokuwa nayo ya kwamba anatamani kuona *arena* inajengwa. Hata hivyo, nilipofuatilia kwa kina nikagundua Babu Tale ni Mjumbe wa Kamati yetu ya Elimu, Utamaduni na Michezo. Nikasema Msigwa nimekukosea nini ndugu yangu kiasi kwamba kabrasha ulilompa Babu Tale umenyofoa *page* namba 79(1)(b) kinachoelezea mkakati wa Serikali wa kujenga *arena?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Habari, Sanaa, Michezo na Utamaduni tumejipanga kikamilifu. Ukisikiliza hotuba ya Waziri wetu wa Uwekezaji aliongelea mpango wa ujenzi wa *arena* ndani ya bajeti ya miaka mitano. Pia, Ilani ambayo ndugu yangu Mheshimiwa Sanga ameisoma imeeleza kwa kina; ni Ilani ya 2025-2030. Mipango ya ujenzi wa *arena* iko palepale na tayari kwenye bajeti ambayo leo Wabunge wataipitisha tumeweka *token* ya shilingi bilioni moja ikiwa ni sehemu ya fedha za kuanza *feasibility study.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wakiangalia kwenye picha, wataona michoro ya kwanza ambayo tumeshaipata na tayari eneo tunalo la pale Tanganyika *Packers,* Kawe na eneo hilo tunalo la heka 12. Tunasubiri tu tukamilishe tuingie kwenye *feasibility study,* kwa mpango mkubwa wa Mheshimiwa Dkt. Samia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ninaomba niende taratibu. Mheshimiwa Dkt. Samia alifanya mazungumzo na Serikali ya Korea kuomba fedha zaidi ya dola bilioni 2.5. Katika fedha zile miongoni mwa hizo fedha tumepangiwa Wizara ya Habari, Sanaa, Michezo na Utamaduni, kwa ajili ya ujenzi wa *arena* ya kisasa yenye thamani ya shilingi bilioni 300, kwa ajili ya ujenzi wa *studio* yenye thamani ya zaidi ya shilingi bilioni 150. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo fedha siyo rahisi kuiona kwenye bajeti yetu, kwa sababu hiyo fedha inategemea mazungumzo yanavyozidi kwenda, lakini dhamira ya Mheshimiwa Dkt. Samia amesema hata kama hii fedha ikichelewa ndani ya miaka miwili au mitatu ijayo, malengo yangu kwenye miaka yangu mitano lazima nijenge *arena* ya kisasa itakayokuwa na uwezo mkubwa zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, tumeendelea kuhamasisha wadau, kuwaomba wadau wote wenye uwezo waje. Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia iko tayari kushirikiana katika *private sector* na kuhakikisha kwamba tunajenga *arena.* Hivi ninavyoongea tayari tunaye mwekezaji pale Ubungo anajenga *arena* ya kubeba watu 2,500, lakini tayari tunaye mwekezaji kupitia timu yetu ya Dar City ambaye tayari amepata eneo Kinondoni na yeye anajenga uwanja wa *basket* kwa ajili ya timu yetu ya hapa ndani na timu zetu za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nikuhakikishie ndani ya miaka hii mitano itakuwepo *arena.* Pia, *studio* inayokwenda kujengwa, nimeusikiliza vizuri sana mchango wa Mheshimiwa Mbunge ndugu yetu ambaye tena ni Naibu Katibu wa mambo ya chama chetu. Kaeleza kwa kina sana habari ya mavazi, ameeleza habari ya vifaa vya wasanii wanapokwenda kuigiza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika, si kila Mtanzania amefika Marekani, lakini kila mtu anajua ukubwa wa Jeshi la Marekani kupitia kwenye taarifa ya habari pamoja na habari ya *movie.* Kila mtu hajafika Marekani, lakini tunajua *White House* imekaaaje. Hiyo yote ni kazi iliyofanywa na uwekezaji mkubwa, ambapo hilo jengo tunalokwenda kulijenga, tukisema *studio* Waheshimiwa Wabunge siyo *studio* yenye *microphone* na kiti na *soundproof,* hapana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *studio* ambayo; basi tu kwa sababu humu Bungeni siruhusiwi, lakini ningesema Waheshimiwa hebu waingie kwenye simu zao waangalie namna au jinsi ilivyotengenezwa *Titanic movie.* Ile *Titanic movie* ukiitazama unaweza ukahisi ni bahari moja kubwa, mabarafu makubwa; watu walikuwa kwenye chumba tu Waheshimiwa. Hiyo kazi yote ndiyo Mheshimiwa Dkt. Samia anataka kuwajengea vijana wake na watoto wake ndani ya nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, habari ni habari. Kwa muda mrefu habari mbaya zimechukua nafasi ya kuharibu fikra za Watanzania. Kwa bahati mbaya watu waliofanikiwa kutumia baadhi ya watu wenye ushawishi kujenga mazingira ya kwamba Tanzania siyo sehemu nzuri na haina fursa. Watu hao wanakwenda mbali zaidi kuwafanya watu wawape taarifa za kuichukia nchi yao halafu wageni wanakuja na kwa sababu wageni hawajui Kiswahili, kwa hiyo, hawasikii umbea, wanakuja wanasoma ripoti wanaona fursa. Hakuna mgeni anayekuja Tanzania akakubali kuondoka kwa fursa zilizoko ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanakwenda hatua zaidi, wageni hao wakija nchini wana-*compare* kule walikotoka na kwetu. Mimi niko pale katika Jimbo la Arusha, huwa ninasema mara nyingi Jimbo la Arusha linaongoza dunia. Tuna Wahindi, tuna Wachina, tuna Waarabu, tuna Wadachi, wamejaa pale na wanaishi pale na wakifa wanazikwa pale. Nyumbani kwao imekuwa pale Arusha, kwa sababu gani? Kwa sababu kuna fursa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kutumia hadhara hii kuwaomba waandishi wa habari; moja, tusikubali kujaza habari za kukatisha tamaa Watanzania wenzetu wakati tunazo fursa za kujenga nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, maadili ya Taifa letu yako mikononi mwa wanahabari. Vyombo vya habari vikiamua kutokuwapa *spotlight* watu wenye maadili mabovu tutalijenga Taifa hili la Baba wa Taifa na kuhakikisha kwamba maadili yetu yanabaki salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaendelea kuwaomba na kuwasihi kwa unyenyekevu mkubwa; tusingetamani kutumia vyombo tulivyonavyo kama *TCRA* pamoja na Mamlaka ya Ithibati, tungetamani na wewe uone mchango gani unautoa katika kulinda maadili ya watoto wa Kitanzania. Ujiulize, mtoto huyu unayempelekea habari za kumbadilisha tabia yake na kuingia kwenye matendo mabovu yasiyompendeza hata Mwenyezi Mungu, kama ni mtoto wako unajisikiaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawaomba kwa unyenyekevu mkubwa tuachane na *spotlight* za watu wanaofanya mambo mabaya, tuibue fursa tulizonazo na ubora wa Taifa letu katika kujenga uchumi wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikia kilio kikubwa cha vyombo vya habari. Mheshimiwa Kija amesema vizuri sana na Mheshimiwa Dotto kasema kwa mchango mzuri sana. Niwahakikishie tu, kama kuna vyombo vya habari havijalipwa na Mheshimiwa Dkt. Samia aliagiza na taasisi hizo ziko ndani ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ninawaomba wamiliki wote wa vyombo vya habari kesho saa nne asubuhi wanipatie majina nianze kufuatilia madeni yao kuhakikisha kwamba wanalipwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani Rais wa Jamhuri ya Muungano akatoa maelekezo halafu kuna mtu akamnyima fursa mwanahabari kupata haki yake. Niwahakikishie vyombo hivi vinapokosa fedha ni ukweli usiopingika vinashindwa kuajiri hata watu wenye taaluma zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, imefika hatua mwandishi wa habari anaambiwa wewe tengeneza *microphone* yako, nenda utalipwa posho huko. Wako watu wana habari za msingi na za faida kwa Taifa, lakini hawaonekani popote, kwa nini? Kwa sababu hawana posho ya kumlipa yule kijana aliyebeba *microphone.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, habari ni haki ya kila Mtanzania. Ninawahakikishia Waheshimiwa Wabunge watakapopitisha bajeti hii, mimi na timu yangu nikiwa pamoja na Naibu wangu, tutahakikisha kwamba yale majina yote tunawaandikia wale wote ambao wanadaiwa na pale ambapo itaonekana wameshindwa kulipwa tutampelekea Mheshimiwa Rais, "*Mama huyu ndiye ambaye hataki kutekeleza agizo lako.*"

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mambo yaliyotajwa hapa yametajwa mambo ya Kiswahili, Mheshimiwa Naibu Waziri amejibu vizuri. Yametajwa mambo ya michezo ndugu yangu Mbunge wa Kigoma Mjini, kaeleza vizuri sana tena kwa kina, lakini yeye alijikita kwenye upande mmoja tu baada ya kwamba upande wa pili kazi imefanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwahakikishie tu Waheshimiwa Wabunge fedha hizi tulizozitenga kwa ajili ya *content creators* pamoja na Mfuko wa Utamaduni wanaruhusiwa pia hata wamiliki wa vyombo vya habari kukopa. Mkopaji wa kwanza ambaye alipata fedha yake juzi tu na akapiga simu ni Babalevo kupitia *media* yake. Kwa hiyo, hii fedha siyo kwamba unazuiwa wewe kukopa, hata mmiliki wa chombo cha habari ana haki ya kuja kwetu na kuchukua mkopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yako mambo mengi ambayo yametajwa na ufahamu kabisa, Mheshimiwa Sanga katoa mawazo mazuri sana na yote nimeyachukua tena kwa kina. Mheshimiwa Elibariki Kingu katoa mawazo mazuri sana tumeyachukua tena kwa kina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utamaduni wetu mbele yako Mheshimiwa Mwenyekiti na watendaji wetu wako upande wa pili pale. Alichosema Mheshimiwa Naibu Waziri ni kweli Wizara ya

Habari, Utamaduni, Sanaa, na Michezo wana kazi mbili. Ukiacha kazi hii kuna kazi ya mimi kuwepo kwao. Hivi ninavyoongea wanaelewa kila mwenye jambo lake ameshayadaka na tukitoka hapa hatutakuwa na muda wa kupoteza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati mbaya waganga siwajui, heshima niliyonayo mimi ni kazi ifanyike. Kama kazi haijafanyika maana yake heshima yangu haipo. Mtoto mimi nimetoka kwenye familia ambayo baba yangu hajawahi kwenda hata la kwanza. Alikuja kuchukuliwa na jeshi tu akaingia kwenye vita kule anajua kutumia bunduki. Mama yangu mzazi ndiye msomi kuliko watu wote nyumbani kwetu, darasa la saba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi mimi nikiacha kufanya kazi kweli ninaringia kitu gani kingine? Kwa hiyo, hapa ninajua kinachonikalisha ni kazi, itakayonifanya niendelee kuwepo ni kazi na ili niendelee kudumu lazima kazi ifanyike. Niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge, michango yao yote waliyoitoa kuanzia kwenye vyombo vya habari, kwenda kwenye utamaduni, kwenda kwenye michezo, kwenda kwenye sanaa na kote. Jana tuliwaalika na leo walikuwepo wasanii akina Fid Q wanafanya kazi kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepanga na Mheshimiwa Waziri wangu Mama yangu Gwajima tunakwenda kuunda Kamati ya Maadili na kuandaa makongamano ya nchi nzima. Tutahitaji viongozi wa dini, tutahitaji wasanii, tutahitaji makundi yote ili tushirikiane wakiwemo na Waheshimiwa Wabunge kuhakikisha kwamba tunaleta matokeo sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo yangu hayo marefu nikushukuru tena wewe, niishukuru na timu nzima ya Katibu wetu wa Bunge. Pia, niwashukuru Mheshimiwa Naibu Waziri pamoja na timu yetu ya watendaji ikiongozwa na ndugu yetu Gerson Msigwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee kwa upendeleo mkubwa ninaomba nimshukuru baba yangu Profesa Palamagamba Kabudi. Profesa amefanya kazi kubwa na nzuri sana. Nimeikuta

Wizara ameshaweka msingi na mimi kazi yangu ni kuwaambia tu yale waliyokubaliana na Profesa yanatakiwa yakamilike kwa 100%. Tunafanya kazi vizuri na amejenga msingi mkubwa mzuri ambao mimi kijana wake ninahakikisha kwamba ninauendeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeendelea kuomba *support* kutoka kwa kaka yangu Nape na Mawaziri wote waliopita mahali pale wananipa ushirikiano wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kuwashukuru watu binafsi walioanzisha timu na kutengeneza *centre* za kulea vijana. Watu hawa wamekuwa na mchango mkubwa sana. Katika kila kona ya nchi yetu ukienda utawakuta. Wanaweza kuwa wanahangaika na watu wawili, wanahangaika na watu watatu, wanahangaika na watu wanne, lakini mwisho wa siku wamekuwa na mchango mkubwa na hawa wachezaji wengi tunawaona kwenye timu zetu ni miongoni mwa wachezaji ambao wamelelewa na wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua mchango wao na tunawasihi wasichoke. Tutaendelea kuwapa ushirikiano na tuna mpango katika Wizara yetu kuwatambua watu wote waliowezesha Wizara hii kufanya vizuri ili na wao wapate motisha ya kuendelea kuifanya katika kujenga mustakabali mpana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, tumemwomba Waziri wetu wa TAMISEMI. Nilipokuwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam tulisimamia kujenga kile kiwanja cha Kinondoni cha *KMC*. Kiwanja kile siyo mali ya Wizara, kile kiwanja ni mali ya Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni. Tunaomba kupitia hadhara hii mbele ya Bunge lako Tukufu kumwomba Mheshimiwa Waziri wetu ambaye tayari tumeshampelekea maombi, kila halmashauri zenye uwezo zijenge viwanja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kaka yangu ameniambia habari ya Songwe, ninaelewa kwamba uwezo huo wa Wizara yetu kwa sasa nisiwe mwongo, hatuna kutokana na mambo yaliyoko mbele yetu na *commitment* za kimataifa ambazo Serikali imeingia. Niwaombe kwa unyenyekevu mkubwa, kupitia halmashauri na

kwa sababu sisi Wabunge ni Wajumbe wa Baraza la Madiwani twendeni tukashawishi tutenge fedha tuanze ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ninavyoongea Waheshimiwa Wabunge chini yako, tayari katika Jimbo letu la Arusha Mjini, Halmashauri ya Jiji la Arusha Mjini tunajenga uwanja wenye kubeba mashabiki 10,000 na wenye uwezo wa ku-*host* Rais pamoja na Makamu wa Rais na wenye uwezo wa kuwa na vyumba vya kubadilishia nguo wachezaji, vyumba vinne vyenye *level* ya kukaribia standard ya *CAF category 4*, lakini pia tunajenga viwanja viwili vya *basketball.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge ninajua tayari kwenye maeneo mengine mambo yanaendelea vizuri. Wale ambao kwenye halmashauri zenu bado hakuna miradi ya namna hiyo, tumuombe Mheshimiwa wetu Waziri wa TAMISEMI atusaidie kusukuma. Kwa kweli tukifanikisha hili jambo ni rahisi sana, sana, sana kuvikuza vipaji tulivyokuwa navyo ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunao mpango tunaendelea nao katika ujenzi wa *swimming pool* ya *Olympic* Dar es Salaam zaidi ya mita 50, na hapa Dodoma tunajenga mita 25. Pia, viko viwanja nimemsikia dada yangu Mheshimiwa Asha Baraka akisema kwamba kile kiwanja cha *leaders* pale hajui kinaendelea nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kesho baada ya Bunge hili Tukufu jioni, nimpatie tiketi ya *SGR,* dada yangu Mheshimiwa Asha Baraka aende akaone, pale atakuta kuna trekta zinafanya kazi. Pale tunajenga uwanja wenye uwezo wa kubeba watu 5,000 ndani ya *Leaders Club* ikiwa ni sehemu ya ile miradi ya viwanja vya maandalizi kwa ajili ya mafunzo ya watu wanaokuja kufanya *training ya AFCON*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa unyenyekevu mkubwa mbele yako na mbele ya Mwenyezi Mungu, ninaomba sasa nitoe hoja Bunge lako Tukufu liridhie kumalizia kipengele kilichobaki cha kupitisha bajeti ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Samahani Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Hoja imetolewa na imeungwa mkono.

Katibu.

**NDG. MICHAEL CHIKOKOTO, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR – KATIBU MEZANI:**

**KITABU CHA PILI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 96 – Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo**

Kifungu 1001 - *Administration and Human Resources Management*......................................Sh. 8,904,042,000

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa hilo ndilo Fungu la mshahara wa Waziri. Nimepokea taarifa ya kuomba maelezo ya Mheshimiwa Ester Bulaya.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Kwanza, niwapongeze Waziri na Naibu wake, wanafanya kazi nzuri sana na tutaona mabadiliko kupitia Mawaziri hawa vijana na sijutii kumwachia Idara mdogo wangu Makonda. Ninajua uthubutu wake na ninajua *commitment* yake. Mungu atamsaidia na tutampa ushirikiano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kupata ufafanuzi wa Mheshimiwa Waziri kuhusiana na mkakati wa kuinua soka la wanawake. Sijaona kinagaubaga kwenye hotuba yake kuhusiana na soka la wanawake, ni kama limesahaulika hivi. Vilabu vina-*struggle* kwelikweli na mpaka sasa hivi kwenye ligi ya wanawake hakuna wadhamini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watoto wetu wa kike wameshaona fursa kwenye mpira wa wanawake. Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha soka la wanawake linakua kama ilivyo soka la wanaume. Wanaona kama wametengwa hivi na mimi kule Bunda nina Bunda *Queens* wanajitahidi kwelikweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi tunavyozungumza Mheshimiwa Waziri anajua Twiga *Stars* imefuzu *WAFCON* mwaka huu na yenyewe pia Wizara wana mkakati gani kama ambavyo tuna mkakati wa Timu ya Taifa ya Wanaume kuhakikisha na hawa nao wanafanya vizuri ili wawe mfano kama dada zao akina Sofia ambaye alipata fursa ya kucheza Ligi Kuu ya Uingereza (Brighton), Clara Luvanga kule Saudi Arabia; akina Esther na wengine wengi. Wanahisi wametengwa na ninajua Waziri anajali akina mama na anawajali wanawake. Sema neno kwa soka la wanawake.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Hoja yako imeeleweka Mheshimiwa Ester Bulaya.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tuki-*invest* tutahakikisha wadhamini watakwenda. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Imeeleweka. Mheshimiwa Waziri, nikupe nafasi uweze kutoa maelezo.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru na ninamshukuru sana dada yangu Mheshimiwa Ester Bulaya kwa swali lake zuri. Nimhakikishie tu, soka hili linajengwa kuanzia kwenye misingi ya uongozi wa vyama vya michezo. Tulipata bahati kukutana viongzi wa vyama vyote na kujadiliana umuhimu wa kuinua michezo kupitia kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama unavyofahamu chama cha wanawake kilipitia changamoto hapa katikati ambayo tumefanikiwa kui-*resolve* katika kipindi hiki cha muda mfupi. Nimhakikishie kupitia BMT na kazi inayoendelea na hata kwenye *Vote* ya BMT ataona pale, ni kwa ajili ya maendeleo ya michezo yote siyo ya wanaume tu, bali wakiwemo wanawake, watu wenye ulemavu na sekta nyingine mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutaendelea kushirikiana na vyama vyote vya michezo kuhakikisha kwamba michezo hii inapata nguvu na sisi Serikali tukiwa walezi wakubwa wa michezo hii kama ambavyo inafanya vizuri TFF kwenye upande wa mpira wa miguu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwomba sana dada yangu Mheshimiwa Ester Bulaya aridhie hii bajeti. Bahati nzuri pia tulipata viongozi wa michezo wanawake hata kwenye Bunge lako Tukufu hapa. Tutashirikiana kwa pamoja kuhakikisha ya kwamba tunainua michezo hii ili Taifa letu liendelee kufanya vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwenye rekodi pia ukumbuke, miongoni mwa wachezaji wazuri, kwa mfano tunamfahamu mtu wetu anaitwa Ronaldo kama ndiye mchezaji mzuri kwenye upande wa *Middle East,* lakini nimhakikishie mtoto wa Kitanzania kutoka Iringa ndiye anayewaburuza katika hiyo nchi akiwa namba moja katika wachezaji bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ester Bulaya, baada ya maelezo hayo, unaridhika?

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Ndiyo.

**MWENYEKITI:** Ahsante.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nilishaongeza muda bila kuwahoji kwa mujibu wa Katiba zetu. Kwa hiyo, sasa tunakwenda kwenye *guillotine*.

Katibu.

**NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR – KATIBU MEZANI:**

**Fungu 96 – Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo**

Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*.................Sh. 700,096,000
Kifungu 1003 - *Policy and Planning Unit*.......................Sh. 967,675,000
Kifungu 1004 - *Government Communication Unit*.....Sh. 522,359,000
Kifungu 1005 - *Procurement Management Unit*.........Sh. 461,192,000
Kifungu 1006 - *Internal Audit Unit*.................................Sh. 395,795,000
Kifungu 1007 - *Information and Communication Technology Unit*...................................Sh. 583,618,000
Kifungu 1008 - *Legal Service Unit*.................................Sh. 330,750,000
Kifungu 1009 - *Monitoring and Evaluation Unit*...........Sh. 380,545,000
Kifungu 6001 - *Culture Development Division*..........Sh. 3,315,449,000
Kifungu 6004 - *Sports Development*..........................Sh. 4,501,741,000
Kifungu 6005 - *Arts Development Division*..............Sh. 11,523,801,000
Kifungu 7003 - *Information Services*........................Sh. 34,550,006,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR – KATIBU MEZANI:**

**KITABU CHA NNE**

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 96 – Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo**

Kifungu 1003 - *Policy and Planning Unit*...................Sh. 4,242,530,000
Kifungu 1004 - *Government Communication Unit*.......................Sh. 0
Kifungu 6001 - *Culture Development Division*.........Sh. 7,401,576,000
Kifungu 6004 - *Sports Development*......................Sh. 404,346,682,000
Kifungu 6005 -*Arts Development Division*...............Sh. 10,500,000,000
Kifungu 7003 - *Information Services*.........................Sh. 31,700,000,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge Lilirejea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae. Mtoa hoja, taarifa.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 126(3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Agosti, 2025, ninaomba kutoa taarifa kwamba Bunge lako limekaa kama Kamati ya Matumizi na limekamilisha kazi zake. Ninaomba taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaafiki.

**MWENYEKITI:** Hoja imetolewa na imeafikiwa. Tukae. Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni ya 124(4), sasa nitawahoji kuhusu hoja ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya

Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, kwa mwaka 2026/2027. Walioafiki wameshinda. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 Yalipitishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, sasa ninatangaza rasmi kwamba Bunge hili limepitisha kwa kauli Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri na timu yake yote. Mheshimiwa Waziri umeona maoni ya Wabunge yaliyo mengi na mengi umesema kwamba timu yako inayachukua kwenda kuyafanyia kazi. Bunge lina matumaini makubwa na lina imani kubwa sana kwako kama vile Mheshimiwa Rais alivyoonesha imani kubwa kukupa hii kazi na Wabunge umewasikia wakisema.

Vilevile, nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri, msaidizi wako wa karibu na wasaidizi wengine: Katibu Mkuu, Ndugu Gerson Msigwa na Naibu Katibu Mkuu, Ndugu Methusela Ntonda na watendaji mbalimbali ndani ya Wizara hii katika ngazi mbalimbali wote kwa umoja wenu.

Waheshimiwa Wabunge, kwa namna ya pekee niipongeze sana Kamati yetu ya Elimu, Utamaduni na Michezo inayoongozwa na Mheshimiwa Husna Sekiboko kwa kazi nzuri ya uchambuzi ambao umetusaidia kupata maoni mazuri. Tunawatakia kazi njema kama Bunge. Tuna kazi kubwa ya *AFCON* na tuna matumaini makubwa sana kwamba nchi yetu kama ulivyosema itatamalaki kidunia kwenye kuonesha kwamba nini tumekiandaa kwenye *AFCON* 2027.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo machache, ninaahirisha Bunge hili mpaka kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 1.46 Usiku Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumanne, Tarehe 5 Mei, 2026 Saa Tatu Asubuhi)*

PARLIAMENT OF TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA